1 APRILI, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Pili – Tarehe 1 Aprili, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:

KIAPO CHA UAMINIFU NA AHADI YA UZALENDO KWA WABUNGE

SPIKA: Kiapo.

NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:

Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed;
Mhe. Dkt. Lazaro Killian Komba Bunungu;
Mhe. Mariam Said Khamis;
Mhe. Said Ali Mbarouk;
Mhe. Shaame Ali Ali; na
Mhe. Simai Mohammed Said.

(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliotajwa hapo juu waliapa Kiapo cha Uaminifu na Kutoa Ahadi ya Uzalendo)

SPIKA: Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA K.n.y. WAZIRI MKUU:

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MHE. DEVOTHA D. MBURARUGABA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MHE. YAGI M. KIARATU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MHE. HAPPINESS D. NGWANDO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII: -

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Mahusiano) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MHE. JAFARI W. CHEGE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

SPIKA: Ahsante.

Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD - KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza maswali na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola.

Na. 1

Ukamilishaji wa Maboma Jimbo la Mwibara

MHE. KANGI A. LUGOLA aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha maboma 49 ya madarasa ya shule za msingi na maboma matatu ya zahanati za vijiji vitatu vya Jimbo la Mwibara?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, Mbunge wa Jimbo la Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 hadi kufikia 2025/2026, Serikali imetoa jumla ya shilingi milioni 379 kukamilisha maboma 33 ya madarasa na shilingi milioni 250 kukamilisha maboma matano ya zahanati za Nambaza, Muranda, Mwiseni, Neruma na Sozia katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imetoa jumla ya shilingi milioni 241 kwa ajili ya ukamilishaji na uimarishaji wa huduma za mama na mtoto katika Zahanati ya Kabainja na shilingi milioni 50 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma manne ya madarasa. Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya madarasa na zahanati katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Lugola.

MHE. KANGI A. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa majibu niliyojibiwa ni tofauti na swali nililouliza, ninauliza swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuja Mwibara ili aone nilichouliza cha maboma ya zahanati ya Kigaga, Nambugi na Sikiro, na maboma niliyouliza ya shule ya msingi Mwibara, Sunsi, Gwanza, Busambu, Mwiruruma, Mgara ‘A’ na ‘B’, Sikiro, Majoro, Igundu, Buramba, Berendabufwe na Marama, Kasaunga, Masaunga na Magunga, Kenkombe pamoja na

Nampangala ili baadaye afanyie kazi aone utofauti wa alichonijibu na kile nilichouliza? Je, yuko tayari?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Kangi Lugola kwa kazi kubwa anayoifanya kuwasemea Wananchi wa Jimbo la Mwibara.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tumekuwa tukifanya ziara tukiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mimi na Mheshimiwa Mbunge tutafika Jimboni Mwibara na kujionea maboma hayo. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Mwibara kwamba Serikali imejielekeza kukamilisha maboma haya na tutaendelea kutenga fedha.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Christina.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, tatizo hili la maboma hata katika Jimbo la Itwangi na Solwa ni changamoto kubwa sana. Ni upi mpango mkakati endelevu wa kuhakikisha kwamba yale maboma yaliyoanza kujengwa na wananchi yanakamilika?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali inatambua nguvu za wananchi na tunaendelea na utekelezaji wa kuhakikisha maboma haya yote yanakamilika. Mkakati endelevu na wa kudumu, kwanza tumesitisha uanzishwaji wa maboma mengine mapya na tunahakikisha tunakamilisha maboma yote ambayo tumeanzisha katika Majimbo yetu.

SPIKA: Mheshimiwa Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza. Maeneo ambayo pia yana changamoto ya kuwa na maboma kwenye sekta ya elimu pamoja na afya ni pamoja na Jimbo la Bunda Mjini. Ni lini sasa watamalizia ili wananchi wapate huduma ya afya na elimu?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Spika, hata kupitia katika randama zetu za mikoa, tumekuwa tukielekeza kwamba tutenge bajeti hasa katika Halmashauri zetu ili kukamilisha maboma haya. Pia, upo mpango mkakati wa Serikali kupitia fedha za ruzuku ili kuhakikisha tunakamilisha maboma haya nchi nzima.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Neema Gerald.

Na. 2

Ujenzi wa Uzio Hospitali Zote za Wilaya Nchini

MHE. NEEMA G. MWANDABILA aliuliza: -

Je, upi mpango wa Serikali katika kuhakikisha hospitali zote za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati zinakuwa na uzio?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uzio ni hitaji muhimu kwenye vituo vyetu vya kutolea huduma za afya nchini kwa ajili ya usalama wa watoa huduma wetu, wagonjwa, jamii inayozunguka vituo vya kutolea huduma za afya, mali pamoja na kuzuia uvamizi wa ardhi

ya kituo. Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tayari imetoa maelekezo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha maeneo yote ya taasisi za umma, hususan vituo vya huduma za afya na shule yanapimwa na kutengenezewa hatimiliki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa uzio kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, kwa sasa Serikali imejielekeza katika kukamilisha miundombinu muhimu ya kutolea huduma za afya, ikiwemo jengo pacha la huduma za uzazi/upasuaji, jengo la kufulia, wodi na jengo la kuhifadhia maiti. Aidha, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri itaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa uzio kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kote nchini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Neema.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, ujenzi wa uzio katika vituo vya afya na hospitali zetu huko Halmashauri haujawa kipaumbele, ni ipi kauli ya Serikali kuzielekeza Halmashauri zijenge uzio kwenye vituo vya afya, zahanati pamoja na hizo hospitali za Wilaya?

Mheshimiwa Spika, pia, ninatamani kufahamu, ni upi mpango wa Serikali kupeleka zile fedha ambazo ilikuwa imeahidi kumalizia katika Kituo cha Kamsamba Jimbo la Momba? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye majibu yangu ya msingi, kipaumbele cha Serikali hasa katika hivi vituo vyetu vya afya na zahanati zetu ni kuhakikisha angalau zile huduma za *maternity complex,* kuokoa maisha ya mama na mtoto. Pia, hatujaacha nyuma kujenga uzio katika maeneo yote ya hospitali.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Neema kwa kuendelea kuwasemea wananchi hawa, nasi tutaendelea kupeleka bajeti kwa ajili ya kujenga uzio.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili aliloelezea kuhusu hiki kituo cha afya, tayari tumeshazungumza kwenye vikao vyetu vya halmashauri, na tulikutana na Wakurugenzi ili kuhakikisha zile fedha ambazo Serikali imezielekeza, ni kweli ziende zikafanye kazi ya kumalizia ujenzi wa kituo cha afya.

SPIKA: Mheshimiwa Azza Hamad.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Kituo cha Afya cha Tinde kimezungukwa na barabara kuu tatu; barabara iendayo Dar es Salaam, Kahama na Mwanza. Kituo hiki hakina uzio. Je, ni nini mpango mkakati wa Serikali kuhakikisha Kituo cha Afya cha Tinde kinajengewa uzio?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Azza kwa kuwapambania wananchi wa Jimbo la Itwangi. Kituo cha Afya cha Tinde ni njia yangu ya kuelekea Jimboni Busanda. Huwa mara zote ninapita pale na tunajionea sote kwa sababu kile kituo kiko njiani.

Mheshimiwa Spika, nilifanya ziara katika kituo hiki cha afya, hakika kinahitaji uzio kwa maana ya kwamba kipo karibu sana na barabara. Pia tunawaomba wenzetu wa *TANROADS* waweze kuzungumza na wale wafanyabiashara waliopo katika kingo ile ya barabara ili kukipa nafasi kituo na kuendelea kutenga bajeti.

Mheshimiwa Spika, nimeshafanya mawasiliano na Mkurugenzi ili kuweza kutenga bajeti na kufanya tathmini ya uzio huu na hitaji la kibajeti ili tuone namna gani ya kuweza kuanza kujenga uzio.

SPIKA: Mheshimiwa *Engineer* Amos.

MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini kituo chetu cha afya kilichopo Kata ya Kipili, Jimbo la Sikonge, kitajengewa jengo la wagonjwa wa nje *(OPD)?*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Spika, Serikali tumejielekeza katika mwaka huu wa fedha angalau kukamilisha majengo ya *OPD* katika vituo hivi vya afya na yaanze kutoa huduma. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, katika mwaka huu wa fedha tutakamilisha jengo hilo la *OPD* na lianze kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Ngonyani kwa niaba yake, Mheshimiwa Ngwando.

Na. 3

Ujenzi wa Soko la Mfaranyaki Manispaa ya Songea

MHE. HAPPINESS D. NGWANDO K.n.y. MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa Soko la Mfaranyaki katika Manispaa ya Songea utaanza kwa kuwa hali iliyopo ni hatarishi kwa usalama wa watumiaji?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani, Mbunge wa Mkoa wa Ruvuma, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Soko la Mfaranyaki ni soko la muda lililotengwa pamoja na maeneo ya Mji Mwema na Bombambili, kwa ajili ya kuhifadhi wafanyabiashara waliopisha ujenzi wa Masoko ya Manzese A na B katika Manispaa ya Songea.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa masoko ya kudumu ya Manzese A na B unaendelea kwa gharama ya shilingi bilioni 23.5 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Disemba, 2026. Masoko hayo yakikamilika yatatumika kwa wafanyabiashara walioondolewa kupisha ujenzi na wafanyabiashara wengine.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mfaranyaki ni eneo la muda na halina miundombinu stahiki, wafanyabiashara wanakabiliwa na changamoto za kutokuwepo kwa jengo la wafanyabiashara, hivyo kusababisha kutiririka kwa maji, usalama mdogo, na kushindwa kudumisha ubora wa bidhaa zinazouzwa katika soko hilo.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Songea imetenga shilingi milioni 80 katika bajeti ya mwaka 2026/2027 kwa ajili ya ujenzi wa paa katika soko la Mfaranyaki wakati tukisubiri kukamilika kwa ujenzi wa masoko ya kudumu ya Manzese A na B.

SPIKA: Mheshimiwa Happiness.

MHE. HAPPINESS D. NGWANDO: Mheshimiwa Spika, maswali ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi yameshajibiwa. Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Haidary Sumry.

MHE. HAIDARY H. SUMRY: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Manispaa ya Mpanda ni miongoni mwa Manispaa ambazo zilipata mradi wa *TACTIC* na katika mradi huo tulikuwa na miradi miwili; mradi wa barabara, na mradi wa soko la kisasa pale Kazima. Mradi wa barabara tayari tulishaanza, na mradi wa soko bado haujaanza.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuiuliza Serikali, ni lini mradi wa soko la kisasa la Kazima utaanza kujengwa?

SPIKA: Watu wa Sumbawanga mkiingia humu ndani, vile vitu vyenu viacheni nyumbani huko. Maana vinaingiliana na mitambo humu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO): Mheshimiwa Spika, kama alivyotangulia kuuliza, Serikali imefanya kazi kubwa sana kupitia mradi huu wa *TACTIC*. Kwenye eneo analotoka Mheshimiwa Mbunge, zimejengwa barabara za lami karibu kilomita 13 kwa zaidi ya shilingi bilioni 23.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili itakayofuata itakuwa ni ujenzi wa soko, na tumefanya hivyo kwenye *TACTIC* awamu ya kwanza, maeneo ambayo tulianza na barabara awamu ya pili tulianza na ujenzi wa soko. Maeneo ambayo tulianza na ujenzi wa masoko awamu ya pili tulianza na ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Zainab Kawawa.

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Katika Mkoa wa Lindi, Halmashauri za Wilaya za Liwale, Nachingwea, Ruangwa, Mtama pamoja na Kilwa, hazina masoko ya kisasa. Je, ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba Halmashauri hizi zinajengwa masoko ya kisasa?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, hilo swali haliendani na swali la msingi. *Okay,* jibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO): Mheshimiwa Spika, utaratibu wa masoko ya kimkakati huwa yanaanza na andiko kutoka kwenye Halmashauri husika. Andiko hilo huwasilishwa TAMISEMI, nasi kwenye Wizara yetu hufanya mapitio

na baadaye kulipeleka kwenye Wizara ya Mipango ambao wakiridhia hulifikisha Wizara ya Fedha kwa ajili ya kupatiwa fedha na kuanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, hivyo, kwa uhitaji alioutaja Mheshimiwa Mbunge wa Mkoa wa Lindi, ninawaelekeza Wakurugenzi wa maeneo yote yaliyotajwa kuwa na ushirikiano na wawakilishi wa wananchi ili kufuata hatua hizo na hatimaye Serikali iweze kuwahudumia wananchi wa maeneo hayo.

SPIKA: Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Shangazi.

Na. 4

Kuwapatia Wananchi Sehemu ya Shamba la Miti Shume

MHE. RASHID A. SHANGAZI aliuliza: -

Je, lini ahadi ya kuwapatia maeneo wakazi wa Kata za Lukozi, Shume na Manolo kutoka Shamba la miti Shume itatekelezwa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua ahadi na maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa Wizara ya Maliasili na Utalii ya kuangalia uwezekano wa kupata ardhi kidogo kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya jamii kama ilivyoombwa na Mheshimiwa Mbunge wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais Wilayani Lushoto mwezi Februari, 2025.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilianza kufanyia kazi maelekezo hayo kwa kufanya uchambuzi wa maombi mbalimbali

yaliyowasilishwa na ofisi mbalimbali kuanzia ngazi za Vijiji, Kata na Halmashauri ya Lushoto yakiomba kumegewa maeneo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kijamii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia maombi yaliyowasilishwa, Wizara iko tayari kumega sehemu ya eneo la shamba hilo kwa ajili ya shughuli za kijamii ikiwemo ujenzi wa shule na eneo la maziko.

SPIKA: Mheshimiwa shangazi, ungekuwa una-*swipe*. Kama hamtumii hizi kadi, mashine zenu haziwezi kufanya kazi.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru kwa majibu mazuri sana ya Serikali kwamba wameridhia kutoa eneo hili kwa ajili ya shughuli za kijamii kama ambavyo amesema. Kwa hiyo, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa usikivu wake kwa sababu alivyokuja Februari mwaka 2025 tulimpa hili ombi na sasa Wizara imeridhia kugawa eneo hili. Nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, huu ni utekelezaji wa ahadi ya Rais ambayo ameitoa kwa wananchi wa Lushoto, ni kwa haraka kiasi gani maeneo haya yaliyoombwa kumegewa maeneo kutoka Shamba la Miti Shume utekelezaji utaanza?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninamshukuru Mbunge wa Mlalo, Mheshimiwa Rashid Shangazi na tumepokea shukrani kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, na kwa sababu haya ni maelekezo yake na hatua karibu zote tumeshazifanya.

Mheshimiwa Spika, ninakuthibitishia, kuanzia mwaka wa fedha unaoanza, Serikali itakuwa tayari kutoa maeneo hayo kwa ajili ya wananchi. Ahsante sana.

SPIKA: Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Enock Zadock Koola.

Na. 5

Ujenzi wa Skimu za Umwagiliaji Jimbo la Vunjo

MHE. ENOCK Z. KOOLA aliuliza :-

Je, lini Serikali itajenga skimu za umwagiliaji kwa ajili ya kilimo cha chakula katika Jimbo ya Vunjo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umwagiliaji katika Mkoa wa Kilimanjaro ikiwemo Jimbo la Vunjo. Kwa mwaka 2025/2026, miradi mitano inaendelea kutekelezwa katika Jimbo la Vunjo ikihusisha mradi wa ujenzi wa Skimu ya Mawala wenye ukubwa wa hekta 2,500 unaogharimu kiasi cha shilingi bilioni 4.1.

Mheshimiwa Spika, vilevile, miradi minne imepangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha ujao wa 2026/2027 inayojumuisha skimu nne za Mananga, Ndekambeko, Masaera na Masaga ambapo mkandarasi ameshapatikana.

SPIKA: Mheshimiwa Enock, aliyeuliza swali.

MHE. ENOCK Z. KOOLA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kazi kubwa inayofanywa na Serikali ya Mheshimiwa Rais kwenye sekta ya kilimo, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Kwa kuwa Serikali ilitangaza mpango wa kuchimba visima virefu 500 nchi nzima kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Je, Serikali inaweza kutoa taarifa kuhusu idadi ya visima vilivyopangwa kutekelezwa katika Jimbo la Vunjo ili kusaidia vijana na wanawake wanaoshughulika na kilimo cha mbogamboga?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa tayari Serikali imeanza kutekeleza ahadi ya kutoa miche mipya ya kahawa na

tulishazindua hiyo ziara kwenye Jimbo letu la Vunjo kwa wakulima wa Jimbo la Vunjo, je, Serikali ina mkakati gani wa kufufua skimu ya mifereji ya asili, ukanda wa juu itakayowawezesha wakulima kumwagilia miche hii mipya ya kahawa? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, nami ninampongeza Mheshimiwa Koola, Mbunge wa Vunjo kwa maswali yake ya msingi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha ambao tunaendeleanao, na katika bajeti ya kilimo tulikuwa tumepanga kuchimba walau visima vitano katika kila Jimbo nchini kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Wizara ya Kilimo tumesha-*hire* magari kwa ajili ya kufanya shughuli hiyo na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji pamoja na Wizara, kupitia miradi mbalimbali tuliyonayo pale, wanaendelea na shughuli hiyo.

Mheshimiwa Spika, namhakikishia tu kwamba tayari Wizara ya Kilimo tumeshapokea magari kwa ajili ya kufanya shughuli hiyo. Tume ya Taifa ya Umwagiliaji pamoja na Wizara kupitia miradi mbalimbali tuliyonayo pale, wanaendelea na shughuli hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kufufua skimu za asili kwa ajili ya kumwagilia kahawa, hilo ndilo jukumu letu. Tunaendelea kuzifufua zile za asili pamoja na kuzikarabati zilizopo ili kuhakikisha kuwa wananchi wa Vunjo na maeneo mengine nchini wananufaika na Wizara ya Kilimo ambayo ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Saashisha.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali ilifanya *feasibility study* ya skimu kubwa za Wilaya ya Hai Metrom, Bolutu, Makeresho, Kikafu Chini na Longoi. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa skimu hizi pamoja na zile skimu ndogo, kwa maana ya mifereji?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge wa Hai *Comrade* Saashisha, kwamba tukishamaliza hatua ya usanifu, ambapo katika baadhi ya maeneo ambayo ameyataja hapa yakiwemo Mbokomu pamoja na Makeresho, tumeshakamilisha. Hatua inayofuata sasa hivi ni kutangaza kwa ajili ya kupata mkandarasi, na baada ya hapo mkandarasi akabidhiwe *site* na kuanza kazi ya ujenzi wa mabwawa pamoja na skimu katika maeneo hayo.

SPIKA: Mheshimiwa Subira.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Serikali iliwaahidi wakulima wadogo wadogo wa kilimo cha miwa katika eneo la Bagamoyo kwa ajili ya Kiwanda cha Sukari cha Bakhresa, na kwa kuwa kuna changamoto ya upatikanaji wa maji, je, Serikali ule mpango wake wa ujenzi wa bwawa la umwagiliaji kwa ajili ya kuwasaidia wakulima hawa na kiwanda cha sukari Bagamoyo unaendeleje?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Niungane na Mheshimiwa Mbunge wa Bagamoyo, Mheshimiwa Subira Mgalu kumhakikishia tu kwamba mpango wa Serikali unaendelea, na tupo katika hatua za mwisho za usanifu wa mradi ule. Mara baada ya kukamilika, tutaingia katika hatua inayofuata ya kutangaza na kupata mkandarasi kwa ajili ya kusaidia wananchi wa maeneo hayo.

SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Nape.

Na. 6

Mfumo wa Upatikanaji wa Bei kwenye Minada ya Korosho

MHE. NAPE M. NNAUYE aliuliza: -

Je, Serikali ipo tayari kupitia upya mfumo wa bei kwenye minada ya korosho kwa kuwa kuna malalamiko ya namna bei zinavyopatikana?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, ninaomba kujibu Swali la Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge wa Mtama, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo kupitia Bodi ya Korosho Tanzania imeendelea kushirikiana na wadau kuendesha minada kwa njia ya kidijiti kupitia Soko la Bidhaa Tanzania *(TMX)* kwa lengo la kuongeza uwazi, ushindani na kuimarisha bei ya mkulima. Hatua hiyo imesaidia uwazi na upatikanaji wa bei shindani kwa wakulima kulingana na upatikanaji na mahitaji ya korosho kwa wakati husika.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2025/2026, korosho za Tanzania ziliuzwa kwa wastani wa shilingi 2,550 kwa kilo, ikilinganishwa na wastani wa shilingi 1,750 kwa kilo katika nchi za Msumbiji, *Ivory Coast,* Ghana, Nigeria na Benin. Hali hiyo inadhihirisha kuwa Mfumo wa *TMX* una mchango mkubwa katika upatikanaji wa bei shindani kwa wakulima kulingana na hali ya Soko la Dunia.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali ipo tayari kupokea maoni na ushauri ili kufanya maboresho zaidi pale inapobidi ili kuendelea kuimarisha mfumo wa uuzaji wa korosho kwa manufaa ya wakulima.

SPIKA: Mheshimiwa Nape.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninaomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa kwa mfumo tulionao sasa hivi, katika msimu mmoja wa korosho kuna uwezekano wa bei ikapishana sana, wakati mwingine kutoka

shilingi 4,000 kwenda mpaka shilingi 2,000. Hili *gap* ni kubwa sana katika msimu mmoja wa uuzaji wa korosho.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali iko tayari kushirikiana na wadau kwenda kupitia upya mfumo huu ili kupunguza *gap* hili tuwape wakulima wetu faida wanayostahili kuipata?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwenye maghala haya ambayo yanahifadhi korosho, katika wakati mmoja ghala moja linachukua korosho za wakulima wengi; na wakati tunakwenda mnadani, wanaokuja kununua wakati mwingine wanakuja wananunua korosho kidogo kidogo na kwa bei tofauti tofauti, jambo ambalo linapelekea sintofahamu korosho ya nani inakwenda kwa bei gani, kutoka kwenye ghala moja la wauzaji wa korosho.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali iko tayari tuupitie upya mfumo huu ili tuwatendee haki wakulima kwa kuongeza uwazi, na kuhakikisha kuwa wakulima wetu wanatendewa haki kwenye bei na uuzaji wa korosho yao?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninamshukuru Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge wa Mtama kwa maswali ya msingi hususan kwenye tasnia ya korosho.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la kwanza, jambo moja ambalo ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, sisi kama Serikali tupo tayari kushirikiana na wadau kukutana pamoja na kuhakikisha kwamba tunaangalia huu mfumo kutoka eneo moja mpaka lingine ili kuhakikisha kwamba mfumo huu unanufaisha wakulima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tofauti ya bei hususan katika maeneo ya maghala, na lenyewe namthibitishia tu Mheshimiwa Mbunge, hatutakubali kwenda katika mfumo ujao bila kukaa pamoja na wadau na kupitia upya ili kuhakikisha wakulima ndio wanakuwa wanufaika wakubwa. Kwa hiyo, ninamthibitishia tu, kwamba Serikali tuko tayari na tutalifanya hivyo.

SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela.

Na. 7

Matumizi ya *Export Levy* ya Korosho

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA aliuliza: -

Je, tangu kurejeshwa kwa *Export Levy* kwenda Bodi ya Korosho Tanzania ni kiasi gani kimekusanywa hadi sasa na kimetumikaje?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2024/2025 hadi Februari, 2026 Bodi ya Korosho Tanzania imepokea fedha za *Export Levy* jumla ya shilingi bilioni 350.63. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 183.58 zilipokelewa mwaka wa fedha 2024/2025 na shilingi bilioni 167.06 zimepokelewa mwaka 2025/2026 kufikia Februari, 2026.

Mheshimiwa Spika, kati ya jumla ya fedha hizo zilizopokelewa, ni kiasi cha shilingi bilioni 339.17 kimetumika kulipa madeni ya wazabuni wa pembejeo za korosho zilizotolewa kwa wakulima kwa ruzuku ya 100%, na shilingi bilioni 11.46 zimetumika kugharamia miradi ya maendeleo katika tasnia ya korosho.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali kupitia Bodi ya Korosho Tanzania itaendelea kulipa madai ya wazabuni na kulipia gharama za pembejeo kwa wakulima.

SPIKA: Mheshimiwa Mchungahela.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Spika, ninaomba niseme kwamba majibu yaliyojibiwa yamekuwa *too general,* na hizi fedha ni za wakulima, bila shaka wangetamani kufahamu kinagaubaga jinsi fedha zao zinavyotumika baada ya kukatwa.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna majibu ya kusema kwamba wamepewa wazabuni, wamelipiwa wazabuni, lakini wazabuni hao ni wapi? Halikadhalika, zimelipwa kwa ajili ya maendeleo. Je, miradi hii ya maendeleo ni ipi, kwa sababu swali linaonekana limeulizwa vizuri, lakini majibu yamefungwafungwa. Bado tunahitaji kufahamu, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimshukuru Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi kwa maswali yake ya msingi. Sisi kama Wizara kupitia Bodi ya Korosho tuko tayari kumpatia orodha ya wazabuni wote waliolipwa pamoja na miradi ya maendeleo ambayo inatekelezwa kupitia fedha hizi za *Export Levy* ambazo Bodi imepokea. Kwa hiyo, kwa sababu ni orodha kubwa, tutampatia.

SPIKA: Haya Mheshimiwa Mchungahela utaonana na Mheshimiwa Waziri baadaye.

Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu aulize swali lake.

Na. 8

Ujenzi wa Chuo cha Maji Singida

MHE. YAGI M. KIARATU aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Chuo cha Maji katika Mkoa wa Singida?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu, Mbunge wa Jimbo la Singida Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maji ni Wakala wa Serikali ulio chini ya Wizara ya Maji ulioanzishwa Mwaka 1974 kwa lengo la kuzalisha wataalam wa maji pamoja na sekta nyingine zikiwemo umwagiliaji na ujenzi. Pamoja na majukumu mengine, chuo hicho kinatoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi ya kozi zipatazo 25 kwa ngazi ya Stashahada, Shahada ya kwanza na Shahada ya Uzamili kupitia Kampasi zake za Dar es Salaam na Singida.

Mheshimiwa Spika, Makao Makuu ya Chuo cha Maji yapo Jijini Dar es Salaam na hutumia majengo yaliyopo Ubungo kwa ajili ya shughuli za kitaaluma. Upande wa Kampasi ya Singida, Chuo cha Maji kinatumia Majengo ya Bodi ya Maji ya Bonde la Kati Singida kutolea mafunzo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imepanga kuanza kwa awamu ujenzi wa majengo ya chuo kwa Kampasi ya Singida katika eneo lenye ukubwa wa ekari 41.5 lililopo katika Mtaa wa Mwankoko Manispaa ya Singida ili kurahisisha na kuongeza ufanisi katika utoaji wa mafunzo.

SPIKA: Mheshimiwa Yagi.

MHE. YAGI M. KIARATU: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninapenda tu kumkumbusha kwamba chuo hicho cha Singida kimeanza muda mfupi uliopita kikiwa na wanafunzi 39, lakini hadi leo tunapoongea wapo wanafunzi 450, mwitikio ni mkubwa.

Mheshimiwa Spika, chuo kina ekari 41 kama alivyosema, lakini tayari wamefanya usanifu. Kinachosumbua sasa ni gharama kubwa za uendeshaji. Pale ukumbi wa Bonde wameshahama, wamepanga eneo ambalo wanalipa shilingi 150,000,000 kwa mwaka.

Myheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko la wanafunzi, chuo pia kimeongeza *program* za mafunzo kutoka programu mbili hadi nane. Mpaka ikifika Oktoba mwaka huu chuo kinakusudia kupokea wanafunzi 1,500. Kwa maana hiyo, eneo lile walilopo sasa halitatosha, lakini pia gharama za uendeshaji zitaendelea kuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba *commitment* ya Serikali, chuo hicho ni kikubwa na bado wanafunzi wanapata shida kupata masomo hayo, na ukizingatia chuo hicho sasa kinatoa mafunzo yanayofundishwa na *VETA,* kwa hiyo, idadi ya wanafunzi itaendelea kuwa kubwa. Naomba majibu mazuri ya Serikali.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninamshukuru sana Mheshimiwa Yagi kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya. Kikubwa zaidi, kwa muda mfupi kabisa ameelewa kazi kubwa inayofanywa na vyuo vyetu vya maji hususan katika hiki Chuo cha Maji Singida. Kiuhalisia, alichokiongea Mheshimiwa Mbunge ni ukweli kabisa kwamba tulianza na wanafunzi wachache, na sasa wanafunzi wamezidi kuongezeka. Hii maana yake ni kwamba, imani ya Watanzania katika chuo hiki imezidi kuwa kubwa na uhitaji wa majengo umekuwa mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana Serikali kupitia Wizara ya Maji, tumeamua kuweka kwenye Mpango na kwenye bajeti ya mwaka 2026/2027 ili kuhakikisha sasa tunaanza ujenzi ili kuweza ku-*accommodate* wanafunzi ambao watakuwa wanadahiliwa katika chuo hiki ili kuepusha chuo kuingia kwenye gharama za kupanga majengo ambayo yatasababisha hasara, badala ya kujikita katika kuboresha huduma ya utoaji wa mafunzo.

Mheshimiwa Spika, Serikali tumepokea na ninakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

Na. 9

Uhitaji wa Maji Salama Kata ya Mpinji Same Mashariki

MHE. ANNE K. MALECELA aliuliza: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka Mradi wa Majisafi Kata ya Mpinji kwa Vijiji vyote vinne?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba vijiji vyote 12,333 vilivyopo nchini vinafikiwa na huduma ya majisafi na salama kufikia mwaka 2030. Aidha, hadi sasa jumla ya vijiji 10,758 vimeshafikishiwa huduma ya majisafi na salama kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini *(RUWASA)*.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufikisha huduma ya maji katika vijiji 1,575 vilivyobaki, ikiwemo vijiji vinne vya Mpinji, Sambweni, Kirongwe na Ivuga vilivyopo Kata ya Mpinji Wilaya ya Same Mkoani Kilimanjaro.

SPIKA: Mheshimiwa Anne Kilango.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Spika, Kata hii ya Mpinji ina wananchi takribani 10,999, kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2022. Ukizunguka vijiji vyote vinne hutakutana na bomba la maji salama hata moja. Je, Serikali haioni kwamba wananchi hawa 10,999 wanaishi maisha hatarishi, wakalichukua suala hili la maji Kata ya Mpinji kwamba ni suala la dharura sana?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, na nimshukuru sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Kwanza kabisa nampongeza, wakati anaingia katika Jimbo la Same Mashariki, huduma ya maji ilikuwa mbaya sana. Mpaka sasa tunapoongelea kati ya vijiji vile 1,575, na vijiji vyake ambavyo ni vinne lakini kuna kata nyingine pia ambapo ndiyo wamebaki kuwa wana changamoto ya maji.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunalichukua kwa uzito stahiki ili eneo hili kwa ajili ya wananchi wa Kata ya Mpinji waweze kupata huduma ya majisafi na salama kulingana na mahitaji ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyasema.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuwekeza vizuri kuhakikisha vijiji vyote 1,575 vinapata huduma ya majisafi na salama ili kukamilisha vijiji 12,333 nchi nzima ambavyo wananchi ndiyo wanaishi katika maeneo hayo na wanahitaji upatikanaji wa majisafi na salama.

SPIKA: Mheshimiwa Waitara.

Mheshimiwa Waitara hiyo kadi yako unatakiwa ui-s*wipe* hapo.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, ipo *on* hapa.

SPIKA: Unaona sasa, haya siyo mambo ya Musoma bwana.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, haya, sawa Mheshimiwa Mbunge wa Ilala. Ninakushukuru kwa nafasi. Naomba kujua, mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria una gharama ya shilingi bilioni 134, ni mkubwa; na nimeomba mara kadhaa kwenye Bunge hili kwamba matoleo ya tenki la maji Sirari, Mogabiri na Komaswa yawekwe.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kama Serikali ipo tayari kunipa majibu kwa maandishi kuhusu *commitment* hiyo, kwa sababu maelezo ambayo waliniambia kule Tarime ni tofauti kabisa na maelezo ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri wamenijibu huku Bungeni. Je, wanaweza wakanipa hayo majibu

ya maeneo hayo matatu matoleo ya mradi ule kwenye jimbo langu kwa maandishi?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa swali hili kwanza alishaliuliza Mheshimiwa Waitara na alishatoa ushauri na Seriklai tulipokea ushauri na tulituma wataalam wetu walikwenda kufanyia kazi kulingana na yale matoleo ambapo alikuwa anahitaji ishuke kwa wananchi ambao walikuwa wanayahitaji.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Serikali inaendelea kulifanyia kazi. Hivyo, nimwombe awe na subira kidogo ili Serikali ihakikishe kwamba utaalam umezingatiwa katika kuhakikisha kwamba maji yanapokwenda kutolewa kwa ajili ya vile vijiji, basi kusiwe na madhara yoyote.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali iko tayari kutoa *commitment* kwa maandishi ili kuhakikisha kwamba wananchi wake wa Jimbo la Tarime wawe na uhakika wa upatikanaji wa maji kutokana na miundombinu ambayo tayari imeshajengwa. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Kabati.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini wananchi wa Kata ya Ng'ang'ange mkandarasi atapatiwa fedha ili ule mradi uweze kukamilika kwa sababu ule mradi umesubiriwa kwa muda mrefu sana na pale hakuna kisima chochote, wananchi wanapata mateso hakuna majisafi na salama?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, mradi huu bahati nzuri ninaufahamu na nilifika pale kwa ajili ya uzinduzi wake. Nimhakikishie katika Mradi huu wa Ng'ang'ange, mkandarasi tayari yuko *site* na tayari anaufanyia kazi na tuko kwenye ujenzi wa tenki. Kikubwa tu ni kwamba tunafahamu mkandarasi alikuwa amewasilisha hati za madai, na tayari Serikali inafanyia kazi hati

yake ya madai yaweze kulipwa na kuharakisha ukamilishaji wa mradi huu ili wananchi wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati wapate huduma ya maji safi na salama. Ninakushukuru sana.

SPIKA: Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Mheshimiwa Matiko.

Na. 10

Ujenzi wa Kiwanda cha Kimkakati – Tarime

MHE. ESTHER N. MATIKO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kiwanda cha kimkakati ndani ya Mji wa Tarime?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Viwanda na Biashara naomba nijibu swali namba 10 la Mheshimiwa Esther Matiko.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunafanya kazi, na tumeandaa mpango wa ujenzi wa Viwanda nchini katika kuongeza thamani ya bidhaa zetu ikiwemo Mji wa Tarime ambapo itazingatia uongezaji wa thamani katika mazao ya kilimo, mifugo na madini ambayo yanapatikana huko.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji wa ndani na nje katika ujenzi wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa vyenye mkakati kupitia Taasisi za *TISEZA* na *SIDO*. Wakati huo huo tunahamasisha balozi zetu, wadau mbalimbali na wananchi wote wa Tanzania kwa pamoja kutangaza rasilimali na vivutio ambavyo vipo katika Mji wa Tarime na Mkoa wa Mara kwa ujumla ili hamasa hiyo iende sambamba na kutoa vivutio vya kikodi na visivyo kikodi ambavyo vinaendelea kutolewa chini ya Taasisi ya *TISEZA*.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, kufuatia majibu ya Serikali, kwanza kabisa ningependa kusema wazi wawekezaji wengi hasa wale wakubwa wanapenda kuwekeza Mkoa wa Pwani, labda kwa sababu kupo karibu na Dar es Salaam. Huku pembezoni na kama ilivyo Mji wa Tarime, siyo rahisi sana kuweza kuvutia wawekezaji wakubwa kuja kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru Serikali imekiri kwamba kwa jiografia ya Mji wa Tarime, tuna upatikanaji mkubwa wa malighafi za kilimo, mifugo pamoja na madini. Pia, Mji wetu wa Tarime uko mpakani, na hivyo kuifanya Tarime Mji kuwa kituo kizuri tu cha kiwanda cha kuzalisha thamani.

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa kujua kwa kuwa hasa bidhaa za ujenzi ni ghali sana kwa kule kwetu Mkoa wa Mara, na asilimia kubwa inatoa Kenya, Serikali haioni kwamba ni wakati mwafaka kuhakikisha kwamba inavutia wawekezaji wakubwa wa vifaa vya ujenzi kama uzalishaji wa mabati, nondo, vifaa vya maji ili waje kuwekeza kule ili kupunguza watu kwenda Kenya au kupata bidhaa Tanzania kwa gharama kubwa zaidi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa malighafi za kilimo zinapatikana, na pia tungependa kupata mwekezaji mkubwa ambaye anaweza kuchakata na kuwa na Kiwanda cha Biskuti kwa sababu tuna viazi vingi sana vinasafirishwa kuja huko mikoani au *crips* ambazo zinatokana na ndizi. Serikali haioni pia kuna haja sasa ya kumleta mwekezaji huyu mkubwa kuacha wale wadogo ambao umeeleza kwenye jibu lako la msingi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, kwanza nikiri maelezo ya Mheshimiwa Mbunge. Tarime ni Wilaya ya kimkakati na hasa tunapozungumzia Jumuiya ya Afrika Mashariki iko mpakani na iko

kimkakati, na ndio maana mkakati ambao tunao sasa hivi ni kuimarisha biashara katika mtengamano huu wa Jumuiya ya Afrika Mashiriki na kutumia Tarime na mikoa ya mipakani kama maeneo ya kimkakati wa Tanzania ku-*access* masoko katika Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana Serikali inatoa rai kwamba tunatangaza vivutio ambavyo ni vya kikodi na visivyo vya kikodi hususan kwenye miradi ya kimkakati ambayo inaweza kuwekezwa katika maeneo maalum ya kiuchumi na hii ikiwemo misamaha na nafuu ya kikodi ili kuhamasisha wawekezaji kwenda nje ya maeneo ambayo tumeyazoea hasa katika mikoa ya Pwani ili ku-*access* soko kubwa zaidi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwemo Tarime ambalo ni eneo la kimkakati ku-*access* masoko hayo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kuhusiana na suala la kutafuta wawekezaji wakubwa. Kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Dira ya 2020-2050, lengo letu ni kuongeza thamani ya mazao, thamani ya madini yetu ambayo tunazalisha nchini, viwanda vya kimkakati ambavyo vinatoa ajira na kutuhakikishia pia uwepo wetu katika Jumuiya na ku-*access* masoko ya *SADC* pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Waziri unisaidie. Dira ya Taifa imeshatoka 2050, ninyi bado hamna mkakati Mkoa wa Mara, lakini mwekezaji tayari ana mkakati, lakini bado mnamzuia kwa sababu ninyi hamjajiandaa na mkakati na dira imeshatoka. Hebu nendeni mkajipange vizuri huko kwenu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, tumepokea. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yameisha.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni viongozi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Wakuu wa Taasisi na Viongozi wa Dini.

Yupo Dkt. Jim James Yonazi - Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu; Ndugu Mary Maganga ambaye ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu; Dkt. James Kilabuko, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu; na Ndugu Adolf Ndunguru, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Wengine ni Mhandisi Rogatius Mativila, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Miundombinu); Ndugu Sospeter Mtwale, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Profesa Tumaini Nagu, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Afya); na Ndugu Atupele Mwambene, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Elimu). *(Makofi)*

Vilevile yupo Ndugu Ramadhani Kailima, Mkurugenzi wa Tume Huru ya Uchaguzi; Askofu Filbert Mwanga, Askofu Mkuu wa Kanisa la *SDA*; Dkt. Vernon Fernandez, Kanisa la Agape Tanzania; Maulana Sheikh Hemed Jalala, Jumuiya ya *SHIA Tanzania*; Sheikh Dkt. Alhad Mussa, Mwenyekiti, Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania; Mheshimiwa Martha Mlata, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida na Ndugu Neema Mwigulu, Mke wa Mheshimiwa Waziri Mkuu.*(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wakuu wa Mikoa, Mheshimiwa Amos Makalla - Arusha; Mheshimiwa Rosemary Senyamule - Dodoma; Mheshimiwa Albert Chalamila - Dar es Salaam; Mheshimiwa Martin Shigella - Geita; Mheshimiwa Kheri James - Iringa; Mheshimiwa Kanali Yahya Kido - Kagera; Mheshimiwa Mwanamvua Mrindoko - Katavi; Mheshimiwa Balozi Simon Sirro - Kigoma; na Mheshimiwa Nurdin Babu, Kilimanjaro. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Zainab Telack - Lindi; Mheshimiwa Queen Sendiga - Manyara; Mheshimiwa Kanali Evans Mtambi - Mara; Mheshimiwa Beno Malisa - Mbeya; Mheshimiwa Adam Kighoma Malima - Morogoro; Mheshimiwa Kanali Donald Msengi - Mtwara; Mheshimiwa Anthony Mtaka - Njombe; Mheshimiwa

Abubakar Kunenge - Pwani; na Mheshimiwa Brigedia Jenerali Ahmed Abas – Ruvuma. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mboni Mhita - Shinyanga; Mheshimiwa Anamringi Macha - Simiyu; Mheshimiwa Halima Dendego - Singida; Mheshimiwa Jabir Makame - Songwe; Mheshimiwa Paul Chacha - Tabora; na Mheshimiwa Balozi Dkt. Batilda Buriani - Tanga; *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Wawakilishi wa Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Viongozi kutoka Mikoa na Wilaya za Singida pamoja na Wakurugenzi na Watendaji. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni 10 wa Mheshimiwa Deo Sangu - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano ambao ni viongozi kutoka Taasisi na Vyama vya Wafanyakazi Nchini. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Kaspar Kaspar Mmuya - Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni walimu kutoka Halmashauri ya Ruangwa, Mkoani Lindi. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Mariam Said Khamis ambao ni familia yake kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Wapo wageni 10 wa Mheshimiwa Dkt. Lazaro Killian Komba ambao ni familia yake na viongozi wa CCM kutoka Peramiho, Mkoani Ruvuma. *(Makofi)*

Wengine ni wageni watano wa Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe ambao ni wananchi wao kutoka Wilaya ya Mpanda, Mkoani Katavi. *(Makofi)*

Wageni 35 wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ambao ni viongozi na makada wa CCM kutoka Mkoani Songwe. *(Makofi)*

Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD - KATIBU WA BUNGE:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Mapitio ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2025/2026, na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, aidha, kutokana na taarifa zilizowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii; na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambazo zilichambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge, sasa ninaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zilizopo chini yake na Mfuko wa Bunge kwa Mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya njema iliyotuwezesha kukutana mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha na kupokea Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa kipindi cha Mwaka 2025/2026 na mwelekeo wake kwa Mwaka 2026/2027. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nitumie fursa hii kuwapongeza Waislamu wote Tanzania kwa kumaliza salama mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na kusherehekea Sikukuu ya *Eid al Fitr* kwa amani na utulivu. Vilevile, niwatakie kila la heri Wakristo wote

walio katika Mfungo wa Kwaresma na kuwatakia maandalizi mema ya Sikukuu ya Pasaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 25 Machi, 2026 tuliondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, mwanasiasa mahiri aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) na Mbunge wa Jimbo la Isimani.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, nitoe pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondokewa na Waziri mahiri na mchapakazi katika Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nitoe pole kwako, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, familia, ndugu, jamaa, marafiki, wafanyakazi, wananchi wa Jimbo la Isimani na Watanzania wote kwa ujumla kutokana na msiba huo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uhai wake Mheshimiwa Lukuvi alihudumu katika nafasi mbalimbali. Baadhi ya nafasi hizo ni Naibu Katibu Mkuu wa UVCCM Taifa, Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa, Mkuu wa Wilaya ya Bukoba na Mkuu wa Mkoa katika Mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma. Vilevile, alikuwa Waziri katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utendaji kazi wake mahiri na uzoefu katika masuala ya siasa pamoja na ushawishi mkubwa aliokuwanao, mnamo tarehe 13 Juni, 2023 Mheshimiwa Rais alimteua kuwa Mshauri wake wa Siasa na Uhusiano wa Jamii. Vilevile, Mheshimiwa Lukuvi aliwahi kuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa vipindi tofauti kati ya mwaka 2010 – 2015, 2021 – 2022 na mwaka 2024 hadi umauti ulipomfika akiwa *Chief Whip*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lukuvi pia alikuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani kwa kipindi cha miaka 31 hadi umauti ulipomfika. Mheshimiwa Lukuvi atakumbukwa kwa uongozi na uthubutu wake katika uratibu wa shughuli za Serikali pamoja na

ushawishi mkubwa wa kisiasa katika nchi yetu. Tunamwomba Mungu aendelee kumpa marehemu pumziko la amani. Amina.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ninatoa pole kwa kifo cha Mheshimiwa Halima Idd Nassor Mbunge wa Viti Maalum (Wafanyakazi), kilichotokea tarehe 18 Januari, 2026 Jijini Dar es Salaam. Tutaendelea kumkumbuka kwa mchango wake na utumishi uliotukuka ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 3 Februari, 2026 tulipokea kwa masikitiko kama Taifa kufuatia taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Munde Tambwe aliyekuwa Mbunge Mstaafu Viti Maalumu (Mkoa wa Tabora). Vilevile, aliwahi kuhudumu katika nyadhifa mbalimbali ndani ya Chama cha Mapinduzi ikiwemo Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM na Mjumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uhai wake, aliwatumikia wananchi wa Tabora na Watanzania kwa ujumla kwa ari na uzalendo wa hali ya juu. Ninatoa pole kwa wananchi wa Mkoa wa Tabora, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa msiba huo.

Mheshimiwa Spika, kadhalika tarehe 30 Machi, 2026 tulipokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Seleman Said Bungala aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kusini kupitia Chama cha *ACT Wazalendo* kuanzia mwaka 2010 hadi 2020.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bungala almaarufu Bwege. Atakumbukwa kwa ujasiri, uwezo wake wa kuwasilisha hoja, ucheshi pamoja na kauli zake za kusisimua zilizompatia umaarufu ndani na nje ya Taifa letu. Ninatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki, wananchi wa Kilwa na Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, vilevile, tarehe 19 Februari, 2026 tuliondokewa na Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Muadhama Polycarp Kardinali Pengo. Kwa moyo wa simanzi na huzuni kubwa ninatoa pole kwa Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Baraza la Maaskofu Katoliki

Tanzania, waumini wa Kanisa Katoliki pamoja na ndugu jamaa na marafiki.

Mheshimiwa Spika, Marehemu Kardinali Pengo atakumbukwa kwa mchango mkubwa alioutoa katika huduma za kiroho na kuiunganisha jamii. Wakati wa uhai wake, alisisitiza watu wote waishi maisha ya uadilifu, upendo, umoja na mshikamano wa Kitaifa. Tutaendelea kuenzi mchango wake katika kuwaletea maendeleo Watanzania katika nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 20 Machi, 2026 tulipokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Julie Catherine Manning aliyekuwa mwanamke wa kwanza Tanzania kusoma Shahada ya Sheria na kuweka rekodi ya kushika wadhifa wa Jaji wa Mahakama Kuu katika Afrika Mashariki na Kati. Pamoja na wadhifa wake huo, Mheshimiwa Julie Catherine Manning aliwahi kuhudumu nafasi ya Waziri wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuungana na Mheshimiwa Rais kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki, wadau wote wa sheria pamoja na Watanzania wote. Mheshimiwa Julie Catherine Manning, atakumbukwa kwa alama kubwa aliyoiweka katika kuwainua wanawake na kuchagiza maendeleo ya sekta ya sheria na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, tarehe 17 Februari, 2026, nchi pia ilimpoteza Mwanamuziki Mkongwe Mzee Steven Hiza ambaye ni mtunzi na mwimbaji wa wimbo maarufu uitwao "Tanzania Yetu ni Nchi ya Furaha." Sina shaka mtakubaliana nami kuwa wimbo huo umekuwa ukichochea uzalendo na umoja wa Watanzania kwa miaka mingi tangu ulipotungwa kati ya mwaka 1966 na 1967.

Mheshimiwa Spika, ninatoa pole kwa familia, wapenzi wa muziki na Watanzania wote kwa ujumla. Mzee Hiza atakumbukwa kwa uzalendo wake alioudhihirisha kwa kutunga wimbo huo ambao ubora wake hata sasa haujachuja katika historia ya muziki wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha hivi karibuni, wapo Watanzania wenzetu waliopatwa na maafa katika mikoa mbalimbali. Baadhi ya Mikoa hiyo ni pamoja na Mbeya, Iringa, Morogoro, Shinyanga, Mwanza, Lindi, Arusha, Manyara, Dodoma, Pwani, Ruvuma, Kigoma, Tanga, Dar es Saalam, Kilimanjaro na Singida.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania wote waliopoteza ndugu zao, ndugu, jamaa, marafiki na mali zao kutokana na maafa hayo. Nitumie Bunge lako Tukufu kutoa rai kwa Watanzania wote kuzingatia kwamba maji ni hatari hata pale tunapoona maji ni machache, tusijaribu kupita kwa sababu wingi wake unaweza ukabadilika ghafla na ukasababisha maafa yanayoweza kuepukika.

Mheshimiwa Spika, sambamba na maafa yanayotokana na mafuriko, katika kipindi hiki wapo Watanzania wenzetu waliopatwa na ajali mbalimbali. Nitumie nafasi hii kutoa salamu za pole kwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma na wananchi wote walioguswa na ajali ya Boti iliyotokea tarehe 13 Machi, 2026.

Mheshimiwa Spika, ninatoa pole kwa waathirika wote wa ajali ya Boti ya Nungwi pamoja na wote waliopata ajali mbalimbali zikiwemo za magari, pikipiki na vifaa vingine vya moto. Tunawaombea majeruhi wote uponyaji wa haraka na marehemu wetu wapumzike kwa amani.

Mheshimiwa Spika, tukihamia upande wa utekelezaji wa shughuli za Serikali nitumie fursa hii adhimu kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na juhudi zake za kuwatumikia wananchi wa Tanzania kwa mapenzi ya dhati.

Mheshimiwa Spika, sote ni mashahidi kwamba kazi kubwa ameifanya, na kazi hiyo imeleta maendeleo makubwa katika maeneo yetu na kuonesha dira na mwelekeo wa Taifa hususan katika kuitekeleza falsafa yake ya "Kazi na Utu, Tunasonga Mbele."

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu pamoja na wananchi wote kuendelea kumwombea kwa Mwenyezi Mungu Rais wetu, Mungu aendelee kumpa afya njema, nguvu, ulinzi na kila lililo la heri katika kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina shaka nyote mtakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa ya kusimamia na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mitano wa Mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

Mheshimiwa Spika, kupitia usimamizi wa utekelezaji wa mipango hiyo, mafanikio makubwa yamepatikana kama yaliyoelezewa kupitia Bunge la Kumi na Mbili, Mkutano wa Kumi na Tisa, kikao cha pili, Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi uliofanyika Mei, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo makubwa, wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi mbalimbali kwa lengo la kuleta maendeleo na kukuza ustawi wa wananchi. Baadhi ya ahadi zilizotolewa ni pamoja na zile zilizoelekezwa kutekelezwa ndani ya siku 100 baada ya kuchaguliwa na kuingia madarakani.

Mheshimiwa Spika, aidha, ahadi hizo zililenga kuimarisha utoaji wa huduma za afya, elimu, maji; kuimarisha sekta isiyo rasmi; na kuwezesha upatikanaji wa mitaji ya biashara ndogo ndogo za kati na uendeshaji wa kampuni changa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika Bunge la Kumi na Tatu, Mkutano wa Pili, ahadi hizo zimetekelezwa kwa mafanikio makubwa kupitia Sera, Mipango na Mikakati mbalimbali ya Kitaifa pamoja na usimamizi madhubuti. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuanza utekelezaji wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote Awamu ya Kwanza kwa wananchi 1,457,602 na kaya 276,004 zisizo na uwezo. Vilevile, kuanza

kugharimia magonjwa sugu, yaani Saratani, Figo, Moyo, Kisukari na Mifupa kwa watu wasio na uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakubaliana nami kwamba haya ni magonjwa ambayo yalikuwa yanasababisha shida kubwa kwa wananchi wasio na uwezo, kushindwa kukabilianayo. Pia kuondoa zuio la kuchukua miili ya marehemu katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya kote nchini kwa kigezo cha kutokulipa gharama za matibabu, ni moja ya jambo ambalo limetekelezwa ndani ya siku mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu, Mpango Mkakati wa Kisayansi wa Kujenga Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa Watoto wa Elimu ya Awali na Wanafunzi wa Darasa la Kwanza na la Pili ulizinduliwa na Mheshimiwa Rais tarehe 29 Januari, 2026. Mpango huo wenye kaulimbiu ya 'Mtoto Asome, Aandike na Ahesabu Bila Shida' unalenga kuongeza ubora wa elimu ya msingi na mbinu bora za ufundishaji.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni pamoja na kuzinduliwa kwa Mpango wa Kitaifa wa Pamoja Kati ya Waajiri, Vyuo vya Ufundi Stadi na Vyuo Vikuu. Mpango huo ulizinduliwa tarehe 9 Februari, 2026 na Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na unalenga kujenga uwezo na ubunifu wa ujasiriamali kwa wanafunzi na kuwawezesha kujiajiri ama kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya maji, Serikali inaendelea na kutekeleza miradi 10 yenye thamani ya shilingi trilioni 1.58. Miradi hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Gridi ya Taifa ya Maji ya kusambaza maji kutoka Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa pamoja na mito mikubwa kwenda kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana ni kutoa ajira na kuwapangia vituo watumishi 12,000 ambao kati ya hao, 5,000 ni wa sekta ya afya na 7,000 ni wa sekta ya elimu. Watumishi hao wameongeza ufanisi wa utoaji huduma katika sekta za afya pamoja na elimu.

Mheshimiwa Spika, katika kuweka mazingira wezeshi kwa vijana kujiajiri, tarehe 5 Februari, 2026 Serikali ilitoa shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kundi hilo. Fedha hizo zitaongeza uzalishaji wa ajira katika sekta mbalimbali ikiwemo kilimo, mifugo na uvuvi, viwanda na biashara, mawasiliano pamoja na maeneo mengine ambayo vijana wetu wanafanya shughuli katika kuhangaika kukuza uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo ni baadhi tu ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika siku 100 za utawala wa Serikali ya Awamu ya Sita kipindi cha pili chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wahenga walisema "mwenye macho haambiwi tazama." Mafanikio hayo ni ishara tosha ya misingi imara aliyoiweka Mheshimiwa Rais ya utekelezaji wa Dira 2050 katika kipindi cha miaka mitano ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo ya utekelezaji wa ahadi za siku 100 yaliyoelezewa, mafanikio mengine yamepatikana katika sekta mbalimbali yataendelea kuelezewa kwa kina tutakapokuwa tunawasilisha Bajeti za Wizara ya Kisekta. Leo nitagusa katika baadhi ya maeneo tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ya uchumi hapa nchini, uchumi umeendelea kukua kwa kasi ambapo katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2025, pato halisi la Taifa limekua kwa asilimia sita nukta sifuri ikilinganishwa na asilimia tano nukta tano.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa tulipopata UVIKO-19, pato la Taifa lilishuka chini ya asilimia nne nukta saba. Miaka michache baadaye tumesharudi kwenye asilimia sita na tunaendelea kupanda kukiwa na matarajio makubwa zaidi. Ukuaji huo umechangiwa na uwekezaji mkubwa katika miradi ya kimkakati ya miundombinu ikiwepo nishati, mawasiliano, usafiri na usafirishaji, huduma za kijamii na kuimarika kwa shughuli za uzalishaji katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi pekee ukanda wa Afrika Mashariki na *SADC* ina ziada ya zaidi ya *Megawatts* 2,000 za umeme ikiwa inatekeleza mradi wa gridi imara kuhakikisha

umeme haukatikikatiki. Nchi yetu imeendelea kuwa na utulivu wa bei uliotokana na utekelezaji wa sera madhubuti za kifedha, kuimarika kwa bei ya mafuta na bidhaa katika soko la dunia, utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya dola za Marekani.

Mheshimiwa Spika, utulivu huo ulichangiwa kwa kasi ya ongezeko la bei ya bidhaa na huduma. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2025, wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia tatu nukta tano na kiwango hicho kipo ndani ya lengo la chini ya asilimia, kati ya asilimia tatu nukta sifuri hadi tano nukta sifuri.

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei kwa Januari, 2026 ulikuwa asilimia tatu nukta tatu ikilinganishwa na asilimia tatu nukta moja kipindi kama hicho kwa 2025. Kiwango hicho kipo ndani ya lengo la nchi za Afrika Mashariki za kutozidi asilimia nane nukta sifuri na kuwa kati ya asilimia tatu nukta sifuri hadi saba nukta sifuri.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kufuatilia hali ya masuala ya bei kwa kuzingatia mambo yanayotokea duniani. Yapo matarajio kwamba bei zitapanda zikianza na bei za mafuta kutokana na uhaba ama matatizo ya uzalishaji, masuala ya vita yanayoendelea katika nchi ambazo ni wazalishaji wakubwa wa mafuta ama kupanda kwa bima ya usafirishaji wa bidhaa hizo kutokana na kuyumba kwa mambo ya usalama katika nchi zinazozalisha bidhaa hiyo ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yameongezeka kutoka dola za Kimarekani bilioni 16.3 Januari, 2025 hadi dola za Kimarekani bilioni 18.7 kwa Januari, 2026. Ongezeko hilo ni sawa na 12.7%. Ongezeko hilo limechangiwa na mauzo ya bidhaa mbalimbali ikiwemo dhahabu, tumbaku, kahawa, bidhaa za viwandani, utalii na huduma za usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, Januari, 2026, akiba ya fedha za kigeni ilifika dola za Kimarekani bilioni 6.3. Kiasi hicho, kinawezesha kuagiza bidhaa na huduma kwa zaidi ya miezi 4.8 ikiwa ni juu ya kiwango cha chini kinachokubalika Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, mikopo iliyotolewa na benki hasa kwa sekta binafsi imeongezeka kutoka 12.8% Januari, 2025 hadi kufikia 23.5% kwa Januari, 2026. Mikopo hiyo, imenufaisha na inachochea shughuli za uwekezaji pamoja na uzalishaji katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza makusanyo. Mikakati hiyo ni pamoja na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji hapa nchini; kupanua wigo wa kodi; kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, kutokana na jitihada hizo, shilingi trilioni 26.63 zilikusanywa katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026 kati ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 25.68, ikiwa ni sawa na ufanisi wa 103.7%. Taarifa kamili ya hali ya uchumi itatolewa na Waziri wa Fedha atakapokuwa anawasilisha Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha mfumo wa kodi nchini na kufanya kuwa jumuishi, Mheshimiwa Rais aliunda Tume ya Kutathmini Maboresho ya Mifumo ya Kodi. Lengo lilikuwa ni kufanyia tathmini ya kina mfumo uliopo na kutoa mapendekezo yatakayowezesha kuondoa malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wafanyabiashara, wawekezaji na wadau wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu mpendwa kwa maono hayo makubwa, moyo wa uzalendo na uamuzi sahihi wa kufanya mapitio makubwa ya mfumo wa kodi ambayo hayajawahi kufanyika kwa kipindi cha zaidi ya miaka 30. Sina shaka mtakubaliana nami kuwa mfumo wa kodi ni nyenzo muhimu katika kufikia malengo yaliyoainishwa kwenye dira 2050. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, licha ya hayo, utekelezaji wa mapendekezo ya taarifa ya Tume hiyo utaongeza wigo wa kodi na kuhakikisha kila mtu anachangia kulingana na kipato chake. Hili ni kutokana na ukweli kwamba taarifa ya Tume hiyo imeainisha mikakati mbalimbali ya kudhibiti mianya inayotumika katika ukwepaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kusimamia mikakati itakayoongeza ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kiuchumi, kijamii ikiwemo kuboresha mazingira ya biashara, uwekezaji; kupanua wigo wa kodi; na kuimarisha kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA. Mikakati hiyo itahakikisha shabaha ya uchumi zilizoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, nitoe maelekezo kwa Wizara ya Fedha pamoja na Wizara zote za kisekta zilizoguswa na taarifa ya Tume ya Mheshimiwa Rais kuanza kutekeleza mapendekezo yale yaliyobainishwa kwa yale ambayo hayahitaji mabadiliko ya kimuundo wala ya kisheria na yale ambayo yanaweza yakaanza kutekelezwa kupitia Muswada wa Fedha ambao tayari wataalam wetu wanakaa kuuangalia upya.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa ikiongozwa kwa mipango thabiti ya maendeleo. Sote tunakumbuka kuwa katika kipindi cha miaka 25 iliyopita, tuliongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambayo ilitafsiriwa katika mipango mitatu ya maendeleo ya Taifa ya miaka mitano mitano. Mpango wa kwanza Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulitekelezwa kwa mwaka 2011/2012 - 2015/2016 ukiwa na dhima ya "Kufungua Fursa Fiche za Ukuaji wa Uchumi."

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulitekelezwa mwaka 2016/2017 – 2020/2021 ukiwa na dhima ya "Kukuza Uchumi wa Viwanda na Maendeleo ya Watu." Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulitekelezwa kwa mwaka 2021/2022 – 2025/2026, ukiwa na dhima ya "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu" ambao ndiyo unaokamilisha utekelezaji wa Dira 2025.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 17 Julai, 2025 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua rasmi Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Dira hiyo itaongoza mipango yetu ya maendeleo katika miaka 25 ijayo.

Mheshimiwa Spika, vilevile, inalenga kujenga Taifa jumuishi, lenye ustawi kwa wote, lenye haki na linalojitegemea. Kama sehemu ya mkakati wa utekelezaji wa Dira 2050, Serikali iliandaa na Bunge lako Tukufu likapitisha katika mkutano wake uliopita, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano utakaotekelezwa katika kipindi cha miaka mitano 2026/2027 – 2030/2031.

Mheshimiwa Spika, dhima ya mpango huo wa sasa baada ya kutoka kwenye hizi dhima nyingine zote nilizozisema za mpango wa kwanza, wa pili, na wa tatu, mpango huu wa nne dhima yake ni "Mageuzi katika Kukuza Uchumi na Kuzalisha Ajira."

Mheshimiwa Spika, naomba niirudie. Dhima ya sasa ya Mpango wa Nne ambao ni Mpango wa Kwanza kwenye Dira mpya ni "Mageuzi katika Kukuza Uchumi na Kuzalisha Ajira," tunahitaji mageuzi katika kukuza uchumi na tunahitaji kuzalisha ajira kwa sababu ni tatizo kubwa kwa sasa ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti itakayopitishwa na Bunge hili ni hatua ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2026/2027 - 2030/2031 na Dira 2050.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Dira hiyo utawezesha Taifa kuwa na uchumi wenye thamani ya Dola za Kimarekani trilioni moja, na wastani wa pato la mtu mmoja mmoja kuwa Dola za Kimarekani 7,000 ifikapo mwaka 2050. Kwa hiyo, Dira tunayo na dhima tunaYo na malengo tunayotaka kuyafikia tunayo, tena malengo ya watu wanaojiamini. Dola 7,000 kwa mtu mmoja, uchumi wa Dola za Kimarekani trilioni moja ifikapo mwaka 2050. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Dira 2050 ndiyo mwelekeo wa Taifa letu. Kwa kuzingatia hilo, kipaumbele cha Serikali kitawekwa katika utekelezaji wa malengo kama yalivyoainishwa katika dira hiyo. Suala hilo litawezekana tu ikiwa wadau wote watakuwa na

ufahamu wa kutosha kuhusu vipaumbele vilivyoainishwa katika Dira 2050.

Mheshimiwa Spika, ninatoa rai kwa viongozi wa Serikali, viongozi wa sekta binafsi, viongozi wa asasi za kiraia, viongozi wa dini, na wadau wa maendeleo wote hapa nchini kuhakikisha kwamba mipango hiyo inawiana na vipaumbele vya Dira 2050, mipango yao inawiana na vipaumbele vya Dira 2050 na kuiunga mkono Dira hiyo katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, hii siyo Dira ya Serikali, ni Dira ya nchi na inamhusu kila Mtanzania, na kila Mtanzania ashiriki katika kutimiza ndoto hiyo ya Taifa ya kufikia lengo hilo tulililoliweka katika Dira yetu. Aidha, tunaielekeza Tume ya Mipango kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Dira 2050 ili kuwezesha ushiriki kikamilifu wa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mipango, ameanza vyema kazi hiyo ya kutoa elimu kama ambavyo tumeshuhudia, wakiwa wanakutana na makundi mbalimbali kwa lengo hilo la kutoa elimu ya Dira 2050.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga uchumi unaoongozwa na uwekezaji katika sekta binafsi ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kuboresha ustawi wa wananchi. Ili kuonesha dhamira ya dhati ya kutekeleza malengo hayo katika mwaka 2025/2026, miradi 927 yenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 11.08 ilisajiliwa. Hatua hiyo inaonesha kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji nchini na kuongezeka kwa amani ya wawekezaji na imani kubwa ya wawekezaji ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea na uwekezaji wa kimkakati katika maeneo mbalimbali ikiwemo eneo maalumu la kiuchumi la Bagamoyo, Liganga na Mchuchuma, pamoja na miradi ya magadi soda kule Engaruka. Vilevile, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kukuza na kuvutia uwekezaji hapa nchini na kuratibu uwekezaji kama ambavyo umeelekezwa kupitia utekelezaji wa Dira ya 2050 kupitia mipango ya mwaka ya muda mrefu pamoja na muda wa kati.

Mheshimiwa Spika, tukirejea upande wa sekta za uzalishaji, tukianza na kilimo mazao, Baba wa Taifa na Mwanafalsafa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika kitabu chake kiitwacho 'Mtu na Maendeleo' cha 1974 alisema kuwa, ninaomba kunukuu: "Maendeleo ya kweli huanza pale wananchi wanapoweza kuzalisha chakula cha kutosha na kuwatosha wenyewe." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu huo imeendelea kuimarisha hali ya upatikanaji wa chakula ambapo tani 23,783,128 zilizalishwa katika msimu wa mwaka 2024/2025, ikilinganishwa na mahitaji ya tani 18,273,054 kwa mwaka 2025/2026. Kwa maana hiyo, tuna ziada ya chakula, tulizalisha tani milioni 23.7 mahitaji yakiwa tani milioni 18.3. Hivyo, kuihakikishia nchi usalama wa chakula wa zaidi ya 130%.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la uzalishaji limetokana na upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakati na Serikali itaendelea kutoa ruzuku ya mbolea. Aidha, katika msimu wa kilimo wa mwaka 2025/2026, Serikali imetoa tani 1,098,990 za mbolea sawa na 73.26% ya lengo. Kati ya hizo, tani 574,664.99 zenye thamani ya zaidi ya shilingi trilioni 1.03 zimesambazwa kwa wakulima 526,044 kupitia mpango wa ruzuku. Hatua hiyo inachochea ongezeko la matumizi ya mbolea na tija katika uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa uhakika wa mbolea umeongeza matumizi ya mbolea kwa 14.6% kutoka tani 848,884 kwa mwaka 2023/2024 hadi tani 972,506 kwa mwaka 2024/2025. Vilevile, matumizi ya virutubisho yameongezeka kutoka kilogramu 19 hadi 24 kwa hekta na hivyo kuongeza mwitikio chanya kwa wakulima, na mafanikio ya mkakati huo yameainishwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha kilimo cha kisasa na kuwainua wakulima wadogo wadogo, Serikali imeanzisha vituo 79 vya kutoa huduma ya zana za kilimo. Vilevile, imenunua matrekta 360 na kuyaweka kwenye vituo hivyo kwa ajili ya kutoa huduma kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha kilimo cha kisasa, Serikali itaendelea kutekeleza mradi huo wa upatikanaji wa zana za kilimo ili kuweza kuhakikisha kwamba wakulima wa Tanzania wanapata zana bora na za kisasa katika kulima.

Mheshimiwa Spika, ili kuleta tija inayotarajiwa katika kilimo, nimeielekeza Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuweka mpango mahsusi wa usimamizi wa vipimo. Nimekataza utaratibu wa lumbesa. Utaratibu wa lumbesa ni utaratibu unaonyonya wakulima. Mazao yote yanayofungashwa yawekwe kwenye vifungashio na yauzwe kwa kuzingatia vipimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitoa mwezi mmoja. Kuanzia sasa sitatarajia kuona tena mizigo ya mazao ya wakulima ikiwa inasafirishwa ikiwa imefungwa kwenye utaratibu huu unaojulikana kama lumbesa. Nchi imeshaingia uchumi wa kati, hatuna uhaba wa vifungashio wala hatuna uhaba wa vipimo. Twende kwenye vipimo halisi, tuache kuwanyonya wakulima.

Mheshimiwa Spika, suala hili litekelezwe sambamba na udhibiti wa ushuru holela wa mazao ya kilimo, ikiwa ni pamoja na halmashauri zote kusitisha mara moja ushuru wa holela unaotozwa kwa mazao ya kilimo bila kuzingatia utaratibu na uwiano wa maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nimeelekeza kusitishwa kwa utaratibu wa wakulima kukopwakopwa mazao na *AMCOS* zetu. *AMCOS* zinazojiandaa kununua mazao waende wakiwa na mitaji, watafute mikopo ili wanapokwenda kwa wakulima wanunue mazao. Wanunue mazao ili wakulima wapate mara moja fedha ya mazao yao, ili tusiwahangaishe kufuatilia madai ya fedha za mazao ambayo walishavuna na wamehangaika kwa muda mrefu kuweza kupata mavuno hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa pembejeo na huduma za ugani, afya ya udongo, hifadhi ya chakula, na masoko ya mazao. Lengo kuu ni kuongeza uzalishaji, kuimarisha usalama wa chakula na lishe, kukuza kilimo na biashara, na kuongeza mchango wa

sekta ya kilimo katika ukuaji wa uchumi. Serikali itaendelea kuimarisha sekta ya kilimo ili kuweza kuhakikisha kaulimbiu ya kwamba wananchi wengi wako katika sekta hiyo, iwe ya uhalisia.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifugo, Serikali itaendelea kuimarisha Sekta ya Mifugo kwa kuboresha mazingira ya ufugaji na biashara ya mifugo. Jitihada zilizochukuliwa ni pamoja na kufanya Kampeni ya Kitaifa ya Chanjo, ambapo mifugo milioni 49.4 kati ya milioni 76.3 sawa na 64% imechanjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Serikali imeendelea na zoezi la utambuzi wa mifugo na kusambaza vifaa vya chanjo. Pamoja na utoaji wa chanjo, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa mbegu za malisho kwa kuzalisha tani 149.9 zilizosambazwa kwa wafugaji katika mikoa 16 ya Tanzania Bara. Upatikanaji wa malisho, uhakika na umuhimu katika kufikia wafugaji, ni moja ya lengo la ufugaji endelevu na kupunguza migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uvuvi, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa bandari ikiwemo ujenzi wa Bandari ya Kilwa Masoko katika Mkoa wa Lindi, ambapo gharama ya takribani shilingi bilioni 280.58 ambazo ni fedha za ndani imetumika. Hadi Februari, 2026, ujenzi umefikia 95%. Kukamilika kwa bandari hii kutaimarisha utoaji wa huduma kwa wavuvi wakubwa na wadogo wa ndani na nje ya nchi na kuzalisha ajira zaidi ya 30,000 na kuboresha miundombinu ya uvuvi na kupunguza kiwango cha umaskini katika eneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo mambo yanayotambulisha kaulimbiu ya Mheshimiwa Rais ya 'Kazi na Utu.' *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua mchango na umuhimu wa shughuli zilizotekelezwa na wavuvi wadogo wadogo, ninaelekeza Kamati za Usalama ziimarishe ulinzi katika maeneo yote ambayo shughuli za uvuvi zinafanyika. Aidha, ni lazima kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na utu wakati wa utekelezaji na kusimamia masuala ya wavuvi hasa wadogo wadogo kwenye shughuli zao za kila siku.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kufanya tafiti za kimkakati katika uzalishaji wa mnyororo wa thamani ya uvuvi, kutekeleza mikakati ya uvuvi katika bahari kuu, ikiwemo ununuzi wa meli na ujenzi wa bandari za uvuvi. Vilevile, kudhibiti magonjwa ya mifugo kupitia ununuzi wa chanjo, ujenzi wa majosho na kutekeleza miradi ya kuongeza tija, ajira na mapato kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maliasili na utalii, sekta ya maliasili na utalii imeendelea kuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi, ajira na pato la Taifa. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuinua sekta hiyo muhimu kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mikakati hiyo ni pamoja na kuongeza idadi ya watalii waliotembelea hifadhi za Taifa kwa 10.73%, kutoka watalii milioni 5.3 kwa mwaka 2024 hadi watalii milioni 5.9 kwa mwaka 2025, na hivyo kuongeza mapato yatokanayo na utalii kutoka Dola za Marekani bilioni 3.9 kwa mwaka 2024 hadi Dola za Marekani bilioni 4.4 Desemba 2025, tukiwa na ongezeko la takribani 12.82%.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la watalii limechangiwa kwa kiasi kikubwa na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo zimetambuliwa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Katika kutambua mchango huo, tarehe 31 Januari, 2026, Mheshimiwa Rais alitunukiwa Tuzo ya Kiongozi Mwenye Maono katika hafla ya utoaji wa Tuzo ya *Serengeti Awards*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa, Serikali ilipokea Ripoti ya Tume ya Rais ya Kutathmini Zoezi la Uhamaji wa Hiari kwa Wakazi wa Eneo la Hifadhi la Ngorongoro na Tume ya Rais ya Kutathmini Masuala ya Ardhi katika Wilaya ya Ngorongoro. Ninalihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali itafanyia kazi mapendekezo ya ripoti hizo kwa lengo la kupata suluhu ya kudumu ya kuimarisha utalii katika ukanda huo.

Mheshimiwa Spika, ninaelekeza Wizara zinazohusika: Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI; Mkoa wa Arusha; na Mkoa wa Tanga kuendelea na mkakati wa utekelezaji wa zoezi hilo na utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Rais katika maeneo hayo mawili.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madini, Serikali imeendelea kuimarisha sekta ya madini kwa kutekeleza mikakati mbalimbali inayoongeza mapato ya Serikali na fursa za ajira kwa wananchi. Kama ilivyo kwa sekta ya maliasili na utalii, sekta ya madini ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na pato la Taifa. Kwa kuzingatia umuhimu huo, mikakati mbalimbali imeendelea kutekelezwa ikiwemo kuimarisha usimamizi na utendaji wa masoko 44 na vituo 118 vya ununuzi wa madini.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha Taifa kuwa na taarifa za uhakika kuhusu kiasi cha ubora wa rasilimali za madini, ninaelekeza Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Madini kuweka utaratibu wa kutenga fedha zitokanazo na mapato ya madini kwa ajili ya tafiti na ufuatiliaji wa madini. Taratibu hizo zianze kutumika katika mwaka wa fedha huu 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji kujua rasilimali tuliyonayo, tunahitaji kuongeza wigo wa Watanzania kujihusisha na uchimbaji ili kuweza kuinua pato la Taifa na pato la mtu mmoja mmoja kutokana na sekta hiyo na utajiri huo tulionao.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kutoa fursa kwa Watanzania kunufaika na rasilimali za madini. Nimeelekeza Wizara ya Madini kuweka utaratibu wa kudhibiti mikataba wanayoingia Watanzania wenye vitalu na wawekezaji wa nje ili kulinda maslahi ya Watanzania na rasilimali za Taifa. Pamoja na kwamba tunahitaji uwekezaji, pamoja na kwamba tunahitaji vijana waingie mikataba hiyo, lakini lazima rasilimali hii iwanufaishe Watanzania kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hii itasaidia pia kuondoa migogoro kati ya wachimbaji wadogo wadogo na wawekezaji. Kumeanza kuzuka katika baadhi ya maeneo, ukifika unaweza ukadhani uko

nje ya nchi, unakutana na wageni watupu na wanashughulika kwenye maeneo ya uchimbaji wao watupu, huku wakiwaondoa Watanzania. Hili siyo lengo alilolitegemea Mungu kwa kuweka rasilimali hizi Tanzania, lazima Watanzania wanufaike na rasilimali zilizowekwa kwenye Taifa lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na mnyororo wa thamani katika madini muhimu na madini mkakati. Vilevile, itahamasisha uwekezaji, kuimarisha uendeshaji wa minada na maonesho ya madini ya vito na kuongeza uwekezaji kwenye tafiti za madini za kina, na kuwaimarisha na kuwaendeleza wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, tutakuwa na vikao vya kila sekta na wadau wa kila sekta ili tuweze pia kupata maoni yao kutoka kwenye sekta zao na uzoefu wa kule *site* wanakochimba ili tuweze kuboresha sekta hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nishati, sina shaka, nyote mtakubaliana na mimi kwamba, nishati ya umeme ni *engine* ya kuimarisha na kurahisisha maendeleo ya kisasa, hususan inapotumika katika shughuli za uendeshaji wa viwanda, teknolojia, pamoja na matumizi ya nyumbani. Serikali kwa kutambua hilo, imeendelea kutekeleza mikakati mahususi ya kuhakikisha nishati ya umeme inazalishwa hapa nchini, inakidhi mahitaji yatokanayo na kasi kubwa ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa miradi mbalimbali ikiwemo uzalishaji wa umeme ikiwemo ya ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere kwa kutumia fedha za ndani, hivi sasa nchi yetu kama nilivyosema, ina ziada ya zaidi ya Megawati 2,000. Serikali itaendelea kujenga na kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa umeme ili kuondoa changamoto ya kukatikakatika kwa umeme katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ukiona mahali umeme umekatika, siyo upungufu wa umeme, ni masuala ya uimara wa gridi ambapo tayari Serikali chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan imeweka zaidi ya shilingi trilioni 1.1 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Gridi Imara ili kutibu jambo la kukatikakatika umeme.

Mheshimiwa Spika, ninawaelekeza Wizara ya Nishati pamoja na Wizara ya Fedha, kukamilisha utekelezaji wa miradi hiyo ya kupeleka umeme katika kuimarisha Gridi ya Taifa, ili kuondokana na kukatikakatika kwa umeme. Vilevile tuendelee na utekelezaji wa kupeleka umeme kwenye vitongoji, viwekwe vipaumbele katika kuunganisha umeme katika hospitali, vituo vya afya, zahanati, shule, taasisi za dini na visima vya maji.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara ya Fedha, kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati, kuimarisha utekelezaji kama nilivyosema wa gridi imara, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha fedha zilizotengwa zinatolewa kwa wakati, ili tukamilishe mradi huo wa gridi imara na kuwaondolea wananchi adha ya kukatikakatika umeme. Lengo ni kuondoa tatizo hilo maeneo yote kwa mara moja hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mafuta na gesi, pamoja na juhudi za upatikanaji wa nishati ya umeme, Serikali imeendelea kuhakikisha ongezeko la matumizi ya gesi asilia katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026. Serikali imeongeza mtandao wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika viwanda, taasisi na nyumbani hadi kilometa 243.6 ikilinganishwa na kilometa 184 zilizokuwa kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha matumizi ya gesi asilia iliyosindikwa, ninaelekeza Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Nishati zishirikiane kuandaa viwango msawazo *(specifications)* vitakavyotumika katika mahitaji ya vyombo vya moto vya Serikali, ili Serikali iongoze kwa mfano kuhama kwenye kutumia vyombo vya moto vinavyotumia mafuta kwenda kwenye vyombo vya moto vinavyotumia nishati ya gesi. Vilevile ijengwe miundombinu ya kutosha ya kuwezesha vyombo hivyo kuanza kutumia gesi asilia iliyosindikwa.

Mheshimiwa Spika, leo tunaongelea tatizo la kupanda kwa bei za mafuta kutokana na hali ya kisiasa, hali ya amani katika Mashariki ya Kati, lakini sisi tuna gesi yetu ambayo itatupa uhakika.

Tukishakuwa na gesi yetu na vifaa vyetu vinatumia nishati ya gesi, maana yake ni kwamba, hatutaathirika sana yanapotokea matatizo kama haya kwenye nchi zinazozalisha mafuta. Licha ya uwepo wa changamoto za kiusalama za kikanda na Kimataifa ikiwemo ile ya Mashariki ya Kati, Serikali itaendelea kusimamia upatikanaji wa bidhaa hizi za mafuta, petroli pamoja na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kuhakikisha kuwa bidhaa hizo zinaendelea kuwa himilivu, tumeona bei zimeanza kupanda. Tutakaa ndani ya Serikali kuweza kuhakikisha tunakabilianalo vipi hilo, ili wananchi waendelee kupata mafuta kwa bei watakayoweza kumudu na kudhibiti kupanda kwa gharama za maisha.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Serikali imeendelea kusimamia mifumo ya kuagiza, kuhifadhi, kusambaza mafuta pamoja na kuongeza uwezo wa kupokea na kuhifadhi mafuta katika Bandari yetu ya Dar es Salaam na Mtwara. Katika kufanikisha hilo, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa ghala la kupokea na kuhifadhi mafuta lenye uwezo wa kupokea tani 308,110 katika Bandari ya Dar es Salaam ambapo umefikia 30%.

Mheshimiwa Spika, aidha, miundombinu ya kuhifadhi mafuta katika Bandari ya Mtwara imeongezeka kutoka tani 29,280 hadi tani 110,221 ambazo zitawezesha kupokea meli zenye shehena ya tani 30,000.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2026/2027 Serikali imeendelea kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme, ili kukidhi mahitaji ya nishati hapa nchini, kusambaza umeme katika vitongoji ambavyo havijapangiwa umeme, kuendelea na shughuli za kutafuta, kusafirisha, kuhifadhi na kusambaza mafuta na gesi asilia. Pia, kukamilisha mpango wa matumizi ya nishati safi ya kupikia katika taasisi, kuimarisha ushirikiano wa sekta binafsi na kutekeleza mkakati wa Taifa wa matumizi ya nishati safi ya kupikia 2024 - 2034.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu mafuta na gesi yanapatikana katika aya ya 90 hadi 96 ya hotuba hii na yatatolewa kwa kina na Waziri wa Sekta atakapokuwa anaelezea, atakapowasilisha Bajeti ya Serikali ya Sekta ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ardhi, Sekta ya Ardhi ni mtambuka na ni muhimu sana katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli za sekta nyingine za uzalishaji na maendeleo ya Taifa. Hata hivyo, sekta hii imekumbwa na changamoto na migogoro mingi ambayo imekuwa kero kubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, changamoto na migogoro hiyo ni pamoja na maeneo mengine nchini kutokupimwa, ucheleweshaji wa utoaji wa hati, umilikishaji wa eneo moja kwa zaidi ya mtu mmoja na baadhi ya watendaji kutokuwa waaminifu, uuzaji wa maeneo ya wananchi kinyemela pamoja na kero nyingine za aina hii.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizo zimesababisha uwepo wa migogoro baina ya makundi mbalimbali katika jamii, ikiwemo ya wakulima na wafugaji; migogoro ya mipaka baina ya vijiji na vijiji; na migogoro ya ardhi baina ya mtu na mtu, mtu na taasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya jambo linalotishia undugu wa Watanzania kwa sasa ni ardhi. Maeneo mengi watu wanataka kuchukiana kwa sababu ya ardhi. Serikali imeendelea kutatua migogoro hiyo kupitia Kliniki za Ardhi, Kamati za Wataalamu, Mabaraza ya Ardhi na ziara za viongozi. Hadi Januari, 2026 migogoro 5,333 imetatuliwa, maombi ya umiliki 10,113 yalipokelewa na hatimiliki 7,182 zimeandaliwa, pamoja na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji 191.

Mheshimiwa Spika, nimeelekeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kukaa waliangalie upya na kuja na mapendekezo mahususi kuhusu ni namna gani tutakabiliana na kulimaliza tatizo hili ambalo limewakabili wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba, changamoto na migogoro hiyo inafika kikomo, nimesema ni lazima sasa tuifikishe mwisho, kwa sababu, tumeilimbikiza sana. Wizara ya Ardhi pamoja na watumishi wake wote, wapimaji wa maeneo na watendaji kazi katika maeneo mbalimbali na wenyewe waendelee kutatua changamoto ambazo tayari tumeshazipokea.

Mheshimiwa Spika, vilevile hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa watumishi wote watakaobainika kuwa chanzo cha migogoro hiyo. Aidha, Wizara ihakikishe taratibu za mifumo inayotumika kutoa huduma za ardhi inakuwa ya wazi na rafiki kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027 Serikali itaendelea kusimamia upangaji na upimaji wa ardhi mijini na vijijini na maeneo ya kimkakati, kuimarisha mifumo ya TEHAMA na kuboresha huduma za uthamini na ulipaji fidia. Pia, itaimarisha utatuzi wa migogoro, kuendelea na ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na kuboresha miundombinu ya upimaji na ramani, ili kuongeza tija, uwazi na kasi ya utoaji wa huduma hizo. Serikali itaangalia upya namna inavyoshughulikia masuala haya ya migogoro.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Viwanda na Biashara. Sekta ya viwanda na biashara imeendelea kuwa nguzo muhimu katika kuleta mageuzi ya kiuchumi. Katika mwaka 2025/2026 Serikali imeendelea kuwezesha ujenzi wa kongani za *Sino Tan Industrial Park* pale Kwala, ambapo umefikia 80% na viwanda vinne vimeanza uzalishaji wake.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa mbalimbali ni hatua muhimu ya kupunguza matumizi ya fedha za kigeni. Moja ya bidhaa ambayo imekuwa ikiagizwa kutoka nchi za nje kwa fedha za kigeni ni sukari ya viwandani. Hata hivyo kuanzia Novemba, 2025 Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi kilianza rasmi uzalishaji wa sukari ya viwandani ambapo hadi Februari, 2026 tani 256 za sukari ya viwandani zimezalishwa.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji huo unatarajiwa kupunguza mahitaji ya uagizaji wa sukari ya viwandani kutoka nje kwa 20%. Ili kuimarisha biashara za Watanzania nimeielekeza Wizara ya Viwanda na Biashara kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza biashara, kuongeza uzalishaji na kuimarisha ushindani.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kuboresha maeneo ya kufanyia biashara za wajasiriamali wadogo wadogo, wakiwemo Wamachinga, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaanza kutenga asilimia tano ya nyongeza kwenye 4:4:2 ya mapato ya ndani, ili kuweza kujenga na kuboresha miundombinu na kuwapatia maeneo wafanyabiashara, almaarufu kama Machinga, katika maeneo ambayo watapata wateja wao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027 Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya biashara na kuchochea ukuaji wa sekta binafsi ikiwemo utafutaji wa masoko na vilevile itaendelea kuchochea maendeleo ya viwanda na biashara kupitia ubunifu wa matumizi ya teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usafiri na usafirishaji, miundombinu ya usafiri na usafirishaji ni msingi wa uchumi wa Taifa letu. Katika kuhakikisha huduma hiyo inakuwa bora katika mwaka 2025/2026, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara, madaraja, viwanja vya ndege, vivuko, majengo ya Serikali, pamoja na kuwajengea uwezo wakandarasi wa ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu hapa nchini, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilometa 4,818.12 na za changarawe kilometa 5,741.17. Vilevile imeendelea kufanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometa 23,871.59. Ili kuimarisha uchumi wa nchi, ni vyema kuhakikisha miundombinu ya barabara inajengwa, inakamilika kwa wakati na kutumika katika kutoa huduma hizo za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kuendeleza na kuimarisha barabara za mijini na vijijini, hasa barabara za vipaumbele katika majimbo, nimeielekeza Wizara ya Fedha iimarishe vyanzo vya

upatikanaji wa fedha za Mfuko wa Barabara na ihakikishe fedha hizo kutoka kwenye vyanzo vilivyotengwa kwa ajili ya mifuko vinauwianishwa na bajeti na vinapelekwa moja kwa moja kwenye mifuko iliyotengwa bila kupitia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, tunataka fedha hizo ziende moja kwa moja kwenye mifuko hiyo bila kupitia mfuko wa Serikali, ili kutokuathiri mtiririko wa fedha hizo zinazokwenda kwenye miradi hiyo inayotekelezwa. Nimeielekeza Wizara ya Fedha pamoja na Wizara zenye mifuko; Wizara za kisekta ambako mifuko hiyo ipo, wakae wauwianishe fedha hizo na bajeti, makusanyo na bajeti, na baada ya hapo zikishakusanywa, kuanzia zinakokusanywa, zipelekwe moja kwa moja kwenye mifuko. Zisiende kwenye Mfuko Mkuu, ili kutoathiri mtiririko wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na upanuzi wa mtandao wa barabara, Serikali imekamilisha ujenzi wa madaraja ya Mkili kule Ruvuma, Mbangala kule Mtwara na Ngoyami na Chakwele kule Morogoro. Aidha, itaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa madaraja makubwa 13 ambayo ni Mirumba na Mitomoni kule Ruvuma, Pangani kule Tanga, Simiyu kule Simiyu, Mambe kule Pwani, Damu kule Morogoro, Mwanjiri na Nzali kule Dodoma, Suguta kule Mara, Sukuma kule Mwanza, Jangwani pale Dar es Salaam, Kalebe kule Kagera, na Kavuu kule Katavi. Kukamilika kwa ujenzi wa madaraja hayo kutarahisisha mawasiliano na kuchochea shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa usafiri wa anga katika kuharakisha shughuli za kiuchumi na za kijamii, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa viwanja vya ndege, kikiwemo Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato. Ujenzi wa kiwanja hicho umefikia 84% kwa upande wa miundombinu na 70% kwa upande wa majengo. Kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua kwa ndege na uzio wa usalama pamoja na barabara za mizigo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027 Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara za kimkakati za kufungua fursa za

kiuchumi na barabara zinazounganisha Makao Makuu ya Mikoa, wilaya na nchi jirani. Vilevile itaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara za michepuko, mzunguko na mwendokasi, ili kupunguza msongamano katika majiji na miji inayokua kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uchukuzi, sambamba na uwekezaji mkubwa ambao umefanywa katika sekta ya usafiri na usafirishaji Serikali itaendelea kuwekeza katika miundombinu ya kimkakati ya *Standard Gauge Railway*. Hadi Februari, 2026 ujenzi wa kipande cha Mwanza – Isaka, kilometa 341, umefikia zaidi ya 67%, Makutupora – Tabora, kilometa 368, 18.54%, Tabora – Isaka, kilometa 165, asilimia nane nukta tisa tano, Tabora – Kigoma, kilometa 506, asilimia tisa nukta sita.

Mheshimiwa Spika, fedha ya kutekeleza mradi huo kutoka Mwanza – Isaka ipo, inasubiri kazi za mkandarasi. Siku siyo nyingi tutalala Mwanza, tutakunywa chai Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile hatua za maandalizi ya ujenzi wa kipande cha Uvinza – Malagarasi kwenda Msongati zinaendelea. Kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka, Agosti 16, 2025 jiwe la msingi la ujenzi wa mradi huo limewekwa, na mkandarasi tayari ameshalipwa malipo ya awali. Aidha, kipande cha Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma usafirishaji wa mizigo ulioanza Juni, 2025 katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026 tani 52,305 za mizigo zimeshasafirishwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027 Serikali itaendelea na ujenzi na ukarabati wa reli, bandari, meli, vivuko, viwanja vya ndege na utekelezaji wa bandari kavu, ili kuimarisha huduma hii ya usafiri na usafirishaji. Vilevile tutaendelea kuboresha miundombinu ya matenki ya kupokea mafuta bandarini na maeneo ya kuhifadhia. Ufafanuzi zaidi utatolewa na Waheshimiwa Mawaziri wa sekta watakapokuwa wanawasilisha bajeti za Wizara za kisekta.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mawasiliano na teknolojia, Serikali katika kutekeleza sekta ya mawasiliano na teknolojia imeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa na mawasiliano, ili kuunganisha Tanzania na Jamhuri ya

Kidemokrasia ya Kongo kupitia Ziwa Tanganyika. Hatua hii inalenga kuchochea biashara kati ya nchi zetu hizo na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilwa, Maswa, Bariadi, Sikonge, Urambo, Ushirombo, Chunya, Karagwe, Nzega na Butiama na zenyewe zimeunganishwa kwenye Mkongo wa Taifa, hivyo kufanya jumla ya wilaya zilizounganishwa kufikia 120 kati ya wilaya 139, sawa na 86%. Hili ni jambo lingine linalotambulisha kazi ya Mheshimiwa Rais, Mama yupo kazini. Wilaya 120 zimeunganishwa na Mkongo wa Taifa kati ya wilaya 139. Kwa hiyo, bado 19 tu, bila hata kutumia *calculator*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na upanuzi wa mtandao wa Mkongo wa Taifa, Serikali imekamilisha ujenzi wa minara 758 kati ya minara 713 kwa gharama ya shilingi bilioni 126, ili kuongeza kasi ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano. Vilevile minara 304 imeongezewa uwezo kutoka teknolojia ya *2G* kwenda *3G* na *4G*. Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma ya mawasiliano kwa kujenga na kuimarisha minara ya simu na redio na vilevile itaendelea kuunganisha wilaya zilizobaki, ili ziweze kuunganishwa na Mkongo wa Taifa, kama nilivyotoka kusema hivi punde.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za jamii, Serikali imeendelea kuimarisha sekta ya elimu kwa kuzingatia Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023, mitaala iliyoboreshwa na mipango mikakati. Lengo ni kuzalisha rasilimali watu wenye ujuzi na maarifa stahiki yatakayowezesha kumudu ushindani wa ajira na uwezo wa kujiajiri. Tathimini inaonesha kuwa, wanafunzi 3,021,177 wanatarajiwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2028.

Mheshimiwa Spika, pale tunapoongelea elimu ya lazima kuwa ni mpaka kidato cha nne, tunatarajia wanafunzi watakaoingia kidato cha kwanza ni 3,021,177. Hii inaenda kufuta kwamba, huyu hajachaguliwa, wote wanakwenda kidato cha kwanza. Jumla ya gharama zinazohitajika ni shilingi trilioni 1.77, kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 23,226, matundu ya

vyoo 46,632, maabara 9,366, ajira mpya za walimu 40,192, ruzuku ya vitabu na uendeshaji pamoja na ruzuku ya mitihani na upimaji.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha wanafunzi wote wanapata nafasi ya kuendelea na masomo, kwa mwaka 2026/2027, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri imetenga shilingi bilioni 139.28 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa. Nimewaelekeza Wakuu wa Mikoa wote kufanya maoteo ya mahitaji ya rasilimali na miundombinu itakayotuwezesha kuanza elimu ya lazima mpaka Kidato cha Nne kwa mwaka 2028.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Serikali imetoa shilingi bilioni 88.84 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya 103 za amali. Kati ya hizo, ujenzi wa shule 27 umekamilika na tayari shule hizo zimeanza kutumika. Vilevile, hadi Februari, 2026, shule 158 za Sekondari nchini zinatekelezwa kwa mkondo wa amali wa mitaala iliyoboreshwa ikilinganishwa na shule 41 zilizoanza mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa shule mpya 103 za amali, zimejengwa kwa mpigo zikiwemo *technical schools.* Zamani tulikuwa na shule takribani tano tu za ufundi, chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan miaka takribani minne kwenda mitano shule 103 zimejengwa. Hapo ndipo ninapowapongeza Wakuu wa Mikoa; na kwa kuwa wapo hapa, shule hizi zimejengwa mikoani kwao hawakuwa na likizo wala *weekend* kuweza kuhakikisha ndoto hiyo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inatimia. Hongereni sana Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa. Ndiyo maana Rais anawaita jeshi lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya kuboresha ufundishaji wa masomo ya amali, Serikali imepeleka walimu 150 kwenye mafunzo ya muda mfupi nchini India. Nimepita shule moja, nimekuta mtoto wa miaka 15 anasoma *engineering* na yuko ki-*engineer, engineer* kama wale tuliokuwa tunasoma wote Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ili kutekeleza hilo, Rais amepeleka mafunzo walimu 150 kwa mpigo, wameenda nchini India. Walimu 156,948 kati 172,609 kutoka shule za msingi 17,111 pia walishiriki

mafunzo endelevu kazini. Hawa walimu 150, kati yao hakuna hata mmoja aliyewahi kuwa hata na *passport*. Wametafutiwa *passport,* wamekwenda nje ya nchi kujifunza ili waje wafundishe shule zetu za *technical* za amali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu pamoja na kukamilisha maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi. Lengo ni kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu katika maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2025/2026 Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa shule mpya za msingi 277. Vilevile, imeongeza miundombinu ya shule za msingi na sekondari na kujenga madarasa 5,439, majengo ya utawala saba, mabweni 21, hosteli 26, nyumba za walimu 69, maabara 46, mabwalo matano na vituo vya walimu 70.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ukarabati, Serikali imekamilisha ukarabati wa shule za msingi 228. Vilevile, imekamilisha ujenzi wa miundombinu iliyojengwa kwa nguvu za wananchi. Aidha, ninatoa pongezi na shukrani kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupeleka vifaa vya maabara katika shule za sekondari 231 zikiwemo shule mpya 26 za Kitaifa za sayansi za wasichana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zamani tulikuwa tunazijua shule chache za wasichana zikiwemo zile zenye hadhi ya Kilakala, Msalato, *Tabora Girls* na nyingine. Rais amejenga kila Mkoa shule maalum ya wasichana yenye hadhi ya chuo. Nimezingukia nimeziona ni shule bora kabisa.

Mheshimiwa Spika, nilipopita kwenye shule mojawapo kule, niliweza kuisema hii inafanana na chuo kamili, shule maalum za wasichana zenye maabara za masomo yote na ziada, nafasi ya kujifunza, miundombinu ya kujifunzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza mpango wa elimu bila ada kwa kugharimia elimu ya awali hadi elimu ya sekondari ya juu na baadhi ya vyuo vya kati vyenye masomo

mahsusi. Hadi Februari, 2026 shilingi bilioni 383.22 zimetumika kati ya shilingi bilioni 510.96 ikiwa ni ongezeko la 75%. Sambamba na hilo, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa vyuo vya *VETA* 64 vya kila Wilaya ambazo zilikuwa bado hazijapata vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha fursa za masomo ya elimu ya kati na elimu ya juu inapatikana kwa makundi yote ya kijamii, Serikali imeendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na elimu ya kati. Jumla ya shilingi bilioni 899.21 zimetolewa kwa mwaka 2024/2025 ambapo shilingi bilioni 348.77 zimetolewa kwa wanafunzi 107,541 wa mwaka wa kwanza na shilingi bilioni 550.44 zimetolewa kwa wanafunzi 177,492 wanaoendelea na masomo.

Mheshimiwa Spika, Dkt. Samia Suluhu Hassan aliongeza kiwango wanachopata wanafunzi almaarufu kinaitwa *boom*. Pia alihakikisha kila wakati vyuo vinapofunguliwa wanafunzi hawa wapate fedha kwa wakati. Ndiyo maana katika siku za hivi karibuni na miaka ya hivi karibuni hausikii tena migomo ya wanafunzi ili wapelekewe fedha zao za matumizi. Hii na yenyewe inatambulisha kauli mbiu ile ya kazi na utu. Mheshimiwa Rais anazingatia utu wa watoto hawa wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Serikali imetoa ufadhili wa shilingi bilioni 9.46 kupitia *Samia Scholarship* kwa wanafunzi 1,786 wenye ufaulu unaojipambanua wanaosoma masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati katika vyuo vikuu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile, imetoa ufadhili wa shilingi bilioni 5.487 kupitia *Samia Scholarship Extended* kwa wanafunzi 50 wenye ufaulu wa juu wa kidato cha sita katika fani za sayansi waliochaguliwa kusoma Shahada ya Kwanza katika fani za Sayansi *Data*, Akili Unde na Sayansi Shirikishi katika vyuo bora duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii aliyoitoa Rais, imekuwa fursa ya mtoto kutoka kijijini kukwea pipa na kwenda chuo bora duniani ilimradi tu amefanya vizuri *with distinction* katika masomo yake. Wapo

waliokuwa wanabeza zilipojengwa shule hizi za Kata katika fungu hili la watoto 50 atakapokuja Mheshimiwa Waziri wa sekta ya elimu sayansi na teknolojia atawaambia. Kuna watoto waliofanya vizuri kitaifa wameshika nafasi hizo 50 za kwanza, wametoka kwenye shule za Kata kule vijijini. Watoto wanaotoka kwenye familia za watu wa kawaida wamekwenda vyuo bora duniani, utaratibu aliokuwa anautumia Mwalimu Nyerere kutengeneza wasomi wenye *distinction. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya na kuimarisha upatikanaji na utoaji wa huduma ya afya, Serikali imeendelea kusimamia ubora, usalama na ufanisi wa utoaji wa huduma za afya. Katika kuimarisha upatikanaji bora wa huduma za afya zinazotolewa ngazi zote, kuanzia zahanati hadi hospitali za Taifa, hadi ubingwa na ubingwa bobezi pamoja na kuimarisha uwekezaji wa viwanda vya dawa, Serikali itaendelea kuongeza nguvu katika hatua hizo zote ili kuweza kuhakikisha kwamba nchi yetu inajitosheleza kwenye masuala ya afya.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma bingwa na bobezi, Serikali imeendelea na mikakati mahsusi ya kuongeza madaktari bingwa na bingwa bobezi. Moja ya mikakati hiyo ni kuanzisha programu ya ufadhili ya *Samia Health Super-Specialization Program*. Kupitia programu hiyo, jumla ya wataalamu 1,483 wamepata ufadhili wa masomo katika fani za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hakika Rais amethibitisha kwa vitendo dhamira yake njema ya kuthamini na kujali afya na utu wa Watanzania kwa kuhakikisha huduma za kibingwa na ubingwa bobezi zinapatikana hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zamani Watanzania walikuwa wanatoka hapa kufuata matibabu Afrika Kusini, Kenya na kwingineko. Sasa Mataifa mbalimbali ndani ya nchi za *SADC* yanakuja kufuata huduma za kibingwa za afya hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha utoaji wa huduma bora za afya. Hatua hizo ni pamoja na kuongeza uwezo wa nchi kuzalisha dawa na vifaatiba, mifumo ya ugharimiaji wa huduma za afya, kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA, kuboresha miundombinu, kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya, kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi, utafiti na kuimarisha tiba utalii kama nilivyokwisha kusema.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI, jitihada zilizofanywa na Serikali kwa kuimarisha, na kwa kushirikiana na wadau, kuwezesha Taifa letu kupiga hatua kubwa katika kupunguza maambukizi mapya ya VVU, kudhibiti maradhi pamoja na vifo vitokanavyo na UKIMWI na kuimarisha na kuweza kuhakikisha kwamba wale wenye VVU waishi maisha yenye afya na tija kutokana na matibabu bora ya kufubaza VVU. Mafanikio hayo yameainishwa katika tathmini ya hali ya mwitikio dhidi ya UKIMWI hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati ya kukabiliana, na ili kufikia lengo la kutokomeza UKIMWI kama janga la afya ya jamii ifikapo mwaka 2030. Mikakati hiyo ni pamoja na kuendeleza kushirikiana na wadau wote wa maendeleo katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI kwa kugharimia kinga, tiba pamoja na matunzo. Ufafanuzi zaidi wa kina unapatikana katika hotuba hii ukurasa wa aya ya 158 hadi 172.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maji, huduma ya maji ni muhimu sana kwa uhai wa viumbe vyote. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya maji na kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji katika maeneo mbalimbali nchini. Jitihada hizo zimeimarisha wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya vijijini kutoka 83.0% Desemba, 2024 hadi 85.2% Desemba, 2025 na kwa maeneo ya mijini kutoka 91.6% Desemba, 2024 hadi 92.5% Desemba, 2025.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ya kimkakati iliyokamilika ni pamoja ile miji 28 ambayo itatekelezwa katika maeneo ambayo bado haijakamika. Utekelezaji wa miradi miji hiyo baadhi

ya maeneo umeshafika 89.8%. Maeneo mengine ni kukamilika ambayo itanufaisha wananchi takribani 5,985,500 kwenye maeneo ambayo yamepitiwa na miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya kimkakati itakayounganishwa kwenye gridi ya Taifa ya maji itakayohusisha kutoa maji maeneo yenye vyanzo vya uhakika na kupeleka maeneo yenye uhaba wa maji. Vilevile, Serikali itaandaa mpango kabambe kwa lengo la kutoa mwelekeo wa muda mrefu na wa kimkakati wa Kitaifa wa kusimamia, kuendeleza na kutumia rasilimali za maji kwa njia iliyo endelevu.

Mheshimiwa Spika, pia nimeelekeza Wizara ya Maji kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI kutumia mitambo ambayo Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshanunua kwa kila mkoa kwa ajili ya kuchimba visima ili maeneo yanayohitaji visima wachimbiwe visima na maeneo yanayohitaji mabwawa waweze kuchimbiwa mabwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa jamii ya watu wenye ulemavu imeendelea kupata huduma muhimu za kuimarisha haki na ustawi pamoja na kuwawezesha kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali. Ili kufanikisha azma hiyo, Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu imetoa ruzuku ya shilingi milioni 283.92 kwa ajili ya vyama 13 vya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeiwezesha Bohari ya Dawa kuzalisha na kusambaza vifaa saidizi na mafuta kinga kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Vilevile, kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imetoa chupa 105,557 za mafuta ya kujikinga na mionzi ya jua kwa wale wenye ualbino katika mikoa 24 ya Tanzania Bara. Kadhalika, imewezesha upasuaji wa saratani ya ngozi kwa watu wenye ualbino katika Taasisi ya Utafiti wa Saratani ya *Ocean Road* na Hospitali ya *KCMC*.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Serikali imetoa huduma ya afya ya macho, kufanya uchunguzi kwa watu 91,227 ambapo watu 11,047 waliobainika kuwa na matatizo ya macho na walipatiwa miwani. Vilevile, imetoa usaidizi kwa watu wenye

ulemavu katika Mikoa ya Kigoma, Ruvuma, Mbeya, Tanga, Shinyanga, Mara na Dodoma ambapo watu 6,618 wamenufaika.

Mheshimiwa Spika, mimi nikiwa Balozi wa Watu Wenye Ulemavu, pia kote kwenye ziara nilikopita, angalau tumepatia mtu mmoja mwenye ulemavu bajaji ili kuweza kukidhi katika shughuli za kuzalisha mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha huduma kwa watu wenye ulemavu kwa kuratibu afua za ulinzi na ustawi, kuratibu programu za uwezeshaji kiuchumi na kuendeleza ujuzi. Vilevile, Serikali itaandaa utaratibu maalumu wa kuwawezesha na kuwasaidia watu wenye ulemavu pamoja na wale wanaowahudumia.

Mheshimiwa Spika, tutaongea na wenzetu wa Wizara ya Fedha kuona ni namna gani wataweka kwenye sheria ili wale wanaowahudumia watu wenye ulemavu na wenyewe waweze kupata angalizo.

Mheshimiwa Spika, pia tunataka kukomesha utaratibu wa watu wenye ulemavu kupewa barua ya kwenda kuchangisha michango. Tutafute utaratibu mzuri wenye staha wa kuweza kupatia usaidizi watu hawa. Hii ya kuwapa barua waende kuanza kuchangisha huko inavunja heshima yao na siyo halisia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2025/2026, Serikali imeendelea kuratibu shughuli zake Bungeni. Moja ya shughuli zilizofanywa katika Mkutano wa Pili wa Bunge la Kumi na Tatu ni kuratibu uwasilishaji wa Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hotuba aliyoitoa tarehe 14 Novemba, 2025 wakati wa ufunguzi rasmi wa Bunge la Kumi na Tatu na kujadiliwa hapa Bungeni. Nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali inaahidi kuendelea kutekeleza ahadi zote zilizotolewa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mjadala wa hotuba ya Rais, miswada miwili ilisomwa kwa mara ya kwanza na nyaraka muhimu za kimkakati ziliwasilishwa na kuidhinishwa na Bunge. Nyaraka hizo ni pamoja na Mpango Elekezi wa Maendeleo wa

Muda Mrefu 2026/2027 - 2050/2051, Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027 – 2030/2031), Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/2027 na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/2027 - 2028/ 2029. Aidha, maswali ya msingi 146, maswali ya nyongeza 482 na maswali ya papo kwa papo saba yaliulizwa na Wabunge na kujibiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uchapaji wa nyaraka za Serikali, ili kuongeza ufanisi na utoaji huduma za uchapishaji wa nyaraka za Serikali, mikakati mbalimbali imetekelezwa. Mikakati hiyo ni pamoja na kuiongezea hadhi iliyokuwa Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kuwa Wakala.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko hayo yanaenda sambamba na kuimarisha wakala huo kwa kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa kiwanda cha uchapishaji, kununua na kufunga mashine mpya za uchapishaji. Vilevile, kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala na uzio ambao umefikia zaidi ya 78%.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ulinzi na usalama, mipaka ya nchi yetu ni suala muhimu katika kuhakikisha wananchi wanaendelea kufanya shughuli za uzalishaji mali bila bughudha. Pamoja na ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeshiriki katika ulinzi na usalama kikanda na Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jeshi letu lilishiriki katika operesheni mbalimbali za ulinzi wa amani kikanda na Kimataifa. Operesheni hizo ni pamoja na zile zinazoendeshwa na Umoja wa Mataifa na Jumuiya za Kikanda katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Afrika ya Kati, Lebanon na Sudan Kusini. Aidha, ushiriki katika operesheni hizo umeiwezesha nchi yetu kujenga uwezo, kuimarisha diplomasia ya ulinzi, uhusiano na kutimiza matakwa ya Umoja wa Mataifa na Jumuiya za Kikanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa kulinda usalama wa raia na mali zao, Serikali imeendelea kuimarisha vyombo vya usalama. Eneo mojawapo lililopewa kipaumbele ni

kulijengea uwezo Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kulipatia vifaa na kujenga vituo vipya vya zimamoto.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2025/2026 vifaa na mitambo ya kuzima moto yenye thamani ya dola za Marekani milioni 100 imenunuliwa na kusambazwa katika mikoa yote nchini. Aidha, imejenga vituo saba vya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika Mikoa ya Songwe, Simiyu, Katavi, Geita, Manyara, Njombe na Kagera.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa wazazi na walezi kuendelea kushirikiana kwa karibu na taasisi za elimu na dini kuimarisha malezi ya watoto na vijana kuhusu misingi imara ya maadili, uzalendo na matumizi sahihi ya teknolojia na utandawazi yatawawezesha watoto na vijana kufikia ndoto zao.

Mheshimiwa Spika, katika zama za sasa ambako dunia inakumbwa na changamoto za kiusalama, ni muhimu kwa wananchi wote, bila kujali itikadi, dini, siasa kulinda rasilimali za Taifa, kuongeza uzalendo, kupinga chuki, vitendo vyovyote vinavyoweza kuvuruga mshikamano wa Taifa letu. Hili ni jambo muhimu na ninaomba nilirudie.

Mheshimiwa Spika, katika zama za dunia ambapo dunia inakumbwa na changamoto za kiusalama ni muhimu kwa wananchi wote bila kujali itikadi za dini, siasa kulinda rasilimali za Taifa, kuongeza uzalendo, kupinga chuki na vitendo vyote vinavyoweza kuvuruga mshikamano wa Taifa. Jitihada hizo zitaepusha maadui wanaoweza kujipenyeza na kuhatarisha ulinzi na usalama wa Taifa letu pamoja na tamaa za rasilimali tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027 Serikali itaendelea kuimarisha ulinzi wa mipaka ya nchi yetu na usalama wa raia na mali zao. Aidha, itaendelea kuviimarisha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuvipatia zana, vifaa na rasilimaliwatu. Jambo la ulinzi wa nchi yetu na rasilimali zake siyo jambo la *option,* ni jambo la lazima.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kukuza fursa za ajira na ujuzi, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuratibu uzalishaji wa fursa za ajira nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na kubaini fursa kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hadi Februari, 2026, fursa za ajira 625,273 zilizalishwa. Kati ya ajira zilizozalishwa ajira 242,656 za wazawa zilitokana na vibali 12,549 vilivyotolewa kwa upande wa wageni.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Serikali imewezesha upatikanaji wa fursa za ajira 6,367 kwa Watanzania katika nchi za Saudia, Qatar, Oman na Umoja wa Falme za Kiarabu. Nchi nyingine ni pamoja na Bahrain, Denmark, Ujerumani, Kuwait, Poland, Bosnia, Sweden, Romania, Guyana, Marekani, Mauritius na Ireland. Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kisera kwa lengo la kukuza fursa za ajira jumuishi kwa vijana wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa masuala ya kazi na wafanyakazi, watumishi wa umma ni nguzo ya msingi katika utekelezaji wa sera, dira, mipango na mikakati ya Serikali. Kwa kutambua umuhimu wa watumishi wa umma, Serikali ya Awamu ya Sita baada ya kuingia madarakani, hadi Machi, 2026 imepandisha vyeo/madaraja jumla ya watumishi 600,602 kati ya 678,115 waliopo kwenye orodha ya wanaolipwa mishahara.

Mheshimiwa Spika, kadhalika, katika kipindi hicho Serikali imebadilisha kada/miundo kwa watumishi 42,515 kwa gharama ya shilingi bilioni 3.52. Vilevile, imelipa madai ya malimbikizo ya mishahara kwa watumishi 148,137 yenye jumla ya shilingi bilioni 248.52. Kadhalika, Serikali imeajiri watumishi wapya 155,008. Aidha, Serikali itaendelea kuajiri, kupandisha vyeo na madaraja, kuongeza mishahara na kuwaendeleza watumishi ndani ya utumishi wa umma kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, ninatambua viongozi wa vyama vya wafanyakazi akiwemo Rais wa Shirikisho la TUKTA, yuko nasi, wanatambua jinsi Mheshimiwa Rais ambavyo amekuwa na jicho la utu; na kauli mbiu yake ya utu akitekeleza kwa vitendo kwa kuwapatia haki wanazostahili watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mwenendo wa malipo ya mishahara unaonesha kuwa lipo kundi la watumishi wapatao zaidi ya 7,447 ambao wanalipwa mishahara binafsi isiyoendana na majukumu wanayofanya. Hadi tarehe 26 Machi, 2026 watumishi hao wamelipwa mishahara binafsi kwa gharama ya shilingi bilioni 14.34.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Serikali itafanyia kazi masuala yafuatayo: Mosi, kuwianisha mishahara ya watumishi wa umma pamoja na kupunguza tofauti kubwa ya viwango vya mishahara katika utumishi wa umma na sekta binafsi. Pili, kuhuisha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 na kanuni zake kuhusu idhini ya utoaji wa kibali cha mshahara binafsi. Tatu, kuhuisha waraka unaohusu watumishi watakaobadilishwa kazi ili kuendana na mahitaji ya sasa. Vilevile, kufanya mapitio ya waraka kuhusu utaratibu wa kushughulikia maombi ya mishahara binafsi kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, tumeelekeza Wizara ya Utumishi kushughulikia masuala hayo. Miaka takribani 15 mpaka 20 iliyopita yamejitokeza hayo ya mtu kuendelea kulipwa mshahara wa nafasi ambayo alishaondolewa. Tumekuwa na halmashauri 184, Wakurugenzi 800. Hili ni jambo ambalo halikubaliki. Ni lazima tubadilishe kama ni sheria, kama ni kanuni, ni lazima tubadilishe ili kuhakikisha kodi za Watanzania zinatumika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usalama mahali pa kazi, Serikali itaendelea kuhakikisha maeneo ya kazi yanakuwa na mifumo ya kudhibiti athari za vihatarishi ili kupunguza ajali, magonjwa na vifo vitokanavyo na kazi na kufanya kaguzi mbalimbali. Hadi Februari, 2026 kaguzi maalum 196,701 zimefanyika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuhakikisha maeneo ya kazi yanaendelea kuwa salama kwa wafanyakazi kwa kuendelea kusimamia sheria, kanuni na miongozo ya usalama mahali pa kazi. Vilevile, itaendelea kuimarisha uwezo wa wataalamu na kitaasisi katika kushughulikia masuala ya usalama na afya mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maendeleo ya vijana, sote tunatambua kuwa, vijana ni nguvukazi muhimu ya kujenga uchumi wa Taifa letu. Kutokana na ukweli huo, Serikali imeendelea kuhakikisha vijana wa Tanzania wanawezeshwa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha Wizara maalumu inayoshughulikia masuala ya vijana ili kuwapa sauti ya kuwasilisha mawazo yao ambayo yatajumuishwa kwenye mipango ya maendeleo, hasa katika utekelezaji wa Dira ya 2050.

Mheshimiwa Spika, katika kukuza majadiliano ya Kitaifa ya vijana, Serikali iliratibu kongamano la wajasiriamali na bodaboda lililofanyika tarehe 8 Januari, 2026 Jijini Dar es Salaam na kuwakutanisha washiriki zaidi ya 1,200. Kupitia kongamano hilo, vijana walipata fursa ya kuwasilisha changamoto zao na Serikali inaendelea kutafuta ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuratibu masuala ya maendeleo ya vijana, na taarifa za kina zitatolewa na Waziri wa Vijana atakapokuwa anawasilisha bajeti yake ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kinga ya jamii, ni ukweli usiopingika kuwa, huduma ya kinga ya jamii ni muhimu sana kwa mustakabali wa ustawi wa jamii yoyote. Ukweli huo ndiyo msingi wa hatua na mikakati yote inayotekelezwa na Serikali katika kuimarisha na kuratibu utekelezaji wa afua mbalimbali za Kinga ya Jamii hapa nchini. Moja ya mikakati hiyo ni pamoja na Sera ya Taifa ya Kinga ya Jamii ya Mwaka 2023 ambayo ilizinduliwa rasmi tarehe 9 Februari, 2026.

Mheshimiwa Spika, ili kupanua wigo wa kinga ya jamii kwa wananchi wanaojiajiri katika sekta isiyo rasmi, Serikali imezindua mpango maalumu wa wananchi wanaojiajiri. Mpango huo uitwao *Hifadhi Scheme* unatarajiwa kuwafikia mamilioni ya Watanzania walio nje ya mfumo rasmi wa pensheni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuboresha huduma za kinga ya jamii nchini. Vilevile, itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya usajili wa wanachama wapya.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, Serikali imeendelea kuimarisha uratibu na utendaji wa mifuko na programu za uwezeshaji 75 zinazomilikiwa na Serikali na sekta binafsi. Hadi Januari, 2026, mifuko na programu za uwezeshaji zimetoa mikopo na dhamana zenye thamani ya shilingi trilioni 1.69 kwa wanufaika 422,921. Mifuko na programu hizo pia zimetoa ruzuku yenye thamani ya shilingi bilioni 598.72 kwa wanufaika 6,454,580.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mikopo ya 10% ya mapato ya ndani ya halmashauri, hadi Februari, 2026 shilingi bilioni 130.42 zimekopeshwa kwa vikundi 12,997 vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Aidha, Serikali imeimarisha usimamizi wa mikopo hiyo na hivyo kuwezesha kiasi cha shilingi bilioni 49.11 kurejeshwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuratibu ushiriki wa Watanzania katika fursa na shughuli za kiuchumi zinazotekelezwa katika miradi ya kimkakati na uwekezaji. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Januari, 2026 jumla ya kampuni 389 za makundi maalum kati ya kampuni 166,477 zimepata zabuni.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kufanya mapitio kwa lengo la kuboresha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2023 na Sheria ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya Mwaka 2023. Hatua hiyo itawezesha kuongeza idadi ya Watanzania wanaonufaika na uwekezaji wa miradi ya kimkakati; na vilevile itakamilisha maandalizi ya kunusuru kaya maskini ili kutambua walengwa wanaotakiwa kunufaika na fursa hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapambano dhidi ya rushwa, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati ya Kitaifa ya kupambana na rushwa kwa kuweka mkazo kwenye kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi. Aidha, imeendelea kufanya uchunguzi ili kudhibiti vitendo vya rushwa.

Kutokana na jitihada hizo, kiasi cha shilingi bilioni 60.231 zimeokolewa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 60.038 zilirejeshwa Serikalini na shilingi milioni 192.88 zilirejeshwa kwenye miradi, huduma na wananchi waliodhulumiwa. Matokeo ya juhudi hizo yameleta nidhamu, uadilifu na uwajibikaji katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matokeo hayo mazuri, kwa mara nyingine ninaelekeza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kuweka mikakati ya kuzuia vitendo vya rushwa badala ya kusubiri vitendo hivyo kusababisha madhara. Wahenga walisema tahadhari kabla ya hatari, wakiweka msisitizo wa kuzuia badala ya kusubiri athari zitokee.

Mheshimiwa Spika, licha ya kuendelea kutekeleza kikamilifu suala la usimamizi wa tamko la rasilimali na madeni kwa viongozi wa umma, baadhi ya maeneo yana mianya mingi inayoleta ukosefu wa maadili. Maeneo hayo ni pamoja na ununuzi wa umma, makusanyo ya mapato, makadirio ya kodi, mikataba, utoaji wa leseni za madini, sekta ya ardhi, Wajumbe wa zabuni, ukaguzi na udhibiti.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya watumishi katika maeneo hayo hawawajibiki na sheria ya maadili. Kwa mara nyingine, wao wanajaza ahadi ya uadilifu; wanajaza fomu ya uadilifu. Hatuchukii watu kutajirika, lakini kwa sababu ya mianya hii ndiyo maana unaona watu wengine wanafanya kazi mpaka wanazeeka maisha yao yapo vilevile, wengine hata *probation* hawajamaliza wanamea kwa sababu hawalazimiki kujaza walicho nacho. Kama ni urithi, huwa wanapata urithi tu pale ambapo wanaanza kukusanya mapato ya Serikali?

Mheshimiwa Spika, tumesema, baadhi ya watumishi wa maeneo hayo hawawajibiki na sheria ya maadili. Hivyo, nimewaelekeza Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ifanye marekebisho ya sheria na kanuni ili kujumuisha watumishi hao kujaza fomu na matamko ya rasilimali na madeni ili kuweza kufuatilia mienendo ya watumishi wote wanaofanya kazi kwenye maeneo ambayo yanakithiri kwenye vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa. Ni ukweli usiopingika, ukichukuwa Diwani na Mbunge pamoja na baadhi ya viongozi wengine, awe Naibu Waziri au nani, hayupo *exposed* kwenye maeneo ya rushwa kama yule aliyeko kwenye manunuzi ya umma, makusanyo ya mapato, makadirio ya kodi, mikataba mbalimbali, leseni za madini, sekta ya ardhi, Wajumbe wa Zabuni pamoja na maeneo mengine yote yanayogombaniwa na wale wanaotafuta maslahi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kupeleka fomu hii kwa Mbunge, Diwani, Naibu Waziri sijui nani huko, wenye vyeo vya kisiasa ni kupotosha ukweli kwamba yapo maeneo ambayo watu wanapiga rushwa; na hayo maeneo ndiyo yanatakiwa yapelekewe rangi ya hatari ya fomu ya kujaza.

Mheshimiwa Spika, haya mambo lazima tuyaendee na macho makavu kama yalivyo. Ninajua ni mambo yanayochukiza, lakini ni lazima wawepo watu wa ku-*sacrifice* kwa ajili ya nchi. Ni lazima haya yafanyike ili kuweza kuthibiti mianya hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa kwa kuziwezesha taasisi za utawala bora, maadili na uwajibikaji kutekeleza majukumu yao. Vilevile, itaendelea kuimarisha mifumo ya kisheria na kitaasisi ili kuongeza ufanisi kwenye kukabiliana na rushwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais amelitekeleza hilo kwa vitendo. Mimi niwatoe hofu Watanzania kwamba wanapoona masuala haya yanajitokeza, ni kwa sababu Mheshimiwa Rais ameimarisha utendaji kazi wa kitaasisi, sio kila mwananchi angeweza kugundua sehemu ipo rushwa, sio kila mwananchi angeweza kugundua mradi ulipotekelezwa chini ya kiwango, sio kila Mtanzania angeweza kugundua sehemu fedha zimeibiwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameziongezea taasisi zetu hizi za ukaguzi fedha na meno na akazifanya zikague miradi

ilhali miradi ikiwa inaendelea ili zile taasisi nyingine za kisheria ziweze kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha juhudi za kukabiliana na dawa za kulevya kupitia mikakati mbalimbali. Mikakati hiyo inalenga kupunguza upatikanaji, uhitaji, madhara na matumizi ya dawa za kulevya. Vilevile, imeendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na Kimataifa katika kukabiliana na dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, kupitia utekelezaji wa mikakati hiyo, Serikali imefanikiwa kukamata kilogramu 360,479.9 za aina mbalimbali za dawa za kulevya zilizohusisha watuhumiwa 5,776. Dawa zilizokamatwa ni pamoja na bangi, mirungi, skanka, *heroin*, *cocaine*, dawa tiba zenye asili ya kulevya na kemikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha juhudi za kukabiliana na dawa za kulevya na ushirikiano wa kikanda na Kimataifa katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Undani wa taarifa hii upo katika aya ya 240 hadi aya ya 245. Niwapongeze sana wenzetu wa TAKUKURU pamoja na wenzetu wa madawa ya kulevya kwa kazi kubwa ambayo wameifanya.

Mheshimiwa Spika, katika uratibu wa maafa, Serikali imeanzisha mfumo wa kidijitali wa mawasiliano *'Call Centre'* katika Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura. Mfumo huo unawawezesha wananchi kupiga simu bure kupitia namba 190 kwa ajili ya kutoa taarifa za matukio ya maafa.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeandaa Mfumo wa Ramani za Vihatarishi vya Majanga yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa za maeneo hatarishi kwa majanga. Katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa maafa ili kuongeza ustahimilivu wa jamii dhidi ya majanga kwa kuandaa na kutekeleza mipango na mikakati ya kupunguza vihatarishi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mamlaka zetu za ukaguzi, uthibiti na uchunguzi kama nilivyotoka kusema, upande

wa TAKUKURU na uthibiti wa madawa ya kulevya, ili kuhakikisha uadilifu katika matumizi ya rasilimali za umma, Serikali chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuimarisha mifumo ya ukaguzi na usimamizi. Lengo lake hapa ni kutibiti upotevu wa rasilimali za umma, kodi za Watanzania. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuziwezesha taasisi zetu za udhibiti, ukaguzi na uchunguzi kwa kufanya mabadiliko katika sheria.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alielekeza sheria zibadilishwe ili watu wanapobainika wafikishwe Mahakamani. Juzi mmeona katika taarifa hizi, wapo ambao walishafikishwa Mahakamani na Serikali ikashinda.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais aliongeza pia bajeti, rasilimali watu na vitendea kazi. Hatua hizo zimewezesha taasisi zetu za udhibiti kutekeleza kikamilifu majukumu yao na kuwasilisha taarifa kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kila ifikapo tarehe 31 ama kabla ya tarehe 31.

Mheshimiwa Spika, kaguzi zilizofanyika zimewezesha kubaini upungufu katika usimamizi wa matumizi ya rasilimali za Serikali na kujua thamani ya fedha kwenye miradi ya maendeleo. Vilevile zimewezesha kuimarisha uwajibikaji, kuimarisha taasisi na uwazi katika matumizi, ufuatiliaji na kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imepokea hoja na mapendekezo yaliyoainishwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, na Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma kwa ajili ya kuzifanyia kazi kama ambavyo Mheshimiwa Rais alisema katika hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itawasilisha taarifa ile kama ilivyopangwa ya *CAG* na itafanyia kazi hoja zilizojitokeza. Aidha, nimewaelekeza Maafisa Masuuli wote, taasisi zote za umma kujibu hoja hizo na kufanyia kazi mapendekezo kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwajuza Watanzania kwamba taarifa kama ile ikitolewa, kunakuwepo na hoja za

kikaguzi, hoja za kiuhasibu ambazo zinatakiwa kujibiwa. Pia kunakuwepo na hoja za kichunguzi ambazo zinabainisha wizi. Yale yaliyo na hoja za kiuhasibu nimewaelekeza Maafisa Masuuli waweze kujibu na yale ambayo yana hoja za kikaguzi zilizobaini wizi kama Mheshimiwa Rais alivyowaelekeza, taasisi zinazohusika za kisheria zitaendelea kuchukua hatua za kisheria na hatua za kinidhamu kwa wale wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ambayo ukaguzi umebaini wizi wa fedha za umma, mali za umma, ama hujuma yoyote, nimewaelekeza vyombo vinavyohusika kama Mheshimiwa Rais alivyoelekeza na mamlaka za kinidhamu zinazohusika kuchukua hatua zinazostahili za kinidhamu, za kiutumishi na za kisheria.

Mheshimiwa Spika, kwenye maeneo ambayo hoja zake ni za kiuhasibu, Bunge lako ndilo linalotunga sheria na sisi Serikali tunaheshimu sheria. Yale yanayohusisha hoja za kiuhasibu tunawapa nafasi Maafisa Masuuli kujibu hoja hizo.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo ni hoja za kiuhasibu ambazo ni upotevu ama upungufu wa nyaraka, ni utaratibu wa utawala wa sheria kuweza kutoa fursa ya kujibu hoja hizo. Kwa yale ambayo Mheshimiwa Rais alielekeza kuanza kufanyika *Real Time Audit* kukagua miradi, ingali inaendelea kutekelezwa, na ukifanyika ukaguzi wa kichunguzi na pakabainisha upotevu wa mali za umma, hatua za kisheria kwa yeyote aliyehusika zitachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo faida halisi iliyotarajiwa na Mheshimiwa Rais ya kumwongezea meno CAG akague miradi ili aweze kubaini maeneo yanayohitaji kuchukuliwa hatua. Hilo ndiyo lengo halisi ili yaweze kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, kwa Serikali isiyojali uadilifu, jambo la kwanza ambalo ingefanya huwenda isingekuwa na taasisi za kukagua au ingefanya taasisi za kukagua ziwe dhaifu (inakagua halmashauri moja, haikagui miradi mikubwa, haina nyenzo wezeshi wala fedha, halafu na taarifa inaminywa haitoi uhalisia).

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa kiongozi wa nchi anayejali uadilifu, Mheshimiwa Rais yeye mwenyewe kwa kauli yake alimwambia *CAG,* "unapokagua usipepese macho." "Usipepese macho!" Alimwambia, "nenda kakague na utoe hali halisi, ili vyombo vya sheria viweze kuchukua hatua."

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa hatua hizo za kuzifanya taasisi zitimize majukumu yao na kuzielekeza taasisi za kisheria kuchukua hatua. Huo ndiyo uongozi unaozingatia utawala bora, kufanya kazi kwa taasisi na kuimarisha taasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati ya kuhakikisha masuala yote yanayohusiana na uwazi kwenye matumizi ya rasilimali za umma yanazingatiwa. Niliwaelekeza makatibu tawala wote wa mikoa, wanapotuma fedha kwenye wilaya, wapeleke nakala ya fedha zilizotumwa kwenye wilaya kila ofisi ya Mbunge, na Wabunge wajue fedha zilizofika katika majimbo yao. Miradi ya maendeleo siyo siri, na wala fedha za maendeleo siyo siri, ili tuimarishe uwazi na kutambua thamani ya fedha kwenye miradi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utaratibu wa kuratibu malalamiko ya wananchi, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati ya kuhakikisha malalamiko yanapatiwa ufumbuzi kwa wakati. Mikakati hiyo ni pamoja na kuboresha mifumo ya e-Mrejesho na kuanzisha kituo cha kitaifa cha mawasiliano ya simu, ili kuwezesha wananchi kuwasilisha kero, kupata ufumbuzi na kutoa mrejesho kuhusu masuala mbalimbali kupitia namba 190 na barua pepe mamlaka@pmo.go.tz Tunataka kila ngazi iwajibike na kutatua kero.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na vikao kazi vingi na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, tumekubaliana hayo. Kituo hicho kitafanya kazi kama ngazi ya rufaa kwa maeneo ambapo wananchi watakuwa hawajasikilizwa. Hii itaimarisha uwajibikaji wa ushughulikiaji wa kero, malalamiko na mrejesho kutoka kwa wananchi. Kila Wizara wameanzisha jambo la aina hiyo la e-Mrejesho ili kuweza kuhakikisha mambo yanayohusu Wizara za kisekta na yenyewe yanatatuliwa katika sekta hizo.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa watumishi wa Serikali hususan Wizara za Kisekta, Taasisi, Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuimarisha mifumo ya kushughulikia kero za wananachi, ikiwa ni pamoja na kuweka utaratibu wa kuwatembelea, kuwasikiliza na kuandaa majedwali, taarifa na kuonesha namna walivyoshughulikia kero hizo.

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe nimefanya hizo ziara. Nitakapomaliza mikoa yote, nitarudi kupitia kero moja moja kwenye kila mkoa, na kwa kweli wale ambao watakuwa hawajashughulikia hizo kero, watakuwa wamejipotezea nafasi ya kukaa kwenye ofisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia mikakati ya mipango ya kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa mazingira, pamoja na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Hatua hizo zinajumuisha kupunguza matumizi ya kuni na mkaa, kuimarisha upandaji miti, kuendeleza uwekezaji katika biashara ya *carbon* na kusimamia utekelezaji wa mikakati ya kikanda. Undani wa maelezo hayo upo aya ya 260 hadi 264 katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Mji wa Serikali umeendelea ambapo Ofisi za Serikali katika Mji wa Serikali pale Mtumba, hadi kufikia 2026 majengo 15 yameanza kutumika na ujenzi wa majengo hayo mengine 14 unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Muungano Serikali imeendelea kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha Muungano kwa manufaa ya wananchi wa pande zote. Katika mwaka 2025/2026 Serikali imeendelea kuimarisha utaratibu wa masuala ya Muungano na yale yasiyo ya Muungano kushughulikiwa na Wizara zinazohusika ili kuweza kuhakikisha tatizo hilo katika baadhi ya maeneo yanaisha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ushirikiano wa kikanda, Serikali imeendelea kutekeleza sera ya mambo ya nje ambayo imekuwa chanzo cha kuchochea maendeleo na kuimarisha diplomasia ya Kimataifa na diplomasia ya kiuchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ushirikiano wa Kimataifa, Tanzania imeendelea kuimarisha ushiriki wake kwenye majukwaa ya Kimataifa, pamoja na kuratibu ushiriki katika mikutano ya ngazi za juu katika maeneo mbalimbali duniani. Mikutano hiyo imekuwa ni pamoja na Mkutano wa Pili wa Wakuu wa Nchi ambao ulifanyika kule Addis Ababa, Ethiopia ambapo ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa Tanzania kwenye mikutano ya kikanda na Kimataifa umeiwezesha nchi yetu kuielezea misimamo yake kwenye masuala mbalimbali yenye maslahi Kimataifa. Aidha, Serikali itatumia majukwaa hayo kutangaza mazingira wezeshi ya fursa za kibiashara na uwekezaji pamoja na masuala ya utalii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa michezo Tanzania imeendelea na maandalizi ya kuwa mwenyeji katika mashindano ya *AFCON* 2027. Maandalizi hayo yanahusisha ujenzi na ukarabati wa viwanja pamoja na miundombinu wezeshi, ikiwemo ujenzi wa uwanja wa Arusha na Dodoma ambapo uwanja wa Arusha umeshafikia 75%. Ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa ambao umeshafikia 95%, ujenzi wa Uwanja wa Dodoma umeshafikia 10%.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imekamilisha ujenzi na ukarabati wa viwanja vya Meja Jenerali Isamuhyo, *Gymkhana Club* na Shule ya Sheria ya Tanzania kwa ajili ya mazoezi. Aidha, Serikali itaendelea na ujenzi wa Viwanja vya *Farasi, Gymkhana* Annex na *Leaders Club.*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia fursa hii pia kulipongeza Shirikisho la Michezo la Mpira wa Miguu la Tanzania na uongozi wake chini ya Rais Karia, kwa uongozi, uratibu na usimamizi mzuri wa mchezo huo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, niwapongeze Wizara chini ya Mheshimiwa Waziri Paul Christian Makonda na timu yote ya Wizara. Kupitia uongozi huo kwa mara ya kwanza Tanzania

imefanikiwa kuingiza vilabu vinne pamoja katika hatua ya makundi ya mashindano ya Klabu Bingwa Barani Afrika. Vilevile, Timu ya Taifa imeweza kucheza 16 bora ambapo ni hatua ambayo ni ya mfano kwa ukanda wa kwetu na nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilabu vilivyoingia Klabu Bingwa na Shirikisho Barani Afrika ni pamoja na Klabu ya Michezo ya Yanga, timu ya wananchi; Klabu ya Michezo ya Simba, wenyenchi; Klabu ya Michezo ya Azam, wanalambalamba; na Klabu ya Michezo ya Singida, wanakilemankundi. Ni dhahiri kuwa mafanikio katika michezo ya mpira wa miguu, ni chachu ya kuchochea hamasa katika nyanja za michezo hapa nchini na Afrika.

Mheshimiwa Spika, nizipongeze Klabu za Simba na Yanga kwa mafanikio makubwa ambayo zimefikia kuchora ramani ya mpira hapa nchini. Katika mwaka 2026/2027 ni dhahiri kwamba mafanikio katika michezo ya mpira wa miguu na michezo mingine kwa ujumla ni matokeo ya uwekezaji na hamasa iliyotolewa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mafanikio hayo siyo tu yanaleta burudani kwa mashabiki, bali yanatoa fursa ya ajira na uwekezaji kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alipoweka goli la Mama, ilichochea ushindani na hamasa kwa vilabu vyetu kupambana. Siku hizi timu zote barani Afrika, ikiwemo kanda ya Kaskazini na Magharibi ambazo zilikuwa tishio kwenye Soka la Afrika, zinapokuja Tanzania zinajiuliza mara mbili mbili kama zitatoka salama. Hiyo ni kutokana na kukua kwa soka la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kusimamia na kuratibu ushiriki wa Tanzania katika michezo ya Kimataifa na maandalizi ya *AFCON* 2027 ili kuacha urithi endelevu wa michezo, ajira, utalii na heshima kwa Taifa. Aidha, itaendelea kusimamia ushiriki wa wanafunzi katika michezo ili kuweza kuibua vipaji.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza wawekezaji waliofanya uwekezaji mkubwa katika michezo *GSM* kwa upande wa Klabu ya Yanga, Mzee Bakhresa kwa Azam ambaye ameutambulisha

mpira wa Tanzania, Mohammed Dewji kwa upande wa Simba na vilabu vya taasisi ambavyo na vyenyewe vimeendelea kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapoelekea kumaliza, nijielekeze katika maeneo machache yenye msisitizo. Mosi, kuanza utekelezaji wa Dira ya 2050 kupitia mpango na bajeti iliyoandaliwa. Kila sekta ihakikishe rasilimali za Taifa zinaelekezwa katika maeneo yenye tija na matokeo makubwa ili kupunguza utegemezi kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kama unavyoona dunia inachafuka, ni lazima tujipange kuitekeleza dira hii kwa kutumia rasilimali zetu. Vilevile tuendelee kushirikisha sekta binafsi na wadau wa maendeleo katika kuhakikisha utekelezaji wa Dira ya 2050 ili kujenga uchumi jumuishi, shindani unaotegemea uzalishaji wenye tija, megeuzi ya kiuchumi na kutengeneza ajira. Wakuu wa Mikoa wasimamie kikamilifu maandalizi ya mapokezi ya wanafunzi wa elimu ya msingi ya lazima kwa miaka kumi watakaojiunga kidato cha kwanza mwaka 2028.

Mheshimiwa Spika, tunaposema elimu ya lazima kwa miaka 10, kimsingi tunasema tulikuwa na sekondari kila kata, sasa tunaongelea kuwa na sekondari kila Kijiji. Ni lazima tujiandae kwa miundombinu pamoja na maoteo ya mahitaji yote ya kutekeleza mpango huu.

Mheshimiwa Spika, tatu, tuendelee kuimarisha usimamizi wa makusanyo ya mapato kwa kutumia mifumo ya kielektroniki na mashine za *POS* kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, kuziba mianya ya ufujaji wa fedha za umma na kuendelea na rasilimali fedha katika miradi ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana ndani ya Serikali kupunguza safari za nje, kupunguza makongamano, warsha, lakini pia na mikutano mingine tutaendelea kuifanya kwa njia ya mtandao, ili fedha nyingi tuzielekeze kwenye hii miundombinu tunayosema. Tuna mwaka mmoja tu wa kwenda kwenye utekelezaji wa mpango huo.

Mheshimiwa Spika, unakumbuka kabla ya hapa wanafunzi walikuwa wanasubiri chaguo la pili *(Second Selection),* wamefaulu, lakini wanasubiri madarasa. Hatutaki turudi huko Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alishatuvusha, tunataka madarasa yaendelee kusubiri wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii habari ya *second selection* na wanafunzi kusubiri madarasa kwamba wamechaguliwa, lakini wasubiri madarasa; ukienda kule kwetu Usukumani wakati wanasubiri madarasa, unakuta wameshachaguliwa kwenye shughuli nyingine *(chagulaga maayo)* wanachaguliwa kwenye maeneo mengine na kuwakosesha fursa hasa watoto wa kike kwenda shule. Pia, watoto wa kiume unakuta wameshaenda kambini kuchunga. Kwa hiyo, ndiyo shule inakuwa imeishia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tano, Wizara na taasisi na mamlaka zinazoshiriki katika uwezeshaji wananchi kiuchumi, ziweke malengo yanayopimika, viashiria vya utendaji na ratiba za utekelezaji ili kuhakikisha mitaji hiyo inazalisha ajira, kipato na biashara endelevu kwa vijana wetu, wanawake na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, pia, nimeelekeza wakandarasi wote wanaotekeleza miradi ya Serikali, watimize wajibu wao kwa mujibu wa mikataba wanayoingia ikiwa ni pamoja na kutekeleza miradi inayoendana na thamani ya fedha wanazokuwa wamepokea, na pia kuwalipa watoahuduma wanaoshirikiana nao katika utekelezaji wa miradi husika. Vivyo hivyo kwa wakandarasi wanotoka nje ya nchi, kuwalipa wakandarasi wazawa pale wanapokuwa wamepokea fedha.

Mheshimiwa Spika, wakandarasi wanaotoka nje ya nchi, wao wakicheleweshewa malipo, huitoza riba Serikali na nchi yetu, lakini wao huwacheleweshea wakandarasi wazawa kuwalipa fedha hizo ilhali Serikali ikiwa imeshalipa fedha za miradi hiyo. Hili ni jambo lisilokubalika na tutaanza kuwatoa kwenye orodha ya watu wanaoweza kutekeleza miradi ndani ya nchi, wakiendelea kukiuka masharti hayo.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Mikoa ndani ya miezi sita baada ya kuanza kutekeleza bajeti hii, washughulikie masuala yanayohusu matundu ya vyoo, kwa kuwianisha na mahitaji ya wanafunzi. Tumesema hili ni jambo lisilokubalika kuwa na wanafunzi wamekusanyika maeneo mengi na huku tukijua kabisa katika eneo hilo hakuna vyoo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji ihakikishe huduma za maji zinapatikana katika maeneo ya muhimu ya taasisi zetu kama shule; Vituo vya Afya; Zahanati; Hospitali na hivyo hivyo na kwa Wizara ya Nishati na Taasisi zetu za Dini. Tumesema tuna vitendea kazi vya kuchimba visima. Hakuna ulazima kila maeneo wanafunzi kuwa wanatembea na vidumu kiunoni kwa ajili ya kubeba maji.

Mheshimiwa Spika, nane, ubora wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika sekta mbalimbali nchini uwiane na thamani ya halisi ya fedha. Fedha zinazotolewa na Serikali kwenye miradi hiyo zitumike kama zilivyokuwa zimekusudiwa. Wakandarasi wetu wawe wazalendo, watumie ipasavyo fursa hizo za kutekeleza miradi hiyo ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tumesema tuendelee kujenga uwezo wa Wakandarasi Wazawa ili kuweza kujenga uchumi wa ndani ya nchi. Kuna Kampuni zimekuja hapa zikiwa changa kabisa kutoka nje; changa kuliko kampuni za Tanzania, zimekuja kukua kwa kutumia fedha zetu. Tukuze taasisi zetu ili kuweza kukuza ajira na uchumi wa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara za Kisekta, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha zinalipa fidia wananchi wanaopisha maeneo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kabla ya kutwaliwa kwa maeneo hayo kwa kuzingatia taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo, mnakuta mwananchi mnyonge, mwananchi wa kawaida ametoa eneo limejenga kituo cha afya, limejenga shule na anachodai ni kidogo tu miaka yote anaendelea kudai hajalipwa. Mheshimiwa Rais alishaelekeza, pamoja na kwamba tunataka miradi ya maendeleo, na tunataka uwekezaji, tusipore maeneo ya wananchi kwa vigezo hivyo bila kuwalipa fidia.

Mheshimiwa Spika, Taasisi zote za Umma ziimarishe ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali ikiwemo mipango, programu, miradi na kuongeza tija. Wenzetu wanaohusika na ufuatiliaji wasikae ofisini. Tunataka kazi ya ufuatiliaji ifanyike ili tujue tumetimiza lengo kwa kiwango gani?

Mheshimiwa Spika, kumi, Wizara, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi, Wakala na Idara zinazojitegemea kuanza kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Rais ya Kutathmini Maboresho ya Mifumo ya Kodi kama alivyoelekeza Mheshimiwa Rais alielekeza na taarifa za Tume nyingine ambazo zimekwisha kupokelewa.

Mheshimiwa Spika, ninapomalizia, nimpongeze Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutekeleza vema wajibu wake wa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuliongoza Taifa letu. Ninamtakia afya njema na nguvu katika kutekeleza majukumu yake ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika, ninatoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuiongoza vema Zanzibar na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Baraza la Mapinduzi. Hakika uongozi wake thabiti na mapinduzi makubwa ya kiuchumi anayoyafanya yameonesha nia yake ya dhati ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2025 kwa vitendo. Hakika mkasi unaongea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kukupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Musa Azzan Zungu na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kazi kubwa na nzuri ya kuliongoza Bunge letu. Ninawaombea kila la heri kwa Mungu katika kuongoza mijadala hii yote ya Bunge letu Tukufu. Sote tunajua jinsi ambavyo mmefanya kazi nzuri na ya kutukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza pia Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Jimbo la Songea; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI chini ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Johannes Lembulung Lukumay, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi; na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Chakoma Mchafu, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Jimbo la Maswa Magharibi; na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo Mbunge wa Jimbo la Missenyi.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati hizo umesaidia kuboresha Makadirio ya Mapato na matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge kwa Mwaka 2026/2027. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, ninawapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu ambayo mmekuwa mkiitoa katika kuboresha na kutekeleza shughuli za Serikali katika uwakilishi wenu kwa wananchi. Hakika wananchi wamechagua Wabunge machachari, Wabunge wanaojali maslahi ya majimbo yao na Wabunge wanaowajali wananchi waliowachagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huu, niwapongeze pia Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kuwa Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge pamoja na Wawakilishi wa Nchi yetu katika Taasisi nyingine za Kikanda: Jukwaa la Bunge la Afrika; Jukwaa la Bunge la *SADC*; Umoja wa Mabunge Duniani; Jukwaa la Kibunge la Nchi zinazozunguka Ukanda wa Maziwa Makuu. Ninawatakia kila la heri katika kutimiza majukumu yenu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 07 Machi, 2026, Mheshimiwa Balozi Stephen Patrick Mbundi aliteuliwa kuwa Katibu

Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kabla ya uteuzi wake, Mheshimiwa Balozi Mbundi alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayesimamia masuala ya Afrika Mashariki. Kipekee ninampongeza Balozi Mbundi kwa uteuzi, na ninamtakia kila la heri katika majukumu hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia, Mheshimiwa Dkt. Lazaro Bunungu Komba, kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Peramiho kuwa mwakilishi wao katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kipekee niwapongeze Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kutokea Baraza la Wawakilishi na kuingia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 66(1)(C) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Mheshimiwa Fatma Ramadhan Mohamed, Mheshimiwa Mariam Said Khamis, Mheshimiwa Said Ali Mbarouk, Mheshimiwa Shaame Ali Ali, Mheshimiwa Simai Mohammed Said, *me for you*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa maeneo haya wamepata wawakilishi katika Bunge letu Tukufu, tunawapongeza na kuwatakia kila la heri katika kutimiza majukumu yenu hayo ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri walioko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Waheshimiwa Mawaziri wote, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu ambao wamekuwa nasi, Makatibu Tawala, Wakuu wetu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Mashirika, Wakala na Idara Zinazojitegemea kwa ushirikiano mkubwa ambao wanatupatia.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Hamza Saidi Johari Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ushauri wake wakati wote. Mtakubaliana nami Mheshimiwa Hamza Johari amekuwa hana muda mahsusi wa kufanya kazi. Masaa yote, *weekend*, sikukuu yote ni siku za kazi kwake, kama kuna jambo la Kitaifa,

ambalo linahitaji uangalizi wake. Mheshimiwa *AG* ninakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia, kumpongeza Balozi Dkt. Moses Mpogole Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi, kwa ushirikiano na kazi anazozifanya za utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Kipekee ninamshukuru ndugu Baraka Ildephonce Leonard, Katibu wa Bunge kwa uratibu wa shughuli za Bunge ambazo anazifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa George Mcheche Masaju, Jaji Mkuu wa Tanzania pamoja na watendaji wote wa Muhimili wa Mahakama kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia na kuimarisha mifumo ya utoaji wa haki. Jitihada zao zimekuwa chachu ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kuhakikisha haki inapatikana kwa Watanzania na siyo tu kupatikana na inaonekana imetendeka.

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa dhati, ninapenda kutumia fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya ya kulinda Taifa letu. Vilevile, niwapongeze maafisa na askari wote, majeshi yetu, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, wanafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha tunadumisha amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tunapolala na tunaamka salama, baada ya Mungu wanaotuhakikishia kwamba kuna usalama, kuna amani inatuzunguka katika maeneo yetu ni wale wanaofanya kazi usiku na mchana sisi tukiwa tumelala. Wakati wote wamekuwa wakitekeleza majukumu yao kwa ubunifu, uzalendo, utii, ujasiri na weledi. Hakika tunatambua na kuthamini mchango wao na kazi yao katika ujenzi wa nchi yetu na tunawashukuru kwa moyo huo wa kizalendo na uwajibikaji kwa Taifa lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru viongozi na watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Ninaomba niwataje wachache tu kwa niaba ya wengi waliofanya kazi katika utendaji wangu wa kazi za kila siku. Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela na Waziri

wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Mahusiano); Mheshimiwa Prof. Riziki Silas Shemdoe, Mbunge wa Lushoto na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI); na tuendelee kumkumbuka Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi ambaye naye tumefanya naye kazi, na alifanya kazi katika Ofisi ya Waziri Mkuu ziwe nyepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika, nawashukuru Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu); Mheshimiwa Rahma Riyadh Kisuo, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Mahusiano); Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI (Elimu) na Mheshimiwa Dkt. Jafar Rajab Seif, Mbunge wa Busanda na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, (Afya) kwa kuendelea kufanya kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, ninawashukuru Makatibu Wakuu Dkt. Jim James Yonazi (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu); Bi. Mary Ngelela Maganga (Kazi, Ajira na Mahusiano); Bw. Adolf Hyasinth Ndunguru (TAMISEMI); Naibu Makatibu Wakuu Dkt. James Henry Kilabuko (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu); Bi. Zuhura Yunus Abdallah (Kazi, Ajira na Mahusiano); Mhandisi Rogatius Hussein Mativila (TAMISEMI - Miundombinu); Bw. Sospeter Mambile Mtwale (TAMISEMI); Bw. Atupele Webster Mwambene (TAMISEMI - Elimu); na Profesa Tumaini Joseph Nagu (TAMISEMI - Afya).

Mheshimiwa Spika, pia ninawapongeza Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu pamoja na Wafanyakazi wote kwa ushirikiano wanaofanya. Wanafanya kazi kubwa hata wasipopata pongezi nyingi, wajue aliyepika huwa hapewi *tip* ya chakula kizuri ila anayetenga ndiyo huwa anapewa *tip* kwamba chakula hicho kilikuwa kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ninawashukuru watumishi wa umma kwa kazi kubwa wanayoifanya na sekta binafsi. Kama nilivyosema, leo tuko na viongozi wa wafanyakazi ambao

tumekuwanao, tunawapongeza sana kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba michango yao ni mikubwa katika kuleta ufanisi wa utekelezaji wenye tija kwa shughuli za Serikali na utekelezaji wa maendeleo wa Taifa. Dira ya Maendeleo ya Taifa, unategemea sekta ya umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuwashukuru washirika wa maendeleo zikiwemo nchi rafiki, taasisi na mashirika ya Kitaifa, kikanda na Kimataifa, madhehebu ya dini na mashirika yasiyo ya kiserikali, kwa kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita katika kujenga uchumi na kuleta maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kipekee nitoe shukrani za dhati kwa Sekta Binafsi kwa kuendelea kuwa mshirika mkuu wa Serikali katika kuiletea nchi yetu maendeleo. Ushirika wao umekuwa chachu ya kuchochea ukuaji wa uchumi na kuzalisha fursa za ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa rai kwa watendaji wote wa Serikali kuheshimu Sekta Binafsi kama mnavyoheshimu Sekta ya Umma, kwa sababu huyu ni mdau na mbia mkubwa wa maendeleo, mshirika mkubwa katika kutekeleza shughuli za maendeleo na mshirika mkubwa katika kufikia malengo ya Dira ya 2050.

Mheshimiwa Spika, watendaji wote Serikalini wawe wawezeshi wa Sekta Binafsi badala ya udhibiti wa Sekta Binafsi. Tuwezeshe Sekta Binafsi itusaidie kutimiza malengo haya yaliyobainishwa katika Dira yetu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii adhimu kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa kuendelea kushirikiana nami na kuniunga mkono katika kipindi chote cha kutekeleza majukumu ya Serikali. Hali hii inaonesha ni kwa namna gani wamekuwa wastahimilivu na waungwana kwa Serikali yao kwa kuruhusu nitumikie majukumu ya Kitaifa ilhali wao

wakiniwakilisha huko jimboni katika kuleta maendeleo ya wana-Iramba, *Songele zigi zigi*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru pia wananchi wote kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Imani na ushirikiano wao kwa Mheshimiwa Rais imekuwa chachu ya mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuleta maendeleo kwa wananchi. Wananchi mmefanya kazi kubwa ya kuiunga mkono Serikali katika kutekeleza majukumu haya ambayo Serikali imefanikisha.

Mheshimiwa Spika, wapo wananchi wametoa maeneo yao kujenga miradi ya maendeleo, wapo waliopisha miradi ya maendeleo, wapo waliochangia katika miradi hiyo ya maendeleo. Hongereni sana Watanzania kwa uzalendo huo na moyo huo wa kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali katika kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, niruhusu kipekee, nimpongeze na nimshukuru mke wangu mpendwa Bi. Neema Mwigulu Nchemba pamoja na watoto, ambaye naye leo tumeungana naye. Mke wangu ni *Prayer Warrior* (Mwanamaombi Shujaa), kwa hiyo, hata maeneo ambayo yanaogopesha kidogo huwa naenda bila uwoga kwa kujua nipo na jeshi lisiloonekana.

Mheshimiwa Spika, pia, ninawapongeza na kuwashukuru wanangu kwa kunivumilia; Joshua Mwigulu, Gracious Mwigulu, Isaac Mwigulu, pamoja na Bernice Mwigulu kwa upendo na uvumilivu ambao nao wamekuwa wakitoa. Nikiri kwamba, maombi yao yamekuwa ni ngao ya kunipa nguvu wakati wote ninapotekeleza majukumu ya kulitumikia Taifa. Ninawashukuru na ninawapenda sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru wanahabari ikiwa ni pamoja na Waandishi wa Habari, na mitandao ya kijamii. Nina imani nanyi Waandishi wa Habari pamoja na wanahabari wote wa vyombo vyote vya habari ikiwemo na mitandao ya kijamii. Imani yangu ni kuwa

mtaendelea kuwahabarisha wananchi kuhusu yanayojiri katika Mkutano huu wa Bunge, lakini pia na kuibua mikakati ya kutekeleza Dira yetu ya 2050.

Mheshimiwa Spika, nihitimishe hotuba yangu kwa kuwaahidi wananchi kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, itaendelea kuwatumikia Watanzania kwa moyo wa dhati kwa kuzingatia kaulimbiu ya Kazi na Utu, Tunasonga Mbele. Katika kuwahakikisha hilo, ninasisitiza watumishi wote wa umma kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili kutoa huduma bora kwa wananchi bila upendeleo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi mingi iliyofanyika ni ushahidi kwamba Rais wetu ni mtu wa matokeo, maneno kidogo, vitendo vingi, ambavyo vinaongea katika maeneo mengi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa nimesema hayo, ninaomba sasa kuleta maombi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba idhini ya kukusanya maduhuli ya mapato ya ndani ya jumla ya shilingi 2,411,548,152,302.47. Kwa upande wa matumizi, kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake, inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 12,502,356,160,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 8,734,043,089,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 764,313,071,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba vilevile Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 225,021,730,000 kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Kati ya fedha hizo, shilingi 207,992,798,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 17,028,982,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo maombi, sasa ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

1 APRILI, 2026

HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA (MB), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KUHUSU MAPITIO NA MWELEKEO WA KAZI ZA SERIKALI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2026/2027 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Mapitio ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2026/2027. Aidha, kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii; na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambazo zilichambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge, sasa ninaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zilizopo chini yake na Mfuko wa Bunge kwa Mwaka 2026/2027.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema iliyotuwezesha kukutana mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha na kupokea Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa kipindi cha Mwaka 2025/2026 na mwelekeo wake kwa Mwaka 2026/2027. Aidha, nitumie fursa hii kuwapongeza Waislamu wote kwa kumaliza salama mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani nakusherehekea Sikukuu ya Eid el Fitri kwa amani na utulivu. Vilevile, niwatakie kila la heri Wakristo wote walio katika Mfungo wa Kwaresma na kuwatakia maandalizi mema ya Sikukuu ya Pasaka.

SALAMU ZA POLE

3. *Mheshimiwa Spika,* tarehe 25 Machi, 2026 tuliondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, mwanasiasa mahiri aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) na Mbunge wa Jimbo la Isimani.

4. Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa nitoe pole kwa Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondokewa na Waziri mahiri na mchapakazi katika Baraza la Mawaziri. Vilevile, nitoe pole kwako Mheshimiwa Spika, waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, familia, ndugu, jamaa, marafiki, wafanyakazi, wananchi wa Jimbo la Isimani na Watanzania wote kwa ujumla kutokana na msiba huo.

5. Mheshimiwa Spika, wakati wa uhai wake Mheshimiwa Lukuvi alihudumu katika nafasi mbalimbali. Baadhi ya nafasi hizo ni Naibu Katibu Mkuu wa UVCCM Taifa, Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa, Mkuu wa Wilaya ya Bukoba na Mkuu wa Mkoa katika Mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma. Vilevile, alikuwa Waziri katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

6. *Mheshimiwa Spika,* kutokana na utendaji kazi, umahiri na uzoefu katika masuala ya siasa pamoja na ushawishi wake, mnamo tarehe 13 Juni, 2023 Mheshimiwa Rais alimteua kuwa Mshauri wake Siasa na Uhusiano wa Jamii. Vilevile, Mheshimiwa Lukuvi aliwahi kuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa vipindi tofauti kati ya mwaka 2010 – 2015, 2021 – 2022 na mwaka 2024 hadi umauti ulipomfika.

7. *Mheshimiwa Spika,* Mheshimiwa Lukuvi pia alikuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani kwa kipindi cha miaka 31 hadi umauti ulipomfika. Mheshimiwa Lukuvi atakumbukwa kwa uongozi na uthubutu wake katika uratibu wa shughuli za Serikali pamoja na ushawishi mkubwa wa kisiasa katika nchi yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa marehemu pumziko la amani. Amina!

8. *Mheshimiwa Spika,* vilevile, ninatoa pole kwa kifo cha Mheshimiwa Halima Idd Nassor Mbunge wa Viti Maalum (Wafanyakazi), kilichotokea tarehe 18 Januari, 2026 Jijini Dar es

Salaam. Tutaendelea kumkumbuka kwa mchango wake na utumishi uliotukuka ndani ya Bunge lako Tukufu.

9. *Mheshimiwa Spika,* mnamo tarehe 3 Februari, 2026 tulipokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe aliyekuwa Mbunge Mstaafu Viti Maalumu (Mkoa wa Tabora). Vilevile, aliwahi kuhudumu katika nyadhifa mbalimbali ndani ya Chama Cha Mapinduzi ikiwemo Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa na Mjumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania. Wakati wa uhai wake, aliwatumikia wananchi wa Tabora na Watanzania kwa ujumla kwa ari na uzalendo wa hali ya juu. Ninatoa pole kwa wananchi wa Mkoa wa Tabora, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa msiba huo.

10. *Mheshimiwa Spika,* vilevile, tarehe 19 Februari, 2026 tuliondokewa na Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Muadhama Polycarp Kardinali Pengo. Kwa moyo wa simanzi na huzuni kubwa ninatoa pole kwa Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania, waumini wa Kanisa Katoliki pamoja na ndugu jamaa na marafiki. Marehemu Kardinali Pengo atakumbukwa kwa mchango mkubwa alioutoa katika huduma za kiroho. Wakati wa uhai wake, alisisitiza watu wote waishi maisha ya uadilifu, upendo, umoja na mshikamano wa kitaifa. Tutaendelea kuenzi mchango wake katika kuwaletea maendeleo Watanzania katika nyanja zote.

11. *Mheshimiwa Spika,* mnamo tarehe 20 Machi, 2026 tulipokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Julie Catherine Manning aliyekuwa mwanamke wa kwanza Tanzania kusoma Shahada ya Sheria na kuweka rekodi ya kushika wadhifa wa Jaji wa Mahakama Kuu katika Afrika Mashariki na Kati. Pamoja na wadhifa huo, Mheshimiwa Julie Catherine Manning aliwahi kuhudumu nafasi ya Waziri wa Sheria. Nitumie nafasi hii kuungana na Mheshimiwa Rais kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki, wadau wote wa sheria pamoja na Watanzania wote. Mheshimiwa Julie Catherine Manning, atakumbukwa kwa alama kubwa aliyoiweka katika kuwainua wanawake na kuchagiza maendeleo ya sekta ya sheria na Taifa kwa ujumla.

12. *Mheshimiwa Spika,* tarehe 17 Februari 2026, nchi ilimpoteza Mwanamuziki Mkongwe Mzee Steven Hiza ambaye ni mtunzi na mwimbaji wa wimbo maarufu uitwao Tanzania yetu ndiyo nchi ya furaha. Sina shaka mtakubaliana nami kuwa wimbo huo umekuwa ukichochea uzalendo na umoja wa Watanzania kwa miaka mingi tangu ulipotungwa kati ya mwaka 1966/1967. Ninatoa pole kwa wanafamilia, wapenzi wa muziki na Watanzania wote kwa ujumla. Mzee Hiza atakumbukwa kwa uzalendo wake alioudhihirisha kwa kutunga wimbo huo ambao ubora wake hata sasa haujachuja katika historia ya muziki.

13. *Mheshimiwa Spika,* katika kipindi cha hivi karibuni, wapo Watanzania wenzetu waliopatwa na maafa katika mikoa mbalimbali. Baadhi ya Mikoa hiyo ni Mbeya, Iringa, Morogoro, Shinyanga, Mwanza, Lindi, Arusha, Manyara, Dodoma, Pwani, Ruvuma, Kigoma, Tanga, Dar es Saalam, Kilimanjaro na Singida. Nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa, marafiki na mali zao kutokana na maafa hayo.

14. *Mheshimiwa Spika,* sambamba na maafa yatokanayo na mafuriko, katika kipindi hiki wapo Watanzania wenzetu waliopatwa na ajali mbalimbali. Nitumie nafasi hii kutoa salamu za pole kwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma na wananchi wote walioguswa na ajali ya Boti iliyotokea tarehe 13 Machi, 2026. Ninatoa pole kwa waathirika wote wa ajali ya Boti ya Nungwi pamoja na wote waliopata ajali mbalimbali zikiwemo za gari na pikipiki. Ninawaombea majeruhi wote uponyaji wa haraka na marehemu wote pumziko la amani. Amina!

UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA SERIKALI KWA MWAKA 2025/2026

15. *Mheshimiwa Spika*, nitumie fursa hii adhimu kumpongeza sana Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na juhudi zake za kuwatumikia wananchi kwa mapenzi ya dhati. Sote ni mashahidi wa kazi kubwa anayoifanya ya kuleta maendeleo na kuonesha dira ya mwelekeo wa Taifa hususan katika kuitekeleza falsafa yake ya ***"Kazi na Utu - Tunasonga Mbele".*** Nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu

pamoja na wananchi wote kumwomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa Rais wetu nguvu, ulinzi, afya njema na kila lililo la heri katika kuwatumikia Watanzania.

16. *Mheshimiwa Spika*, sina shaka nyote mtakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa ya kusimamia na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030. Kupitia usimamizi wa utekelezaji wa mipango hiyo, mafanikio makubwa yamepatikana kama yalivyoelezwa kupitia Bunge la 12, Mkutano wa 19, kikao cha pili na Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi uliofanyika Mei, 2025.

17. *Mheshimiwa Spika,* pamoja na mafanikio hayo makubwa, wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi mbalimbali kwa lengo la kuleta maendeleo na kukuza ustawi wa wananchi. Baadhi ya ahadi zilizotolewa ni pamoja na zile zilizotekelezwa ndani ya siku 100 baada ya kuchaguliwa na kuingia madarakani. Ahadi hizo, zililenga kuimarisha utoaji wa huduma za afya, elimu, maji; kurasimisha sekta isiyo rasmi; na kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya biashara ndogo na za kati na uendeshaji wa kampuni changa.

18. *Mheshimiwa Spika,* kama nilivyoeleza katika Bunge la 13, Mkutano wa Pili, ahadi hizo zimetekelezwa kwa mafanikio makubwa kupitia Sera, Mipango na Mikakati mbalimbali ya Kitaifa pamoja na usimamizi madhubuti. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuanza utekelezaji wa mpango wa Bima ya Afya kwa Wote Awamu ya Kwanza kwa wananchi 1,457,602 sawa na kaya 276,004 zisizo na uwezo. Vilevile, kuanza kugharimia magonjwa sugu ya Saratani, Figo, Moyo, Kisukari na Mifupa kwa watu wasio na uwezo; na kuondoa zuio la kuchukua miili ya marehemu katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya kote nchini kwa kigezo cha kutokulipa gharama za matibabu na madeni.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa elimu, Mpango Mkakati wa Kisayansi wa Kujenga Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa Watoto wa Elimu ya Awali na Wanafunzi wa Darasa la Kwanza na la Pili ulizinduliwa na Mheshimiwa Rais tarehe 29 Januari, 2026. Mpango huo wenye kaulimbiu ya ***'Mtoto Asome, Aandike na Ahesabu Bila Shida'*** unalenga kuongeza ubora wa elimu ya msingi na mbinu bora za ufundishaji.

20. Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kuzinduliwa kwa Mpango wa Kitaifa wa Pamoja Kati ya Waajiri, Vyuo vya Ufundi Stadi na Vyuo Vikuu. Mpango huo uliozinduliwa tarehe 9 Februari, 2026 na Mheshimiwa *Balozi Dkt.* Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unalenga kujenga uwezo wa ubunifu na ujasiriamali kwa wanafunzi ili kuwawezesha kujiajiri na kuajiriwa.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa sekta ya maji, Serikali inaendelea kutekeleza miradi 10 yenye thamani ya shilingi trilioni 1.58. Miradi hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Gridi ya Taifa ya Maji ya kusambaza maji kutoka Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa na mito mikubwa kwenda kwenye maeneo mbalimbali nchini.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine yaliyopatikana ni kutoa ajira na kuwapangia vituo vya kazi watumishi 12,000 ambapo kati ya hao, 5,000 ni wa sekta ya afya na 7,000 wa sekta ya elimu. Watumishi hao wameongeza ufanisi wa utoaji huduma katika sekta za afya na elimu.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuweka mazingira wezeshi kwa vijana kujiajiri, tarehe 5 Februari, 2026 Serikali ilitoa shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kundi hilo. Fedha hizo zitaongeza uzalishaji wa ajira katika sekta mbalimbali ikiwemo kilimo, mifugo na uvuvi, viwanda na biashara, na mawasiliano na hivyo kuwezesha vijana kuongeza kipato na kuchangia katika ukuaji wa uchumi.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** hayo ni baadhi ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika siku 100 za utawala wa Serikali ya Awamu ya Sita kipindi cha pili chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania. Wahenga walisema "**mwenye macho haambiwi tazama".** Mafanikio hayo ni ishara tosha ya misingi imara aliyoiweka Mheshimiwa Rais ya utekelezaji wa Dira 2050 katika kipindi cha miaka mitano ya kwanza.

25. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na mafanikio ya utekelezaji wa ahadi za siku 100 niliyoyaeleza, mafanikio mengine yaliyopatikana kisekta kwa mwaka 2025/2026 ni kama ifuatavyo:

HALI YA UCHUMI

Ukuaji wa Uchumi

26. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2025, kiwango sawa na mwaka 2024. Mwenendo huo unatokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika teknolojia mpya, hususan teknolojia ya akili unde, pamoja na juhudi za nchi mbalimbali kudhibiti mfumuko wa bei na kuchochea shughuli za uzalishaji katika uchumi wao.

27. Mheshimiwa Spika, hapa nchini, uchumi umeendelea kukua kwa kasi ambapo katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2025, pato halisi la Taifa limekua kwa asilimia 6.0 ikilinganishwa na asilimia 5.5 kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huo umechangiwa na uwekezaji mkubwa katika miradi ya kimkakati ya miundombinu ikiwemo nishati, mawasiliano, usafiri na usafirishaji, huduma za kijamii na kuimarika kwa shughuli za uzalishaji katika sekta mbalimbali za uchumi.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** katika ngazi ya kikanda, uchumi wa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara umeendelea kuimarika na kufikia wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2025, ikilinganishwa na asilimia 4.1 mwaka 2024. Ukuaji huo umechangiwa na kuimarika kwa uwekezaji katika miundombinu, kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji na kuimarika kwa mauzo ya bidhaa katika soko la kimataifa. Uchumi wa ukanda huo unatarajiwa kuendelea kuimarika na kufikia wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2026 na 2027. Aidha, katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, ukuaji wa uchumi unatarajiwa kufikia wastani wa

asilimia 7.7 mwaka 2025 na 2026, hali inayoonesha uwezo mkubwa wa ukanda huo kuwa moja ya maeneo yenye ukuaji wa kasi zaidi barani Afrika.

29. *Mheshimiwa Spika,* ukuaji wa uchumi wa dunia unatarajiwa kubaki katika wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2026 na kushuka hadi asilimia 3.2 mwaka 2027. Hali hiyo itawezesha uchumi wa dunia kuendelea kuwa himilivu licha ya changamoto zinazotokana na migogoro ya kikanda, mabadiliko ya sera za biashara na hali ya kifedha ya kimataifa.

Mfumuko wa Bei

30. *Mheshimiwa Spika*, nchi yetu imeendelea kuwa na utulivu wa bei uliotokana na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha, kuimarika kwa bei ya mafuta na bidhaa katika soko la dunia na utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani. Utulivu huo ulichangia kupunguza kasi ya ongezeko la bei ya bidhaa na huduma. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2025, wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.5. Kiwango hicho kipo ndani ya lengo la nchi la asilimia 3.0 hadi 5.0.

31. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, mfumuko wa bei kwa Januari, 2026 ulikuwa asilimia 3.3 ikilinganishwa na asilimia 3.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Kiwango hicho kipo ndani ya lengo la Jumuiya ya Afrika Mashariki la kutozidi asilimia 8.0 na lengo la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika la asilimia 3.0 hadi 7.0. Aidha, Serikali itaendelea kufuatilia hali ya kisiasa na kiuchumi duniani na kuchukua hatua stahiki ili kuwa na utulivu wa mwenendo wa bei za bidhaa.

Mauzo ya Nje na Akiba ya Fedha za Kigeni

32. *Mheshimiwa Spika,* mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 16.3 Januari, 2025 hadi dola za Marekani bilioni 18.7 Januari, 2026 sawa na ongezeko la asilimia 12.7. Ongezeko hilo lilichangiwa na mauzo ya bidhaa mbalimbali ikiwemo dhahabu, tumbaku, kahawa, bidhaa za viwandani, utalii na huduma za usafirishaji. Aidha, Januari, 2026, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani bilioni 6.3.

Kiasi hicho, kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kwa zaidi ya miezi 4.8 ikiwa ni juu ya kiwango cha chini kinachokubalika kimataifa.

Mikopo kwa Sekta Binafsi

33. ***Mheshimiwa Spika,*** mikopo iliyotolewa na benki kwa sekta binafsi imeongezeka kutoka asilimia 12.8 Januari, 2025 hadi asilimia 23.5 Januari, 2026. Mikopo hiyo, imenufaisha na kuchochea shughuli za uwekezaji pamoja na uzalishaji katika sekta mbalimbali za uchumi ikiwemo madini, biashara, kilimo, viwanda, usafirishaji na ujenzi.

Mwenendo wa Mapato

34. ***Mheshimiwa Spika****,* Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza makusanyo. Mikakati hiyo ni pamoja na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini; kupanua wigo wa kodi; na kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato. Kutokana na jitihada hizo, shilingi trilioni 26.63 zilikusanywa katika kipindi cha Julai 2025 hadi Februari, 2026 kati ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 25.68, sawa na ufanisi wa asilimia 103.7 na ukuaji wa asilimia 19.27 ikilinganishwa na mapato ya shilingi trilioni 22.32 yaliyokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2024/2025.

35. ***Mheshimiwa Spika****,* kati ya mapato hayo, shilingi trilioni 22.09 ni mapato yaliyotokana na kodi, shilingi trilioni 3.78 ni mapato yasiyo ya kodi na shilingi bilioni 754.26 ni misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo. Kati ya fedha zilizokusanywa, shilingi trilioni 12.28 zilitumika kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo mradi wa SGR; Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato; ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya na elimu; miradi ya maji; miundombinu ya nishati, usafiri na usafirishaji; na skimu za umwagiliaji.

36. ***Mheshimiwa Spika****,* kwa upande wa makusanyo ya maduhuli ya mikoa na mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, hadi Februari, 2026 shilingi trilioni 1.08 zimekusanywa kati ya lengo la shilingi trilioni 1.68 sawa na asilimia 64.61 ya lengo la

mwaka. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 172.87 ni maduhuli ya mikoa na shilingi trilioni 1.08 ni mapato ya ndani ya halmashauri. Makusanyo hayo yalitokana na tozo, madeni na mauzo ya bidhaa mbalimbali.

37. *Mheshimiwa Spika,* Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kusimamia ukusanyaji wa kodi za majengo. Hadi Februari, 2026 shilingi bilioni 61.13 zimekusanywa kutoka kwenye kodi ya majengo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 48.9 zimewasilishwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na shilingi bilioni 12.23 zimepelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 184 kwa ajili ya kuimarisha ukusanyaji wa kodi ya majengo.

38. *Mheshimiwa Spika,* ili kuimarisha mfumo wa kodi nchini na kuufanya kuwa jumuishi, Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliunda Tume ya Kutathmini Maboresho ya Mfumo wa Kodi nchini. Lengo lilikuwa ni kufanya tathmini ya kina ya mfumo wa kodi kufuatia malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wafanyabiashara, wawekezaji pamoja na wadau wa maendeleo ili kuandaa mapendekezo ya kuboresha mfumo huo.

39. *Mheshimiwa Spika,* Tume ilikamilisha kazi hiyo na kuwasilishwa taarifa kwa Mheshimiwa Rais tarehe 18 Machi, 2026. Taarifa hiyo imeainisha kuwa, maboresho ya mfumo wa kodi ni nyenzo muhimu katika kufikia malengo ya muda mrefu yaliyoainishwa katika Dira 2050. Vilevile, imeainisha mikakati mbalimbali kwa ajili ya kudhibiti mianya ya ukwepaji wa kodi.

40. *Mheshimiwa Spika,* niendelee kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa moyo wa uzalendo na maamuzi sahihi ya kufanya mapitio makubwa ya mfumo mzima wa kodi nchini ambayo hayakufanyika kwa kipindi cha miaka 30. Utekelezaji wa mapendekezo ya taarifa hiyo utawezesha kuongeza wigo wa kodi na kuhakikisha kila mtu anachangia kadri ya kipato chake.

41. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kusimamia mikakati itakayoongeza ukusanyaji wa

mapato kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii ikiwemo kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini; kupanua wigo wa kodi; na kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA. Mikakati hiyo itahakikisha shabaha za uchumi jumla zilizobainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027 zinafikiwa.

Dira 2050

42. ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu imekuwa ikiongozwa kwa mipango thabiti ya maendeleo. Sote tunakumbuka kuwa katika kipindi cha miaka 25 iliyopita, tuliongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambayo ilitafsiriwa katika mipango mitatu ya maendeleo ya Taifa ya miaka mitano. Mpango wa kwanza Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulitekelezwa mwaka 2011/2012 - 2015/2016 ukiwa na dhima ya "Kufungua Fursa Fiche za Ukuaji wa Uchumi".

43. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulitekelezwa mwaka 2016/2017 – 2020/2021 ukiwa na dhima ya "Kukuza Uchumi wa Viwanda na Maendeleo ya Watu". Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulitekelezwa mwaka 2021/2022 – 2025/2026, ukiwa na dhima ya "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu" ambao ndiyo unakamilisha utekelezaji wa Dira 2025.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** mnamo tarehe 17 Julai, 2025 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua rasmi Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Dira hiyo itaongoza mipango yetu ya maendeleo katika miaka 25 ijayo. Vilevile, inalenga kujenga Taifa jumuishi, lenye ustawi kwa wote, lenye haki na linalojitegemea. Kama sehemu ya mkakati wa utekelezaji wa Dira 2050, Serikali iliandaa na Bunge lako likapitisha katika mkutano uliopita Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano utakaotekelezwa katika kipindi cha miaka mitano 2026/2027 – 2030/2031. Dhima ya mpango huo ni "Mageuzi katika Kukuza Uchumi na Kuzalisha Ajira".

45. ***Mheshimiwa Spika***, Mpango na Bajeti itakayopitishwa na Bunge hili ni hatua ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/2027 - 2030/2031 na Dira 2050. Utekelezaji wa Dira hiyo, utawezesha Taifa kuwa na uchumi wenye thamani ya dola za Marekani trilioni moja na wastani wa pato la mtu mmoja mmoja kuwa dola za Marekani 7,000 kwa mwaka ifikapo 2050.

46. ***Mheshimiwa Spika***, Dira 2050 ndiyo mwelekeo wa Taifa letu. Kwa kuzingatia hilo kipaumbele cha Serikali kitawekwa katika utekelezaji wa malengo kama yalivyobainishwa katika Dira hiyo. Suala hilo litawezekana ikiwa wadau wote watakuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu vipaumbele vilivyoainishwa katika Dira 2050. Nitoe rai kwa viongozi wa Serikali, Dini, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia na Wadau wa Maendeleo kuhakikisha kwamba mipango yao inawiana na vipaumbele vya Dira 2050 na kuiunga mkono katika utekelezaji wake. Aidha, ninailekeza Tume ya Mipango kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Dira 2050 ili kuwezesha kushiriki kikamilifu katika utekelezaji.

UWEKEZAJI NA UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI

47. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kujenga uchumi unaoongozwa na uwekezaji kutoka sekta binafsi ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kuboresha ustawi wa wananchi. Ili kuonesha dhamira ya dhati ya kutekeleza malengo hayo, katika mwaka 2025/2026, miradi 927 yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 11.08 ilisajiliwa. Hatua hiyo, inaonesha kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji nchini na kuongezeka kwa imani ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na uwekezaji huo, Serikali imeendeleza maeneo maalum ya uwekezaji ili kuimarisha ukuaji wa uchumi wa viwanda na kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kutenga Maeneo Maalum ya Kiuchumi 34 na kuendelea na utekelezaji wa miradi 25 yenye thamani ya dola za Marekani milioni 280.8. Miradi hiyo inatarajiwa kuzalisha mauzo ya nje yenye thamani ya dola za Marekani milioni 672.63. Mikakati mingine ni pamoja na kupunguza tozo 245; kurekebisha sheria 28; na kuimarisha utoaji

wa huduma kupitia Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Tanzania. Jitihada hizo zimeendelea kuboresha mazingira ya biashara na kupunguza gharama za uwekezaji.

49. *Mheshimiwa Spika,* katika kuhakikisha uwekezaji unaofanyika unakuwa na manufaa kwa Watanzania na kuzingatia mipango ya ndani ya nchi, Serikali imeimarisha ulinganifu wa sera, mipango na bajeti ili taasisi zote zitekeleze vipaumbele vya Taifa kwa mwelekeo mmoja. Vilevile, imeweka kipaumbele katika usimamizi wa miradi ya kielelezo ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati, kwa gharama zilizopangwa na viwango vinavyotarajiwa. Hatua hiyo inalenga kuharakisha matokeo katika kukuza uchumi, kuongeza ajira, kuimarisha uzalishaji viwandani na kuboresha huduma kwa wananchi.

50. *Mheshimiwa Spika,* hatua zinazochukuliwa zinaakisi dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kujenga uchumi wa matokeo unaoongeza tija katika sekta za uzalishaji. Licha ya hayo, hatua hizo zinaongeza kipato cha Mtanzania mmoja mmoja na hivyo kufikia malengo ya kuwa na uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu wenye pato la taifa la takribani dola za marekani trilioni moja ifikapo mwaka 2050.

51. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendeleza uwekezaji wa kimkakati katika maeneo mbalimbali ikiwemo Eneo Maalum la Kiuchumi la Bagamoyo, Liganga na Mchuchuma pamoja na mradi wa Magadi Soda Engaruka. Vilevile, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kukuza na kuvutia uwekezaji nchini na kuratibu utekelezaji wa Dira 2050 kupitia mipango ya mwaka na muda wa kati.

SEKTA ZA UZALISHAJI

Kilimo

52. Mheshimiwa Spika, Baba wa Taifa na mwanafalsafa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika kitabu chake kiitwacho *Mtu na Maendeleo (1974)* alisema kuwa, ninaomba kunukuu **"maendeleo ya kweli huanza pale wananchi wanapoweza kuzalisha chakula cha kuwatosha wenyewe"** mwisho wa kunukuu. Serikali kwa kutambua umuhimu huo, imeendelea kuimarisha hali ya upatikanaji wa chakula ambapo tani 23,783,128 zilizalishwa katika msimu wa mwaka 2024/2025 ikilinganishwa na mahitaji ya tani 18,279,054 kwa mwaka 2025/2026 na hivyo kuihakikishia nchi usalama wa chakula kwa asilimia 130.

53. Mheshimiwa Spika, ongezeko la uzalishaji limetokana na upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakati na Serikali kuendelea kutoa ruzuku ya mbolea. Aidha, katika msimu wa kilimo wa mwaka 2025/2026, Serikali imetoa tani 1,098,990 za mbolea sawa na asilimia 73.26 ya lengo. Kati ya hizo, tani 574,664.99 zenye thamani ya zaidi ya shilingi trilioni 1.03 zimesambazwa kwa wakulima 526,044 kupitia mpango wa ruzuku. Hatua hiyo ilichochea ongezeko la matumizi ya mbolea na tija katika uzalishaji.

54. Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa uhakika wa mbolea umeongeza matumizi ya mbolea kwa asilimia 14.6 kutoka tani 848,884 mwaka 2023/2024 hadi tani 972,506 mwaka 2024/2025. Vilevile, matumizi ya virutubisho yameongezeka kutoka kilogramu 19 hadi 24 kwa hekta na hivyo kuonesha mwitikio chanya wa wakulima na mafanikio ya mikakati ya Serikali ya kuhamasisha kilimo chenye tija.

55. Mheshimiwa Spika, sambamba na upatikanaji wa mbolea, Serikali imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Januari 2026, jumla ya tani 61,003.42 za mbegu zimepatikana. Kati ya hizo, asilimia 58.31 zimetokana na uzalishaji wa ndani ya nchi. Aidha, Serikali imeendelea kutoa ruzuku ya mbegu za mahindi na kuzalisha miche zaidi ya milioni 28 ya mazao mbalimbali kwa ajili ya kusambazwa kwa wakulima. Hatua hiyo inalenga kuongeza uzalishaji na kupunguza utegemezi wa mbegu kutoka nje ya nchi.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha kilimo cha kisasa na kuwainua wakulima wadogo, Serikali imeanzisha vituo 79 vya kutoa huduma ya zana za kilimo. Vilevile, imenunua matrekta 360 na kuyaweka kwenye vituo hivyo kwa ajili ya kutoa huduma kwa wakulima.

57. ***Mheshimiwa Spika***, ili kurasimisha na kuimarisha huduma za ugani kwa kuwafikia wakulima kwa wakati bila kupitia mlolongo mrefu, Serikali ipo kwenye hatua za kuanzisha Wakala ya Huduma za Ugani Kilimo. Lengo ni kuongeza tija kwa wakulima kwa kuwawezesha kufanya maamuzi sahihi ya kilimo, kuhaulisha teknolojia, kutoa ushauri wa kilimo bora na matumizi ya mbinu endelevu.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji, Serikali imeendelea kutekeleza miradi 146 ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Kati ya hiyo, ujenzi wa skimu 20 na mabwawa 6 ya umwagiliaji umekamilika. Juhudi hizo zimeongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 727,280.06 mwaka 2024/2025 hadi hekta 983,466.60 mwaka 2025/2026.

59. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa miundombinu ya masoko, Serikali imeimarisha masoko ya mazao kwa kuendelea na ujenzi wa masoko matano ya kimkakati katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama (Busoka) na Halmashauri za Wilaya za Ngara (Kabanga), Kyerwa (Nkwenda na Murongo) na Tarime (Sirari). Ujenzi wa masoko hayo umefikia wastani wa asilimia 81.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ujenzi wa vituo sita vya masoko katika Halmashauri ya Mji wa Nzega (Ushirika) na Halmashauri za Wilaya za Karatu (Endashangwet), Mpwapwa (Kibakwe), Monduli (Losirwa), Rombo (Mamsera) na Hai (Masama mula) umefikia wastani wa asilimia 29.3. Kukamilika kwa ujenzi wa masoko na vituo hivyo kutarahisisha ukusanyaji na uuzaji wa mazao ndani na nje ya nchi na kuongeza kipato cha mkulima.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuleta tija inayotarajiwa katika kilimo, naelekeza Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuweka mpango mahsusi wa usimamizi wa katazo la utaratibu wa lumbesa. Aidha, mazao yote

yanayofungashwa kwenye vifungashio yauzwe kwa kuzingatia vipimo. Suala hili litekelezwe sambamba na udhibiti wa ushuru holela wa mazao ya kilimo ikiwa ni pamoja na Halmashauri zote kusitisha mara moja ushuru holela unaotozwa kwa mazao ya kilimo. Vilevile, kusitisha utaratibu wa wakulima kukopwa mazao na AMCOS.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa pembejeo, huduma za ugani, afya ya udongo, hifadhi ya chakula na masoko ya mazao. Lengo kuu ni kuongeza uzalishaji, kuimarisha usalama wa chakula na lishe, kukuza kilimo biashara na kuongeza mchango wa sekta ya kilimo katika ukuaji wa uchumi.

Mifugo

63. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha sekta ya mifugo kwa kuboresha mazingira ya ufugaji na biashara ya mifugo. Jitihada zilizochukuliwa ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa karantini ya Kwala Mkoani Pwani yenye thamani ya shilingi milioni 997.99 ambapo umefikia asilimia 45. Kukamilika kwa karantini hiyo itawezesha kuongeza idadi ya mifugo itakayokidhi vigezo vya kusafirishwa nje ya nchi.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa minada 21 yenye thamani ya shilingi bilioni 4.76 katika Mikoa ya Morogoro, Mbeya, Mara, Mwanza, Dodoma, Geita, Singida, Iringa, Tabora, Simiyu, Tanga, Shinyanga, Kagera na Arusha. Pia, Serikali imekamilisha ujenzi wa mabwawa mawili na inaendelea na ujenzi wa mabwawa 6 yaliyo katika hatua mbalimbali. Kukamilika kwa ujenzi wa mabwawa hayo utakaogharimu shilingi bilioni 5.44 utawezesha upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo katika kipindi chote cha mwaka.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeendesha kampeni ya kitaifa ya chanjo ambapo mifugo milioni 49.4 kati ya milioni 76.3 sawa na asilimia 64 imechanjwa. Sambamba na hilo, imeendelea na zoezi la utambuzi wa mifugo na kusambaza vifaa vya chanjo.

66. *Mheshimiwa Spika,* pamoja na utoaji wa chanjo, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa mbegu za malisho kwa kuzalisha tani 149.9 zilizosambazwa kwa wafugaji katika mikoa 16 ya Tanzania Bara. Upatikanaji wa malisho ya uhakika ni muhimu katika kufikia lengo la ufugaji endelevu na kupunguza migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Uvuvi

67. *Mheshimiwa Spika,* kwa upande wa Sekta ya Uvuvi, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko katika Mkoa wa Lindi kwa gharama ya shilingi bilioni 280.58 ambazo ni fedha za ndani. Hadi Februari 2026, ujenzi umefikia asilimia 95. Kukamilika kwa bandari hiyo kutaimarisha utoaji wa huduma kwa wavuvi wakubwa na wadogo wa ndani na nje ya nchi, kuzalisha ajira 30,000 na kuboresha miundombinu ya uvuvi ili kupunguza kiwango cha umaskini.

68. *Mheshimiwa Spika,* kwa kutambua umuhimu wa uvuvi katika Bahari Kuu, Serikali imenunua meli maalumu ya uvuvi kwa njia ya mishipi yenye urefu wa mita 22 iliyowasili nchini Februari, 2026. Meli hiyo itawezesha uvuvi wa Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari Kuu (EEZ) na hivyo kuongeza kiwango cha uvuvi, kukuza ajira na ujuzi hasa kwa vijana na kuongeza pato la wananchi na Taifa kwa ujumla.

69. *Mheshimiwa Spika,* katika hatua nyingine, Serikali imetoa mikopo ya masharti nafuu kwa wavuvi na wakuzaji viumbe maji kwa ajili ya kuwawezesha kuendeleza shughuli za uvuvi ikiwemo ununuzi wa boti 219 na boti saidizi 118. Kadhalika, imetoa elimu kwa wadau zaidi ya 254,000 katika mnyororo wa thamani wa uvuvi na kuzalisha vifaranga vya samaki vilivyosambazwa katika maeneo mbalimbali.

70. *Mheshimiwa Spika,* kwa kutambua mchango na umuhimu wa shughuli zinazotekelezwa na wavuvi wadogo, kamati za usalama ziimarishe ulinzi katika maeneo yote ambapo shughuli za uvuvi zinafanyika. Aidha, ni lazima kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na utu wakati wa kuwasimamia wavuvi wadogo kwenye shughuli zao za kila siku.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kufanya tafiti za kimkakati katika uzalishaji wa mnyororo wa thamani wa uvuvi, kutekeleza mikakati ya uvuvi katika bahari kuu ikiwemo ununuzi wa meli na ujenzi wa bandari ya uvuvi. Vilevile, kudhibiti magonjwa ya mifugo kupitia ununuzi wa chanjo, ujenzi wa majosho na kuendeleza miradi ya kuongeza tija, ajira na mapato ya Taifa.

Maliasili na Utalii

72. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maliasili na Utalii imeendelea kuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi, ajira na pato la Taifa. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuinua sekta hiyo muhimu kwa uchumi wa nchi yetu. Mikakati hiyo imeongeza idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi za Taifa kwa asilimia 10.73 kutoka watalii 5,360,247 mwaka 2024 hadi 5,935,561 mwaka 2025 na hivyo kuongeza mapato yatokanayo na utalii kutoka dola za Marekani bilioni 3.9 mwaka 2024 hadi dola za Marekani bilioni 4.4 Desemba 2025 sawa na ongezeko la asimilia 12.82.

73. Mheshimiwa Spika, ongezeko la watalii limechangiwa kwa kiasi kikubwa na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo zimetambuliwa kitaifa, kikanda na kimataifa. Katika kutambua mchango huo, tarehe 31 Januari, 2026, Mheshimiwa Rais alitunukiwa tuzo ya Kiongozi Mwenye Maono katika hafla ya utoaji tuzo ya *Serengeti Awards*.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** isitoshe, Tanzania imechaguliwa kuwa mwanachama wa Kamati ya Urithi wa Dunia na kushinda tuzo mbalimbali zilizotolewa na taasisi ya *World Travel Awards*. Tuzo hizo ni Tanzania kuwa Kituo Bora Duniani kwa Utalii wa Safari; Serengeti kuwa Hifadhi Bora Duniani; Zanzibar kuwa Kituo Bora cha Mikutano ya Kampuni na Mapumziko; Kampuni ya *Serengeti Balloon Safaris* kushinda nafasi ya Kampuni Bora ya Safari za Puto Duniani; na Kisiwa cha Jumeirah Thanda kilichopo Mafia kushinda nafasi ya Kisiwa Bora cha Mapumziko Duniani.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** itakumbukwa kuwa, Serikali ilipokea ripoti ya Tume ya Rais ya Kutathmini Zoezi la Uhamaji wa Hiari wa Wakazi wa Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Tume ya Rais ya Kutathmini Masuala ya Ardhi katika Wilaya ya Ngorongoro. Nilihakikishie Bunge lako tukufu kuwa Serikali itafanyia kazi mapendekezo ya ripoti hizo kwa lengo la kupata suluhu ya kudumu na kuimarisha utalii katika ukanda huo.

Madini

76. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha sekta ya madini kwa kutekeleza mikakati mbalimbali inayoongeza mapato ya Serikali na fursa za ajira kwa wananchi. Kama ilivyo sekta ya Maliasili na Utalii, sekta ya madini ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na pato la Taifa. Kwa kuzingatia umuhimu huo, mikakati mbalimbali imeendelea kutekelezwa ikiwemo kuimarisha usimamizi na utendaji wa masoko 44 na vituo 118 vya ununuzi wa madini.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza rasilimali muhimu ya madini, Serikali imesaini makubaliano ya kuendeleza Mradi wa Niobium wa Panda Hill, Mkoani Mbeya ambao utakuwa kitovu cha uzalishaji na usindikaji wa madini mkakati. Kupitia mradi huo, Tanzania inalenga kuwa mzalishaji wa nne duniani kwa kuchangia takriban asilimia 4 ya mahitaji ya dunia na kuzalisha takriban tani 100,000 kwa mwaka.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia mradi huo utakaokuwa na uwekezaji wa awali wa dola za Marekani milioni 442, Serikali inatarajia kupata mapato ya takribani shilingi trilioni 2 kutokana na mrabaha, kodi pamoja na gawio la hisa za Serikali ambazo zitachangia katika maendeleo ya miundombinu na huduma muhimu za kijamii kama barabara, shule na hospitali. Aidha, zaidi ya watu 1,600 wanatarajiwa kuajiriwa.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, Serikali inatambua nafasi ya wachimbaji wadogo na wakubwa wa madini katika kuendeleza sekta hiyo muhimu. Hivyo, imetoa leseni 8,418 za uchimbaji madini. Kati ya leseni hizo, za uchimbaji mdogo ni 5,983,

leseni ndogo za biashara ni 1,339, leseni za uchimbaji wa kati ni 14, leseni za utafutaji ni 207, leseni kubwa za biashara ni 848 na leseni za uchenjuaji ni 27.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imewawezesha wachimbaji wadogo 1,239 kwa kuwapatia mafunzo kuhusu uchimbaji salama, utunzaji wa mazingira, huduma ya uchorongaji, uchenjuaji na afya migodini sambamba na kuwatengea maeneo 99 ya uchimbaji madini. Mikakati hiyo imewezesha kukusanya mapato ya madini ya shilingi bilioni 771.53 sawa na asilimia 64.3 ya lengo la shilingi trilioni 1.2 katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Januari, 2026 na hivyo kuchangia uendeshaji wa miradi ya maendeleo.

81. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuwezesha Taifa kuwa na taarifa za uhakika kuhusu kiasi na ubora wa rasilimali za madini, ninaelekeza Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Madini kuweka utaratibu wa kutenga fedha zitokanazo na mapato ya madini kwa ajili ya tafiti za utafutaji wa madini. Utaratibu huo uanze kutumika mwaka 2026/2027.

82. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, ili kutoa fursa kwa Watanzania kunufaika na rasilimali za madini, ninaelekeza Wizara ya Madini kuweka utaratibu wa kudhibiti mikataba wanayoingia Watanzania wenye vitalu na wawekezaji wa nje ili kulinda maslahi ya Watanzania na Taifa. Hatua hii itasaidia pia kuondoa migogoro kati ya wachimbaji wadogo na wawekezaji wakubwa.

83. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na mnyororo wa thamani katika madini muhimu na madini mkakati. Vilevile, itahamasisha uwekezaji, kuimarisha uendeshaji wa minada na maonesho ya madini ya vito, kuongeza uwekezaji kwenye tafiti za madini za kina na kuwarasimisha na kuwaendeleza wachimbaji wadogo.

Nishati

Umeme

84. ***Mheshimiwa Spika****,* sina shaka, nyote mtakubaliana nami kwamba, nishati ya umeme ni injini ya kuharakisha na kurahisisha maendeleo ya kisasa hususan inapotumika katika shughuli za uendeshaji wa viwanda, teknolojia pamoja na matumizi ya nyumbani. Serikali kwa kutambua hilo, imeendelea kutekeleza mikakati mahsusi ya kuhakikisha nishati ya umeme inayozalishwa hapa nchini, inakidhi mahitaji yatokanayo na kasi kubwa ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** mikakati hiyo ni pamoja na kuongeza miundombinu ya kusafirisha umeme kutoka kilomita 7,745.4 mwaka 2025 hadi kufikia kilomita 8,500.38 Februari, 2026. Pia, imekamilisha awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme wa MW 50 kwa kutumia jua katika Wilaya ya Kishapu Mkoani Shinyanga.

86. ***Mheshimiwa Spika****,* vilevile, kuendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovolti 400 kutoka Chalinze kupitia Kinyerezi hadi Mkuranga (kilomita 135) ambao umefikia asilimia 53.53, na kutoka Chalinze hadi Dodoma (kilomita 345) ambao umefikia asilimia 64.14. Kukamilika kwa miradi hiyo kutawezesha umeme unaozalishwa katika Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere kusambazwa katika Mikoa mbalimbali na hivyo kuendelea kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini.

87. ***Mheshimiwa Spika*****,** ili kuchochea kasi ya ukuaji wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika ngazi ya Kitongoji, Serikali imeanza kuchukua hatua za kuhakikisha nishati ya umeme inafika katika maeneo hayo. Hadi Februari, 2026, jumla ya vitongoji 39,003 kati ya 64,359 vya Tanzania Bara sawa na asilimia 61 vimeunganishwa na huduma ya umeme. Aidha, kazi ya kupeleka umeme katika vitongoji 9,009 vya Tanzania Bara kupitia mradi wenye thamani ya shilingi trilioni 1.2 inaendelea.

88. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya kukamilika kwa miradi mbalimbali ya uzalishaji wa umeme ikiwemo ujenzi wa bwawa la Julius Nyerere kwa kutumia fedha za ndani, hivi sasa nchi ina ziada ya umeme. Aidha, Serikali itaendelea kujenga na kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa umeme ili kuondoa

changamoto ya kukatika kwa umeme katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na kuunganisha wilaya ambazo hazipo katika gridi ya Taifa.

89. ***Mheshimiwa Spika***, ninaelekeza Wizara ya Nishati ikamilishe utekelezaji wa miradi ya kupeleka umeme katika vitongoji. Vilevile, iweke kipaumbele katika kuunganisha umeme katika hospitali, vituo vya afya, zahanati, shule, taasisi za dini na visima vya maji. Aidha, Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati kuimarisha utekelezaji wa wa mradi wa Gridi Imara ikiwa ni pamoja na kuhakikisha fedha zilizotengwa zinatolewa kwa wakati. Lengo ni kuondoa tatizo la kukatika mara kwa mara kwa umeme nchini.

Mafuta na Gesi

90. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na juhudi za upatikanaji wa nishati ya umeme, Serikali imeendelea kuhakikisha ongezeko la matumizi ya gesi asilia. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Februari, 2026, Serikali imeongeza mtandao wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika viwanda, taasisi na nyumbani hadi kilomita 243.6 ikilinganishwa na kilomita 184.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/2025. Vilevile, Serikali imekamilisha ujenzi wa vituo 14 vya kujaza gesi asilia iliyoshindiliwa ili kutoa huduma ya usambazaji wa gesi asilia kwenye vyombo vya moto.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha matumizi ya gesi asilia iliyoshindiliwa, ninaelekeza Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Nishati zishirikiane kuandaa viwango msawazo *(specifications)* vitakavyoainisha mahitaji ya vyombo vya moto vya Serikali. Vilevile, zijenge miundombinu ya kutosha kuwezesha vyombo hivyo kuanza kutumia gesi asilia iliyoshindiliwa.

92. ***Mheshimiwa Spika***, licha ya uwepo wa changamoto za kiusalama kikanda na kimataifa ikiwemo ile ya Mashariki ya Kati, Serikali imeendelea kusimamia upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli na kuhakikisha bei ya bidhaa hizo inaendelea kuwa himilivu. Usimamizi huo umewezesha shughuli za kiuchumi na kijamii kutekelezwa bila kuathiriwa na changamoto yoyote.

93. *Mheshimiwa Spika*, katika hatua nyingine, Serikali imeendelea kusimamia mifumo ya kuagiza, kuhifadhi na kusambaza mafuta pamoja na kuongeza uwezo wa kupokea na kuhifadhi mafuta katika Bandari za Dar es Salaam na Mtwara. Katika kufanikisha hilo, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa ghala la kupokea na kuhifadhi mafuta lenye uwezo wa kupokea tani 308,110 katika Bandari ya Dar es Salaam ambao umefikia asilimia 30. Aidha, miundombinu ya kuhifadhi mafuta katika Bandari ya Mtwara imeongezeka kutoka tani 29,280 hadi tani 110,221 ambayo itawezesha kupokea meli yenye shehena ya tani 30,000.

94. *Mheshimiwa Spika*, ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani – Tanga umefikia asilimia 81 ikilinganishwa na asilimia 52 zilizokuwa zimefikiwa Februari, 2025. Hii ni hatua kubwa na mradi unatekelezwa kwa viwango tarajiwa. Kama nilivyoelekeza nilipotembelea mradi huo hivi karibuni, mradi utakapokamilika, kipaumbele cha kutoa ajira kiwe kwa wale waliofanya kazi wakati wa ujenzi wa mradi. Lengo ni kuendeleza utaalamu uliopatikana kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mingine inayotekelezwa na Serikali na wadau.

95. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande mwingine, Serikali imeendelea kuhamasisha wananchi kutumia nishati safi ya kupikia ili kuhakikisha asilimia 80 ya Watanzania wanaacha matumizi ya kuni na mkaa ifikapo mwaka 2034. Jitihada zilizochukuliwa na Serikali hadi Februari, 2026 ni pamoja na kugawa majiko banifu 13,575 kwa ruzuku ya asilimia 85, mitungi ya gesi asilia 28,653 ya kilo sita kwa ruzuku ya asilimia 50 na majiko janja ya umeme 7,292. Vilevile, Serikali imewezesha taasisi 1,136 zinazolisha zaidi ya watu 100 kwa siku kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia. Hatua hizo zitasaidia kupunguza uharibifu wa mazingira na kulinda afya za wananchi wanaotumia nishati hiyo.

96. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ili kukidhi mahitaji ya nishati nchini; kusambaza umeme katika vitongoji ambavyo havijapatiwa umeme; kuendeleza shughuli za kutafuta, kusafirisha, kuhifadhi na kusambaza mafuta

na gesi asilia. Pia, kukamilisha mpango wa matumizi ya nishati safi ya kupikia katika taasisi na kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi katika kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 – 2034).

Ardhi

97. *Mheshimiwa Spika*, sekta ya ardhi ni muhimu katika kuwezesha uzalishaji na maendeleo ya sekta nyingine. Hata hivyo, sekta hiyo imekumbwa na changamoto na migogoro mbalimbali ikiwa ni pamoja na maeneo mengi kutopimwa, ucheleweshaji wa utoaji wa hati, umilikishaji wa eneo moja kwa zaidi ya mtu mmoja na baadhi ya watendaji kutokuwa waaminifu. Changamoto hizo zimesababisha uwepo wa migogoro baina ya makundi mbalimbali katika jamii yakiwemo ya wakulima na wafugaji. Pia migogoro ya mipaka baina ya vijiji.

98. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kutatua migogoro iliyopo kupitia kliniki za ardhi, kamati za wataalamu, mabaraza ya ardhi na ziara za viongozi. Hadi Januari, 2026 migogoro 5,333 imetatuliwa, maombi ya umiliki 10,113 yalipokelewa na hatimiliki 7,182 ziliandaliwa pamoja na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji 191.

99. *Mheshimiwa Spika*, aidha, ninaelekeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kufanya tathmini kwa lengo la kuboresha mifumo ya kushughulikia migogoro ya ardhi. Vilevile, kuendelea kutatua changamoto zilizopo kupitia mikakati mbalimbali ikiwemo kuimarisha matumizi ya TEHAMA.

100. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha changamoto na migogoro hiyo inafikia kikomo, ninaelekeza Wizara ya Ardhi kuhakikisha watumishi wake wote wanapimwa utendaji kazi wao kwa idadi ya changamoto na migogoro waliyoitatua pamoja na hati walizotoa. Vilevile, hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa watumishi wote watakaobainika kuwa chanzo cha migogoro hiyo. Aidha, Wizara ihakikishe taratibu na mifumo inayotumika katika kutoa huduma za ardhi, inakuwa ya wazi na rafiki kwa wananchi wote.

101. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kusimamia upangaji na upimaji wa ardhi mijini, vijijini na maeneo ya kimkakati; kuimarisha mifumo ya TEHAMA; na kuboresha huduma za uthamini na ulipaji fidia. Vilevile, itaimarisha utatuzi wa migogoro, kuendeleza ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na kuboresha miundombinu ya upimaji na ramani ili kuongeza tija, uwazi na kasi ya utoaji huduma.

Viwanda na Biashara

102. *Mheshimiwa Spika*, sekta ya viwanda na biashara inaendelea kuwa nguzo muhimu katika kuleta mageuzi ya kiuchumi nchini. Hii ni kutokana naukweli kwamba, sekta hiyo ni kichocheo katika ukuaji wa Pato la Taifa, kuongeza ajira, kuvutia uwekezaji na kuimarisha ushindani wa Tanzania katika masoko ya kikanda na kimataifa.

103. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2025/2026, Serikali imeendelea kuwezesha ujenzi wa kongani ya *Sino Tan Industrial Park* (Kwala) ambao umefikia asilimia 80 na viwanda 4 vimeanza uzalishaji. Vilevile, imekamilisha ujenzi wa miundombinu muhimu katika kongani ya *Modern Industrial Park* (Mlandizi) na ujenzi wa viwanda 5 unaendelea. Kukamilika kwa kongani hizo kutachangia kuzalisha ajira zaidi ya 130,000.

104. *Mheshimiwa Spika,* uwepo wa viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa mbalimbali ni hatua muhimu ya kupunguza matumizi ya fedha za kigeni. Moja ya bidhaa ambayo imekuwa ikiagizwa kutoka nchi za nje kwa fedha za kigeni ni sukari ya viwandani. Hata hivyo, kuanzia Novemba, 2025 Kiwanda cha Sukari Mkulazi kilianza rasmi uzalishaji wa sukari ya viwandani ambapo hadi Februari, 2026 tani 256 zilizalishwa. Uzalishaji huo unatarajiwa kupunguza mahitaji ya uagizaji wa sukari ya viwandani kutoka nje kwa asilimia 20 kwa mwaka. Kiwanda hicho ni cha kwanza kuzalisha sukari ya viwandani ndani ya nchi.

105. *Mheshimiwa Spika*, katika hatua nyingine, Serikali inaendelea kufanya tathmini ya viwanda nchini ambapo katika mikoa tisa, tathmini imekamilika na kuwezesha kutambuliwa kwa viwanda 25,650 vilivyoingizwa kwenye kanzidata. Tathmini hiyo itawezesha Serikali kupanga mipango ya kuviendeleza kwa

kuzingatia mahitaji ya msingi ili kuongeza mchango wa viwanda hivyo katika kuzalisha ajira na kuchangia kukua kwa uchumi.

106. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa biashara, Serikali imekamilisha Mkakati wa Utekelezaji wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika. Mkakati huo utawezesha Tanzania kufikia soko la zaidi ya watu bilioni 1.4 lenye thamani ya zaidi ya dola za Marekani trilioni 3.4. Vilevile, imesaini mkataba wa Mfumo Rahisi wa Biashara na Malawi kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo.

107. *Mheshimiwa Spika*, mkataba huo unalenga kuwawezesha wafanyabiashara wadogo wa mpakani kununua na kuuza kwa urahisi kupitia mifumo iliyorahishwa ya nyaraka za kiforodha na vyeti vya uasili wa bidhaa ukihusisha bidhaa 61. Vilevile, wafanyabiashara hawatalipa ushuru wa forodha kwa bidhaa zilizo ndani ya kiwango cha dola za Marekani 2,000 kwa siku. Aidha, utekelezaji wa mkataba huo utasaidia kuhamasisha wafanyabiashara wadogo kurasimisha biashara zao na kutumia njia rasmi za ufanyaji biashara na hivyo kuongeza biashara baina ya Tanzania na Malawi.

108. *Mheshimiwa Spika,* pamoja na hayo, Serikali imesaini tamko la kuanzisha Kamati ya Pamoja ya Biashara kati ya Tanzania na Uturuki, hatua itakayosaidia kuongeza ujazo wa biashara. Vilevile, imeanza utekelezaji wa Mkataba wa Eneo la Biashara Huru la Utatu ambalo ni COMESA, EAC na SADC unaopanua fursa za biashara kwa wafanyabiashara wa Kitanzania katika masoko ya kikanda.

109. *Mheshimiwa Spika*, ili kuleta uwiano kati ya huduma zinazotolewa, kusafirisha bidhaa na miundombinu iliyopo, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati ya kutatua changamoto ya msongamano wa malori katika mipaka. Mikakati hiyo inajumuisha upanuzi wa barabara ya kuingia kituo cha ukaguzi cha mpaka wa Tunduma kutoka njia mbili hadi nne ambapo utekelezaji umefikia asilimia 15. Vilevile, kuunganisha mifumo ya forodha baina ya Tanzania na Zambia ili kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa.

110. *Mheshimiwa Spika*, aidha, kuendelea kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari kavu na kuharakisha upimaji wa mizigo kwa upande wa Zambia kwa kukamilisha ujenzi wa mdaki *(scanner)* wenye kasi. Utekelezaji wa mikakati hiyo utarahisisha biashara baina ya Tanzania, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

111. *Mheshimiwa Spika,* katika hatua nyingine Serikali imeanza kutekeleza mradi wa upanuzi wa kituo cha Forodha cha Tarakea ambapo hadi Februari, 2026 uhakiki wa fidia kwa ajili ya Wananchi waliopisha mradi huo ulikuwa unaendelea. Hatua hiyo itawezesha kuimarisha utoaji wa huduma na kurahisisha biashara baina ya Tanzania na Kenya.

112. *Mheshimiwa Spika*, ili kuimarisha biashara za Watanzania, ninaelekeza Wizara ya Viwanda na Biashara kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza biashara, kuongeza uzalishaji na kuimarisha ushindani. Vilevile, katika kuboresha maeneo ya kufanyia biashara za wajasiriamali wadogo ikiwemo machinga, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitenge asilimia 5 ya mapato ya ndani ili kujenga na kuboresha miundombinu ya maeneo hayo.

113. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya biashara na kuchochea ukuaji wa sekta binafsi ikiwemo utafutaji wa masoko. Vilevile, itaendelea kuchochea maendeleo ya viwanda na biashara kupitia ubunifu na matumizi ya teknolojia ya kisasa, elimu na mafunzo ya ujuzi.

USAFIRI NA USAFIRISHAJI

Ujenzi

114. *Mheshimiwa Spika*, miundombinu ya usafiri na usafirishaji ni msingi wa uchumi wa Taifa na inachangia katika kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii. Katika kuhakikisha huduma hiyo inakuwa bora, katika mwaka 2025/2026, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara, madaraja, viwanja vya ndege,

vivuko na majengo ya Serikali pamoja na kuwajengea uwezo makandarasi wa ndani.

115. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara nchini, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 4,813.12 na changarawe kilomita 5,741.17. Vilevile, inaendelea kufanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 23,871.59.

116. *Mheshimiwa Spika,* ili kupunguza msongamano wa vyombo vya moto na kurahisisha usafiri, usafirishaji na upatikanaji wa huduma katika Jiji la Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Mbeya, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya upanuzi na ujenzi wa barabara. Kwa upande wa Jiji la Dodoma, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje yenye urefu wa kilomita 112.3 ambapo barabara ya Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa *Dry Port* yenye urefu wa kilomita 52.3 umefikia asilimia 93 na Ihumwa *Dry Port* – Matumbulu – Nala yenye urefu wa kilomita 60 umefikia asilimia 95. Barabara hiyo itawezesha magari kutumia njia hiyo na kuendelea na safari bila kulazimika kupita katikati ya jiji na hivyo kupunguza foleni.

117. *Mheshimiwa Spika,* kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam, miradi inayotekelezwa na Serikali ni pamoja na upanuzi wa barabara ya kilomita 5.2 kutoka njia nne hadi njia nane kati ya Ubungo na Kimara pamoja na upanuzi wa barabara ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe (km 3.8). Miradi mingine ni ujenzi wa barabara za mabasi yaendeyo haraka awamu ya tatu hadi ya tano ambao upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

118. *Mheshimiwa Spika,* kwa upande wa Jiji la Mbeya, Serikali inaendelea kufanya upanuzi wa barabara ya Igawa – Tunduma sehemu ya Uyole – Ifisi (km 29). Aidha, katika Jiji la Mwanza, Serikali imeendelea kutekeleza na kukamilisha mradi wa ujenzi wa Barabara ya Buhongwa – Kishiri – Nyamhongolo (km 12). Utekelezaji wa miradi hiyo upo katika hatua mbalimbali.

119. *Mheshimiwa Spika,* ili kuimarisha uchumi wa nchi ni vema kuhakikisha miundombinu ya barabara inajengwa, inakamilika kwa wakati na kutumika katika kutoa huduma ya usafiri na usafirishaji. Katika kufikia azma hiyo, Wizara ya Ujenzi isimamie ukamilishaji wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara inayoendelea pamoja na kuhakikisha wakandarasi waliosaini mikataba wanatekeleza na kukamilisha miradi hiyo kwa wakati.

120. *Mheshimiwa Spika,* vilevile, katika kuendelea kuimarisha barabara za mijini na vijijini hasa barabara za vipaumbele katika majimbo, ninaelekeza Wizara ya Fedha iimarishe vyanzo vya upatikanaji wa fedha za Mfuko wa Barabara. Aidha, ihakikishe fedha hizo zinapelekwa moja kwa moja kwenye mfuko kama ilivyotengwa kwenye bajeti.

121. *Mheshimiwa Spika,* sambamba na upanuzi wa mtandao wa barabara, Serikali imekamilisha ujenzi wa madaraja ya Mkili (Ruvuma); Mbangala (Mtwara); na Nguyami na Chakwale (Morogoro). Aidha, inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa madaraja makubwa 13 ambayo ni Mirumba, Mitomoni (Ruvuma); Pangani (Tanga); Simiyu (Simiyu); Mbambe (Pwani); Doma (Morogoro); Mwanjiri na Nzali (Dodoma); Suguta (Mara); Sukuma (Mwanza); Jangwani (Dar es Salaam); Kalebe (Kagera); na Kavuu (Katavi). Kukamilika kwa ujenzi wa madaraja hayo, kutarahisisha mawasiliano na kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii.

122. *Mheshimiwa Spika,* kutokana na umuhimu wa usafiri wa anga katika kuharakisha shughuli za kiuchumi na za kijamii, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa viwanja vya ndege kikiwemo Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato. Ujenzi wa kiwanja hicho umefikia asilimia 84 kwa upande wa miundombinu na asilimia 70 kwa ujenzi wa majengo. Kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, uzio wa usalama pamoja na barabara za viungio.

123. *Mheshimiwa Spika,* hatua hizo za Serikali zimeenda sambamba na kuhakikisha wakandarasi wazawa wanajengewa uwezo ili kumudu ushindani katika utekelezaji wa miradi

mbalimbali. Hatua mahsusi iliyochukuliwa na Serikali ni pamoja na kukusanya mitaji ya kuwawezesha wakandarasi wazawa kupitia hatifungani ya Miundombinu iitwayo *Samia Infrastructure Bond*.

124. *Mheshimiwa Spika,* hadi Februari, 2026, shilingi bilioni 9.09 zimekopeshwa kwa wakandarasi wazawa 87 wanaotekeleza miradi ya TARURA. Kupitia hatifungani hizo, wakandarasi wazawa wamepata mitaji ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara na hivyo kukamilisha miradi kwa wakati pamoja na kuepuka gharama za kuhudumia mradi zaidi ya muda uliopangwa.

125. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara za kimkakati ili kufungua fursa za kiuchumi na barabara zinazounganisha makao makuu ya mikoa, wilaya na nchi jirani kwa kiwango cha lami. Vilevile, itaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara za mchepuko, mzunguko na mwendokasi ili kupunguza msongamano katika majiji na miji inayokua kwa kasi pamoja na kuendelea kuimarisha miundombinu na huduma za vivuko, madaraja; na viwanja vya ndege.

Uchukuzi

126. *Mheshimiwa Spika,* sambamba na uwekezaji mkubwa uliofanywa katika sekta ya usafiri na usafirishaji, Serikali imeendelea kuwekeza katika miundombinu ya kimkakati ya reli ya *Standard Gauge Railway* (SGR). Hadi Februari, 2026 ujenzi wa kipande cha Mwanza – Isaka (km 341) umefikia asilimia 67.85; Makutupora – Tabora (km 368) asilimia 14.54; Tabora – Isaka (km 165) asilimia 8.95; na Tabora – Kigoma (km 506) asilimia 9.06.

127. *Mheshimiwa Spika,* vilevile, hatua za maandalizi ya ujenzi wa kipande cha Uvinza – Malagarasi – Msongati (km 282) zinaendelea. Kama waheshimiwa wabunge mtakumbuka tarehe 16 Agosti, 2025 jiwe la msingi la ujenzi wa mradi huo liliwekwa na mkandarasi amelipwa malipo ya awali.

128. *Mheshimiwa Spika,* aidha, kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma, usafirishaji wa mizigo ulianza Juni, 2025 ambapo katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026 tani 52,305 za mizigo zilisafirishwa. Kutekelezwa kwa mradi huo, kumewezesha wananchi, wafanyabiashara na watalii kusafiri kwa haraka na hivyo kupunguza muda wa safari na kuchochea ongezeko la shughuli za kiuchumi.

129. *Mheshimiwa Spika,* kwa upande wa usafiri wa majini, Serikali imeendelea kuongeza ufanisi wa utendaji wa Bandari ya Dar es Salaam kwa kuendelea na ujenzi wa gati mbili kati ya 10 yenye urefu wa mita 500 kila moja ambao umefikia asilimia 10. Pia, inaendelea na ujenzi wa matenki 15 ya kupokelea mafuta mita za ujazo 378,000 ambao umefikia asilimia 41. Uboreshaji wa bandari hiyo utawezesha kuhudumia shehena tani milioni 60 ikilinganishwa na tani milioni 32 zinazohudumia kwa sasa.

130. *Mheshimiwa Spika,* katika kuimarisha miundombinu na huduma za usafiri katika Maziwa Makuu, Serikali imekamilisha maboresho ya Bandari ya Kemondo na kuendelea na maboresho ya Bandari ya Bukoba na Mwanza Kaskazini ambayo yamefikia asilimia 99 na 75 mtawalia. Vilevile, Serikali imekamilisha ujenzi wa meli ya MV New Mwanza yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na mizigo tani 400. Meli hiyo iliyozinduliwa Januari, 2026 inaendelea kutoa huduma kati ya bandari ya Mwanza Kusini, Bandari ya Bukoba na Bandari za Jinja na *Port Bell* zilizopo nchini Uganda.

131. *Mheshimiwa Spika,* ili kuimarisha usalama wa watu, mali na vyombo vya usafiri, Serikali imeanza kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Kuratibu Utafutaji na Uokoaji cha Kikanda *(Maritime Rescue Cordination Centre)* kilichopo katika Ziwa Viktoria. Vilevile, imekamilisha ununuzi wa boti maalum kwa ajili ya huduma za afya za dharura na matibabu ambayo imeanza kutoa huduma.

132. *Mheshimiwa Spika,* kwa upande mwingine, Kampuni ya Ndege Tanzania imeongeza mtandao wa safari na kufikia vituo 33 ikilinganishwa na vituo 26 vilivyohudumiwa mwaka 2024/2025. Kati ya vituo hivyo, vituo 16 ni vya ndani ya nchi, 14 ni

vya kikanda, na vitatu ni vya kimataifa ambavyo ni Victoria Falls (Zimbabwe), Cape Town (Afrika Kusini) na Accra (Ghana). Kuongezeka kwa mtandao wa safari kumewezesha ATCL kusafirisha tani 3,500 za mizigo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Januari 2026 ikilinganishwa na tani 2,567 zilizosafirishwa mwaka 2024/2025. Aidha, abiria 845,275 walisafirishwa katika kipindi hicho.

133. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea na ujenzi na ukarabati wa reli, bandari, meli, vivuko, viwanja vya ndege na uendelezaji wa bandari kavu ili kuimarisha huduma ya usafiri na usafirishaji. Vilevile, itaendelea kuboresha miundombinu ya matanki ya kupokea mafuta bandarini na maeneo ya kuhifadhi shehena.

MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

134. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali katika kuendeleza Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, imeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kuunganisha Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia Ziwa Tanganyika. Hatua hiyo, inalenga kuchochea biashara kati ya nchi zetu na kuongeza mapato ya Serikali kupitia huduma za Mkongo huo.

135. ***Mheshimiwa Spika***, Wilaya za Kilwa, Maswa, Bariadi, Sikonge, Urambo, Ushirombo, Chunya, Karagwe, Nzega na Butiama zimeunganishwa kwenye Mkongo wa Taifa. Hivyo kufanya jumla ya wilaya zilizounganishwa kufikia 120 kati ya 139 sawa na asilimia 86.

136. ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na upanuzi wa mtandao wa mkongo wa Taifa, Serikali imekamilisha ujenzi wa minara 758 katika kata 713 kwa gharama ya shilingi bilioni 126 ili kuongeza kasi ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano. Vilevile, minara 304 imeongezewa uwezo kutoka teknolojia ya 2G kwenda 3G na 4G ili kuongeza kasi ya intaneti na kurahisisha shughuli za biashara na uzalishaji.

137. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano

kwa kujenga na kukamilisha minara ya simu na redio. Vilevile, itaendelea kuhakikisha wilaya zilizobaki zinaunganishwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

HUDUMA ZA JAMII

Elimu

138. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha sekta ya elimu kwa kuzingatia Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 (Toleo la 2023), mitaala iliyoboreshwa, mipango na mikakati mbalimbali. Lengo ni kuzalisha rasilimaliwatu wenye ujuzi na maarifa stahiki yatakayowezesha kumudu ushindani wa ajira na uwezo wa kujiajiri ndani na nje ya nchi.

139. ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini inaonesha kuwa wanafunzi 3,021,177 wanatarajiwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2028. Jumla ya gharama zinazohitajika ni shilingi trilioni 1.77 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 23,226; matundu ya vyoo 46,632; maabara 9,366; ajira mpya za walimu 40,192; ruzuku ya vitabu na uendeshaji pamoja na ruzuku ya mitihani na upimaji.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha wanafunzi wote wanapata nafasi ya kuendelea na masomo, kwa mwaka 2026/2027, Serikali kupitia mapato ya ndani ya halmashauri imetenga shilingi bilioni 139.28 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 4,193 na matundu ya vyoo 13,943. Aidha, kupitia Serikali kuu zimetengwa shilingi bilioni saba kwa ajili ya ujenzi wa maabara 233.

141. ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua nyingine, Serikali imetoa shilingi bilioni 88.84 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya 103 za amali. Kati ya hizo, ujenzi wa shule 27 umekamilika na zinatumika. Vilevile, hadi Februari 2026, shule 158 za Sekondari ya Chini zinatekeleza mkondo wa amali wa mitaala iliyoboreshwa ikilinganishwa na shule 41 zilizoanza mwaka 2024.

142. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa ajili ya kuboresha ufundishaji wa masomo ya amali, Serikali imepeleka walimu 150 mafunzo ya

muda mfupi nchini India. Aidha, walimu 156,948 kati 172,609 kutoka shule za msingi 17,111 walishiriki mafunzo endelevu kazini.

Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu

143. *Mheshimiwa Spika,* Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu pamoja na kukamilisha maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi. Lengo ni kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu katika maeneo yote na kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

144. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2025/2026, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa shule mpya za msingi 277. Vilevile, imeongeza miundombinu katika shule za msingi na sekondari zilizopo kwa kujenga madarasa 5,439, majengo ya utawala saba, mabweni 21, hosteli 26, nyumba za walimu 69, maabara 46, mabwalo matano na vituo vya walimu 70.

145. *Mheshimiwa Spika,* kwa upande wa ukarabati, Serikali imekamilisha ukarabati wa shule za msingi 228. Vilevile, imekamilisha ujenzi wa miundombinu iliyojengwa kwa nguvu za wananchi ikiwemo maboma 132 ya mabweni ya shule za sekondari, vyumba vya madarasa 697 katika shule za msingi na vyumba vya maabara 175. Aidha, ninatoa pongezi na shukrani kwa Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupeleka vifaa vya maabara katika shule za sekondari 231 zikiwemo shule mpya 26 maalumu za kitaifa za sayansi za wasichana.

146. *Mheshimiwa Spika,* kutokana na jitihada za Serikali za kuboresha miundombinu na mazingira ya kujifunzia na kufundishia, uandikishaji na ufaulu wa wanafunzi katika ngazi mbalimbali za elimu umeongezeka. Kwa upande wa uandikishaji, hadi Februari, 2026, wanafunzi 1,407,761 wa darasa la awali sawa na asilimia 70.8 ya lengo la 1,987,472 wameandikishwa na wanafunzi 1,681,549 wa darasa la kwanza sawa na asilimia 86.2 ya lengo la 1,950,783 wameandikishwa. Vilevile, wanafunzi 739,676 sawa na asilimia 78.89 ya lengo la 937,581 wameandikishwa kujiunga na kidato cha kwanza. Nitumie fursa hii pia kuwataka wazazi na walezi kuhakikisha wanawapeleka watoto wote wenye

sifa shuleni. Aidha, nawaelekeza Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kusimamia na kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kwenda shule wanaandikishwa.

147. *Mheshimiwa Spika,* kwa upande wa wanafunzi wa darasa la nne ufaulu umeongezeka kutoka asilimia 86.24 mwaka 2024 hadi asilimia 88.91 mwaka 2025 na kwa darasa la saba umeongezeka kutoka asilimia 80.87 mwaka 2024 hadi asilimia 81.80 mwaka 2025.

148. *Mheshimiwa Spika,* kwa upande wa kidato cha pili, ufaulu umeongezeka kutoka asilimia 85.41 mwaka 2024 hadi asilimia 86.93 mwaka 2025 na kidato cha nne, ufaulu umeongezeka kutoka asilimia 92.37 mwaka 2024 hadi asilimia 94.98 mwaka 2025. Vilevile, kwa kidato cha sita ufaulu umefikia asilimia 99.95 mwaka 2025.

149. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango wa Elimu Bila Ada kwa kugharimia elimu ya awali hadi elimu ya sekondari ya juu. Hadi Februari, 2026 shilingi bilioni 383.22 kati ya shilingi bilioni 510.96 sawa na asilimia 75 zilitolewa kwa shule za msingi 18,119 na shule za sekondari 5,179.

150. *Mheshimiwa Spika,* vilevile, Serikali imewezesha upatikanaji wa vifaa vyenye thamani ya shilingi bilioni 5.4 kwa ajili ya matumizi ya walimu na wakufunzi wenye mahitaji maalum. Vifaa hivyo ni pamoja na kompyuta mpakato, vifaa vya kuandikia na kuhifadhi taarifa kwa *braille*, vinasa sauti, vishkwambi vinavyotafsiri kwa lugha ya alama, vikuza sauti, kivunge cha vifaa vya kuongeza uwezo wa kuona na vifaa vya kupima usikivu. Serikali itaendelea kugharimia vifaa kwa ajili ya wanafunzi na walimu hao kwa lengo la kutoa fursa sawa katika kufundisha na kujifunza.

151. *Mheshimiwa Spika*, sambamba na hilo, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa vyuo vya VETA 64 vya wilaya ambao umefikia wastani wa asilimia 67 na chuo kimoja cha Mkoa wa Songwe kilichofikia asilimia 68. Hatua hii ni utekelezaji wa azma ya Serikali ya kuwa na chuo cha VETA katika kila mkoa na wilaya. Lengo ni kusogeza huduma za mafunzo ya

ufundi stadi karibu na wananchi ili kuongeza ujuzi, kukuza ajira, na kuongeza kasi ya maendeleo ya uchumi wa viwanda.

152. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na umuhimu wa elimu ya kati na elimu ya juu, Serikali inaendelea kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu hiyo nchini. Kwa upande wa elimu ya juu, kwa mwaka 2025/2026 wanafunzi 170,916 wamedahiliwa katika vyuo vikuu ikilinganishwa na wanafunzi 137,781 waliodahiliwa mwaka 2024/2025. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 24.

153. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha fursa za masomo ya elimu ya kati na elimu ya juu inapatikana kwa makundi yote ya kijamii, Serikali imeendelea kutoa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na elimu ya kati. Jumla ya shilingi bilioni 899.21 zimetolewa katika mwaka 2024/2025 ambapo shilingi bilioni 348.77 zimetolewa kwa wanafunzi 107,541 wa mwaka wa kwanza na shilingi bilioni 550.44 imetolewa kwa wanafunzi 177,492 wanaoendelea na masomo.

154. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Serikali imetoa ufadhili wa shilingi bilioni 9.46 kupitia *SAMIA Scholarship* kwa wanafunzi 1,786 wenye ufaulu unaojipambanua wanaosoma masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati katika vyuo vikuu hapa nchini. Vilevile, imetoa ufadhili wa shilingi bilioni 5.487 kupitia *SAMIA Scholarship Extended* kwa wanafunzi 50 wenye ufaulu wa juu wa kidato cha sita katika fani za sayansi waliochaguliwa kusoma Shahada ya Kwanza katika fani za Sayansi Data, Akili Unde na Sayansi Shirikishi katika vyuo bora duniani.

155. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na utoaji wa mikopo, Serikali inaendelea kuimarisha miundombinu katika taasisi za elimu ya juu. Katika mwaka 2025/2026 imekamilisha ujenzi wa kampasi mpya 2 na inaendelea na ujenzi na ukarabati wa Kampasi nyingine 14 ambao umefikia hatua mbalimbali za ukamilishaji. Lengo ni kusogeza huduma ya elimu ya juu karibu na wananchi kwa kuhakikisha kila mkoa unakuwa na taasisi ya elimu ya juu.

Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

156. *Mheshimiwa Spika*, Serikali inatekeleza afua mbalimbali za kuendeleza wabunifu na kufanya teknolojia zao kuwa bidhaa. Afua hizo ni pamoja na uwepo wa Mfuko wa *Samia Innovation Commercialization Fund* kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wabunifu ambapo jumla ya shilingi milioni 667 zimetolewa katika awamu ya kwanza kwa wabunifu saba. Miongoni mwa bunifu zilizokopeshwa ni pamoja na uchakataji na usambazaji wa asali bora na mafuta ya mawese kwa ajili ya masoko ya nje pamoja na mfumo wa kudhibiti foleni katika hospitali. Vilevile, Serikali imekamilisha na kuidhinisha Mkakati wa Kitaifa wa Kuhamasisha mchango wa Diaspora katika shughuli za Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu.

157. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuboresha na kuongeza miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu. Vilevile itaendelea kutekeleza mpango wa elimu bila ada na kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na vyuo vya kati. Aidha, itaendelea kuimarisha uwezo wa nchi katika utafiti, matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchochea ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Afya

158. *Mheshimiwa Spika,* pamoja na kuimarisha upatikanaji na utoaji wa huduma ya elimu, Serikali imeendelea kusimamia ubora, usalama na ufanisi wa utoaji wa huduma za afya nchini kwa kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa katika ngazi zote kuanzia zahanati hadi Taifa. Vilevile, imeendelea kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi pamoja na kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya dawa, vitendanishi, vifaa na vifaa tiba ili kuhakikisha nchi inakuwa na utoshelevu.

159. *Mheshimiwa Spika,* jitihada hizo zinaenda sambamba na kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya kwa kuendelea kutekeleza miradi ya ujenzi 113 ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kati ya miradi hiyo, miradi 45 inatekelezwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa; miradi 11 katika Hospitali ya Taifa, Maalum na Hospitali za Kanda; miradi 9 katika vyuo vya mafunzo; na miradi 48 katika Hospitali za Halmashauri.

160. *Mheshimiwa Spika,* vilevile, Serikali imeajiri wataalamu 4,183 kwa utaratibu wa ajira za mikataba ya muda mfupi kwa kutumia mapato ya ndani ya taasisi husika. Kati yao, watumishi 3,202 wameajiriwa kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda, Maalum na Hospitali ya Taifa Muhimbili na watumishi 981 wameajiriwa ngazi ya afya ya msingi. Pia, watumishi 1,000 wa mikataba wameajiriwa kupitia programu ya uwekezaji katika afya ya mama na mtoto Tanzania.

161. *Mheshimiwa Spika,* uwekezaji wa Serikali ya Awamu ya Sita katika huduma za afya umeongeza upatikanaji kwa bidhaa za afya za kipaumbele 290 katika vituo vya kutolea huduma za afya kutoka wastani wa asilimia 80 mwaka 2024 hadi wastani wa asilimia 89 Februari, 2026. Aidha, hadi Januari, 2026, Serikali imetoa ruzuku ya shilingi bilioni 209.5 kwenye vituo kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa za afya. Pia, imetoa shilingi bilioni 33.80 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika Hospitali za Halmashauri 142, vituo vya afya 184 na zahanati 184.

162. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma bingwa na bobezi, Serikali inatekeleza mikakati mahsusi ya kuongeza madaktari bingwa na bingwa bobezi. Moja ya mikakati hiyo ni kuanzisha programu ya ufadhili ya *Samia Health Super-specialization Program*. Kupitia programu hiyo, jumla ya wataalamu 1,483 wamepata ufadhili wa masomo katika fani za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi.

163. *Mheshimiwa Spika,* ufadhili wa masomo kwa wataalamu hao utaongeza idadi ya wataalamu watakaotoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi nchini. Aidha, kuimarika kwa utoaji wa huduma za afya nchini kumewezesha wagonjwa kutoka nje ya nchi kuja nchini kwa ajili ya kupata huduma za matibabu.

164. Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maono haya makubwa. Hakika Mheshimiwa Rais amethibitisha kwa vitendo dhamira yake njema ya kuthamini na kujali afya na utu wa Watanzania kwa

kuhakikisha huduma za kibingwa na bingwa bobezi zinapatikana hapa nchini.

165. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha utoaji wa huduma bora za afya. Hatua hizo ni pamoja na kuongeza uwezo wa nchi kuzalisha dawa na vifaa tiba, mifumo ya ugharimiaji wa huduma za afya, kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA, kuboresha miundombinu, kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya, kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi, utafiti na kuimarisha tiba utalii.

Mapambano Dhidi ya VVU na UKIMWI

166. *Mheshimiwa* Spika, katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI, jitihada zilizofanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, zimewezesha Taifa letu kupiga hatua kubwa katika kupunguza maambukizi mapya ya VVU, kudhibiti maradhi na vifo vitokanavyo na UKIMWI na WAVIU wengi kuishi maisha yenye afya na tija kutokana na matibabu bora ya kufubaza VVU.

167. *Mheshimiwa Spika*, tathmini ya hali ya mwitikio dhidi ya UKIMWI imeonesha kuwa takribani watu 1,700,000 wanaishi na Virusi Vya UKIMWI. Aidha, tathmini hiyo imebaini kuwa kiwango cha watu wanaotambua hali za maambukizi ya VVU imeongezeka kutoka asilimia 91 mwaka 2024 hadi asilimia 92 mwaka 2025; WAVIU wanaotumia dawa za kufubaza VVU imeongezeka kutoka asilimia 98 mwaka 2024 hadi asilimia 98.5 mwaka 2025; na WAVIU wanaotumia dawa za ARV ambao wamefubaza VVU imeongezeka kutoka asilimia 97 mwaka 2024 hadi asilimia 98.1 mwaka 2025.

168. *Mheshimiwa Spika*, mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya vituo vinavyotoa huduma ya tiba na matunzo kwa WAVIU ili kuhakikisha huduma za VVU na UKIMWI zinapatikana kwa urahisi kutoka vituo 7,805 kwa mwaka 2024 hadi vituo 8,203 kwa mwaka 2025; idadi ya mashine kubwa za kupima wingi wa VVU mwilini zimeongezeka kutoka mashine 43 mwaka 2024 hadi 50 mwaka 2025; na kuendelea kuhakikisha

Dawa za kufubaza makali ya VVU zinapatikana kwa asilimia 100 ambazo hutolewa bure kwa WAVIU wote.

169. *Mheshimiwa Spika*, ili kuimarisha uwezo wa ndani katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI, Serikali imeendelea kutafuta vyanzo vya fedha vya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI. Hadi Februari, 2026, Serikali imekusanya shilingi bilioni 26.8 kupitia Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI. Hatua hii ni muhimu kwa nchi yetu kujitegemea na kuimarisha uwezo wa ndani katika kugharimia mwitikio, kinga na tiba dhidi ya VVU na UKIMWI.

170. *Mheshimiwa* Spika, katika mwaka 2026/2027 Serikali itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kufikia lengo la kutokomeza UKIMWI kama janga la afya ya jamii ifikapo mwaka 2030. Mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea kushirikiana na wadau wote wa maendeleo katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI kwa kugharimia kinga, tiba pamoja na matunzo.

Uratibu wa Masuala ya Lishe

171. *Mheshimiwa* Spika, masuala ya lishe ni muhimu sana katika kuimarisha nguvukazi inayotarajiwa kutekeleza mipango na mikakati yote ya Serikali. Kwa kutambua hilo, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa Pili wa Taifa wa Lishe (2021/2022 – 2025/2026) ambao utekelezaji wake unafikia ukomo Juni, 2026. Mafanikio yaliyopatikana kupitia utekelezaji wa mpango huo ni pamoja na kupungua kwa udumavu kwa watoto walio na umri chini ya miaka 5 kutoka asilimia 34 hadi 30. Pia, kuajiri wataalamu 637 wa lishe na kupangwa katika mikoa yote. Vilevile, kupitia programu ya Uwekezaji katika Afya ya Mama na Mtoto Tanzania, watumishi 400 wameajiriwa kwa mkataba ili kutekeleza afua mbalimbali zikiwemo za lishe.

172. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kufanya maandalizi ya mpango wa muda mrefu wa lishe 2026 – 2050 ambao utekelezaji wake utashabihiana na utekelezaji wa Dira 2050. Mpango huo utatoa mwelekeo kwa wadau wote wa masuala ya lishe nchini.

Maji

173. *Mheshimiwa Spika,* huduma ya maji ni muhimu sana kwa uhai wa viumbe vyote. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya maji na kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji katika maeneo mbalimbali nchini. Jitihada hizo zimeimarisha wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya vijijini kutoka asilimia 83.0 Desemba, 2024 hadi asilimia 85.2 Desemba, 2025 na kwa maeneo ya mijini kutoka asilimia 91.6 Desemba, 2024 hadi asilimia 92.5 Desemba 2025.

174. *Mheshimiwa Spika,* miradi mingine ya kimkakati inayotekelezwa ni pamoja na mradi wa maji wa miji 28 ya Tanzania Bara katika miji ya Handeni, Korogwe, Muheza, Pangani, Kilwa Masoko, Nanyumbu, Ifakara, Rujewa, Chunya, Njombe, Makambako, Wanging'ombe na Kiomboi. Miji mingine ni Singida, Manyoni, Mugumu, Chemba, Kasulu, Mpanda, Sikonge, Urambo, Kaliua, Kayanga, Chato, Geita, Newala, Nanyamba na Tandahimba, pamoja na sehemu ya Halmashauri za Wilaya za Mtwara, Mafinga, Rorya - Tarime na Songea. Utekelezaji wa miradi katika miji hiyo umefikia kati ya asilimia 14 na 89.8. Kukamilika kwa miradi hiyo kutanufaisha wananchi wapatao 5,985,500 wa maeneo hayo.

175. Mheshimiwa Spika, vilevile, ujenzi wa Bwawa la Kidunda unaogharimu shilingi bilioni 329.46 umefikia asilimia 40. Mradi huo ukikamilika utaimarisha utiririshaji wa maji ya Mto Ruvu katika kipindi chote cha mwaka na kulisha mitambo ya kuzalisha maji ya Ruvu Juu na Ruvu Chini. Lakini pia, utazalisha umeme megawati 20, kuwezesha shughuli za kilimo cha umwagiliaji na kuzuia mafuriko.

176. *Mheshimiwa Spika,* kwa upande wa vijijini, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati yenye gharama ya shilingi bilioni 349.59. Utekelezaji wa miradi hiyo, umefikia kati ya asilimia 5 hadi 75. Kukamilika kwa miradi hiyo kutahudumia vijiji 225**.**

177. *Mheshimiwa Spika,* kwa mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya kimkakati itakayounganishwa kwenye Gridi ya Taifa ya Maji inayohusisha kutoa maji maeneo yenye vyanzo vya uhakika kupeleka maeneo yenye uhaba wa maji. Vilevile, itaandaa Mpango Kabambe kwa lengo la kutoa mwelekeo wa muda mrefu na wa kimkakati wa kitaifa wa kusimamia, kuendeleza na kutumia rasilimali za maji kwa njia endelevu.

URATIBU WA MASUALA YA WATU WENYE ULEMAVU

178. *Mheshimiwa Spika,* Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa jamii ya Watu Wenye Ulemavu inaendelea kupata huduma muhimu za kuimarisha haki na ustawi wao pamoja na kuwawezesha kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali. Ili kufanikisha azma hiyo, Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu imetoa ruzuku ya shilingi milioni 238.92 kwa vyama 13 vya Watu Wenye Ulemavu ili kuendeleza shughuli zao.

179. *Mheshimiwa Spika,* aidha, Serikali imeiwezesha Bohari ya Dawa kuzalisha na kusambaza vifaa saidizi na mafuta kinga kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu. Vilevile, kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imetoa chupa 105,557 za mafuta ya kujikinga na mionzi ya jua kwa watu wenye ualbino katika mikoa 24 ya Tanzania Bara. Kadhalika, imewezesha upasuaji wa saratani ya ngozi kwa watu wenye ualbino katika Taasisi ya Utafiti wa Saratani ya Ocean Road na Hospitali ya KCMC.

180. *Mheshimiwa Spika,* Serikali imewezesha kituo atamizi kilichopo Chuo cha Ufundi Sabasaba Singida kuimarisha ujuzi kwa wanafunzi Wenye Ulemavu. Vilevile, imeimarisha huduma ya utengamao kwa watoto wenye ulemavu hususan vichwa vikubwa, mgongo wazi na wenye usonji ili kupunguza madhila yanayotokana na kuwahudumia watoto hao.

181. *Mheshimiwa Spika,* katika hatua nyingine, Serikali imetoa huduma ya afya ya macho kwa kufanya uchunguzi kwa watu 91,227 ambapo watu 11,047 waliobainika kuwa na matatizo ya macho walipatiwa miwani. Vilevile, imetoa vifaa saidizi kwa Watu Wenye Ulemavu katika Mikoa ya Kigoma, Ruvuma, Mbeya,

Tanga, Shinyanga, Mara na Dodoma ambapo watu 6,618 wamenufaika.

182. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha mfumo wa uratibu wa Watu Wenye Ulemavu, Serikali imekamilisha ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Kuratibu na Kusimamia Watu Wenye Ulemavu. Mfumo huo unapokea taarifa binafsi na takwimu zote sahihi za Watu Wenye Ulemavu zitakazowezesha kutambua mahitaji yao kwa ajili ya kupanga mipango mikakati na bajeti. Maafisa TEHAMA na Ustawi wa Jamii kutoka Halmashauri zote za Mikoa 14 ya Mara, Simiyu, Mwanza, Shinyanga, Geita, Kagera, Kigoma, Katavi, Tabora, Dodoma, Ruvuma, Mtwara, Lindi na Njombe wamejengewa uwezo kuhusu mfumo huo.

183. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha huduma kwa Watu Wenye Ulemavu kwa kuratibu afua za ulinzi na ustawi, kuratibu programu za uwezeshaji kiuchumi na kuendeleza ujuzi. Vilevile, Serikali itaandaa utaratibu maalumu wa kuwawezesha na kuwasaidia Watu Wenye Ulemavu pamoja na wale wanao wahudumia.

URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI BUNGENI

184. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali imeendelea kuratibu shughuli zake Bungeni. Moja ya shughuli zilizofanywa katika Mkutano wa Pili wa Bunge la 13 ni kuratibu uwasilishaji wa Hotuba ya Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hotuba aliyoitoa tarehe 14 Novemba, 2025 wakati wa ufunguzi rasmi wa Bunge la 13 na kujadiliwa na Bunge. Nilihakikishie Bunge lako tukufu kuwa, Serikali inaahidi kuendelea kutekeleza ahadi zote zilizotolewa na Mheshimiwa Rais.

185. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mjadala wa hotuba ya Mheshimiwa Rais, miswada miwili ilisomwa kwa mara ya kwanza na nyaraka muhimu za kimkakati ziliwasilishwa na kuidhinishwa na Bunge. Nyaraka hizo ni pamoja na Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/2027- 2050/2051, Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027– 2030/2031), Mapendekezo ya Mpango wa

Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/2027 na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Muda wa Kati wa 2026/2027- 2028/ 2029. Aidha, maswali ya msingi 146, maswali ya nyongeza 482 na maswali ya papo kwa papo saba yaliulizwa na wabunge na kujibiwa na Serikali.

UCHAPAJI WA NYARAKA ZA SERIKALI

186. *Mheshimiwa Spika,* ili kuongeza ufanisi na utoaji huduma za uchapishaji wa nyaraka za Serikali, mikakati mbalimbali imetekelezwa. Mikakati hiyo ni pamoja na kuiongezea hadhi iliyokuwa Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kuwa Wakala.

187. Mheshimiwa Spika, mabadiliko hayo yameenda sambamba na kuimarisha Wakala huo kwa kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa kiwanda cha uchapishaji, kununua na kufunga mashine mpya nane za uchapishaji. Vilevile, imeendelea na ujenzi wa jengo la utawala na uzio ambao umefikia asilimia 78.

188. *Mheshimiwa Spika,* nitumie fursa hii kuzikumbusha Wizara, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi, Wakala na Idara za Serikali zinazojitegemea kuchapa nyaraka za Serikali kupitia Wakala huo. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009, Tamko Na. 2 la Serikali kupitia Tangazo la Serikali Na. 750A la tarehe 15 Agosti, 2014 na Waraka wa Uchapishaji wa Nyaraka za Serikali wa tarehe 14 Februari, 2024.

ULINZI NA USALAMA

189. *Mheshimiwa Spika,* ulinzi wa mipaka ya nchi yetu ni suala muhimu katika kuhakikisha wananchi wanaendelea kufanya shughuli za uzalishaji mali bila bughudha yoyote. Pamoja na ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeshiriki katika ulinzi na usalama kikanda na kimataifa.

190. *Mheshimiwa Spika,* Jeshi letu lilishiriki katika operesheni mbalimbali za ulinzi wa amani kikanda na kimataifa. Operesheni hizo ni pamoja na zinazoendeshwa na Umoja wa Mataifa na

Jumuiya za Kikanda katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Afrika ya Kati, Lebanon na Sudan Kusini. Aidha, ushiriki katika operesheni hizo umeiwezesha nchi yetu kujenga uwezo, kuimarisha diplomasia ya ulinzi, uhusiano na kutimiza matakwa ya Umoja wa Mataifa na Jumuiya za Kikanda.

191. *Mheshimiwa Spika,* kutokana na umuhimu wa kulinda usalama wa raia na mali zao, Serikali imeendelea kuimarisha vyombo vya usalama. Eneo mojawapo lililopewa kipaumbele ni kulijengea uwezo Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kulipatia vifaa na kujenga vituo vipya vya zimamoto.

192. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2025/2026 vifaa na mitambo ya kuzima moto yenye thamani ya dola za Marekani milioni 100 imenunuliwa na kusambazwa mikoa yote nchini. Aidha, imejenga vituo saba vya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika Mikoa ya Songwe, Simiyu, Katavi, Geita, Manyara, Njombe na Kagera.

193. *Mheshimiwa Spika,* suala la utambuzi wa raia limeendelea kuwa kipaumbele cha Taifa letu kutokana na umuhimu wake katika ulinzi na usalama lakini pia utoaji wa huduma za jamii. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Januari 2026, Serikali imesajili wananchi 435,953 na hivyo kufikisha idadi ya wananchi 26,477,044 waliosajiliwa nchini sawa na asilimia 84.1 ya watu wote wenye sifa za kusajiliwa. Aidha, taasisi 138 za umma na binafsi zimeunganishwa katika mfumo wa usajili na utambuzi ili kurahisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

194. *Mheshimiwa Spika,* katika zama za sasa ambapo Dunia inakumbwa na changamoto za kiusalama, ni muhimu kwa wananchi wote bila kujali itikadi za dini na siasa kulinda rasilimali za Taifa, kuongeza uzalendo, kupinga chuki na vitendo vyovyote vinavyoweza kuvuruga mshikamano wa Taifa. Jitihada hizo zitaepusha maadui wanaoweza kujipenyeza na kuhatarisha ulinzi na usalama wa Taifa letu pamoja na maendeleo.

195. *Mheshimiwa Spika*, aidha, nitoe wito kwa wazazi na walezi kuendelea kushirikiana kwa karibu na taasisi za elimu na dini katika kuimarisha malezi ya watoto na vijana. Misingi imara ya

maadili, uzalendo na matumizi sahihi ya teknolojia na utandawazi yatawawezesha watoto na vijana kufikia ndoto zao pamoja na kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa.

196. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha ulinzi wa mipaka ya nchi yetu na usalama wa raia na mali zao. Aidha, itaendelea kuviimarisha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuvipatia zana, vifaa na rasilimaliwatu.

KUKUZA FURSA ZA AJIRA NA UJUZI

197. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuratibu uzalishaji wa fursa za ajira nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na kubaini fursa kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali, kujenga mazingira wezeshi kwa wawekezaji na kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali na sekta binafsi.

198. *Mheshimiwa Spika,* hadi Februari, 2026, fursa za ajira 625,273 zilizalishwa. Kati ya ajira zilizozalishwa, ajira 242,656 za wazawa zilitokana na vibali 12,549 vilivyotolewa kwa wageni sawa na uwiano wa mgeni 1 kwa wazawa 19 ikilinganishwa na uwiano wa mgeni 1 kwa wazawa 10 kama ilivyoainishwa katika Sheria ya kuratibu Ajira za Wageni, Sura 436.

199. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Serikali imewezesha upatikanaji wa fursa za ajira 6,367 kwa Watanzania katika nchi za Saudia, Qatar, Oman na Umoja wa Falme za Kiarabu. Nchi nyingine ni pamoja na Bahrain, Denmark, Ujeruman, Kuwait, Poland, Bosnia, Sweden, Romania, Guyana, Marekani, Mauritius na Ireland.

200. *Mheshimiwa Spika*, aidha, Agosti, 2025, Serikali ilizindua Mfumo wa Taifa wa Taarifa za Soko la Ajira ambao unatumika kukusanya, kuchambua na kutangaza taarifa za soko la ajira. Vilevile, Serikali inaendelea kutekeleza Mwongozo wa Uratibu wa Mawakala Binafsi wa Ajira wa Mwaka 2025 na kuendelea kuingia makubaliano na nchi husika ili kuhakikisha Watanzania wanafanya kazi za staha kwa kipato stahiki.

201. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na kuwezesha uzalishaji wa fursa za ajira, Serikali imeendelea kuhakikisha nguvukazi inapata ujuzi utakaowawezesha kujiajiri au kuajiriwa. Ili kufikia azma hiyo, katika mwaka 2025/2026 Serikali imewezesha mafunzo ya ufundi stadi kwa njia ya uanagenzi kwa vijana 5,746 katika vyuo na taasisi za mafunzo 46. Vilevile, imetoa mafunzo ya kukuza ujuzi kwa wakulima na wasindikaji wadogo 1,065 wa mazao mbalimbali ili kupunguza upotevu na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo.

202. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, imewezesha mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa njia ya utarajali kwa vijana 2,500 na mafunzo maalum ya kushindania fursa za ajira ndani na nje ya nchi kwa vijana 7,826. Aidha, Serikali imesaini hati ya ushirikiano na Serikali ya Japan kuhusu utoaji wa mafunzo kwa vitendo kwa vijana katika kampuni mbalimbali za ujenzi nchini Tanzania na Japan.

203. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kisera kwa lengo la kukuza fursa za ajira jumuishi, endelevu na zenye staha kwa kuzingatia mabadiliko ya kijamii, kisayansi, kiteknolojia na kiuchumi yanayotokea duniani.

MASUALA YA KAZI NA WAFANYAKAZI

204. Mheshimiwa Spika, watumishi wa umma ni nguzo ya msingi katika utekelezaji wa sera, dira, mipango na mikakati ya Serikali. Kwa kutambua umuhimu wa watumishi wa umma, Serikali ya Awamu ya Sita baada ya kuingia madarakani hadi Machi, 2026 imepandisha vyeo/madaraja jumla ya watumishi 662,707 kati ya 678,115 waliopo kwenye orodha ya walipwa mishahara. Kadhalika, katika kipindi hicho, Serikali imebadilisha kada/miundo watumishi 42,515 kwa gharama ya shilingi bilioni 3.52. Vilevile, imelipa madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi 148,137 yenye jumla ya shilingi bilioni 248.52 na imeajiri watumishi wapya 155,008. Aidha, Serikali itaendelea kuajiri, kupandisha vyeo na madaraja, kuongeza mishahara na kuwaendeleza watumishi ndani ya utumishi wa umma kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu.

205. *Mheshimiwa Spika,* hata hivyo, mwenendo wa malipo ya mishahara unaonesha kuwa lipo kundi la watumishi wapatao 7,447 ambao wanalipwa mishahara binafsi isiyoendana na majukumu wanayofanya. Hadi tarehe 26 Machi, 2026 watumishi hao wamelipwa mishahara binafsi kwa gharama ya shilingi bilioni 14.34.

206. *Mheshimiwa Spika,* kutokana na hali hiyo, Serikali itafanyia kazi masuala yafuatayo: ***Mosi,*** kuwianisha mishahara ya watumishi wa umma pamoja na kupunguza tofauti kubwa ya viwango vya mishahara katika utumishi wa umma na sekta binafsi. ***Pili,*** kuhuisha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 na kanuni zake kuhusu idhini ya utoaji wa kibali cha mshahara binafsi. ***Tatu,*** kuhuisha Waraka unaohusu Watumishi watakaobadilishwa kazi ili kuendana na mahitaji ya sasa. Vilevile, kufanya mapitio ya Waraka kuhusu utaratibu wa kushughulikia maombi ya mishahara binafsi kwa watumishi wa umma.

207. *Mheshimiwa Spika,* Serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya kazi kwa kukamilisha na kutangaza Amri ya Kima cha Chini cha Mshahara kwa Sekta Binafsi kilichoongezeka kwa viwango tofauti kwa kuzingatia sekta. Utekelezaji wa amri hiyo ulianza rasmi Januari, 2026. Aidha, katika kuimarisha utekelezaji wa amri hiyo, Serikali inaendelea kufanya ukaguzi na kutoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi kote nchini.

208. *Mheshimiwa Spika*, watoto ni kundi maalumu ambalo linahitaji afua mahsusi ili kuhakikisha kila mtoto anapata haki zake kama zilivyoainishwa kwenye sheria za nchi pamoja na mikataba ya kimataifa. Hatua mojawapo iliyochukuliwa na Serikali ni kukamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Kutokomeza Utumikishwaji wa Mtoto (2025/2026 – 2030/2031).

209. *Mheshimiwa Spika*, mkakati huo ni chachu ya kulinda haki ya mtoto dhidi ya utumikishwaji katika kazi zinazoweza kuathiri afya, makuzi na maendeleo ya kielimu na kijamii. Pamoja na mambo mengine, unalenga kukuza uelewa wa jamii kuhusu madhara ya utumikishwaji wa mtoto na kuhamasisha ushiriki wa wadau wote katika kulinda haki za mtoto.

210. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuweka mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi na waajiri kwa kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Majadiliano baina ya Serikali, Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri. Aidha, itaandaa Mwongozo wa Usajili, Usimamizi na Uratibu wa Vyama vya Wafanyakazi, Vyama vya Waajiri na Mashirikisho; na Kuratibu utekelezaji wa Programu ya Nchi ya Kazi za Staha (2025/2026 – 2029/2030).

USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI

211. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuhakikisha maeneo ya kazi yanakuwa na mifumo ya kudhibiti athari za vihatarishi ili kupunguza ajali, magonjwa na vifo vitokanavyo na kazi kwa kufanya kaguzi mbalimbali. Hadi Februari, 2026, kaguzi maalum 196,701 zimefanyika katika maeneo ya viwanda, migodi na sekta ya usafirishaji na kuchukua hatua stahiki kwa maeneo yaliyobainika kuwa na changamoto. Vilevile, imefanya uchunguzi wa afya kwa wafanyakazi 289,611 na kutoa ushauri stahiki kwa wafanyakazi 123,802 waliobainika kuwa na changamoto mbalimbali.

212. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuhakikisha maeneo ya kazi yanaendelea kuwa salama kwa wafanyakazi kwa kuendelea kusimamia sheria, kanuni na miongozo ya usalama mahali pa kazi. Vilevile, itaendelea kuimarisha uwezo wa wataalamu na kitaasisi katika kushughulikia masuala ya usalama na afya mahali pa kazi.

MAENDELEO YA VIJANA

213. *Mheshimiwa Spika,* sote tunatambua kuwa, vijana ni nguvukazi muhimu ya kujenga uchumi wa Taifa letu. Kutokana na ukweli huo, Serikali imeendelea kuhakikisha vijana wa Tanzania wanawezeshwa kiuchumi, kijamii na kielimu ili kujipatia ajira na kutumia uwezo wao kikamilifu kuchangia maendeleo ya Taifa. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imeanzisha Wizara maalumu inayoshughulikia masuala ya vijana ili kuwapa sauti ya kuwasilisha mawazo yao ambayo yatajumuishwa kwenye mipango ya maendeleo ya nchi.

214. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukuza majadiliano ya Kitaifa ya vijana, Serikali iliratibu kongamano la wajasiriamali na bodaboda lililofanyika tarehe 8 Januari, 2026 Jijini Dar es Salaam na kuwakutanisha washiriki zaidi ya 1,200. Kupitia kongamano hilo, vijana walipata fursa ya kuwasilisha changamoto zao ambazo zinaendelea kutafutiwa ufumbuzi na Serikali.

215. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuratibu masuala ya maendeleo ya vijana ikiwemo kuwawezesha kiuchumi, kusimamia ukuzaji biashara zao, na kuimarisha ustawi na makuzi ya vijana.

HUDUMA ZA KINGA YA JAMII

216. Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa, huduma ya kinga ya jamii ni muhimu sana kwa mustakabali wa ustawi wa jamii yoyote. Ukweli huo ndio msingi wa hatua na mikakati yote inayotekelezwa na Serikali katika kuimarisha na kuratibu utekelezaji wa afua mbalimbali za Kinga ya Jamii nchini. Mikakati hiyo inatekelezwa kwa lengo la kuboresha huduma za Kinga ya Jamii.

217. ***Mheshimiwa Spika***, moja ya mikakati hiyo ni pamoja na Sera ya Taifa ya Kinga ya Jamii ya Mwaka 2023 ambayo imezinduliwa rasmi tarehe 9 Februari, 2026. Sera hiyo inalenga kuwawezesha wananchi kuishi katika viwango vinavyokubalika kimataifa na kutumia uwezo wao kuboresha maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

218. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Serikali imeendelea kuimarisha ustawi wa wastaafu kwa kuboresha kiwango cha chini cha pensheni ya kila mwezi kutoka shilingi 100,000 hadi shilingi 250,000 kwa wastaafu wanaolipwa kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma. Aidha, Serikali imeboresha muda wa utoaji wa huduma kwa wanachama ambapo mafao yanalipwa ndani ya siku 30, na pensheni inalipwa tarehe 25 ya kila mwezi.

219. Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imeendelea kuimarika ambapo hadi Februari, 2026 ilikuwa na jumla ya thamani ya shilingi trilioni 24.60. Mifuko hiyo ni pamoja na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

220. *Mheshimiwa Spika,* hadi Februari 2026 Mfuko wa NSSF umesajili wanachama 226,799; umekusanya michango ya shilingi trilioni 1.22; na kulipa mafao ya shilingi bilioni 531.07. Kwa upande mwingine, Mfuko wa PSSSF umesajili wanachama 21,792, umekusanya michango ya shilingi trilioni 1.272 na kulipa mafao ya shilingi bilioni 883.26. Aidha, mfuko wa WCF umesajili waajiri wapya 1,619 na umelipa madai ya mafao ya shilingi billioni 10.14 kwa wanufaika 1,991 walioumia au kuugua. Vilevile, umelipa fidia kwa wategemezi wa waliofariki kutokana na kazi kwa mujibu wa mikataba yao ya kazi.

221. *Mheshimiwa Spika,* ili kupanua wigo wa Kinga ya Jamii kwa wananchi waliojiajiri katika sekta isiyo rasmi, Serikali imezindua mpango maalum wa wananchi waliojiajiri. Mpango huo uitwao 'Hifadhi Scheme' unatarajiwa kuwafikia mamilioni ya Watanzania waliokuwa nje ya mfumo rasmi wa pensheni.

222. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, mpango huo ni sehemu ya mkakati wa kujenga mfumo jumuishi wa kinga ya jamii nchini. Hadi kufikia tarehe 28 Februari 2026, Mfuko ulikuwa na wanachama 601,434 kupitia Skimu ya Uchangiaji wa Hiari.

223. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuboresha huduma za Kinga ya Jamii nchini. Vilevile, itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya usajili wa wanachama wapya na kuhamasisha ushiriki wa wananchi waliojiajiri kupitia sekta binafsi.

URATIBU WA MASUALA YA MAHUSIANO

224. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha umoja wa kitaifa, mshikamano, ustahimilivu na maendeleo jumuishi, Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliikasimisha Ofisi ya Waziri Mkuu jukumu la kuratibu masuala ya mahusiano nchini. Jukumu hilo linahusisha kuratibu makundi ya kijamii ikijumuisha wadau wa siasa, taasisi za dini, asasi za kiraia, na mashirika yasiyo ya kiserikali.

225. *Mheshimiwa Spika*, ili kufikia maono hayo, mwaka 2026/2027 Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Uratibu wa Mahusiano Baina ya Serikali na Makundi ya Kijamii wa Mwaka 2026. Vilevile, itaandaa Mpango Mkakati wa Kitaifa Kuhusu Mahusiano na Kuratibu Afua na Ushirikishwaji wa Wadau wa Mahusiano Nchini. Aidha, Serikali itafanya tathmini ya hali ya mahusiano nchini na kuendelea kukutana na wadau kwa lengo la kuimarisha mahusiano baina ya Serikali na Makundi ya Kijamii.

UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

226. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuimarisha uratibu na utendaji wa mifuko na programu za uwezeshaji 75 zinazomilikiwa na Serikali na sekta binafsi. Hadi Januari, 2026, mifuko na programu za uwezeshaji zimetoa mikopo na dhamana zenye thamani ya shilingi trilioni 1.69 kwa wanufaika 422,921. Mifuko na programu hizo pia, zimetoa ruzuku yenye thamani ya shilingi bilioni 598.72 kwa wanufaika 6,454,580.

227. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo kwa kutafuta fursa za biashara na masoko nje ya nchi ili waweze kukuza biashara zao. Katika mwaka 2025/2026, Serikali imewezesha wajasiriamali wadogo na wa kati 315 kushiriki maonesho ya wajasiriamali wadogo na wa kati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yajulikanayo kama Nguvukazi/ Juakali yaliyofanyika Novemba, 2025 Nairobi, Kenya.

228. *Mheshimiwa Spika,* katika kuwezesha kaya masikini, Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ilitoa shilingi bilioni 43.53 ambazo zilihawilishwa kwa kaya za walengwa 896,746

katika maeneo 186 nchini hadi Februari 2026. Aidha, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele cha mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi kutoka katika kaya masikini ambapo kwa mwaka 2025/2026 wanafunzi 3,179 wa kaya maskini kutoka Tanzania Bara na Zanzibar walinufaika na utaratibu huo.

229. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri, hadi Februari, 2026, shilingi bilioni 130.42 zimekopeshwa kwa vikundi 12,997 vya vijana, wanawake na Watu Wenye Ulemavu. Aidha, Serikali imeimarisha usimamizi wa mikopo hiyo na hivyo kuwezesha kiasi cha shilingi bilioni 49.11 kurejeshwa.

230. *Mheshimiwa Spika,* Serikali imeendelea kuratibu ushiriki wa Watanzania katika fursa zinazotokana na shughuli za kiuchumi zinazotekelezwa katika miradi ya kimkakati na uwekezaji. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Januari, 2026 jumla ya kampuni 389 za makundi maalum kati ya kampuni 166,477 zilipata zabuni za Serikali.

231. *Mheshimiwa Spika,* vilevile, Wakandarasi wa kitanzania walishiriki katika kutekeleza miradi 5,177 sawa na asilimia 97.1 ya miradi iliyotekelezwa. Miradi hiyo ina thamani ya shilingi bilioni 14 ambapo shilingi bilioni 10 sawa na asilimia 72.17 zilienda kwa kampuni za ndani na shilingi bilioni 4 sawa na asilimia 27.83 zilienda kwa Kampuni za kigeni.

232. *Mheshimiwa Spika,* aidha, ajira kwa Watanzania walioshiriki katika miradi ya kimkakati na uwekezaji ziliongezeka kutoka 217,808 mwaka 2024/2025 hadi ajira 286,219 mwaka 2025/2026. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 31.4.

233. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha mifuko na programu za uwezeshaji wananchi zinazomilikiwa na Serikali pamoja na za sekta binafsi. Aidha, itaendelea kufanya mapitio kwa lengo la kuboresha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 na Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi ya Mwaka 2023. Hatua hiyo itawezesha kuongeza idadi ya wananchi wanaonufaika na uwekezaji wa miradi ya kimkakati. Vilevile, itakamilisha maandalizi ya Mpango

wa Kunusuru Kaya Maskini Awamu ya Tatu na kutambua walengwa wapya wa mpango kwenye maeneo ya utekelezaji.

MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA

234. *Mheshimiwa Spika,* Serikali imeendelea kutekeleza mkakati wa Taifa dhidi ya rushwa kwa kuweka mkazo kwenye kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi. Aidha, imeendelea kufanya uchunguzi ili kudhibiti vitendo vya rushwa. Kutokana na jitihada hizo, kiasi cha shilingi bilioni 60.231 zimeokolewa.

235. *Mheshimiwa Spika,* kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 60.038 zilirejeshwa Serikalini na shilingi milioni 192.88 zilirejeshwa kwenye miradi, huduma na wananchi waliodhulumiwa. Matokeo ya juhudi hizo yameleta nidhamu, uadilifu na uwajibikaji katika utumishi wa umma, biashara na uwekezaji.

236. *Mheshimiwa Spika,* pamoja na matokeo hayo mazuri, kwa mara nyingine ninaelekeza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kuweka mikakati ya kuzuia vitendo vya rushwa badala ya kusubiri vitendo hivyo kusababisha madhara. Wahenga walisema "***tahadhari kabla ya hatari"*** wakiweka msisitizo wa kuzuia badala ya kusubiri athari zitokee.

237. *Mheshimiwa Spika,* licha ya kuendelea kutekeleza kikamilifu suala la usimamizi wa tamko la rasilimali na madeni kwa viongozi wa umma, baadhi ya maeneo yana mianya ya ukosefu wa maadili. Maeneo hayo ni pamoja na ununuzi wa umma, makusanyo ya mapato, makadirio ya kodi, mikataba, utoaji wa leseni za madini, sekta ya ardhi, wajumbe wa zabuni, ukaguzi na udhibiti.

238. *Mheshimiwa Spika,* baadhi ya watumishi wa maeneo hayo hawawajibiki na sheria ya maadili. Kwa mara nyingine, ninaelekeza Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ifanye marekebisho ya Sheria na Kanuni ili kujumuisha watumishi hao kujaza fomu ya tamko la rasilimali na madeni.

239. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa kwa kuziwezesha taasisi za utawala bora, maadili na uwajibikaji kutekeleza majukumu yao. Vilevile, itaendelea kuimarisha mifumo ya kisheria na kitaasisi ili kuongeza ufanisi kwenye kukabiliana na rushwa hapa nchini.

MAPAMBANO DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA

240. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuimarisha juhudi za kukabiliana na dawa za kulevya kupitia mikakati mbalimbali. Mikakati hiyo inalenga kupunguza upatikanaji, uhitaji, madhara na matumizi ya dawa za kulevya. Vilevile, imeendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika kukabiliana na dawa za kulevya.

241. *Mheshimiwa Spika,* kupitia utekelezaji wa mikakati hiyo, Serikali imefanikiwa kukamata kilogramu 360,479.9 za aina mbalimbali za dawa za kulevya zilizohusisha watuhumiwa 5,776. Dawa zilizokamatwa ni pamoja na bangi, mirungi, skanka, *heroin, cocaine*, dawa tiba zenye asili ya kulevya na kemikali bashirifu.

242. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kutekeleza mkakati wa kutoa elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya katika shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu ambapo vilabu 15,186 vimeanzishwa kwa ajili ya kupinga rushwa na dawa za kulevya. Vilevile, imetoa elimu kwa wadau 4,343,248 wakiwemo wanafunzi, viongozi wa Serikali, viongozi wa dini, vyombo vya ulinzi na usalama, Mahakama, watumishi wa afya, wasanii, maafisa wa viwanja vya ndege na wafungwa.

243. *Mheshimiwa Spika*, sambamba na hilo, Serikali imeendelea kutoa huduma za tiba na utengamao kwa waraibu 18,048 ambao wamesajiliwa katika vituo 20 vya kutolea tiba ambapo waraibu 4,790 wapo kwenye matibabu. Vilevile, Serikali imeendelea kusimamia uendeshaji wa nyumba maalum za upataji nafuu 77 zinazotoa huduma za utengamao na unasihi kwa waraibu wa dawa za kulevya. Aidha, waraibu 250 waliopata nafuu wamepata mafunzo ya amali katika vyuo vya VETA na Don Bosco ili waweze kujitegemea kiuchumi.

244. *Mheshimiwa Spika,* katika hatua nyingine ya kusaidia waraibu wa dawa za kulevya, Serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Utengamao katika eneo la Itega, Dodoma ambao umefikia asilimia 45. Kituo kitakapokamilika, kitatoa huduma za matibabu, urekebishaji wa tabia pamoja na programu za kuwawezesha waathirika kurejea katika jamii wakiwa na uwezo wa kujitegemea.

245. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha juhudi za kukabiliana na dawa za kulevya na ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

URATIBU WA MAAFA

246. *Mheshimiwa Spika*, katika uratibu wa maafa, Serikali imeanzisha mfumo wa kidijitali wa mawasiliano '*Call Center*' katika Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura. Mfumo huo unawezesha wananchi kupiga simu bure kupitia namba 190 kwa ajili ya kutoa taarifa za matukio ya maafa na kupata elimu kuhusu masuala ya maafa.

247. *Mheshimiwa Spika,* vilevile, Serikali imeandaa Mfumo wa Ramani za Vihatarishi vya Majanga yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa taarifa za maeneo hatarishi kwa majanga. Mfumo huo unalenga kuwawezesha wadau kutekeleza shughuli za maendeleo kwa kuzingatia vihatarishi vya majanga.

248. *Mheshimiwa Spika,* katika hatua nyingine, Serikali imeratibu operesheni ya kukabiliana na tukio la moto katika Hifadhi ya Misitu Asilia ya Mlima Hanang. Aidha, imetoa misaada ya kibinadamu kwa kaya zilizoathirika.

249. *Mheshimiwa Spika,* misaada ya kibinadamu iliyotolewa katika operesheni hizo ina thamani ya shilingi bilioni 1 na inajumuisha chakula na vifaa vya malazi, usafi na ujenzi. Aidha, Serikali imeratibu operesheni ya kukabili maafa na kutoa huduma

za kibinadamu katika maporomoko ya udongo kwenye Mgodi Mdogo wa Dhahabu wa Nyandolwa Mkoani Shinyanga.

250. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa maafa ili kuongeza ustahimilivu wa jamii dhidi ya majanga kwa kuandaa na kutekeleza mipango na mikakati ya kupunguza vihatarishi vya maafa katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

UTAWALA BORA NA SHERIA

251. *Mheshimiwa Spika,* ili kuhakikisha nchi yetu inaendelea kusimamia utawala wa sheria unaozingatia misingi ya utawala bora na haki za binadamu, serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali. Hatua hizo ni pamoja na kutunga sera, kufanya maboresho ya sheria, miongozo na kuandaa mikakati mbalimbali inayolenga kuimarisha utoaji wa haki na kuinua ustawi wa wananchi.

252. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2025/2026, Serikali imekamilisha kutafsiri na kutangaza Sheria Kuu 433 ambazo ni sehemu ya utekelezaji wa programu ya kutumia Lugha ya Kiswahili kwenye utoaji wa haki. Halikadhalika, sheria 13 zilizotungwa katika Lugha ya Kiswahili zimetafsiriwa kwenda katika Lugha ya Kiingereza.

253. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaimarisha sekta ya sheria kwa kusogeza huduma za kimahakama, mashtaka, msaada wa kisheria hususan kwenye usuluhishi wa migogoro mbalimbali ikiwemo ya ardhi. Vilevile, itasimamia matumizi ya lugha ya Kiswahili katika Sekta ya Sheria nchini.

HOJA ZILIZOWASILISHWA NA MAMLAKA ZA UKAGUZI, UDHIBITI NA UCHUNGUZI

254. *Mheshimiwa Spika*, ili kuhakikisha uadilifu katika matumizi ya rasilimali za umma, Serikali imeendelea kuimarisha mifumo ya ukaguzi na usimamizi. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuziwezesha taasisi zetu za Udhibiti, Ukaguzi na Uchunguzi kwa

kufanya mabadiliko ya sheria mbalimbali ili kuziongezea nguvu, bajeti, rasilimaliwatu na vitendea kazi. Hatua hizo zimeziwezesha taasisi za udhibiti kutekeleza kikamilifu majukumu yao na kuwasilisha taarifa kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Machi, 2026.

255. *Mheshimiwa Spika*, kaguzi zilizofanyika zimewezesha kubaini mapungufu katika usimamizi wa matumizi ya rasilimali za Serikali na kujua thamani ya fedha kwenye miradi ya maendeleo. Vilevile, zimewezesha kuimarisha uwajibikaji, kuimarisha taasisi na uwazi katika matumizi, ufuatiliaji na kuchukua hatua stahiki. Aidha, Serikali imepokea hoja na mapendekezo yaliyowasilishwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma kwa ajili ya kuzifanyia kazi. Nitumie fursa hii kulihakikia Bunge lako tukufu kwamba, Serikali itafanyia kazi hoja zote ili kuleta ufanisi wa utendaji wa Serikali.

256. *Mheshimiwa Spika,* aidha, ninawaelekeza Maafisa Masuuli wote wa taasisi zote za umma zenye hoja kujibu hoja hizo na kufanyia kazi mapendekezo kwa mujibu wa sheria. Katika maeneo ambayo ukaguzi umebaini wizi wa fedha na mali za umma au hujuma yoyote, ninaelekeza vyombo vyetu vya dola na mamlaka za nidhamu kufanya uchunguzi na kuchukua hatua stahiki za kisheria, kinidhamu na kiutumishi kwa wote wataobainika kuhusika.

MFUMO WA URATIBU WA MALALAMIKO YA WANANCHI

257. *Mheshimiwa Spika*, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati ya kuhakikisha malalamiko ya wananchi yanapatiwa ufumbuzi kwa wakati. Mikakati hiyo ni pamoja na kuboresha mfumo wa e-Mrejesho na kuanzisha Kituo cha Kitaifa cha Mawasiliano na Simu ili kuwawezesha wananchi kuwasilisha kero, kupata ufafanuzi na kutoa mrejesho kuhusu masuala mbalimbali kupitia namba 190 na baruapepe ya malalamiko@pmo.go.tz.

258. *Mheshimiwa Spika*, kituo hicho kinafanya kazi kama ngazi ya rufaa kwa changamoto ambazo hazijatatuliwa katika

ngazi ya Wilaya, Mikoa na Wizara. Hatua hii itaimarisha uwajibikaji na ushughulikiaji wa kero, malalamiko na mrejesho kutoka kwa wananchi.

259. *Mheshimiwa Spika*, nitoe wito kwa watumishi wa Serikali hususan Wizara za Kisekta, Taasisi, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali Mitaa kuimarisha mfumo wa kushughulikia kero za wananchi ikiwa ni pamoja na kuweka utaratibu wa kuwatembelea, kuwasikiliza na kuandaa jedwali na taarifa kuonesha namna walivyotatua kero za wananchi kila mwezi.

MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

260. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kusimamia mikakati na mipango ya kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa mazingira pamoja na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Hatua hizo zinajumuisha kupunguza matumizi ya kuni na mkaa, kuhamasisha upandaji miti, kuendeleza uwekezaji katika biashara ya kaboni na kusimamia utekelezaji wa mikataba ya kikanda na kimataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi.

261. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuimarisha uratibu wa biashara ya kaboni kama nyenzo ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha Taifa na wananchi wananufaika na fursa zitokanazo na biashara hiyo. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kusajili na kutekeleza miradi 92 kupitia sekta mbalimbali ikiwemo hifadhi ya misitu, nishati jadidifu na kilimo endelevu. Aidha, Halmashauri 24 kati ya 184 zinanufaika na utekelezaji wa miradi ya biashara hiyo.

262. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuhamasisha upandaji miti kupitia kampeni na programu mbalimbali na kuendelea kusimamia na kuratibu biashara ya kaboni. Vilevile, itaendelea kutekeleza mikakati ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kupitia kilimo himilivu, uhifadhi wa vyanzo vya maji, mifumo ya tahadhari ya majanga na mipango ya kupunguza athari za ukame, mafuriko na mabadiliko ya hali ya hewa.

UCHUMI WA BULUU

263. *Mheshimiwa Spika,* Uchumi wa Buluu ni moja ya maeneo mapya ya kimkakati yanayolenga kukuza uchumi wa Taifa kupitia matumizi endelevu ya rasilimali za bahari, maziwa, mito na maeneo oevu. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa za Uchumi wa Buluu kupitia makongamano ya kitaifa. Aidha, imewajengea uwezo wataalam kuhusu usimamizi, uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za Uchumi wa Buluu.

264. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kusimamia utekekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ili kuhakikisha nchi inanufaika na rasilimali za Uchumi wa Buluu na kutekeleza programu na miradi jumuishi ya kimkakati itakayokuwa chachu ya ukuaji wa uchumi kwa maendeleo endelevu.

UJENZI WA MJI WA SERIKALI

265. *Mheshimiwa Spika,* Serikali imeendelea na ujenzi wa Ofisi za Serikali katika Mji wa Serikali Mtumba. Hadi Februari, 2026 majengo 15 yameanza kutumika na ujenzi wa majengo 14 unaendelea. Katika mwaka 2026/2027 Serikali itaendelea kukamilisha majengo yaliyosalia pamoja na miundombinu ikiwemo ya maji na mawasiliano.

MUUNGANO

266. *Mheshimiwa Spika,* Serikali imeendelea kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha Muungano kwa manufaa ya wananchi wa pande zote mbili. Katika mwaka 2025/2026, Serikali imeendelea kuimarisha uratibu wa Masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Uratibu huu umefanywa kupitia vikao vya kamati ya pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya kushughulikia masuala ya muungano.

267. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu, upekee na fursa za Muungano. Vilevile, itaendelea kutunza na kuenzi tunu hii

adhimu ya muungano kwa manufaa ya wananchi wa pande zote mbili.

USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA

268. *Mheshimiwa Spika,* Serikali imeendelea kutekeleza sera ya mambo ya nje ambayo imekuwa nyenzo ya kuchochea maendeleo ya Taifa kwa kuimarisha diplomasia ya uchumi na kuendeleza ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa. Aidha, imeendelea kukuza biashara, kufungua masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi na kutangaza fursa za utalii na kuongeza ushawishi wa Tanzania katika majukwaa ya kikanda na kimataifa.

269. *Mheshimiwa Spika,* kwa upande wa ushirikiano wa kimataifa, Tanzania imeendelea kuimarisha ushiriki wake kwenye majukwaa ya kimataifa kwa kuratibu na kushiriki katika mikutano ya ngazi ya juu iliyofanyika sehemu mbalimbali duniani. Mikutano hiyo ni pamoja na Mkutano wa Pili wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika na Italia. Ujumbe wa Tanzania katika Mkutano huo uliofanyika Jijini Addis Ababa - Ethiopia uliongozwa na Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

270. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, Tanzania ilishiriki Mkutano wa 80 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa uliofanyika Jijini New York – Marekani. Katika mkutano huo ujumbe wa Tanzania uliongozwa na aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa *Dkt*. Philip Isdor Mpango. Pia, Tanzania ilishiriki katika Mkutano Mkuu wa Wakuu wa nchi na Serikali wa Jumuiya ya nchi za Afrika, Karibiani na Pasifiki uliofanyika Jijini Malabo nchini Guinea ya Ikweta. Katika mkutano huo, ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa *Balozi Dkt.* Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

271. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa ushirikiano wa kikanda, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa 45 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC uliofanyika Agosti, 2025 nchini Madagascar. Katika mkutano huo, Tanzania ilishawishi utekelezaji wa maazimio ya kikanda kuhusu sekta ya nishati *(Mission 300)*.

Vilevile, Tanzania iliratibu na kuongoza Mkutano wa 27 wa Kamati ya Mawaziri wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama uliofanyika mwezi Julai, 2025 Jijini Dar es Salaam.

272. Mheshimiwa Spika, ushiriki wa Tanzania kwenye mikutano ya kikanda na kimataifa umeiwezesha nchi yetu kueleza misimamo yake kwenye masuala mbalimbali yenye maslahi kimataifa na kuainisha vipaumbele vyake kwenye majukwaa hayo. Aidha, Serikali imetumia majukwaa hayo kutangaza mazingira wezeshi na fursa za biashara na uwekezaji katika sekta za kipaumbele ikiwemo nishati, kilimo, viwanda, miundombinu, Uchumi wa Buluu na uchumi wa kidijitali.

273. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha utekelezaji wa diplomasia ya uchumi ikiwemo kukuza upatikanaji wa masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi, kuvutia uwekezaji na kukuza utalii. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha uratibu na ushirikiano wa uwili pamoja na ushiriki wa Tanzania katika jumuiya na mashirika ya kikanda na kimataifa kwa lengo la kulinda na kutetea maslahi ya Taifa, pamoja na kustawisha diplomasia ya kisiasa na kujenga uhusiano wa karibu na nchi washirika kwa manufaa ya pande zote.

MAENDELEO YA MICHEZO

274. Mheshimiwa Spika, Tanzania inaendelea na maandalizi ya kuwa mwenyeji katika mashindano ya AFCON 2027. Maandalizi hayo yanahusisha ujenzi na ukarabati wa viwanja pamoja na miundombinu wezeshi ikiwemo ujenzi wa Uwanja wa Arusha uliofikia asilimia 75; ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa uliofikia asilimia 95; na ujenzi wa Uwanja wa Dodoma uliofikia asilimia 4.

275. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imekamilisha ujenzi na ukarabati wa viwanja vya Meja Jenerali Isamuhyo, *Gymkhana Club* na Shule ya Sheria Tanzania kwa ajili ya mazoezi. Aidha, inaendelea na ujenzi wa Viwanja vya Farasi, *Gymkhana Annex* na *Leaders Club*.

276. *Mheshimiwa Spika,* kwa upande wa mashindano ya wanafunzi kitaifa, kikanda na kimataifa, Serikali imeratibu michezo ya UMITASHUMTA na UMISETA pamoja na kuwezesha ushiriki wa wanafunzi katika mashindano ya *CAF Schools Championship* yaliyofanyika Accra nchini Ghana. Vilevile, imeratibu ushiriki kwenye Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wanafunzi wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Agosti, 2025 nchini Kenya.

277. *Mheshimiwa Spika,* katika mashindano ya *CAF Schools Championship,* Tanzania ilipata ubingwa kwa upande wa wavulana. Mashindano hayo ya wanafunzi ni msingi wa upatikanaji wa wachezaji mahiri wa timu kubwa na timu za vijana wa chini ya miaka 15, 17 na 20 nchini.

278. *Mheshimiwa Spika,* ninapenda kutumia fursa hii pia, kulipongeza Shirikisho la Mchezo wa Mpira wa Miguu Tanzania kwa uongozi, uratibu na usimamizi mzuri wa mchezo huo hapa nchini. Kupitia uongozi huo, kwa mara ya kwanza Tanzania imefanikiwa kuingiza vilabu vinne kwa pamoja katika hatua ya makundi ya mashindano ya Klabu Bingwa na Shirikisho Barani Afrika. Vilabu hivyo ni Klabu ya Michezo Yanga (wananchi), Klabu ya Michezo Simba (wenye nchi), Klabu ya Michezo Azam (wana lambalamba) na Klabu ya Michezo Singida (wana kilemankundi).

279. *Mheshimiwa Spika,* ni dhahiri kuwa mafanikio katika mchezo wa mpira wa mguu na michezo mingine kwa ujumla ni matokeo ya uwekezaji na hamasa inayotolewa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mafanikio hayo, siyo tu yanaleta burudani kwa mashabiki, bali yanatoa fursa ya ajira na uwekezaji hapa nchini.

280. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kusimamia na kuratibu ushiriki wa Tanzania katika michezo ya kimataifa na maandalizi ya AFCON 2027 ili kuacha urithi endelevu wa michezo, ajira, utalii na heshima ya Taifa. Aidha, itaendelea kuimarisha ushiriki wa wanafunzi katika michezo ili kuibua na kukuza vipaji vyao.

MAENEO YA MSISITIZO

281. ***Mheshimiwa Spika,*** nimeelezea kwa muhtasari baadhi ya shughuli ambazo Serikali imetekeleza kwa mwaka 2025/2026 na mwelekeo wa kazi zitakazofanyika kwa mwaka 2026/2027. Ninapoelekea kuhitimisha hotuba yangu, ninaomba nitumie fursa hii kutoa msisitizo kwenye maeneo mahsusi kama ifuatavyo:

Mosi: Kuanza utekelezaji wa Dira 2050 kupitia Mpango na Bajeti iliyoandaliwa. Kila sekta ihakikishe rasilimali za Taifa zinaelekezwa katika maeneo yenye tija na matokeo makubwa ili kupunguza utegemezi kutoka nje. Vilevile, kuendelea kuishirikisha sekta binafsi na wadau wa maendeleo katika kuharakisha utekelezaji wa Dira 2050 ili kujenga uchumi jumuishi, shindani na unaotegemea uzalishaji wenye tija.

Pili: Wakuu wa Mikoa simamieni kikamilifu maandalizi na mapokezi ya wanafunzi wa elimumsingi ya lazima ya miaka kumi watakaojiunga na kidato cha kwanza mwaka 2028 kwa kukamilisha miundombinu na huduma zote muhimu.

Tatu: Kuimarisha usimamizi wa makusanyo ya mapato kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na mashine za POS, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, kuziba mianya ya uvujaji wa fedha za umma na kuendeleza rasilimali fedha katika miradi ya kimkakati na kielelezo.

Nne: Wizara, Taasisi na Mamlaka zinazoshiriki katika uwezeshaji wananchi kiuchumi ziweke malengo yanayopimika, viashiria vya utendaji na ratiba za utekelezaji, ili kuhakikisha mitaji hiyo inazalisha ajira, kipato na biashara endelevu hasa kwa vijana, wanawake na wenye ulemavu.

Tano: Makandarasi wote wanaotekeleza miradi ya Serikali watimize wajibu wao kwa mujibu wa mikataba waliyoingia ikiwa ni pamoja na kuwalipa watoa huduma walioshiriki kwenye utekelezaji wa mradi husika. Aidha maafisa masuuli kuhakikisha wazabuni na watoa huduma wanalipwa kwa wakati kwa mujibu wa makubaliano na huduma iliyotolewa.

Sita: Wakuu wa Mikoa, ndani ya miezi sita baada ya kuanza utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2026/2027 wahakikishe shule zote katika halmashauri zina matundu ya vyoo kwa kuzingatia uwiano wa wanafunzi waliopo.

Saba: Wizara ya Maji ihakikishe huduma ya maji inapatikana kwenye shule na vituo vyote vya kutolea huduma ya afya ndani ya miezi sita baada ya kuanza utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2026/2027. Baada ya muda huo, ni marufuku kwa wanafunzi kubeba maji na kupeleka shuleni.

Nane: Ubora wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika sekta mbalimbali nchini uwiane na thamani ya fedha iliyotolewa. Aidha, fedha zinazoelekezwa na Serikali kwenye miradi hiyo zitumike kama ilivyokusudiwa. Vilevile, makandarasi wa ndani wawe wazalendo kwa kutumia ipasavyo fursa inayotolewa ya ushiriki wa kampuni zilizosajiliwa ndani kutekeleza miradi mikubwa.

Tisa: Wizara za Kisekta, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha zinalipa fidia kwa wananchi wanaopisha maeneo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Serikali kabla ya kutwaliwa kwa maeneo yao kwa kuzingatia taratibu zilizopo.

Kumi: Taasisi zote za umma kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali ikiwemo mipango, programu na miradi ili kuongeza tija ya utendaji kazi na kuboresha huduma kwa wananchi.

Kumi na moja: Wizara, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi, Wakala na Idara zinazojitegemea kuanza kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Rais ya Kutathmini Maboresho ya Mfumo wa Kodi kama alivyoelekeza Mheshimiwa Rais.

SALAMU ZA PONGEZI

282. Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutekeleza vema wajibu wake wa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuliongoza Taifa letu. Ninamtakia afya njema na nguvu katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

283. *Mheshimiwa Spika,* vilevile, ninatoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuiongoza vema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Hakika uongozi wake thabiti na mapinduzi makubwa ya kiuchumi anayoyafanya yanaonesha nia ya dhati ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2025 kwa vitendo.

284. *Mheshimiwa Spika*, nitumie fursa hii kukupongeza na kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Musa Azzan Zungu, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kazi kubwa na nzuri ya kuliongoza Bunge letu. Ninawaombea heri na baraka za Mungu katika kuongoza mijadala yote ya Mkutano huu wa Tatu wa Bunge la 13. Sote tuungane kuombea mafanikio mkutano huu na kumwombea Mheshimiwa Spika na wasaidizi wake hekima katika kusimamia shughuli zote za Bunge kama zilivyopangwa.

285. *Mheshimiwa Spika,* ninawapongeza pia, Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa *Dkt*. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa *Dkt*. Johannes Lembulung Lukumay, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Hawa Chakoma Mchafu, Mbunge wa Viti Maalum; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Jimbo la Maswa Magharibi; na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo Mbunge wa Jimbo la Missenyi. Maoni na ushauri wa Kamati hizo

yamesaidia sana kuboresha makadirio ya mapato na matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge kwa Mwaka 2026/2027.

286. *Mheshimiwa Spika,* ninawapongeza na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu ambayo wakati wote imekuwa ikisaidia kuboresha mipango na shughuli zinazotekelezwa na Serikali katika kuwahudumia wananchi. Ninaamini mijadala katika Mkutano huu itaendelea kuthibitisha uimara wa Bunge katika kutekeleza wajibu wake wa Kikatiba wa kuishauri na kuisimamia Serikali kikamilifu.

287. *Mheshimiwa Spika,* katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 07 Machi, 2026, Mheshimiwa Balozi Stephen Patrick Mbundi aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kabla ya uteuzi huo, Mheshimiwa Balozi Mbundi alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayesimamia masuala ya Afrika Mashariki. Kipekee ninampongeza Balozi Mbundi kwa uteuzi huo na kumtakia kila la heri katika kutekeleza majukumu yake mapya.

288. *Mheshimiwa Spika,* vilevile, ninatoa pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kuwa wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge pamoja na wawakilishi wa nchi yetu katika taasisi za kikanda na kimataifa ikiwemo Bunge la Afrika, Jukwaa la Kibunge la SADC, Umoja wa Mabunge Duniani na Jukwaa la Kibunge la nchi zinazozunguka Ukanda wa Maziwa Makuu. Ninawatakia kila la heri katika kuwakilisha na kutetea maslahi ya nchi katika taasisi hizo na kuendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na Kimataifa.

289. Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa *Dkt*. Lazaro Bunungu Komba, kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Peramiho kuwa mwakilishi wao katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wananchi wa Peramiho wamekuamini pasina shaka kuwa utawawakilisha vema. Aidha, ninakukaribisha Bungeni na kukutakia kila la heri katika kutekeleza majukumu yako ya kuwakilisha wananchi.

290. *Mheshimiwa Spika,* nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na Wakuu wa Mashirika, Wakala na Idara Zinazojitegemea kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia. Hakika utendaji wao unaleta tija kubwa sana katika kutekeleza majukumu ya Serikali.

291. *Mheshimiwa Spika,* ninamshukuru Mheshimiwa Hamza Saidi Johari Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ushauri wake wakati wote. Vilevile, ninamshukuru sana Balozi Dkt. Moses Mpogole Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi, kwa ushirikiano wake wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Aidha, kipekee ninamshukuru ndugu Baraka Ildefophonce Leonard, Katibu wa Bunge kwa uratibu wa shughuli za kila siku za Bunge na ushirikiano anaoutoa kwa Waheshimiwa Wabunge.

292. *Mheshimiwa Spika,* ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa George Mcheche Masaju, Jaji Mkuu wa Tanzania pamoja na watendaji wote wa Mahakama kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia na kuimarisha mifumo ya utoaji wa haki. Jitihada zao zimekuwa chachu ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kuhakikisha haki inapatikana kwa Watanzania wote.

293. *Mheshimiwa Spika*, kwa moyo wa dhati, ninapenda kutumia fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Wakuu wa Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya ya kulinda Taifa letu. Vilevile, niwapongeze maafisa na askari wote wa majeshi yetu kwa kufanya kazi usiku na mchana ili kudumisha amani ya nchi yetu. Wakati wote wamekuwa wakitekeleza majukumu yao kwa ubunifu, uzalendo, utii, ujasiri na weledi. Hakika tunatambua, tunathamini na tunawashukuru sana kwa moyo wa kizalendo na uwajibikaji wao.

294. *Mheshimiwa Spika,* nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru viongozi na watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Ninaomba niwataje wachache kwa niaba ya wengi

waliofanya wepesi katika utendaji wangu wa kazi za kila siku. Ninamshukuru Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Mahusiano); Mheshimiwa Prof. Riziki Silas Shemdoe, Mbunge wa Lushoto na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI).

295. *Mheshimiwa Spika,* kadhalika, niwashukuru Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu); Mheshimiwa Rahma Riyadh Kisuo, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Mahusiano); Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI-Elimu); na Mheshimiwa *Dkt*. Jafar Rajab Seif, Mbunge wa Busanda na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI - Afya) kwa kuendelea kunishauri vema na kunisaidia kutekeleza majukumu ya Serikali.

296. *Mheshimiwa Spika,* vilevile, ninawashukuru Makatibu Wakuu *Dkt*. Jim James Yonazi (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu); Bi. Mary Ngelela Maganga (Kazi, Ajira na Mahusiano), Bw. Adolf Hyasinth Ndunguru (TAMISEMI); Naibu Makatibu Wakuu Dkt. James Henry Kilabuko (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Bi. Zuhura Yunus Abdallah (Kazi, Ajira na Mahusiano), *Mhandisi* Rogatius Hussein Mativila (TAMISEMI - Miundombinu), Bw. Sospeter Mambile Mtwale (TAMISEMI), Bw. Atupele Webster Mwambene (TAMISEMI - Elimu), Prof. Tumaini Joseph Nagu (TAMISEMI - Afya); Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu pamoja na Wafanyakazi wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

297. *Mheshimiwa Spika,* aidha, ninawashukuru watumishi wote wa umma na sekta binafsi kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi mkubwa. Nikiri kwamba michango yenu ni mikubwa katika kuleta ufanisi wa utekelezaji wenye tija wa shughuli za Serikali kwa mujibu wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2025/2026.

298. *Mheshimiwa Spika,* ninapenda pia kuwashukuru washirika wa maendeleo zikiwemo nchi rafiki, taasisi na mashirika ya kitaifa, kikanda na kimataifa, madhehebu ya dini na mashirika

yasiyo ya kiserikali, kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita katika kujenga uchumi na kuiletea nchi yetu maendeleo. Michango yao imekuwa muhimu katika kuwezesha nchi yetu kupiga hatua kimaendeleo kwa kuzingatia mipango tuliyojiwekea.

299. Mheshimiwa Spika, kipekee, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Sekta Binafsi kwa kuendelea kuwa mshirika mkuu wa Serikali katika kuiletea nchi yetu maendeleo. Ushiriki wao umekuwa chachu ya kuchochea ukuaji wa uchumi na kuzalisha fursa za ajira kwa Watanzania. Niwahakikishie wadau wote, Serikali itaendelea kushirikiana na Sekta Binafsi katika kufikia malengo ya Dira 2050.

300. *Mheshimiwa Spika,* nitumie fursa hii adhimu kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa kuendelea kushirikiana nami na kuniunga mkono katika kipindi chote cha kutekeleza majukumu ya Serikali. Hali hii inaonesha ni kwa namna gani wamekuwa wastahimilivu na waungwana kwa Serikali yao katika kuhakikisha tunaleta maendeleo ya pamoja.

301. *Mheshimiwa Spika,* ninawashukuru wananchi wote kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Imani na ushirikiano wao umekuwa chachu ya mafanikio makubwa ya Serikali kuleta maendeleo kwa wananchi wa Tanzania.

302. Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, ninapenda kumshukuru mke wangu mpendwa Bi. Neema Mwigulu Nchemba, watoto wangu Joshua Mwigulu, Gracious Mwigulu, Isaac Mwigulu, Bernice Mwigulu kwa upendo, uvumilivu na maombi yao. Nikiri kwamba, maombi yao yamekuwa yakinipa nguvu wakati wote ninapotekeleza majukumu ya kulitumikia Taifa. Ninawashukuru na ninawapenda sana.

303. *Mheshimiwa Spika,* nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitawashukuru wanahabari ikiwa ni pamoja na waandishi katika mitandao ya kijamii. Nina imani kuwa, mtaendelea kuwahabarisha wananchi kuhusu yanayojiri katika mkutano huu

wa Bunge pamoja na masuala mbalimbali ya kijamii na kiuchumi na hivyo kuimarisha umoja na mshikamano wa Kitaifa.

HITIMISHO

304. *Mheshimiwa Spika,* nihitimishe hotuba yangu kwa kuwaahidi wananchi kuwa Serikali ya awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, itaendelea kuwatumikia kwa moyo wa dhati kwa kuzingatia kaulimbiu ya ***Kazi na Utu - Tunasonga Mbele***. Katika kuhakikisha hilo, ninasisitiza watumishi wote wa umma kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili kutoa huduma bora kwa wananchi bila upendeleo.

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2026/2027

Makusanyo ya Mapato

305. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2026/2027 Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba idhini ya kukusanya maduhuli na mapato ya ndani ya jumla ya shilingi **2,411,548,152,302.47.** Mchanganuo wa makusanyo hayo ni kama ilivyo kwenye **Jedwali Na. 1**.

Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Maduhuli na Makusanyo kwa Mwaka 2026/2027	
Jina la Ofisi	**Makusanyo (Shilingi)**
Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu	12,020,000,000.00
Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	2,336,528,152,302.47
Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano	63,000,000,000.00
JUMLA KUU	**2,411,548,152,302.47**

Matumizi

306. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2026/ 2027, Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu

liidhinishe jumla ya **shilingi 12,502,356,160,000.00** kati ya fedha hizo, **shilingi 8,734,043,089,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 3,768,313,071,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

307. *Mheshimiwa Spika,* vilevile ninaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **shilingi 225,021,780,000** kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Kati ya fedha hizo, **shilingi 207,992,798,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 17,028,982,000** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa fedha za matumizi ni kama ilivyo kwenye **Jedwali Na. 2**.

Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka 2026/2027	
Jina la Ofisi	**Makusanyo (Shilingi)**
Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu	183,950,342,000.00
Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	12,268,472,643,000.00
Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano	49,933,175,000.00
JUMLA	**12,502,356,160,000**
Mfuko wa Bunge	**225,021,780,000.00**

308. *Mheshimiwa Spika,* ninaomba kutoa hoja.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu, hoja imeungwa mkono.

Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mama Mwigulu kwa kuwepo ndani ya Bunge, lakini makofi aliyopigiwa Mama Mwigulu ni mengi zaidi ya timu ile uliyoitaja mwanzo ndani ya Bunge. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kumtambulisha Kiongozi wa Chama Cha Mapinduzi, Komredi John Mongella Naibu Katibu Mkuu ambaye anamwakilisha Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu uliobaki ni mdogo na tuna Kamati tano za kutoa ambazo zinakwenda sambamba na Wizara hii. Sasa mniruhusu niiruhusu Kamati ya Kudumu ya Bajeti ambayo taarifa yao siyo ndefu sana wakamilishe halafu zingine tutafanya jioni ya leo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025 kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

Mheshimiwa Spika, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeundwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Ibara ya 62 na Ibara ya 63(2), 63(3) imeaninisha majukumu ya Ofisi ya Bunge ambayo ni kutoa huduma kwa Bunge ili kuwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake. Aidha, Kifungu cha 32 ya Sheria ya Uendeshaji wa Bunge, Sura ya 115 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2015 kilianzisha Mfuko Bunge ili kuwezesha Ofisi ya Bunge kutekeleza majukumu yake na kinatoa maelekezo ya namna Mfuko huo utakavyosimamiwa na kuendeshwa

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu ya Kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti, Kamati ilikutana na Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu); na Mheshimiwa Laurent Deogratius Luswetula, Naibu Waziri wa Fedha; pamoja na Ndugu Baraka Leonard, Katibu wa Bunge ili kupitia utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na kufanya mashauriano kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inatoa tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya majukumu ya Mfuko wa Bunge hadi kufikia Februari 2026 pamoja na vipaumbele na masuala muhimu yaliyopendekezwa katika Mpango wa Bajeti wa Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Bajeti na Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Ofisi ya Bunge inatekeleza Bajeti yake kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sura 439; Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348; Sheria ya Manunuzi ya Umma, Sura 410; Dira ya Taifa 2025; Mpango wa Muda Mrefu wa Miaka 15; Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2025/2026; Mpango wa Ofisi ya Bunge ya Mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026; pamoja na Mwongozo wa Muda wa Kati wa Mwaka 2023/2024 hadi Mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, aidha, utekelezaji wa bajeti umezingatia malengo yanayotarajiwa kufikiwa katika kipindi husika kulingana na mahitaji halisi ya lengo la kuliwezesha Bunge na Wabunge kutimiza majukumu yao ya Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge wa mwaka 2025 hadi Februari 2026. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi 186,753,635,000. Kati ya fedha hizo shilingi 25,632,628,000 ni mshahara, shilingi 149,327,675,000 ni fedha za matumizi mengineyo na shilingi 11,793,332,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo shilingi 11,385,882,000 ni fedha za ndani na shilingi 407,450,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, wakati wa utekelezaji wa Bajeti Ofisi ya Bunge ilipokea kwa njia ya uhamisho nje ya Fungu 42 jumla ya shilingi 4,429,340,865.75 kwa ajili ya kugharamia Mradi wa Usimikaji wa Mifumo ya Sauti (*Digital Congress Network*) kwenye ukumbi wa Bunge na hivyo kufanya bajeti Ofisi ya Bunge kufika shilingi 191,182,975,865.75. Hadi kufikia Februari, 2026 jumla ya shilingi 113,923,024,121.18 zilitolewa sawa na 59.9% kwa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo mishahara ilikuwa ni shilingi 11,608,549,511, matumizi mengineyo shilingi 89,112,135,000 na matumizi ya maendeleo ni jumla ya shilingi 13,202,339,610.18. Aidha, kati ya fedha za maendeleo shilingi 12,868,039,610.18 ni fedha za ndani na shilingi 334,300,000 ni fedha za nje. Mchanganuo huo umetolewa katika jedwali namba moja ambalo liko katika ukurasa wa nne.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Fedha kwa kutoa fedha kwa wakati na kulingana na mahitaji ya Mfuko wa Bunge ili kuwezesha kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maduhuli, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya shilingi 147,966,000 hadi kufikia Februari, 2026 jumla ya shilingi 19,200,000 zilikusanywa ambayo ni sawa na 12.9% ya makisio yaliyopangwa. Fedha zilizokusanywa zimetokana na kodi ya pango kwa jengo la utawala *Annex,* mwenendo huo wa makusanyo wa maduhuli ulitokana na masharti ya kimkataba ambapo kodi ya pango hulipwa mwishoni mwa mwaka wa fedha, hivyo mategemeo ya kukusanya 100% yatakuwepo itakapofikia Juni 2026.

Mheshimiwa Spika, kuna mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Bajeti hiyo ya Mwaka wa Fedha 2025/2026. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Februari, 2026, Mfuko wa Bunge umefanikiwa kutekeleza shughuli zake mbalimbali za Mikutano ya Bunge, Vikao vya Kamati za Bunge, ushiriki wa Mikutano ya Kimataifa, pamoja na shughuli za uendeshaji Ofisi ya Bunge. Baadhi ya mafanikio hayo yameorodheshwa hapa

kuanzia ukurasa wa tano na ukurasa wa sita, ambapo ni kutoka (i) hadi (viii).

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto za utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42), Ofisi ilikabiliwa na changamoto zifuatazo ambazo ni mbili:-

(a) Kuwepo kwa shughuli ambazo hazikutegemewa na bajeti, lakini ni muhimu kutekelezwa, mathalani ongezeko la majimbo nane ya uchaguzi yaliyopokea nyongeza ya Wabunge 11, hivyo kusababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji; na

(b) Kupanda mara kwa mara kwa gharama za bidhaa na huduma na kusababisha mahitaji ya uhamisho wa fedha ndani ya Fungu, za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia changamoto hizo, Ofisi ya Bunge imefanya mashauriano na Wizara ya Fedha kuhusu upatikanaji wa fedha ili kugharamia shughuli muhimu katika utendaji kazi wa Bunge na kuhakikisha Ofisi inatekeleza shughuli zake kulingana na bajeti iliyotengwa na kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo inayosimamia utekelezaji wa bajeti. Hivyo changamoto hizo hazitarajiwi kujitokeza katika Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Makadirio ya Ofisi ya Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 yamezingatia masuala yafuatayo:-

(i) Dira ya Taifa;

(ii) Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Muda Mrefu wa Miaka 25;

(iii) Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano;

(iv) Mpango wa Maendeleo ya Taifa ya Mwaka Mmoja;

(v) Mpango Mkakati wa Ofisi ya Bunge wa Muda wa Kati;

(vi) Majukumu ya Bunge ya Kikatiba;

(vii) Malengo ya Taasisi;

(viii) Majukumu ya Idara na Vitengo;

(ix) Mwongozo wa Maandalizi wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;

(x) Sheria ya Bajeti, Sura namba 439;

(xi) Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348; na

(xii) Sheria ya Manunuzi ya Umma, Sura 410.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/2027. Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Mfuko wa Bunge umetengewa jumla ya shilingi 225,021,780,000. Kati ya fedha hizo shilingi 24,889,142,000 ni mishahara na shilingi 183,103,656,000 ni kwa ajili matumizi mengineyo na shilingi 17,028,982,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya kiasi kilichotengwa katika fedha za maendeleo shilingi 16,385,882,000 ni fedha za ndani na shilingi 643,100,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba bajeti hiyo inatosheleza. Ninarudia, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, bajeti hiyo inatosheleza kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake Kikatiba na kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli: katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Mfuko wa Bunge umepanga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 191,553,000 yatakayotokana na ukodishaji wa Kumbi za Mikutano katika Ofisi Ndogo ya Dar es Salaam na kodi ya pango kwenye Jengo la Utawala *Annex*, pamoja na mgahawa uliopo katika jengo la Utawala Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vipaumbele; katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Mfuko wa Bunge unatarajiwa kutekeleza vipaumbele vifuatavyo na hapa sitaweza kuvitaja vyote, tutavikuta katika ukurasa wa 10 na ukurasa wa 11.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilikuja na maoni. Maoni ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na uendelezaji wa maeneo mapya ya Ofisi za Bunge Dodoma; Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inatenga fedha kwa awamu ili kuwezesha ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Wabunge ili wazitumie kwenye viunga vya Bunge. Hatua hii itasaidia kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kufanya kazi zao za kiofisi ndani ya viunga vya Bunge, sehemu ambayo itakuwa salama na kuzingatia usiri au faragha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninarudia tena, uendelezaji wa maeneo mapya ya Ofisi za Bunge Dodoma; Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inatenga fedha kwa awamu ili kuwezesha ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Wabunge ili wazitumie kwenye viunga vya Bunge. Hatua hii itasaidia kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kufanya kazi zao za kiofisi ndani ya viunga vya Bunge sehemu ambayo itakuwa salama na inazingatia usiri au faragha.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, nitumie fursa hii kutoa pole kwa familia na Wabunge wote na Serikali kwa kuondokewa na Mheshimiwa William Lukuvi, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu. Hakika Bunge limepoteza mwakilishi hodari, mahiri, mchapakazi na mzalendo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Spika wa Bunge pamoja na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Spika kwa miongozo yenu katika kuendesha Shughuli za Bunge. Aidha, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Balozi Khamis Mussa Omar, Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na

Uratibu; Mheshimiwa Mshamu Ali Munde, na Mheshimiwa Laurent Deogratius Luswetula, Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao katika Kamati wakati wa kujadili Bajeti ya Mfuko wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii ya Bajeti kwa umakini wao katika kipindi cha kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge, majina yao yameorodheshwa katika ukurasa wa 13 sitaweza kuyataja yote. Ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru Ndugu Baraka Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninaliomba Bunge lako Tukufu sasa lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu yenye jumla ya shilingi 225,021,780,000 ambapo kiasi cha shilingi 24,889,142,000 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 183,103,656,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 17,028,982,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA BAJETI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE (FUNGU 42) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/27.

Mheshimiwa Spika, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeundwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 Ibara ya 62 na Ibara ya 63(2) na (3) imeainisha majukumu ya Ofisi ya Bunge ambayo ni kutoa huduma kwa Wabunge ili kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake. Aidha, Kifungu cha 32 cha Sheria ya Uendeshaji wa Bunge Sura 115 kama ilivyofanyiwa marekebisho Mwaka 2015, kilianzisha Mfuko wa Bunge, ili kuwezesha Ofisi ya Bunge kutekeleza majukumu yake na kinatoa maelekezo ya namna Mfuko huo utakavyosimamiwa na kuendeshwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1) kipengele cha (c) cha Sheria ya Bajeti, Kamati ilikutana na Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga (Mb), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Mheshimiwa Laurent Deogratius Luswetula (Mb), Naibu Waziri wa Fedha pamoja na Ndugu, Baraka I. Leonard - Katibu wa Bunge, ili kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 pamoja na kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/27.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inatoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti na majukumu ya Mfuko wa Bunge hadi kufikia Februari, 2026 pamoja na vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Mpango na Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2025/26.

2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Bunge inatekeleza Bajeti yake kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Sura ya 439, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Sura ya 348, Sheria ya Manunuzi ya Umma Sura ya 410, Dira ya Taifa 2025, Mpango wa muda mrefu wa miaka 15, Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2025/26, Mpango wa Ofisi ya Bunge Mwaka 2021/222025/26 pamoja na Mwongozo wa Muda wa Kati wa Mwaka 2023/24 – 2025/26.

Aidha, utekelezaji wa bajeti umezingatia malengo yaliyotarajiwa kufikiwa katika vipindi husika kulingana na mahitaji halisi kwa lengo la kuliwezesha Bunge na Wabunge kutimiza wajibu wao wa kikatiba.

2.1 Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge ya Mwaka 2025/26 hadi Februari, 2026

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 186,753,635,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 25,632,628,000.00** ni Mishahara, **Shilingi 149,327,675,000.00** fedha za Matumizi Mengineyo na **Shilingi 11,793,332,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Maendeleo, **Shilingi 11,385,882,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 407,450,000.00** ni fedha za Nje.

Mheshimiwa Spika, wakati wa utekelezaji wa bajeti Ofisi ya Bunge ilipokea kwa njia ya uhamisho nje ya Fungu 42 jumla ya **Shilingi 4,429,340,865.75** kwa ajili ya kugharamia Mradi wa usimikaji wa mfumo wa sauti (Digital Congress Network – DCN) kwenye ukumbi wa Bunge na hivyo kufanya bajeti ya Ofisi ya Bunge kufika **Shilingi 191,182,975,865.75.**

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2026 jumla ya **Shilingi 113,923,024,121.18** zilipokelewa sawa na **asilimia 59.59** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya Fedha hizo, Mishahara ilikuwa **Shilingi 11,608,549,511,** Matumizi mengineyo **Shilingi 89,112,135,000** na matumizi ya maendeleo jumla ya **Shilingi 13,202,339,610.18** Aidha, kati ya fedha za maendeleo, **Shilingi 12,868,039,610.18** ni fedha za ndani na **Shilingi 334,300,000.00** ni fedha za nje. Mchanganuo wa utolewaji wa fedha ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na.1.**

2.1.1 Jedwali Na. 1. Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge hadi Februari 2026

MAELEZO	BAJETI ILIYOIDHINISHWA	KIASI KILICHOPOKELEWA	ASILIMIA
Mishahara	25,632,628,000.00	11,608,549,511.00	45.29
Matumizi Mengineyo	149,327,675,000.00	89,112,135,000.00	59.68
Maendeleo	16,222,672,865.75	13,202,339,610.18	81.38
JUMLA	**191,182,975,865.75**	**113,923,024,121.18**	**59.59**

Chanzo: *Randama ya Mfuko wa Bunge*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Fedha kwa kutoa fedha kwa wakati na kulingana na mahitaji ya Mfuko wa Bunge ili kuwezesha kutekeleza majukumu yake ya kikatiba.

2.2 Maduhuli

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kukusanya Maduhuli ya **Shilingi 147,966,000.00.** Hadi kufikia Februari, 2026 jumla ya **Shilingi 19,200,000.00** zilikusanywa sawa na **asilimia 12.9** ya makisio yaliyopangwa. Fedha zilizokusanywa zimetokana na kodi ya pango katika Jengo la *Utawala Annex*. Mwenendo huo wa makusanyo ya maduhuli ulitokana na masharti ya kimkataba ambapo kodi ya pango hulipwa mwishoni mwa mwaka wa Fedha. Hivyo, mategemeo ni kukusanya **asilimia 100** ifikapo Juni, 2026.

2.3 Mafanikio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2025/26

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Februari, 2026 Mfuko wa Bunge umefanikiwa kutekeleza shughuli mbalimbali zinazohusu Mikutano ya Bunge, Vikao vya Kamati za Bunge, Ushiriki wa Mikutano ya Kimataifa pamoja na shughuli mbalimbali za uendeshaji wa Ofisi ya Bunge. Baadhi ya mafanikio hayo ni kama ifuatavyo:-

i. Kuratibu na kusimamia uendeshaji wa Mikutano miwili(2) ya Bunge (Mkutano wa Kwanza - tarehe 11 hadi 14 Novemba 2025, Mkutano wa Pili - tarehe 27 Januari hadi 06 Februari 2026;

ii. Kufanya ununuzi wa Magari 6 kwa ajili ya kuhudumia Viongozi na Watumishi wa Bunge.

iii. Kuajiri watumishi wapya 28 kwenye kada mbalimbali ili kuongeza ufanisi na nguvu kazi;

iv. Kuratibu mafunzo kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu uendeshaji wa Bunge na kamati zake;

v. Kuanda na kutekeleza Mpango Kazi wa Ununuzi wa Ofisi kwa Mwaka wa Fedha 2025/26;

vi. Kusimika mfumo mpya wa Sauti *(Digital Congress Network* – DCN) katika ukumbi wa Bunge pamoja na kufanya marekebisho mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwajili ya kuongeza tija na ufanisi wa shughuli za Bunge;

vii. Kuboresha majengo ya ofisi pamoja na kumbi mbalimbali za mikutano kama vile ukumbi wa Msekwa na ukumbi Mkubwa wa Mkutano wa Bunge; na

viii. Kuandaa Hesabu ya Mwaka *(Annual Accounts)* kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 pamoja na Taarifa za Ukaguzi kwa Mwaka wa fedha 2025/26.

2.4 Changamoto ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2025/2026

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42). Ofisi ilikabiliwa na changamoto zifuatazo ikiwemo: -

a) Kuwepo kwa shughuli ambazo hazikutengewa bajeti lakini ni muhimu kutekelezwa mathalani ongezeko la **Majimbo 8** ya Uchaguzi yaliyopelekea nyongeza ya Wabunge 11 hivyo kusababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji; na

b) Kupanda kwa mara kwa mara kwa gharama za bidhaa na huduma na kusababisha mahitaji ya uhamisho wa fedha ndani ya Fungu za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia changamoto hizo, Ofisi ya Bunge imefanya mashauriano na Wizara ya Fedha kuhusu upatikanaji wa fedha ili kugharamia shughuli muhimu katika utendaji kazi wa Bunge na kuhakikisha ofisi inatekeleza shughuli zake kulingana na bajeti iliyotengwa na kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo inayosimamia utekelezaji wa bajeti. Hivyo, changamoto hizo hazitarajiwi kujitokeza Mwaka wa Fedha 2026/27.

3.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA BUNGE (FUNGU 42) KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27

Mheshimiwa Spika, makadirio ya bajeti ya Ofisi ya Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2026/27 yamezingatia masuala yafuatayo:-

i) Dira ya Taifa (Dira 2050);

ii) Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa muda mrefu wa miaka 25;

iii) Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2026/2027 - 2030/203);

iv) Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka mmoja wa mwaka mmoja (2026/2027);

v) Mpango Mkakati wa Ofisi ya Bunge wa Mwaka 2026/2027 hadi 2030/2031 unaotekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja mmoja unaolenga kuwezesha Waheshimiwa Wabunge kutekeleza Majukumu yao ya Kikatiba kwa ufanisi;

vi) Majukumu ya Bunge Kikatiba;

vii) Malengo ya Taasisi;

viii) Majukumu ya Idara na vitengo;

ix) Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;

x) Sheria ya Bajeti Sura ya 439;

xi) Sheria ya Fedha za Umma Sura 348; na

xii) Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410.

3.1 Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/27

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2026/27 Mfuko wa Bunge umetengewa jumla wa **Shilingi** 225,021,780,000.00. Kati ya fedha hizo **Shilingi 24,889,142,000.00 ni** Mishahara, **Shilingi 183,103,656,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 17,028,982,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. kati ya kiasi kilichotengwa cha fedha za maendeleo, **Shilingi 16,385,882,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 643,100,000.00** ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba bajeti hiyo inatosheleza kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kikatiba na kisheria.

3.2 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Mfuko wa Bunge umepanga kukusanya Maduhuli jumla ya **Shilingi 191,553,000.00** yatakayotokana na ukodishaji wa kumbi za mikutano Ofisi ndogo ya Bunge Dar es Salaam na kodi ya pango kwenye ya jengo la *Utawala Annex* pamoja na Mgahawa uliopo katika Jengo la Utawala Dodoma.

4.0 VIPAUMBELE VYA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA 2026/27

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2026/27 Mfuko wa Bunge unatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kugharamia shughuli za Mikutano Minne (4) ya Bunge;

ii. Kugharamia shughuli za Mikutano Minne (4) ya Kamati za Bunge;

iii. Kugharamia Posho ya Jimbo, Usafiri na Stahili nyingine kwa Wabunge na Watumishi;

iv. Kugharamia Matibabu ya Wabunge na familia zao ndani na nje ya nchi pamoja na Watumishi;

v. Kuboresha maslahi ya Wabunge na Watumishi;

vi. Kugharamia mafunzo kwa Wabunge na Watumishi;

vii. Kuhudumia Viongozi Wastaafu wa Bunge kwa mujibu wa Sheria ya Mafao ya kustaafu ya Viongozi wa Kisiasa;

viii. Ununuzi wa Samani za Ofisi kwa ajili ya Viongozi na Watumishi;

ix. Ununuzi wa Vitendea Kazi *(Computer, Laptop/Ipad, Printer, Photocopier and Shredder)* kwa Watumishi;

x. Ushiriki katika Mikutano ya Kimataifa, hususan mikutano ya Vyama vya Kibunge ambavyo Bunge letu ni Mwanachama;

xi. Kuwa mwenyeji wa mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU);

xii. Kushiriki katika michezo ya Mabunge ya Afrika Mashariki na Shimiwi;

xiii. Kugharamia maadhimisho ya sherehe ya Kutimiza Miaka 100 ya Bunge la Tanzania;

xiv. Kugharamia uanzishwaji wa Taasisi ya Mafunzo ya Kibunge;

xv. Maboresho ya Mifumo ya TEHAMA ukiwemo Mfumo wa Bunge Mtandao *(e-parliament);*

xvi. Marekebisho ya Miundombinu ya TEHAMA katika Majengo ya Ofisi;

xvii. Kugharamia urushaji wa matangazo ya Bunge Mbashara kupitia Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) pamoja na mikutano ya Elimu kwa Umma;

xviii. Kugharamia gharama nyingine za uendeshaji wa Ofisi zikiwemo umeme, maji, usafiri, usafi na ulinzi;

xix. Kufanya Ukarabati Ofisi ya Dar es Salaam na Nyumba za Viongozi;

xx. Kuendelea kuboresha Mfumo wa Sauti (DCN) katika Ukumbi wa Bunge; xxi. Kusimika Mitambo ya Usalama katika maeneo ya majengo ya Ofisi; na

xxii. Ujenzi wa Uzio kuzunguka eneo la Bunge.

5.0 MAONI YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni yafuatayo:-

5.1 Uendelezaji wa Maeneo Mapya ya Ofisi za Bunge Dodoma

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inatenga fedha kwa awamu ili kuwezesha ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Wabunge ili wzitumie kwenye viunga vya Bunge. Hatua hii itasaidia kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kufanya kazi zao za kiofisi ndani ya viunga vya Bunge, sehemu ambayo itakuwa salama na inazingatia usiri.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kutoa pole kwa Familia, Wabunge wote na Serikali kwa kuondokewa na Mhe. William Lukuvi (Mb), aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, ***Hakika Bunge limepoteza Muwakilishi hodari, mahiri, mchapakazi na mzalendo.***

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mhe. Mussa Azzan Zungu, (Mb) Spika wa Bunge pamoja na Mhe. Daniel Baran Sillo (Mb) Naibu Spika kwa miongozo yenu katika kuendesha shughuli za Bunge. Aidha nitumie fursa hii kumshukuru Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Bal. Khamis Mussa Omar (Mb), Waziri wa Fedha, Mhe. Ummy Hamisi Nderiananga (Mb), Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mhe. Mshamu Ali Munde, (Mb), Mhe. Laurent Deogratius Luswetula, (Mb), Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao wakati Kamati inajadili bajeti ya Mfuko wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb	Mwenyekiti
2.	Mhe. Ally Hassan Omar King, Mb	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Bal.Dkt. Pindi Azara Chana, Mb	Mjumbe
4.	Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb	Mjumbe
5.	Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb	Mjumbe

6.	Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb	Mjumbe
7.	Mhe. Amina Idd Mabrouk, Mb	Mjumbe
8.	Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb	Mjumbe
9.	Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb	Mjumbe
10.	Mhe. Bahati Kenneth Ndingo, Mb	Mjumbe
11.	Mhe. Ally Yahya Mhata, Mb	Mjumbe
12.	Mhe. Kakulu Buchard Kakulu, Mb	Mjumbe
13.	Mhe. Dkt. Catherine Canute Joachim, Mb	Mjumbe
14.	Mhe. Moses Charles Bujaga, Mb	Mjumbe
15.	Mhe. Asma Ali Mwinyi, Mb	Mjumbe
16.	Mhe. Haran Nyakisa Sanga, Mb	Mjumbe
17.	Mhe. Devotha Daniel Mburarugaba, Mb	Mjumbe
18.	Mhe. Thomas Mgonto Kitima, Mb	Mjumbe
19.	Mhe. Enock Zadock Koola, Mb	Mjumbe
20.	Mhe. Nancy Hassan Nyalusi, Mb	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Ndg. Baraka I. Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa Mwaka wa Fedha 2026/27 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu yenye j umla ya **Shilingi 225,021,780,000** ambapo kiasi cha **Shilingi 24,889,142,000** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 183,103,656,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 17,028,982,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA BAJETI
01 Aprili, 2026

SPIKA: Ninakushukuru sana Mwenyekiti kwa kusoma taarifa hii muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kuwatangaza Makatibu Tawala wa Mikoa ambao wako ukumbini. Makatibu Tawala wa mikoa, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Mkutano wa Wabunge wote Kikao cha *Briefing* utafanyika siku ya leo Jumatano tarehe 1 Aprili, saa nane mchana katika Ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, kukaa toka asubuhi hapa nimepata hoja za Wabunge takribani wawili, kutaka kujua hali na mwenendo wa mafuta nchini. Nimewasiliana na Waziri wa Nishati na nimempa maelekezo na haya ni maelekezo rasmi ya Kiti, kuanzia leo wakutane na Kamati ya Nishati kujua mwenendo wa mafuta nchini, gharama na uhakika wa mafuta kupatikana kwenye Taifa. Kwa sababu bila mafuta tunaweza tukakwama kwenye mipango ya nchi na mambo mengine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Katibu wa Bunge atandaa utaratibu maalum wa kukutana kati ya Kamati yetu ya Nishati na Serikali na baada ya hapo Serikali itatoa taarifa Bungeni kujua mwenendo wa mafuta.

Baada ya tamko hilo ninasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11 jioni leo.

(Saa 7.01 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti.

MHE. EDWIN E. SWALLE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, UTAWALA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapitio na Matumizi ya Ofisi hiyo, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utangulizi; awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, ili kusoma Taarifa hii ya Kamati. Aidha, ninaomba taarifa hii ya kamati iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge, yani *Hansard,* kama ilivyowasilishwa Mezani kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kwa kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, ninatumia fursa hii kukushukuru sana wewe binafsi kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge hili Taarifa hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayohusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa taarifa hii umezingatia Masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 kwa kugawanyika katika sehemu kuu tano, kama zilivyoainishwa katika kurasa za taarifa hii ya Kamati. Msingi wa uchambuzi huu wa utekelezaji wa bajeti hiyo, Makadirio ya Mapato ya Ofisi ya Waziri Mkuu 2025/2027, unatokana na Masharti ya Kanuni ya 121(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge; masharti hayo yamezingatiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawanda ya Uchambuzi. Katika uchambuzi huu, Kamati imepitia jumla ya Mafungu Matano, kama ifuatavyo:-

(a) Fungu 25 – Ofisi ya Waziri Mkuu;

(b) Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu;

(c) Fungu 27 – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa;

(d) Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi; na

(e) Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2025/2026 ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) unaangazia maeneo makuu manne, ambayo ni haya yafuatayo:-

(a) Makusanyo ya maduhuli kuanzia Julai, 2025 hadi Februari, 2026;

(b) Upatikanaji wa fedha za Bajeti za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026;

(c) Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(d) Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Makusanyo ya Maduhuli Hadi Februari, 2026. Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) katika Mwaka unaoisha, 2025/2026, ilipangiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi bilioni 12.1, fedha hizo zinatokana na Fungu Na. 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu Na. 61 – Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, ambayo ilikusanya shilingi bilioni 100 na Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu imekusanya shilingi bilioni 12. Mwenendo wa makusanyo unaonesha kuwa, hadi kufikia Februari, 2026 Ofisi ya Waziri Mkuu ilikusanya shilingi bilioni 3.74, ambayo ni sawa na 30.92% ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi hicho kilitokana na makusanyo ya Fungu Na. 61 – Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 111.1 ambayo ni sawa na 111.13% ya lengo na Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu, shilingi bilioni 3.63, ambayo ni sawa na 30.25% ya lengo. Maelezo zaidi kuhusu makusanyo ya maduhuli yanapatikana katika ukurasa wa tano na wa sita wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Upatikanaji wa Fedha za Bajeti kwa Kipindi cha Julai, 2025 Hadi Februari, 2026. Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za bajeti kwa Mafungu Matano ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na. 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 50.47 ambapo shilingi bilioni 42.96 ni, kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha mishahara na OC na shilingi bilioni 7.5 ni fedha, kwa ajili ya maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2026 ambazo zilipokelewa ni shilingi bilioni 57, ambayo ni sawa na 113.46% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo matumizi ya kawaida zilipokelewa shilingi bilioni 40.95, sawa na 95.3% ya lengo la fedha, kwa ajili ya maendeleo na shilingi bilioni 6.31 sawa na utekelezaji wa 88.067% ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, fedha hizo ofisi hii imepokea na kutumia kiasi cha shilingi bilioni 10.05 kutoka kwenye vifungu vingine vya fedha kupitia mfumo wa uhamisho wa fedha, yaani *reallocation*. Maelezo zaidi kuhusu upatikanaji wa fedha kwa Fungu hili unapatikana kwenye ukurasa wa sita hadi wa tisa wa Taarifa hii ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Fungu Na. 25 – Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu. Ofisi iliidhinishiwa shilingi bilioni 29.746, kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ikijumuisha mishahara na OC. Hadi kufikia Februari, 2026 ofisi hii imepokea jumla ya shilingi bilioni 21.91, sawa na 73.6% ya kiasi kilichoidhinishwa. Kupokelewa kwa kiwango hicho cha kuridhisha, kumemwezesha Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kufanya kazi kubwa ya kuwafikia Watanzania waishio vijijini, wilayani na mikoani, kwa ajili ya kutatua matatizo mbalimbali ya wananchi ambao amewafikia moja kwa moja na kuwasikiliza bila kukaa kwenye ofisi yake. Kamati inatoa pongezi nyingi kwake Mheshimiwa Waziri Mkuu na inamtakia kila la kheri katika kuendelea kuyafanyia kazi matatizo mbalimbali ya wananchi na kutatua kero mbalimbali za Watanzania kote vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na. 27 – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa. Ofisi hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 31, katika kiasi hicho shilingi bilioni 1.3 ni, kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 12.45, kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi bilioni 17.56, kwa ajili ya ruzuku ya vyama vya siasa na shilingi bilioni 564, kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2026 mwenendo wa mapokezi ya fedha unaonesha kuwa, fedha za matumizi ya kawaida zilipokelewa shilingi bilioni 22.2, sawa na 70.88% ya lengo, ikijumuisha mishahara shilingi bilioni 733.13, sawa na 55.47% ya lengo. OC shilingi bilioni 9.769 sawa na 78.4%, ruzuku ya vyama ya siasa vyenye sifa ni shilingi bilioni 11.7 sawa na 66.7% ya lengo lililowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kipindi hicho ofisi hiyo haikuwa imepokea fedha za maendeleo. Kamati inashauri kuwa, fedha za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa zitolewe mapema, ili ziweze kusaidia miradi iliyopagwa kutekelezwa kwa wakati.

Maelezo zaidi kuhusu taarifa hii yapo kwenye Ukurasa wa 10 hadi wa 12 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na. 91 – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Ofisi hii ilikuwa imeidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 24.4 ikijumuisha *OC* shilingi 18.037, mishahara shilingi bilioni 5.07 na fedha za maendeleo shilingi bilioni 1.3. Hadi kufikia Februari, 2026 ofisi imepokea shilingi bilioni 20.908 sawa na 85.59% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, mishahara iliyopokelewa ni shilingi bilioni 3.4, fedha za *OC* shilingi bilioni 16.69 na miradi ya maendeleo shilingi bilioni 805.150.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya mapokezi ya fedha kwa Fungu 91 ni ya kuridhisha, kama ilivyo kwenye mafungu mengine. Kupokelewa kwa kiasi hicho cha kuridhisha kumeendelea kuiwezesha Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya kutekeleza majukumu yake vizuri na kuwa na mafanikio makubwa na hivyo kupunguza kiwango cha uingizaji, usambazaji na matumizi ya dawa za kulevya kwa zaidi ya 80%. Ufafanuzi zaidi kuhusu kupokelewa fedha hizo unapatikana ukurasa wa 12 hadi wa 13 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na. 61 – Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi. Ofisi hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 378.28; katika fedha hizo shilingi bilioni 10.66 ni, kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 367.617 ni, kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2026 ofisi hiyo imepokea jumla ya shilingi bilioni 695.056 ambapo kiasi kikubwa kilipokelewa kwenye fedha za maendeleo, kitendo kilichowezesha kutekelezwa kwa miradi ya maendeleo kwa ufanisi mkubwa, ikiwemo kugharamia Bajeti yetu ya Uchaguzi Mkuu kwa 100%, kitendo ambacho kinaenzi na kuupa heshima inayostahili uhuru wa nchi yetu uliopatikana tarehe 9 Disemba, 1961. Maelezo zaidi kuhusu kupokelewa kwa fedha hizi yanapatikana ukurasa wa 13 hadi wa 17 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Kwa upande wa Wizara hii Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu

na Wenye Ulemavu), Kamati ilikagua mradi mmoja kati ya miradi kumi. Mradi huo ni Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Utengamano, Itega, Dodoma, unaogharimu shilingi bilioni 5.667. Kamati imeelezwa kuwa, lengo kuu la ujenzi wa kituo hicho pindi utakapokamilika ni kutoa mafunzo katika programu zitakazowezesha waliokuwa waathirika wa dawa za kulevya, yani warahibu kurejea katika jamii wakiwa na ujuzi unaowawezesha kujitegemea na kuwa na shughuli halali za kujipatia kipato na hivyo kupunguza uwezekano wa mtu huyo kurudi tena katika kutumia dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa ujenzi wa mradi huu ulioanza tarehe 29 Januari, 2025 unatarajiwa kukamilika Tarehe 28 Januari, 2026. Hata hivyo, Kamati ilipotembelea ujenzi wa kituo hiki, ilikuta utekelezaji wake umefikia 45%. Kutokana na kutokukamilika kwa mradi huo Serikali imemwongezea mkandarasi muda wa nyongeza wa siku 207, hivyo mradi huu utakamilika tarehe 12 Septemba, 2026. Kuhusu lengo kuu la kujengwa kwa kituo hicho cha utengamano, ukaguzi wa Kamati ulipata wasiwasi wa kukamilika kwa lengo hilo, kwani miundombinu inayojengwa katika sehemu husika haisadifu kuwa kituo hicho kitakuwa cha mafunzo zaidi au cha vitendo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Uchambuzi wa Kamati ulijikita katika maeneo makuu mawili, ambayo ni Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2026/2027 na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2026/2027. Wizara, pamoja na taasisi zilizo chini yake, inaomba kuidhinishiwa makusanyo ya maduhuli ya jumla ya shilingi bilioni 12.020 kwa Mwaka wa Fedha ujao, 2026/2027. Kiasi hicho ni pungufu ya shilingi bilioni 80 ikilinganishwa na kiasi kilichotengwa katika Mwaka unaoisha, 2025/2026. Maelezo zaidi kuhusu maduhuli hayo yanapatikana kwenye ukurasa wa 23 hadi 24 wa Taarifa ya Kamati. Jumla kuu ya Makadirio na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, ofisi hii inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 171.269, ambapo ni shilingi bilioni 146.27 ambayo ni kwa

ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 24.998 ni kwa ajili maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 yameongezeka kwa shilingi bilioni 8.446 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 137,824,068,000 kilichokuwa kimeidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, ongezeko hili ni wastani wa asilimia 6.13. Kamati imebaini kuwa, ongezeko hilo limeakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma, kuongezeka kwa ajira na kufunguliwa kwa ofisi ya kanda kwa baadhi ya taasisi, ikiwemo Taasisi ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo zinazoombwa shilingi bilioni 24.998. Shilingi bilioni 20.7 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 4.298 ni fedha za nje. Maelezo zaidi kuhusu fedha hizi yanapatikana kwenye ukurasa wa 24 na 26 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati. Ili kusaidia Serikali kutekeleza vizuri bajeti hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(a) Serikali ihakikishe inadhibiti fedha za matumizi mengineyo, yaani *OC*, kwa kuhakikisha kuwa matumizi ya fedha hizo yanajikita katika kutoa huduma zinazogusa wananchi moja kwa moja, hususani wananchi wa hali ya chini.

(b) Serikali ihakikishe inaimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo, ili kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa wakati kwa kuzingatia thamani ya fedha na malengo yaliyokusudiwa.

(c) Wizara ihakikishe katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 inafuatilia na kukamilisha marekebisho ya kanuni inayoweka masharti kuhusu mwongozo na taratibu kwa taasisi za Serikali kuchapisha nyaraka zao kupitia Kiwanda cha Uchapishaji cha Nyaraka cha Serikali ili

kuongeza tija ya kiwanda, kutunza siri za Serikali kwa nyaraka ambazo zinahitaji usiri na hatimaye kuongeza mapato ya Serikali na kuufanya mradi wa kiwanda husika uwe na thamani ya fedha iliyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 91 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya yaani *(DCEA)*:-

(a) Mamlaka iimarishe udhibiti wa mipaka ya bahari na viwanja vya ndege kwa kutumia teknolojia za kisasa na kuongeza doria, ushirikiano na vyombo vingine vya ulinzi na usalama ili kudhibiti uingizwaji wa madawa ya kulevya nchini.

(b) Kwa kuwa mradi wa utengamano unatekelezwa katika eneo la Itega - Dodoma pamoja na malengo yake mengine, lengo kuu ni kutoa mafunzo katika programu zitakazowasaidia watu wenye uraibu wa madawa ya kulevya, kupata ujuzi utakaowawezesha kujiajiri mara baada ya kurejea kwenye jamii zao. Ili kuhakikisha kuwa lengo hili linafikiwa, ujenzi wa kituo hicho cha Itega uzingatie mahitaji ya programu zitakazofundishwa kwa kushirikiana na mamlaka za elimu na ufundi stadi na mamlaka zinazohusika na ustawi na maendeleo ya jamii.

(c) Kwa kuwa, kazi nzuri inayotekelezwa na *DCEA* ya kudhibiti uingizwaji na upatikanaji wa dawa za kulevya nchini imekuwa na matokeo chanya kwa kupunguza uingizaji na matumizi ya dawa za kulevya nchini kwa 80%, baadhi ya watumiaji wa dawa za kulevya wamekuwa wakitafuta mbinu mbadala kupata dawa hizo. Moja ya mbinu inayotumika hivi sasa ni kutengeneza dawa za kulevya kwa kutumia dawa nyingine ambazo matumizi yake yanaruhusiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kudhibiti hali hiyo, *DCEA* iongeze kasi ya ukaguzi wa viwanda na maduka ya dawa ya binadamu yaliyopo nchini na kuwachukulia hatua kali watu wote wanaouza

na kutumia ipasavyo madawa yenye kemikali za dawa za kulevya pasipo kufuata sheria, kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; ninapenda kuchukua nafasi hii kukushukuru sana wewe Naibu Spika, Spika, Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Aidha, kwa dhati kabisa, ninapenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati hii kutenda wajibu wake kwa ufanisi na hatimaye kazi hii kukamilika. Ninaomba kwa unyenyekevu mkubwa majina yao yote yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ninaomba pia nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pili, kwa uchapaji kazi wake hodari ambao sote pia tumeuona na kwa uongozi wake mzuri na mahiri kama Kiongozi Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni. Vilevile ninampongeza kwa namna alivyowasilisha makadirio yake ya mapato na matumizi ya ofisi yake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kwa masikitiko makubwa Kamati yetu inatoa pole kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuondokewa na Waziri wake mahiri, Hayati William Vangimembe Lukuvi aliyetutoka wiki iliyopita tarehe 25 mwaka 2026, baada tu ya tarehe 23 kufika mbele ya Kamati yetu na kuwasilisha randama ya bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee, Kamati inampatia pole nyingi Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na Waziri Mkuu wetu kwa kuondokewa na Waziri wake mahiri aliyekuwa akimsaidia kwenye Ofisi yake ya Waziri Mkuu ya Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu. Pole hizo pia tunazitoa pia kwake Mheshimiwa Ummy Nderiananga, Naibu Waziri wa Ofisi ya Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu kwa

kuondokewa na kiongozi wake, kwa mara nyingi tena tunamwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu William Vangimembe Lukuvi mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pole hizo Kamati inaendelea kumshukuru sana Waziri Mkuu kwa ushirikiano ambao ameendelea kuutoa kwa Kamati na hata baada ya kuondokewa na Waziri wake mahiri. Vilevile Kamati inampongeza Naibu Waziri wake Ummy Nderiananga kwa namna anavyomsaidia Waziri Mkuu katika kutekeleza majukumu yake na kwa ushirikiano wake mkubwa na Kamati hii. Ushirikiano wake umeifanya Kamati hii kufanya wajibu wake vizuri na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zake zote kwa ushirikiano wao kwa Kamati hii ya Utawala, Katiba na Sheria. Kipekee ninamshukuru Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Dkt. Jim Yonazi, Jaji Francis S. Mutungi - Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Jacob Mwambegele – Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Tume hiyo Ndugu Ramadhani Kailima na Ndugu Aretas James Lyimo - Kamishina Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati za Bunge na kuhakikisha kuwa Kamati inafanya wajibu wake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, ninaomba kuwasilisha na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA, KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE NA WENYE ULEMAVU) KWA MWAKA WA

FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, natumia fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

1.1 Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 kwa kugawanyika katika sehemu zifuatazo: -

(a) Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi, misingi na muundo wa taarifa hii;

(b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa fedha 2025/2026 katika maeneo yanayohusu makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati;

(c) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027;

(d) Sehemu ya Nne inahusu maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu Ofisi hii na Serikali kwa ujumla; na

(e) Sehemu ya Tano ni hitimisho ikijumuisha shukrani.

1.2 Msingi wa Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, uchambuzi na Maoni ya Kamati juu ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2026/2027 unatokana na matakwa ya Kanuni ya 121(4) ikisomwa kwa pamoja na vifungu 6(2)(d) na 7(1)(a) vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni na vifungu hivyo vimeweka masharti yanayoelekeza Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

1.3 Mawanda ya Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi huu, Kamati ilipitia jumla ya mafungu matano (5) ambayo ni: -

(a) **Fungu 25** - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu;

(b) **Fungu 37** - Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu;

(c) **Fungu 27** - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa;

(d) **Fungu 61** – Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi; na

(e) **Fungu 91** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 NA UZINGATIAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

2.1 Vipengele vya Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha Kamati kilichoketi tarehe 23 Machi, 2026, Kamati ilipokea, kujadili na kuchambua Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu-Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu iliyohusu Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Taarifa hiyo iliwasilishwa na hayati William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Waziri wa Wizara hiyo. Uchambuzi wa Kamati kuhusu Taarifa hiyo umeangazia maeneo makuu manne ambayo ni: -

(a) Makusanyo ya maduhuli kuanzia Julai, 2025 hadi Februari, 2026;

(b) Upatikanaji wa fedha za Bajeti za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026;

(c) Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha katika Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(d) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa kupitia Taarifa ya Kamati wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

2.2 Makusanyo ya maduhuli hadi Februari, 2026

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu ilipangiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 12,100,000,000.00**. Fedha hizo zinatokana na mafungu mawili kati ya mafungu Matano ya ofisi hiyo. Mafungu hayo ni **Fungu Na. 37** - Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu iliyopangiwa kukusanya **Shilingi 12,000,000,000.00**. Chanzo kikuu cha maduhuli katika fungu hilo ni

makusanyo kutokana na kazi za uchapishaji nyaraka za Serikali zinazotekelezwa na Wakala wa Serikali wa Uchapishaji (TGPA).

Aidha, **Fungu Na. 61** - Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ilipangiwa kukusanya **shilingi 100,000,000.00.** Chanzo kikuu cha makusanyo hayo ni malipo ya dhamana kutoka kwa wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi wa kisiasa.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli katika mafungu yote mawili ni kama ifuatavyo: -

(a) **Fungu 61** - Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, hadi kufika Februari, 2026 imekusanya kiasi cha Sh. **111,130,686.55** kati ya **shilingi 100,000,000,** sawa na ukusanyaji wa **asilimia 111.13** ya lengo la Makusanyo.

(b) **Fungu 37**-Ofisi ya waziri Mkuu imekusanya kiasi cha **Shilingi 3,630,788,440.00** kati ya shilingi **12,000,000,000,** sawa na **asilimia 30.25** ya lengo.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa makusanyo ya maduhuli kwa kila fungu unaoneshwa katika **Jedwali Na. 1.**

Jedwali Na. 1: Makusanyo ya Maduhuli hadi kufikia Februari 2026

FUNGU	Makadirio kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026	Makusanyo hadi Februari, 2026	Asilimia ya Makusanyo
Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu	12,000,000,000.00	3,630,788,440.00	30.25
Fungu 61 – Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi	100,000,000.00	111,130,686.55	111.13
JUMLA KUU	**12,100,000,000.00**	**3,741,919,126.55**	**30.92**

Chanzo: *Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu na Usanifu wa Kamati*

2.3 Tathmini ya Makusanyo

Mheshimiwa Spika, Fungu 61 limevuka malengo ya makusanyo ya maduhuli. Tathmini inaonesha kuwa, Tume hiyo imevuka lengo kutokana na usimamizi mzuri wa makusanyo yaliyotokana na malipo ya dhamana za wagombea wa nafasi za uongozi wa kisiasa katika uchaguzi mkuu uliofanyika mwaka 2025.

Kwa upande wa Fungu 37- Ofisi ya Waziri Mkuu-Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu, kiwango cha makusanyo hakikuwa cha kuridhisha kwani ilikuwa chini ya lengo la **asilimia 66.6** katika kipindi rejewa. Kamati ilielezwa kuwa, licha ya makusanyo kuonekana kuwa chini ya lengo, makusanyo hayo yanatarajiwa kuongezeka kutokana na kazi zinazoendelea za uchapishaji wa rejesta ya makazi na uchapishaji wa nyaraka za wizara ya afya zenye thamani ya **Shilingi 4,300,000,000.00**. Vilevile katika mahojiano na Serikali, Kamati ilifahamishwa kuwa, hali ya makusanyo itaongezeka zaidi baada ya Wizara kupitia Wakala wa Uchapishaji kulipwa fedha zilizotokana na kazi ya kuchapisha nyaraka za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Fungu 37- Ofisi ya Waziri Mkuu-Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu kiwango cha makusanyo ya maduhuli kingeweza kuwa kikubwa zaidi ya kiwango kilichokusanywa, endapo Wizara hiyo ingekusanya madeni inayozidai baadhi ya taasisi za Serikali kutokana na kuzifanyia kazi ya kuchapisha nyaraka za taasisi hizo. **Ni mtazamo wa Kamati kuwa, Wizara iongeze kasi ya kukusanya madeni hayo ili yaweze kulipwa kabla ya mwezi Julai, 2026**.

2.4 Upatikanaji wa Fedha za Bajeti kwa Kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia bajeti ya Ofisi hii, Kamati imeangazia mapokezi ya fedha za matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha mishahara (PE) na matumizi mengineyo (OC) pamoja na fedha kwa ajili ya maendeleo. Ufafanuzi kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:-

2.4.1 Fungu Na. 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi **50,472,143000.00**. Katika fedha hizo, shilingi **42,963,983,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ikujumuisha **Shilingi 8,369,915,000.00** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 34,594,068,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo fungu hili liliidhinishiwa shilingi **7,508,160,000.00** ikijumuisha fedha za ndani shilingi **741,381,000.00** na fedha za nje shilingi **6,766,779,000.00.** Kati ya hizo, shilingi **741,381,000.00** ni fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na kazi ya Ujenzi wa Kiwanda cha Kupiga Chapa cha Serikali Dodoma, shilingi **6,566,179,000.00** ni fedha za nje kwa ajili ya uratibu wa programu ya kuendeleza kilimo na uvuvi, na shilingi **200,600,000.00** ni fedha za nje kwa ajili ya kuimarisha uwezo wa nchi wa kujiandaa na kukabiliana na maafa.

Mheshimiwa Spika, hali ya mapokezi ya fedha hizo hadi februari, 2026 ilikuwa kama ifuatavyo:-

(a) Kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida, hadi kufikia Februari, 2026 fedha zilizopokelewa ni Shilingi **40,954,718,608.42** sawa na **Asilimia 95.3** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Mishahara ni shilingi **5,471,221,248.00** na fedha za Matumizi mengineyo ni shilingi **35,483,497,360.42**.

(b) Kwa upande wa fedha za maendeleo hadi februari, 2026 Fungu 37-Ofisi ya Waziri Mkuu ilipokea jumla ya shilingi **6,311,861,204.96** ya kiasi chote kilichoidhinishwa cha shilingi **7,508,160,000.00**, sawa na utekelezaji wa **asilimia 84.067** ya lengo.

Mheshimiwa Spika, mbali na fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa kama zilivyofafanuliwa hapo awali, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026, ofisi hii ilipokea na kutumia kiasi cha shilingi **10,054,579,803.00.** Kiasi hicho hakikuwemo kwenye kifungu cha fedha za matumizi ya kawaida kilichoidhinishwa, bali

fedha hizo zilipokelewa kutoka kwenye vifungu vingine vya fedha kupitia mfumo wa uhamisho wa fedha (Reallocation).

Uhamisho huo ulifanyika kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 41 cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439. Aidha, fedha hizo zilitumika katika masuala mbalimbali ikiwemo uratibu wa maafa kutokana na maporomoko ya mgodi mkoani Shinyanga, maazimishio ya Kumbukumbu ya Mashujaa na maboresho ya mfumo wa Usimamizi wa Maafa.

Mheshimiwa Spika; kwa ujumla, hali ya upatikanaji wa fedha katika fungu hili kwa mwaka wa fedha unaoisha (2025/2026) ulikuwa wa kuridhisha. Muhtasari wa mapokezi ya fedha hizo unaoneshwa katika **jedwali Na. 2** hapa chini:-

Jedwali Na. 2: Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 kwa Fungu 37

Eneo	Kiasi Kilichoidhinishwa	Kiasi kilichopokelewa	Asilimia
Mishahara (PE)	8,369,915,000	5,471,221,248	5.37
Matumizi Mengineyo (OC)	34,594,068,000	35,483,497,360.42	102.57
Ruzuku	-	10,000,000,000	-
Jumla Ndogo	42,963,983,000	40,954,718,608.42	95.3
Maendeleo	7,508,160,000	6,311,861,204.96	84.07
Jumla Kuu	**50,472,143,000**	**57,266,579,813.38**	**113.46**

Chanzo: *Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu na Usanifu wa Kamati.*

2.4.2 Fungu Na. 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu iliidhinishiwa shilingi **29,746,914,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi

1,630,183,000.00 ni Mishahara na shilingi **28,116,731,000.00** ni Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari 2026, ofisi hiyo ilipokea jumla ya shilingi **21,912,716,332.02**, sawa na asilimia **73.6** ya kiasi kilichoidhinishwa. Fedha hizo zinajumuisha Mishahara shilingi **1,169,932,000.00** na Matumizi Mengineyo shilingi **20,742,784,332.02**. Mchanganuo wa Bajeti na fedha zilizopokelewa hadi Februari 2026 umeoneshwa katika **Jedwali Na. 3** hapa chini.

Jedwali Na. 3: Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 kwa Fungu 25

FEDHA	MATUMIZI	BAJETI ILIYOIDHINISHWA	FEDHA ZILIZOPOKELEWA	% YA MAPOKEZI
MATUMIZI YA KAWAIDA	Matumizi Mengineyo (OC)	28,116,731,000.00	20,742,784,332.02	73.7
	Mishahara (PE)	1,630,183,000.00	1,169,932,000.00	71.7
JUMLA		**29,746,914,000.00**	**21,912,716,332.02**	**73.6**

Chanzo: *Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu na Usanifu wa Kamati*

Mheshimiwa Spika, mapokezi ya fedha za matumizi ya kawaida katika ofisi binafsi ya Waziri Mkuu yalikuwa ya kuridhisha kama yanavyooneshwa katika Jedwali Namba 3. Kupokelewa kwa kiasi hicho cha kuridhisha, kumemuwezesha Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Daktari Mwigulu Lameck Nchemba kufanya kazi kubwa ya kuwafikia watanzania waishio vijijini, katani, wilayani na mikoani kwa ajili ya kutatua matatizo yanayaowakabili moja kwa moja tena kwa ufanisi mkubwa bila kusubiri kuyatatulia matatizo hayo ofisini. Sote ni mashuhuda wa kazi kubwa na nzuri inayotekelezwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kamati inatoa pongezi nyingi kwake, na**

inamtakia kila la kheri katika kuendelea kufanya kazi zake za kutatua kero zinazowakabili wananchi wetu bila kuchoka.

2.4.3 Fungu Na. 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **31,901,469,000.00**. Katika kiasi hicho, shilingi **31,337,469,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ikujumuisha **Shilingi 1,321,730,000.00** kwa ajili ya Mishahara, Shilingi **12,452,739,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi **17,563,000,000.00** kwa ajili ya Ruzuku ya Vyama vya Siasa. Aidha, kiasi cha **Shilingi 564,000,000.00** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwa zote ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, hali ya mapokezi ya fedha zilizoidhinishwa hadi februari, 2026 ni kama ifuatavyo: -

(a) Kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida, hadi kufikia Februari, 2026 zimepokelewa Shilingi **22,210,667,432.17**, sawa na asilimia **70.88** ya kiasi kilichoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Mishahara (PE) ni Shilingi **733,133,728.00** sawa na asilimia **55.47** ya lengo, Matumizi Mengineyo (OC) **Shilingi 9,768,867,037.53** sawa na asilimia **78.45** na Ruzuku ya Vyama vya Siasa vyenye sifa ni **Shilingi 11,708,666,666.64** sawa na asilimia **66.7** ya lengo.

(b) Kwa upande wa fedha za maendeleo, hadi kufikia Februari, 2026 Fungu hili halikupokea fedha. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kiasi kilichotengwa ni kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Zanzibar. Kamati ilipata wasiwasi juu ya kiasi cha shilingi **564,000,000.00** kilichotengwa kwani kilionekana kuwa ni kidogo kwa kuwianisha na mradi unaolengwa kutekelezwa, na hivyo iliomba kufahamu gharama halisia za mradi huo. Hali hii ilitokana na ukweli kwamba, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya jengo hili katika miaka ya fedha iliyopita, ambapo kwa

miaka mingine kilitengwa kiasi kikubwa zaidi ya kilichotengwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, licha ya kutengwa kwa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na miaka mingine ya nyuma, kazi ya ujenzi imekuwa haianzi, na hivyo fedha hizo kutokutolewa. Katika majibu ya Serikali kwa Kamati, ilionekana kuwa kwa sasa bado gharama halisi za ujenzi wa jengo hilo hazijajulikana. Ilielezwa zaidi kuwa, gharama hizo zitajulikana mara baada ya kazi ya uchambuzi wa mchoro wa jengo hilo uliokwisha kukamilika. **Ni rai ya Kamati kuwa, gharama za ujenzi wa mradi huu zijulikane, na ujenzi wake uanze ili fedha zinazotengwa kwenye bajeti ziweze kutolewa**.

2.4.4 Fungu Na. 91 - Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Mamlaka ya kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) iliidhinishiwa jumla ya shilingi **24,425,887,000.00** ambapo shilingi **23,111,381,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kati ya fedha hizo matumizi mengineyo (OC) ni Shilingi **18,037,814,000.00** na mishara (PE) ni Shilingi **5,073,567,000.00**. Aidha kiasi cha Shilingi **1,314,506,000.00** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2026, **DCEA** imepokea jumla ya shilingi **20,908,337,640.29** sawa na **asilimia 85.59** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida imepokelewa shilingi **20,103,187,296.29** sawa na asilimia **86.98** ya lengo. Kiasi hicho kinajumuisha Mishahara shilingi **3,410,739,530.00** na Matumizi Mengineyo ni shilingi **16,692,447,766.29**. Aidha, kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo, fungu hili limepokea shilingi **805,150,344.00**, sawa na **asilimia 61.25** ya lengo.

Kwa ujumla, hali ya mapokezi ya fedha kwa fungu 91 ni ya kuridhisha katika mwaka 2025/2026. Kupokelewa kwa kiasi cha kuridhisha kumeendelea kuiwezesha taasisi ya **DCEA** kutekeleza majukumu yake ya kuzuia na kupambana na dawa za kulevya

kwa ufanisi, na hivyo kupunguza kiwango cha uingizwaji, usambazaji na matumizi ya dawa hizo nchini kwa kiwango cha **asilimia 80**. Muhtasari wa mapokezi ya fedha hizo ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 4 hapa chini.

Jedwali Na. 4: Mapokezi ya fedha hadi Februari 2026 kwa Fungu 91

Aina	Kilichoidhinishwa	Kilichopokelewa	Asilimia
PE	5,073,567,000	3,410,739,530.00	**67.2**
OC	18,037,814,000	16,692,447,766.29	**92.54**
Maendeleo	1,314,506,000	805,150,344	**61.25**
JUMLA	**24,425,887,000**	**20,908,337,640.29**	**85.59**

***Chanzo**: Taarifa ya utekelezaji ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Usanifu wa Kamati*

2.4.5 Fungu Na. 61 – Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026**,** Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **378,282,139,000.00**. Katika fedha hizo, shilingi **10,664,321,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo matumizi mengineyo (OC) ni Shilingi **5,715,586,000.00** na mishahara (PE) ni Shilingi **4,948,735,000.00.** Aidha, shilingi **367,617,818,000.00** iliidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2026, INEC imepokea jumla ya Shilingi **695,056,913,951.72** kwa mchanganuo ufuatao: -

(a) **shilingi 5,831,645,905.01** imepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kiasi ambacho ni **asilimia 55** ya

lengo**.** Kiasi hicho kinajumuisha Mishahara Shilingi **3,176,155,784.00** na matumizi mengineyo Shilingi **2,655,490,121.01**.

(b) Kwa upande wa fedha za maendeleo, zimepokelewa Shilingi **689,225,268,046.71.** Kiasi ambacho ni **asilimia 187.48** ya lengo.

Mchanganuo wa upatikanaji wa fedha hizo ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 5** hapa chini.

Jedwali Na.5: Upatikanaji wa fedha hadi Februari, 2026-Fungu 61

Aina	Kilichoidhinishwa	Kiasi Kilichopokelewa	Asilimia
Mishahara	4,948,735,000	3,176,155,784	64.18
Matumizi Mengineyo	5,715,586,000	2,655,490,121.01	46.46
Maendeleo Ndani	367,617,818,000	689,225,268,046.71	187.48
Maendeleo Nje	**0.00**	**0.00**	**0.00**
JUMLA	**378,282,139,000**	**695,056,913,951.72**	**183.74**

***Chanzo**: Taarifa ya utekelezaji ya Tume kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Usanifu wa Kamati.*

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa fedha kwa INEC ni kama unavyoonekana kwenye jedwali hapo juu ambapo mapokeo yake yalivuka lengo tarajiwa hususani katika kipengele cha fedha za ndani za maendeleo. Kamati ilielezwa kuwa,

kupokelewa kwa kiasi kikubwa zaidi kulichangiwa na Serikali kuamua kugharamia Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na uchaguzi mdogo wa jimbo la Peramiho lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea na Udiwani katika kata ya Shiwinga iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umejiridhisha kuwa, fedha hizo zilipokelewa kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 137 (3) (a) na (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Kwa kuzingatia Ibara hiyo, Bunge lilipokea na kuridhia taarifa ya matumizi ya fedha hizo katika Mkutano wa Pili wa Bunge la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa pongezi za dhati **kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan-Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa uthubutu wake wa kuwezesha nchi kuendesha Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na uchaguzi mdogo, shughuli iliyogharamiwa kwa asilimia 100 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. **Ni mtazamo wa Kamati kuwa, Serikali iendelee kugharamia chaguzi nyingine zijazo kwa asilimia 100. Kufanya hivyo, ni kuenzi na kuupa heshima inayostahiki uhuru wa nchi yetu uliopatikana tarehe 9 Disemba, 1961**.

2.4.6 Jumla Kuu ya Fedha zilizopokelewa hadi Februari, 2026

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu katika mafungu yote matano iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 514,828,552,000.00**. Kiasi hicho kinajumuisha Shilingi **137,824,068,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na **shilingi 377,004,484,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2026 Wizara pamoja na Taasisi zake imepokea jumla ya Shilingi **807,355,215,170.28** sawa na **asilimia 156.82** ya lengo. Kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida, zimepokelewa Shilingi **111,012,935,573.91** sawa na asilimia **80.55** ya lengo na fedha kwa ajili ya Maendeleo zimepokelewa Shilingi **696,342,279,596.37** sawa na asilimia **184.70** Mchanganuo wa mapokezi ya fedha hizo unaoneshwa katika **Jedwali Na. 6** (matumizi ya kawaida) na **Jedwali Na. 7** (fedha za maendeleo) hapa chini mtawalia.

Jedwali Na. 6 Mapokezi ya fedha za matumizi ya kawaida kwa mafungu yote hadi februari, 2026

FUNGU	FEDHA YA MATUMIZI ILIYOIDHINISHWA	KIASI KILICHOPOKELEWA	ASILIMIA
Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu	42,963,983,000.00	40,954,718,608.42	5.32
Fungu 25 – Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu	29,746,914,000.00	21,912,716,332.02	3.66
Fungu 27 – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa	31,337,469,000.00	22,210,667,432.17	0.88
Fungu 91 – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya	23,111,381,000.00	20,103,187,296.29	6.98
Fungu 61 – Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi	10,664,321,000.00	5,831,645,905.01	4.68
JUMLA KUU	**137,824,068,000.00**	**111,012,935,573.91**	**0.55**

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

Jedwali Na. 7: Mapokezi ya fedha za maendeleo kwa mafungu yote hadi februari, 2026

Mradi	Mradi	Kiasi Kilichoidhinishwa	Kiasi Kilichopokelewa	Asilimia
389	Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa-Zanzibar	564,000,000.00	-	-
937	Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Uchapaji Nyaraka za Serikali	741,381,000.00	906,073,958.96	122.21

429	Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP)	6,566,179,000.00	5,030,947,096.70	76.62
575	Mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Nchi wa Kujiandaa na Maafa	200,600,000.00	374.840,150.00	186.86
583	Mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Nchi wa kujiandaa na Maafa	367,617,818,000.00	689,225,268,046.71	187.48
510	Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Utengamao – Itega, Dodoma	1,314,506,000.00	805,150,344.00	61.25
JUMLA KUU		**377,004,484,00 0.00**	**696,342,279,596.37**	**184.70**

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

2.5 Ukaguzi wa Miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 inaweka masharti kwa Kamati za kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha (2025/2026) kabla ya kuanza uchambuzi wa bajeti ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati. Katika kuzingatia masharti hayo, Kamati ilifanya ziara katika mikoa mitano (5) na kukagua jumla ya miradi kumi (10) inayotekelezwa katika Wizara tano zinazosimamiwa na Kamati.

Lengo la ukaguzi huo ni kutathmini utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na kubainisha mafanikio na changamoto ili kuweza kulishauri Bunge kuhusu hatua za kuchukua katika kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara hii (Ofisi ya Waziri Mkuu-Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Kamati ilikagua mradi mmoja, kati ya miradi kumi. Mradi huo na uchambuzi wake ni kama ifuatavyo: -

2.5.1 Mradi Na. 5510: Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Utengamao – Itega, Dodoma

Mheshimiwa Spika, tarehe 18 Machi, 2026 Kamati ilitembelea na kukagua ujenzi wa kituo cha utengamao, katika eneo la Itega-Dodoma. Mradi unatekelezwa na kusimamiwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) kwa gharama ya **shilingi 5,666,515,760.00**. Kiasi hicho kinajumuisha **shilingi 5,367,668,960.00** kwa ajili ya mkandarasi wa ujenzi na **shilingi 298,846,800.00** kwa ajili ya mshauri elekezi.

Kamati ilielezwa kuwa, lengo kuu la ujenzi wa kituo hicho pindi utakapokamilika ni kutoa mafunzo katika progamu zitakazowawezesha waliokuwa waathirika wa dawa ya kulevya (waliokuwa waraibu) kurejea katika jamii wakiwa na ujuzi ili unaowawezesha kujitegemea na kuwa na shughuli za kufanya.

Mbali na lengo hilo kuu, malengo mengine ni kutumika katika kutoa huduma za matibabu na urekebishaji wa tabia kwa watu ambao wataonekana bado hali zao hazijatengamaa ipasavyo kutokana na uraibu wa kutumia dawa za kulevya. Ni maono ya DCEA kuwa, kupitia lengo kuu la mradi huo, kutawasaidia watu waliohitimu katika kituo hicho kutokurejea kwenye matumizi ya dawa za kulevya pindi watakapokuwa huru uraiani.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa ujenzi wa mradi huu ulianza **tarehe 29 Januari, 2025**, na ulitarajiwa kukamilika **tarehe 28 Januari, 2026**. Hata hivyo, Kamati ilipotembelea ujenzi wa kituo hiki, ilikuta utekelezaji wake umefikia **asilimia 45**. Kutokana na kutokukamilika huko, Serikali ilimuongezea mkandarasi muda wa nyongeza ya **siku 207**, hivyo mradi unatarajiwa kukamilika tarehe **12 Septemba, 2026**.

Aidha, hadi tarehe ya ukaguzi wa Kamati, mkandarasi anayejenga kituo hicho alikuwa amelipwa **shilingi 805,150,344.00**

kama malipo ya awali, na alikuwa ameshawasilisha hati za malipo ya **shilingi 1,079,213,024.33.00**, kiasi ambacho kilikuwa bado hakijalipwa. Aidha, kwa upande wa mshauri elekezi, hadi wakati Kamati ilipotembelea mradi huu, alikuwa hajalipwa kiasi chochote.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, kutokukamilika kwa mradi katika muda uliopangwa kulisababishwa na mkandarasi kuchelewa kuanza ujenzi wa mradi huo. Kuchelewa huko kulisababishwa na taratibu za kiserikali zilizotokana na changamoto za umiliki wa kiwanja kilipojengwa kituo. Changamoto hiyo ilikuwa inaikabili Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe ambayo ndio mmiliki wa kiwanja kwa kutokuwa na hati miliki ya kiwanja, iliyosababishwa na kudaiwa deni la **shilingi 270,795,850.00** na Halmashauri ya Jiji la Dodoma lililotokana na madai ya umilikishwaji na upimaji wa kiwanja. Kukosekana kwa hati miliki hiyo, kulichelewesha kukamilika kwa mchakato wa DCEA kuingia katika makubaliano (**MoU**) na Hospitali ya Mirembe juu ya ujenzi wa kituo katika kiwanja hicho.

Mheshimiwa Spika, licha ya sababu ya kuchelewa kwa mradi iliyoelezwa na Serikali, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kuchelewa kwa fedha za malipo ya mkandarasi ni sababu mojawapo inayochangia kutokukamilika kwa mradi huu katika muda uliopangwa. Endapo ulipaji wa fedha zinazoombwa na mkandarasi zitaendelea kuchelewa, kuna hatari ya mradi huu kutokukamilika katika muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tija tarajiwa ya mradi huu, Kamati ilielezwa kuwa mara baada ya kukamilka kwake, kazi kubwa ya kituo itakuwa ni kutoa mafunzo ya programu za kuwawezesha waliokuwa waathirika (waraibu) wa dawa za kulevya na kupata ujuzi utakaowasaidia kujiajiri pindi watakaporejea kwenye jamii zao. Licha ya lengo hili jema, ukaguzi wa Kamati ulibaini kutokuwepo kwa miundombinu ya kutolea mafunzo hayo na kutokuwepo kwa mpango unao ainisha aina ya mafunzo yanayokusudiwa kutolewa, ili miundombinu ya kituo iakisi mafunzo hayo. Zaidi, Kamati ilibaini uwepo wa vyumba vya kulala waraibu na wanafunzi na si madarasa ya karakana za kufundishia.

Mheshimiwa Spika, ni mtazamo wa Kamati kuwa, ili kuwezesha lengo kuu la kituo kutekelezeka kwa ufanisi, ni muhimu hatua zikachukuliwa mapema ili kuwezesha kituo husika kuwa na miundombinu ya kutolea mafunzo zaidi na kuwa na mpango wa aina ya programu zitakazofundishwa.

2.6 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati.

SEHEMU YA TATU

3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, tarehe 23 Machi, 2026; Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Waziri Mkuu-Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi wa Kamati ulijikita katika maeneo makuu mawili ambayo ni Makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa jumla katika maeneo hayo unaonesha kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu-Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu kupitia mafungu yake Matano, Wizara Pamoja na Taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi **12,020,000,000.00** kwa mwaka ujao wa fedha.

Aidha, kwa upande wa fedha za bajeti ikujumuisha matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo, ofisi hiyo inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **171,269,087,000.00,** ambapo shilingi

146,270,699,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **24,998,388,000.00** ni kwa ajili ya maendeleo. Mchanganuo wa maduhuli na fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo ni kama ifuatavyo: -

3.1 Makadirio ya Maduhuli

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 12,020,000,000.00.** Fedha hizo zinatarajiwa kukusanywa kutoka katika mafungu mawili ambayo ni **Fungu 37**-Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) kiasi cha **shilingi 12,000,000,000.00**. Fedha za Fungu 37 zinatarajiwa kukusanywa kupitia Wakala wa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Aidha, kwa upande wa **Fungu 61**-Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi maduhuli yanayoombwa kuidhinishwa ni kiasi cha **shilingi 20,000,000.00**.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, kiasi cha makadirio ya maduhuli kwa mwaka 2026/2027 ni pungufu ya kiasi cha **shilingi 80,000,000.00**, sawa na punguzo la **asilimia 0.66** ikilinganishwa na kiasi kilichotengwa katika mwaka unaoisha wa 2025/2026 cha **shilingi 12,100,000,000.00**.

Mchanganuo na ulinganisho wa maduhuli kwa mwaka 2025/2026 na 2026/2027 umeoneshwa katika **Jedwali Na. 8** la Taarifa ya Kamati.

Jedwali Na. 8: Makadirio ya Maduhuli Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

FUNGU	MAKADIRIO YA MADUHULI MWAKA 2025/2026	MAKADIRIO YA MADUHULI MWAKA 2026/2027	PUNGUFU
Fungu 37 – Wakala wa Mpigachapa Mkuu wa Serikali (TGPA)	12,000,000,000	12,000,000,000	0.0
Fungu 61 – Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi	100,000,000	20,000,000	80,000,000
JUMLA KUU	**12,100,000,000**	**12,020,000,000**	**80,000,000**

Chanzo: *Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu na Usanifu wa Kamati*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonesha kuwa, punguzo la makadirio ya makusanyo ya maduhuli limetokana na INEC kupunguza makadirio yake kwa **asilimia 80**. Kamati ilifahamishwa kwamba, punguzo hilo linatokana na matarajio ya kutokuwepo kwa makusanyo yanayotokana na dhamana za wagombea wa uongozi wa nafasi za kisiasa kufuatia kukamilika kwa shughuli za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Kamati inakubaliana na sababu hiyo, kwa kuwa chanzo hicho ndio kilikuwa chanzo mama cha maduhuli kwa INEC, ambacho kwa mwaka 2026/2027 chanzo hicho hakipo.

3.2 Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu katika mafungu yake Matano inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 146,270,699,000.00 kwa** ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 22,594,088,000.00** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 17,563,000,000.00** ni kwa ajili ya ruzuku kwa vyama vya

Siasa vyenye sifa na **Shilingi 106,113,611,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Mchangauo wa kila fungu unaoneshwa katika katika **Jedwali Na. 9** la Taarifa hii.

Jedwali Na. 9: Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2026/2027

FUNGU	MISHAHARA	MATUMIZI MENGINEYO	RUZUKU	JUMLA
Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu	8,566,573,000	40,680,246,000	0	49,246,819,000
Fungu 25 – Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu	1,850,441,000	30,000,000,000	0	31,850,441,000
Fungu 27 – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa	1,119,550,000	4,051,165,000	17,563,000,000	22,733,715,000
Fungu 91 – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya	6,106,560,000	25,666,614,000	0	33,087,680,000
Fungu 61 – Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi	4,950,964,000	5,715,586,000	0	10,666,550,000
JUMLA KUU	**22,594,088,000**	**106,113,611,000**	**17,563,000,000**	**146,270,699,000**

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 imeongezeka kiasi cha shilingi **8,446,631,000.00**, ikilinganishwa na kiasi cha shilingi **137,824,068,000.00** kilichoidhinishwa mwaka 2025/2026. Ongezeko hilo ni wastani wa **asilimia 6.13**. Uchambuzi wa Kamati imebaini

kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma, kuongezeka kwa ajira na kufunguliwa kwa ofisi za kanda kwa baadhi ya taasisi ikiwemo taasisi ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA).

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwepo kwa sababu za msingi na zinazokubalika za ongezeko hilo, **Kamati inaishauri Serikali kuongeza jitihada za kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima katika matumizi mengineyo (OC), kwa kuhakikisha inaweka vipaumbele katika matumizi yenye tija na yanayogusa moja kwa moja utoaji wa huduma kwa wananchi hususani wananchi wanaoishi katika hali duni na wenye mahitaji maalum, ikizingatiwa kuwa Wizara hii inahusika pia na watu wenye ulemavu na wanaopatwa na maafa mbalimbali yanayoathiri ustawi wa Maisha yao**.

3.3 Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu pamoja na taasisi zake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 24,998,388,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 20,700,777,000.00** ni fedha za ndani, na **Shilngi 4,297,611,000.00** ni fedha za nje. Mchanganuo huo ni kama unavyooneshwa katika **jedwali Na. 10** la Taarifa ya Kamati.

Jedwali Na. 10 : Makadirio ya Fedha za Maendeleo kwa Mwaka 2026/2027

Fungu	Jina la Mradi	Bajeti Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027	
		FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE
Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Uratibu na	**NA. 4937** Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha uchapaji nyaraka	741,381,000	0

Wenye Ulemavu	za Serikali Dodoma		
	NA. 4429 Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi	0	3,979,917,000
	NA. 6575 Kuimarisha Uwezo wa Nchi wa kujiandaa na Maafa		317,694,000
Fungu 27 – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa	**NA. 6389** Ujenzi wa jingo la Ofisi ya Msajili wa vyama vya Siasa Zanzibar	264,000,000	0
Fungu 61 – Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi	**NA. 6583** Program ya Kusaidia Uchaguzi Tanzania	18,380,890,000	0
Fungu 91 – Mamlaka ya Kudhibiti na kupambana na Dawa za kulevya	**NA. 5510** Ujenzi wa Kituo cha taifa cha Utengamao	1,314,506,000	
Jumla Ndogo		**20,700,777,000**	**4,297,611,000**
JUMLA KUU			**24,998,388,000**

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonesha kuwa, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepungua kwa **Shilingi 352,006,096,000.00** sawa na **asilimia 93.37** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha. Kamati imebaini kuwa,

punguzo la fedha hizo kwa sehemu kubwa linahusu fedha za miradi ya maendeleo.Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, sababu kuu ya kupungua kwa fedha katika eneo hilo, kunatokana na kukamilika kwa baadhi ya shughuli zilizohitaji fedha nyingi katika mwaka wa fedha 2025/2026. Shughuli mojawapo kubwa ambayo ilihitaji fedha nyingi na ilikamilika kwa mafanikio makubwa ni uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, licha ya kukamilika kwa baadhi ya miradi kwa mwaka wa fedha unaoisha, Kamati inatambua kuwa bado kuna miradi inayohitaji fedha katika mwaka wa fedha ujao. **Kamati inashauri Serikali kuendelea kubuni vyanzo mbadala vya mapato, ikiwemo kutekeleza baadhi ya miradi kupitia ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (Public Private Partnership-PPP) pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuhakikisha miradi ya maendeleo haiathiriwi na upungufu wa bajeti**.

SEHEMU YA NNE

4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, kufuatia majadiliano ya kina yaliyofanywa na Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mwaka 2025/2026 na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, ili kusaidia katika utekelezaji mzuri wa bajeti hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo: -

4.1 Maoni ya Jumla

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa Mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi hiyo kama ifuatavyo: -

(a) Serikali ihakikishe inadhibiti fedha za matumizi mengineyo (OC) kwa kuhakikisha kuwa matumizi ya fedha hizo yanajikita katika kutoa huduma zinazogusa wananchi moja kwa moja, hususani wananchi wa hali ya chini,

wenye mahitaji maalum na wanaokutwa na majanga yanayo athiri ustawi wa shughuli zao za uzalishaji.

(b) Serikali ihakikishe inaimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa wakati, kwa kuzingatia thamani ya fedha na malengo yaliyokusudiwa.

(c) Serikali ihakikishe inatoa kwa wakati fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa wakati, jambo ambalo litapelekea miradi hiyo kukamilika kwa muda uliopangwa na wananchi kuanza kunufaika mapema.

4.2 Ushauri Mahsusi Fungu kwa Fungu

4.2.1 Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu

(a) Serikali ihakikishe inapitia upya utekelezaji na matumizi ya fedha za **Mradi Na. 4429** unaohusu Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi, ili kuwezesha na kuhakikisha kuwa programu hiyo inakuwa na tija inayowanufaisha na kuwainua wananchi wanaojishughulisha na kilimo na uvuvi, kutoka kulima na kufanya uvuvi duni kwenda katika kilimo na uvuvi wa ngazi ya kati na baadae ngazi ya juu. Aidha, Serikali ihakikishe kuwa utekelezaji wa mradi huo unaambatana na usimamizi madhubuti, ufuatiliaji na tathmini ya mara kwa mara ili kubaini changamoto zinazojitokeza na kuzitatua kwa wakati.

(b) Wizara ihakikishe inafuatilia na kukusanya fedha zote zinazotokana na madeni inayozidai baadhi ya taasisi za Serikali, madeni yanayotokana na kufanya kazi ya kuchapa nyaraka mbalimbali za taasisi hizo kupitia Wakala wa Serikali wa Uchapishaji (TGPA).

(c) Wizara ihakikishe katika mwaka wa fedha 2026/2027, inafuatilia na kukamilisha marekebisho ya Kanuni itakayoweka masharti kuhusu mwongozo na taratibu kwa Taasisi za Serikali kuchapisha nyaraka zao kupitia Kiwanda

cha uchapishaji na nyaraka ili kuongeza tija ya kiwanda, kutunza siri za Serikali kwa nyaraka zinazohitaji usiri na hatimaye kuongeza mapato ya Serikali na kuufanya mradi wa kiwanda husika uwe na thamani ya fedha iliyotarajiwa.

4.2.2 FUNGU 91 – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA)

(a) Mamlaka iimarishe udhibiti wa mipaka ya bahari na viwanja vya ndege kwa kutumia teknolojia za kisasa na kuongeza doria na ushirikiano na vyombo vingine vya ulinzi na usalama ili kudhibiti uingizwaji wa dawa za kulevya nchini.

(b) Kwa kuwa mradi wa utengamao unaotekelezwa katika eneo la Itega-Dodoma pamoja na malengo yake mengine ambata, lengo kuu ni kutoa mafunzo katika programu zitakazowasaidia watu waliokuwa wameathiriwa na uraibu wa madawa ya kulevya kupata ujuzi utakaowawezesha kujiajiri mara watakaporejea kwenye jamii zao. Ili kuhakikisha lengo kuu linafanikiwa, ujenzi wa kituo cha Itega uzingatie mahitaji ya programu zitakazofundishwa, kwa kushirikiana na mamlaka za elimu na ufundi stadi na mamlaka zinazohusika na ustawi na maendeleo ya jamii.

(c) Kwa kuwa, kazi nzuri inayotekelezwa na DCEA ya kudhibiti uingizwaji na upatikanaji wa dawa za kulevya nchini imekuwa na matokeao chanya ya kupunguza uingizaji na matumizi ya dawa hizo nchini kwa asilimia 80, baadhi ya watumiaji wa dawa za kulevya wamekuwa wakitafuta mbinu mbadala za kupata dawa hizo. Moja ya mbinu inayotumika ni kutengeneza dawa za kulevya kwa kutumia dawa nyingine ambazo matumizi yake yanaruhusiwa. Ili kudhibiti hali hiyo, DCEA iongeze kasi ya ukaguzi wa viwanda na maduka ya dawa za binadamu yaliyopo nchini na kuwachukulia hatua kali watu wote wanaouza au kutumia isivyopaswa dawa zenye kemikali

za dawa za kulevya pasipo kufuata sheria, kanuni na taratibu.

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Aidha, kwa dhati kabisa, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb –**Mwenyekiti**
2. Mhe. Edwin Enosy Swalle, Mb – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb.
4. Mhe. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb.
5. Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb.
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.
7. Mhe. Asha Hussein Saleh, Mb.
8. Mhe. Esther Edwin Malleko, Mb.
9. Mhe. Maryam Ussi Yahya, Mb.
10. Mhe. Nassoro Rashid Nassoro, Mb.
11. Mhe. Dkt. Neema Peter Majule, Mb.
12. Mhe. Nyamizi Simon Mhoja, Mb
13. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb.
14. Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mb.
15. Mhe. Sikudhani Yasini Chikambo, Mb
16. Mhe. Timida Mpoki Fyandomo, Mb.
17. Mhe. Dkt. Yahaya Esmail Nawanda, Mb.
18. Mhe. Yohana Stephen Msita, Mb.
19. Mhe. Zena Maulid Katambo, Mb.
20. Mhe. Hussein Nassoro Amar, Mb.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza **Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb),** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwanza kwa kuchaguliwa kuwa Waziri Mkuu wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pili kwa uchapaji kazi wake hodari ambao sote tumeuona na kwa uongozi wake mzuri na mahiri kama Kiongozi mkuu wa shughuli za Serikali Bungeni. Vilevile ninampongeza kwa namna alivyowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa ufanisi Mkubwa.

Aidha, kwa masikitiko makubwa, Kamati inatoa pole kwa **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuondokewa na Waziri wake mahiri, Hayati William Vangimembe Lukuvi, aliyetutoka wiki iliyopita tarehe 25 Machi, 2026, baada ya siku ya tarehe 23 Machi, 2026 kukutana na Kamati yetu na kuwasilisha kwa ufanisi mkubwa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya ofisi yake ya mwaka 2025/2026, na makadirio ya ofisi ya Waziri Mkuu-Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Kwa namna ya kipekee, Kamati inampatia pole nyingi **Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba** (Mb) na Waziri Mkuu wetu kwa kuondokewa na Waziri aliyekuwa akimsaidia katika ofisi yake kwenye eneo la Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu. Pole hizo tunazitoa pia kwa Mhe. Ummy Nderiananga (Mb) na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu kwa kuondokewa na kiongozi wake. Kwa mara nyingine tena, **tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu Wiliam Vangimembe Lukuvi mahala pema peponi Amina**.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pole hizo, Kamati inaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa ushirikiano ambao ameendelea kuipatia Kamati hata baada ya kuondokewa na Waziri wake. Vilevile Kamati inampongeza Naibu Waziri wa Wizara hiyo Mhe. Ummy Nderiananga kwa namna anavyomsaidia Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yake na kwa ushirikiano wake mkubwa kwa Kamati. Ushirikiano wake umefanikisha Kamati kukamilisha shughuli zake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Dkt. Jim Yonazi, Mhe. Jaji Francis S. Mutungi - Msajili wa vyama vya Siasa, Mhe. Jaji Jacobs Mwambegele – Mwenyekiti wa Tume Huru

ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Tume hiyo Ndg. Ramadhani Kailima na Ndg. Aretas James Lyimo, Kamishina Jenerali wa Mamlaka ya kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leornard, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, nawashukuru Sekretarieti ya Kamati hii kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb
MWENYEKITI,
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA,
KATIBA NA SHERIA
01 Aprili, 2026

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Makamu Mwenyekiti kwa taarifa yenu nzuri ya maoni ya Kamati. Sasa nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, Mheshimiwa Dkt. Johannes Lukumay.

MHE. JOHANNES L. LUKUMAY – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI: Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kusema ninapenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kuniwezesha kusimama hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* - Fungu 92, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja

na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Awali ya yote ninaomba taarifa hii iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa huzuni na majonzi makubwa natoa pole kwako na kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na mpendwa wetu, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Hayati Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, aliyefariki Tarehe 25 Machi, 2026, Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2025, ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - Fungu 92, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane, moja ya majukumu ya Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI ni kushughulikia Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania. Jukumu hilo lilitekelezwa Tarehe 26 Machi, 2026, ambapo taarifa ya utekelezaji wa bajeti Fungu 92 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ilichambuliwa na kufanya ulinganisho kuhusu makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha taarifa ya Kamati inayojielekeza katika mambo makuu matatu:-

Moja, uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - Fungu 92 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

Mbili, uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania Fungu 92 kwa mwaka wa fedha 2026/2027;

Tatu, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania Fungu 92.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Kamati ilifanya uchambuzi wa utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa ajili ya kulisaidia Bunge kutambua kwa kina namna utekelezaji ulivyofanyika kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Uchambuzi huo ulizingatia mambo makuu matatu:-

(a) Uzingatiaji na utekelezaji wa ushauri uliotolewa na Kamati ya Bunge wakati wa kujadili makadirio ya matumizi ya Fungu 92 - Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania mwaka wa fedha 2025/2026;

(b) Uchambuzi wa mambo yaliyobainika wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi;

(c) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla uchambuzi huo ulilenga kuliwezesha Bunge kujiridhisha na utoshelevu wa utekelezaji wa mipango na mwenendo wa matumizi, ikilinganishwa na madhumuni ya Bunge kuidhinisha bajeti husika, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi kuhusu Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati. Kamati ilitoa ushauri Bungeni wakati wa majadiliano kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Katika kuhakikisha dhana ya kuisimamia Serikali inatekelezwa kikamilifu, Kamati hii ilijadili na kuchambua utekelezaji wa ushauri uliotolewa kwa Serikali kwa lengo la kuhakiki ikiwa ushauri huo umezingatiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa jumla ya maeneo saba yaliyotolewa ushauri ili kuboresha utendaji wa Serikali, kati ya maeneo hayo yaliyotolewa ushauri, maeneo matatu yametekelezwa kikamilifu na maeneo manne yanaendelea kutekelezwa. Kwa muktadha huo msukumo zaidi unahitajika katika maeneo ambayo utekelezaji wake

unaendelea ili yakamilishwe kwa wakati na kuweza kuleta tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi kuhusu Mambo Yaliyobainika Wakati wa Ziara ya Ukaguzi. Kamati ilifanya ziara Tarehe 19 Machi, 2026 katika Mkoa wa Dar es Salaam. Ziara hiyo ililenga kutembelea na kukagua konga iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilala. Kwa ujumla, Konga ni Baraza la Watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI wanaitwa WAVIU ngazi ya Halmashauri, lenye lengo la kuwaunganisha WAVIU na kuwafanya kuwa na sauti moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara hiyo, Kamati ilibaini uwepo wa mafanikio mbalimbali kama ifuatavyo: -

(i) Kusimamia ufuasi wa huduma ya tiba na mafunzo kwa wanachama wote wa Konga;

(ii) Kurudisha kwenye ufuasi wa dawa wanachama 200 kati ya wanachama 750 waliokuwa wameacha kutumia dawa za kufubaza UKIMWI;

(iii) Kushiriki katika shughuli za mwitikio wa UKIMWI kuanzia ngazi ya jamii hadi kitaifa, ikiwemo kushiriki katika Mikutano na Maonesho ya masuala ya UKIMWI Duniani;

(iv) Kuwafikia vijana 100 (wanaume 45 na wanawake 55) na klabu zenye jumla ya watoto 72 (wanaume 29 na wanawake 43) kwa ajili ya kutoa elimu na hamasa ya masuala ya UKIMWI Virusi Vya Ukimwi;

(v) Kuwaunganisha WAVIU kwenye fursa mbalimbali za kiuchumi ikiwamo mafunzo ya ujasiriamali na fursa za mikopo;

(vi) Kutekeleza Mradi wa 'HEBU TUYAJENGE' kati ya mwaka 2019 na 2024 kupitia ufadhili wa Serikali ya Marekani. Mradi huo unatekelezwa kwenye Kata za Buguruni, Kisukuru, Vingunguti, Majohe na Chanika. Mradi huo umesaidia WAVIU kupata elimu ya Virusi Vya UKIMWI na

UKIMWI na masuala ya kiuchumi, kuhamasisha jamii kupima Virusi Vya UKIMWI na kuhamasisha WAVIU kuanzisha vikundi vya masuala ya elimu, hamasa na uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, kupitia Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania katika kuleta mafanikio hayo, imebainika kuwepo kwa changamoto kadhaa katika maeneo hayo. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mwitikio mdogo wa wanaume kujitokeza kupata huduma na shughuli za mwitikio dhidi ya UKIMWI;

(ii) Unyanyapaa na ubaguzi bado ni changamoto hivyo kurudisha nyuma juhudi za Serikali na wadau katika kutokomeza maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi;

(iii) Upungufu wa rasilimali fedha kwa ajili ya kufadhili utekelezaji wa miradi ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi kuhusu Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Uchambuzi kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa fedha ulifanyika kwa kupitia taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 ambayo iliwasilishwa kwenye Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi huo imebainika kuwa, Mwaka wa Fedha 2025/2026, Tume iliidhinishiwa jumla ya shilingi 29,148,810,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na fedha za maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 8,500,478,932 ni matumizi ya kawaida yenye kujumuisha mishahara, shilingi 3,027,225,932. Shilingi 5,493,253,000 za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, fedha za miradi ya maendeleo ni shilingi 20,867,978,000 ambapo kati yake fedha za maendeleo yaani fedha za ndani, kupitia Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI ni shilingi 5,280,000,000 na fedha za maendeleo kutoka nje ni shilingi 15,587,978,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2026, imebainika kuwa Tume ilipokea kiasi cha shilingi 10,500,651,169.16 sawa na 36% ya bajeti yake yote iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa shilingi 4,467,420,060.18 ni matumizi ya kawaida sawa na 52% ya fedha zote za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa shilingi 1,424,839,522.67 ni kwa ajili ya mishahara sawa na 47% ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya mishahara. Shilingi 3,042,580,537.51 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na 55% ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo, imebainika kuwa hadi mwezi Februari 2026, kiasi cha shilingi 6,033,231,108.98 kimepokelewa, sawa na 28.9% ya fedha zote za maendeleo zilizoidhinishwa. Fedha hizo za maendeleo zilizopokelewa zinajumuisha fedha za maendeleo ya ndani yaani shilingi 1,320,000,000 sawa na 25% ya fedha za maendeleo za ndani zilizoidhinishwa kupitia Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, fedha za maendeleo za nje zilizopokelewa ni shilingi 4,713,231,108.98 sawa na 30.2% ya fedha za maendeleo kutoka nje ya nchi. Kielelezo namba moja kinaonyesha mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa na fedha zilizopokelewa kuanzia Julai, 2025 hadi Februari, 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla mwenendo wa upatikanaji wa fedha ambao ni 36% siyo wa kuridhisha kwani ilitakiwa hadi kufikia mwezi Februari, 2026 angalau fedha zipatikane kwa 70%. Hali hii ya kupatikana kiwango kidogo cha fedha inaathiri utekelezaji wa bajeti iliyopangwa kwani muda mchache umebaki ili kumaliza Mwaka wa Fedha 2025/2026. Aidha, Kamati inaisisitiza Serikali kutoa fedha zilizoidhinishwa na Kamati ya Bunge kwa wakati na kwa kiwango kilichoidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na kutokwamisha utekelezaji wa vipaumbele mbalimbali vilivyowekwa kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Fungu 92 (Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 umefanyika kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa kama vile Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026), Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2025/2030. Aidha, vipaumbele vya Mpango na Bajeti katika Makadirio ya Mwaka wa Fedha 2026/2027 vimezingatia miongozo ya kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha zinazoombwa kwa ajili ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI, kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Tume inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 7,772,971,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,829,043,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 4,943,928,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, Tume inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 4,908,284,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kielelezo namba mbili kinaonyesha mchanganuo wa fedha zinazoombwa kuidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imebainika kwamba bajeti ya Tume imepungua kwa 56.8% ambapo upungufu huo unajumuisha fedha za matumizi ya kawaida na fedha za miradi ya maendeleo. Kwa fedha za matumizi ya kawaida upungufu ni shilingi 747,507,932 sawa na asilimia 8.7 na kwa fedha za miradi ya maendeleo upungufu ni shilingi 15,959,694,000 sawa na 76%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo takwa la kikanuni kwa Kamati kufanya ulinganisho kati ya bajeti ya mwaka unaoisha na makadirio ya matumizi kwa mwaka unaofuata; ulinganisho huo umefanyika kati ya bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha 2025/2026 na makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha unaofuata 2026/2027, na mchanganuo wa ulinganisho huo umeainishwa kwenye kielelezo namba tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla bajeti imepungua hasa katika fedha za maendeleo za nje ambapo upungufu huo ni wa 69%. Hali hii inatokana na wafadhili kujiondoa kutoa fedha za kugharamia shughuli mbalimbali za kudhibiti UKIMWI nchini. Aidha, jedwali la ulinganisho linaonesha kwamba Mwaka wa Fedha 2025/2026, fedha za maendeleo za ndani kupitia Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI zilizotengwa ni shilingi 5,280,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizo zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza afua za kinga kwenye jamii hususani udhibiti wa maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI ikijumuisha utoaji wa elimu ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI; kuwezesha uendeshaji wa mfuko ikiwemo kugharamia vikao vya kila robo mwaka vya Bodi ya Mfuko; na kukabiliana na madhara ya UKIMWI (*Impact mitigation*) ikihusisha kuwawezesha WAVIU kiuchumi *(economic empowerment)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika makadirio ya matumizi ya mwaka 2026/2027, hakuna fedha za maendeleo za ndani zilizotengwa kupitia Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI. Hali hii inatokana na Serikali kusitisha ruzuku kwenda kwenye Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI badala yake imeanzishwa tozo maalum kupitia Sheria ya Fedha Na. 11 ya Mwaka 2025. Tozo hiyo maalum ya mwitikio dhidi ya UKIMWI *(HIV Response Levy)* ni mahsusi kwa ajili ya kuuwezesha Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI Tanzania kuwa himilivu na endelevu kwa kuwa na fedha za ndani za kutosha kugharamia mwitikio dhidi ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jitihada hizo, tunaipongeza sana Serikali kwa kuchukua hatua madhubuti za kuhakikisha nchi inakuwa na fedha za maendeleo za ndani za uhakika na za kutosha kwa ajili ya kudhibiti UKIMWI badala ya kutegemea fedha za nje kutoka kwa wafadhili. Aidha, Kamati inasisitiza Serikali kutumia fedha zinazopatikana mahsusi kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maoni na ushauri wa Kamati; baada ya uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na makadirio ya matumizi kwa

Mwaka wa Fedha unaofuata 2026/2027 kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Kamati imebaini namna utekelezaji wa vipaumbele na shughuli zilizopangwa kwenye bajeti inayoisha ulivyofanyika na kuhusianisha utekelezaji huo na bajeti inayoombwa kwa mwaka unaofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa lengo la kuboresha, kuimarisha na kuongeza uwajibikaji katika utekelezaji wa bajeti, sasa ninaomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kuhusu Mwenendo Usioridhisha wa Utoaji wa Fedha Zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2025/2026. Kutokana na fedha kutolewa kwa kiwango kidogo ikiwa ni 36% hadi mwezi Februari, 2026; athari ya kutokutolewa fedha hizo ni kurudisha nyuma jitihada za mapambano dhidi ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utoaji wa fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji bora wa shughuli zilizopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili, kuhusu Usimamizi wa Fedha za Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (*AIDS TRUST FUND – ATF*). Ili kuongeza usimamizi bora wa fedha za Mfuko, Kamati inaishauri Serikali ifanye yafuatayo:-

(i) Ihakikishe fedha zinazokusanywa kupitia tozo maalumu *(HIV Response Levy)* kwa ajili ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI zinapelekwa moja kwa moja kwenye Mfuko huo; na

(ii) Iweke namna nzuri ya kulinda fedha za mfuko kwa kuweka uzio wa kisheria (*ringfence*) katika makusanyo na matumizi ya Mfuko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba tatu ni kuhusu Kupungua kwa Kasi ya Utoaji wa Elimu kuhusu Virusi vya UKIMWI na UKIMWI. Imebainika kuwa kasi ya utoaji wa elimu kuhusu virusi vya UKIMWI na UKIMWI imepungua. Hali hii inaweza kusababisha kuongezeka kwa maambukizi mapya, hasa miongoni mwa vijana na makundi hatarishi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu virusi vya UKIMWI na UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kuhusu Uzalishaji wa Dawa za Kufubaza virusi vya UKIMWI Ndani ya Nchi. Kamati inatambua jitihada madhubuti zilizofanywa na Serikali katika kuanzisha maandalizi yatakayowezesha kufanya kazi kwa kiwanda cha kuzalisha dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI kilichopo Mkoani Arusha. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa maandalizi ili uzalishaji uanze hivi karibuni kwani uzalishaji wa dawa hizo ndani ya nchi utaongeza upatikanaji wa uhakika wa dawa na kupunguza gharama za kuagiza kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shukrani; ninapenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, ninapenda kukupongeza kwa namna unavyoliongoza Bunge kwa umahiri mkubwa. Vilevile, ninawashukuru na kuwapongeza Naibu Spika ambaye ndiye wewe mwenyewe leo na Wenyeviti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, tunamshukuru aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Hayati Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, ambaye mara zote alikuwa mstari wa mbele kushirikiana na Kamati kwenye masuala yote yaliyomhitaji. Kwa uchapakazi wake, hata siku moja kabla ya umauti kumkuta, alishiriki kikao cha Kamati. Tunamwombea Mwenyezi Mungu aipokee na kuilaza roho yake mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda vilevile kumshukuru Naibu Waziri Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga, kwa ushirikiano mkubwa alioupatia Kamati wakati wote walipohitajika katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Aidha, shukrani ziende kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Dkt. Jim James Yonazi pamoja na Maafisa wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania Dkt. Adam Mrisho na Watendaji wote wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati wakati ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninaomba niwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kujadili na kuchambua Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa mwaka 2025/2026, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Ninaomba majina yao yote yaingie kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu. Baraka I. Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema na kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania – Fungu 92 kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU (TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA – *TACAIDS*, FUNGU 92) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 KAMA ILIVYOWASILISHWA BUNGENI

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Awali ya yote kwa huzuni na majonzi makubwa natoa pole kwako na kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na mpendwa wetu, aliyekua Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Hayati Mheshimiwa William

Vangimembe Lukuvi (Mb), aliyefariki tarehe 25 Machi, 2026. Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake, Amina.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Toleo la Mwaka 2025, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania-*TACAIDS* (Fungu 92) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane, moja ya majukumu ya Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI ni kushughulikia Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania-(*TACAIDS)*. Jukumu hilo lilitekelezwa tarehe 26 Machi, 2026, ambapo Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti (Fungu 92) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ilichambuliwa na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, Naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati inayojielekeza katika mambo makuu matatu (3) ambayo ni yafuatayo:-

(a) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)*- **Fungu 92** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(b) Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)*- **Fungu 92** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027*;* na

(c) Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)*- **Fungu 92**.

SEHEMU YA PILI

UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa ajili ya kulisaidia Bunge kutambua kwa kina namna utekelezaji ulivyofanyika kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Uchambuzi huo ulizingatia mambo makuu matatu (3) ambayo ni yafuatayo: -

(a) Uzingatiaji na Utekelezaji wa ushauri uliotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya **Fungu 92** - Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(b) Uchambuzi wa mambo yaliyobainika wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi; na

(c) Mwenendo wa upatikanaji wa Fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2026.

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla uchambuzi huo ulilenga kuliwezesha Bunge kujiridhisha na utoshelevu wa utekelezaji wa mipango na mwenendo wa matumizi, ikilinganishwa na madhumuni ya Bunge kuidhinisha bajeti husika, kufuatilia na kusimamia utekelezaje wake.

Uchambuzi kuhusu Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitoa ushauri Bungeni wakati wa majadiliano kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Katika kuhakikisha dhana ya kuisimamia Serikali inatekelezwa kikamilifu, Kamati hii ilijadili na kuchambua utekelezaji wa ushauri uliotolewa kwa Serikali kwa lengo la kuhakiki ikiwa ushauri huo umezingatiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa jumla ya maeneo saba (7) yalitolewa ushauri ili kuboresha

utendaji wa Serikali. Kati ya maeneo hayo yaliyotolewa ushauri, maeneo matatu (3) yametekelezwa kikamilifu na maeneo manne (4) yanaendelea kutekelezwa. Kwa muktadha huo msukumo zaidi unahitajika katika maeneo ambayo utekelezaji wake unaendelea ili yakamilishwe kwa wakati na kuweza kuleta tija iliyokusudiwa.

Uchambuzi kuhusu mambo yaliyobainika wakati wa ziara ya ukaguzi

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara tarehe 19 Machi, 2026 katika Mkoa wa Dar es Salaam, ziara hiyo ililenga kutembelea na kukagua Konga iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilala. Kwa ujumla, Konga ni baraza la Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU) ngazi ya Halmashauri lenye lengo la kuwaunganisha WAVIU na kuwafanya kuwa na sauti moja.

Mheshimiwa Spika, Katika ziara hiyo, Kamati ilibaini uwepo wa mafanikio mbalimbali kama ifuatavyo: -

i) Kusimamia ufuasi wa huduma ya tiba na matunzo kwa wanachama wote wa Konga;

ii) Kurudisha kwenye ufuasi wa dawa wanachama 200 kati ya 750 waliokuwa wameacha kutumia dawa za kufubaza UKIMWI;

iii) Kushiriki katika shughuli za mwitikio wa UKIMWI kuanzia ngazi ya Jamii hadi Kitaifa ikiwemo kushiriki katika mikutano na maonesho ya masuala ya UKIMWI Duniani;

iv) Kuwafikia vijana 100 (wanaume 45 na wanawake 55) na klabu zenye jumla ya watoto 72 (wanaume 29 na wanawake 43) kwa ajili ya kutoa elimu na hamasa ya masuala ya VVU/UKIMWI;

v) Kuwaunganisha WAVIU kwenye fursa mbalimbali za kiuchumi ikiwemo mafunzo ya ujasiriamali na fursa za mikopo; na

vi) Kutekeleza mradi wa HEBU TUYAJENGE kati ya mwaka 2019 – 2024 kupitia ufadhili wa Serikali ya Marekani (USAID). Mradi huo umetekelezwa kwenye kata 5 za Buguruni, Kisukuru, Vingunguti, Majohe na Chanika. Mradi huo umesaidia WAVIU kupata elimu ya VVU/UKIMWI na masuala ya kiuchumi, kuhamasisha jamii kupima VVU na kuhamasisha WAVIU kuanzisha vikundi vya masuala ya elimu, hamasa na uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kupitia Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania katika kuleta mafanikio hayo, imebainika kuwepo kwa changamoto kadhaa katika maeneo hayo. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo: -

i) Mwitikio mdogo wa wanaume kujitokeza kupata huduma na shughuli za mwitikio dhidi ya UKIMWI;

ii) Unyanyapaa na ubaguzi bado ni changamoto hivyo kurudisha nyuma juhudi za Serikali na wadau katika kutokomeza maambukizi mapya ya VVU; na

iii) Upungufu wa rasilimali fedha kwa ajili ya kufadhili utekelezaji wa miradi ya kiuchumi.

Uchambuzi kuhusu Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2025/2026

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa fedha ulifanyika kwa kupitia Taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2025/2026 ambayo iliwasilishwa kwenye Kamati. Katika uchambuzi huo imebainika kuwa, mwaka 2025/2026 Tume iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 29,148,810,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na fedha za maendeleo. Kati ya fedha hizo **shilingi 8,520,478,932.00** ni matumizi ya kawaida yenye kujumuisha mishahara **shilingi 3,027,225,932.00** na **shilingi 5,493,253,000.00** za matumizi mengineyo. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo ni **shilingi 20,867,978,000.00** ambapo kati yake fedha za maendeleo (ndani) kupitia Mfuko wa Udhamini wa

UKIMWI *(Aids Trust Fund – ATF)* ni **shilingi bilioni 5,280,000,000.00** na fedha za maendeleo (nje) ni **shilingi billioni 15,587,978,000.00**.

Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia mwezi Februari, 2026, imebainika kuwa Tume ilipokea kiasi cha **shilingi 10,500,651,169.16** sawa na **asilimia 36** ya bajeti yake yote iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa **shilingi 4,467,420,060.18** ni matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 52** ya fedha zote za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa, **shilingi 1,424,839,522.67** ni kwa ajili ya mishahara sawa na **asilimia 47** ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya mishahara na **shilingi 3,042,580,537.51** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na **asilimia 55** ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa fedha za maendeleo, imebainika kuwa hadi mwezi Februari 2026, kiasi cha **shilingi 6,033,231,108.98** kimepokelewa sawa na **asilimia 28.9** ya fedha zote za maendeleo zilizoidhinishwa. Fedha hizi za maendeleo zilizopokelewa zinajumuisha fedha za maendeleo (ndani) **shilingi 1,320,000,000.00** sawa na **asilimia 25** ya fedha za maendeleo za ndani zilizoidhinishwa kupitia Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI *(Aids Trust Fund – ATF)*. Aidha, fedha za maendeleo za nje zilizopokelewa ni **shilingi 4,713,231,108.98** sawa na **asilimia 30.2** ya fedha za maendeleo (nje) zilizoidhinishwa.

Kielelezo 1: MCHANGANUO WA FEDHA ZILIZOIDHINISHWA NA FEDHA ZILIZOPOKELEWA KUANZIA JULAI, 2025 HADI FEBRUARI, 2026

MAELEZO	FEDHA ZILIZOIDHINISHWA	FEDHA ZILIZOPOKELEWA	ASILIMIA
Mishahara	3,027,225,932.00	1,424,839,522.67	47
Matumizi Mengineyo	5,493,253,000.00	3,042,580,537.51	55
JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA	**8,520,478,932.00**	**4,467,420,060.18**	**52**
Fedha za Maendeleo (ndani)	5,280,000,000.00	1,320,000,000.00	25
Fedha za Maendeleo (nje)	15,587,978,000.00	4,713,231,108.98	30
JUMLA YA FEDHA ZA MAENDELEO	**20,867,978,000.00**	**6,033,231,108.98**	**29**

JUMLA KUU (MATUMIZI YA KAWAIDA + FEDHA ZA MAENDELEO)	**29,388,456,932.00**	**10,500,651,169.16**	**36**

Chanzo: Taarifa ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla, mwenendo wa upatikanaji wa fedha ambao ni **asilimia 36** si wa kuridhisha kwani ilitakiwa hadi kufikia mwezi Februari, 2026 angalau fedha zipatikane kwa asilimia 70. Hali hii ya kupatikana kiwango kidogo cha fedha inaathiri utekelezaji wa bajeti iliyopangwa kwani muda mchache umebaki ili kumaliza mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, Kamati inaisisitiza Serikali kutoa fedha zilizoidhinishwa kwa wakati na kwa kiwango kilichoidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na kutokwamisha utekelezaji wa vipaumbele mbalimbali vilivyowekwa kwa kipindi cha mwaka 2025/2026.

UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Fungu 92 (Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania) kwa mwaka wa fedha 2026/2027 umefanyika kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa kama vile Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26), Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025 – 2030. Aidha, vipaumbele vya mpango na bajeti katika makadirio ya mwaka 2026/2027 vimezingatia miongozo ya kitaifa.

Fedha zinazoombwa kwa ajili ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka 2026/2027, Tume inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 7,772,971,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, **shilingi 2,829,043,000.00** ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi 4,943,928,000.00** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, kwa upande wa fedha za

maendeleo, Tume inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 4,908,284,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

KIELELEZO 2: FEDHA ZINAZOOMBWA KUIDHINISHWA KWA MWAKA 2026/2027



Chanzo; Randama ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2026/2027

Mheshimiwa Spika, Kwa Mwaka wa fedha 2026/2027 imebainika kwamba bajeti ya Tume imepungua kwa **asilimia 56.8** ambapo upungufu huo unajumuisha fedha za matumizi ya kawaida na fedha za miradi ya maendeleo. Kwa fedha za matumizi ya kawaida upungufu ni **shilingi 747,507,932.00** sawa na **asilimia 8.7** na kwa fedha za miradi ya maendeleo upungufu ni **shilingi 15,959,694,000.00** sawa na **asilimia 76**.

Mheshimiwa Spika, Kama ilivyo takwa la kikanuni kwa Kamati kufanya ulinganisho kati ya bajeti ya mwaka unaoisha na makadirio ya matumizi kwa mwaka unaofuata. Ulinganisho huo umefanyika kati ya bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha 2025/2026 na makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata 2026/2027, na mchanganuo wa ulinganisho huo umeainishwa kwenye Kielelezo Namba 3.

Kielelezo 3: ULINGANISHO WA BAJETI KWA MWAKA 2025/2026 NA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/2027

MAELEZO	2025/2026	2026/2027	ONGEZEKO/ PUNGUFU	ASILIMIA
MATUMIZI MENGINEYO (OC)	5,493,253,000.00	4,943,928,000.00	-549,325,000.00	**-10**
MISHAHARA	3,027,225,932.00	2,829,043,000.00	+41,464,000.00	**+1**
JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA	**8,520,478,932.00**	**7,772,971,000.00**	-747,507,932.00	**-8.7**
FEDHA ZA MAENDELEO (NDANI)	5,280,000,000.00	00	-5,280,000,000.00	**-100**
FEDHA ZA MAENDELEO (NJE)	15,587,978,000.00	4,908,284,000.00	-10,679,694,000.00	**-69**
JUMLA YA FEDHA ZA MAENDELEO	**20,867,978,000.00**	**4,908,284,000.00**	**-15,959,694,000.00**	**-76**
JUMLA	**29,388,456.000.00**	**12,681,255,000.00**	**-16,707,201,000.00**	**-56.8**

Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) kwa mwaka 2025/2026 na Randama kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2026/2027

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla bajeti imepungua hasa katika fedha za maendeleo za nje ambapo upungufu huo ni wa **asilimia 69**. Hali hii inatokana na wafadhili kujiondoa kutoa fedha za kugharamia shughuli mbalimbali za kudhibiti UKIMWI nchini. Aidha, jedwali la ulinganisho linaonesha kuwa mwaka 2025/2026 fedha za maendeleo za ndani kupitia Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI *(Aids Trust Fund – ATF)* zilizotengwa ni shilingi **5,280,000,000.00**, fedha hizo zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza afua za kinga kwenye jamii hususani udhibiti wa maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI (VVU) ikijumuisha utoaji wa elimu ya VVU na UKIMWI; kuwezesha uendeshaji wa mfuko ikiwemo kugharamia vikao vya kila robo mwaka vya bodi ya mfuko; na kukabiliana na madhara ya UKIMWI *(Impact mitigation)* ikihusisha kuwawezesha WAVIU kiuchumi *(Economic Empowerment)*.

Mheshimiwa Spika, Katika makadirio ya matumizi ya mwaka 2026/2027, hakuna fedha za maendeleo za ndani zilizotengwa kupitia Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI *(Aids Trust Fund – ATF)*. Hali hii inatokana na Serikali kusitisha ruzuku kwenda kwenye Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI *(Aids Trust Fund – ATF)* badala yake imeanzishwa tozo maalumu kupitia Sheria ya fedha na 11 ya mwaka 2025. Tozo hiyo maalumu ya mwitikio dhidi ya UKIMWI *(HIV Response Levy)* ni mahsusi kwa ajili ya kuuwezesha Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI *(Aids Trust Fund – ATF)* kuwa himilivu na endelevu kwa kuwa na fedha za ndani za kutosha kugharamia mwitikio dhidi ya Virusi vya UKIMWI (VVU)na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Kwa jitihada hizo, tunaipongeza sana Serikali kwa kuchukua hatua madhubuti za kuhakikisha nchi inakua na fedha za maendeleo za ndani za uhakika na za kutosha kwa ajili ya kudhibiti UKIMWI badala ya kutegemea fedha za nje kutoka kwa wafadhili. Aidha, Kamati inasisitiza Serikali kutumia fedha zinazopatikana mahsusi kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizopangwa.

SEHEMU YA TATU

MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Baada ya uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026; na makadirio ya matumizi kwa mwaka unaofuata 2026/2027 kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Kamati imebaini namna utekelezaji wa vipaumbele na shughuli zilizopangwa kwenye bajeti inayoisha ulivyofanyika na kuhusianisha utekelezaji huo na bajeti inayoombwa kwa mwaka unaofuata.

Mheshimiwa Spika, Kwa lengo la kuboresha, kuimarisha na kuongeza uwajibikaji katika utekelezaji wa bajeti, sasa naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

Mwenendo Usioridhisha wa Utoaji wa Fedha Zilizoidhinishwa Mwaka 2025/2026

Mheshimiwa Spika, Kutokana na fedha kutolewa kwa kiwango kidogo ikiwa ni asilimia 36 hadi mwezi Februari 2026. Athari ya kutokutolewa fedha hizo ni kurudisha nyuma jitihada za mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utoaji wa fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji bora wa shughuli zilizopangwa.

Usimamizi wa Fedha za Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI *(AIDS TRUST FUND – ATF)*

Mheshimiwa Spika, Ili kuongeza usimamizi bora wa fedha za Mfuko, Kamati inaishauri Serikali ifanye yafuatayo: -

i. Ihakikishe fedha zinazokusanywa kupitia tozo maalumu *(HIV Response Levy)* kwa ajili ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI zinapelekwa moja kwa moja kwenye mfuko huo; na

ii. Iweke namna nzuri ya kulinda fedha za mfuko kwa kuweka uzio wa kisheria *(ringfence)* katika makusanyo na matumizi ya mfuko huo.

Kupungua kwa Kasi ya Utoaji wa Elimu kuhusu Virusi vya UKIMWI na UKIMWI

Mheshimiwa Spika, Imebainika kuwa kasi ya utoaji wa elimu kuhusu Virusi vya UKIMWI na UKIMWI imepungua, hali hii inaweza kusababisha kuongezeka kwa maambukizi mapya, hasa miongoni mwa vijana na makundi hatarishi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu Virusi vya UKIMWI na UKIMWI.

Uzalishaji wa Dawa za Kufubaza Virusi vya UKIMWI Ndani ya Nchi

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua jitihada madhubuti zilizofanywa na Serikali katika kuanza maandalizi yatakayowezesha kufanya kazi kwa kiwanda cha kuzalisha dawa

za kufubaza Virusi vya UKIMWI kilichopo Arusha. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa maandalizi ili uzalishaji uanze hivi karibuni kwani uzalishaji wa dawa hizo ndani ya nchi utaongeza upatikanaji wa uhakika wa dawa na kupunguza gharama za kuagiza kutoka nje ya nchi.

4.5 SHUKRANI

Mheshimiwa Spika, Napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, napenda kukupongeza kwa namna unavyoliongoza Bunge kwa umahiri mkubwa. Vilevile, nawashukuru na kuwapongeza Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya pekee, tunamshukuru aliyekuwa Waziri wa nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Hayati Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi (Mb)ambae mara zote alikuwa mstari wa mbele kushirikiana na Kamati kwenye masuala yote yaliyomuhitaji. Kwa uchapakazi wake, hata siku moja kabla ya umauti kumkuta, alishiriki kikao cha Kamati. **TUNAMUOMBEA MWENYEZI MUNGU AIPOKEE NA KUILAZA ROHO YAKE MAHALI PEMA PEPONI, AMINA.**

Mheshimiwa Spika, Vilevile, napenda kumshukuru Naibu Waziri Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga (Mb) kwa ushirikiano mkubwa alioipatia Kamati wakati wote walipohitajika katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Aidha, shukrani ziende kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Dkt. Jim James Yonazi pamoja na Maafisa wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati wakati wote.

Mheshimiwa Spika, Napenda kumshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) Dkt. Adam Mrisho na Watendaji wote wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati wakati ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Kipekee naomba niwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kujadili na kuchambua Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa mwaka 2025/2026, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, Naomba kuwatambua majina yao kama ifuatavyo: -

1.	Mhe. Dkt. Johannes Lembulung Lukumay, Mb	**MWENYEKITI**
2.	Mhe. Dkt. Zeyana Abdallah Hamid, Mb	**M/MWENYEKITI**
3.	Dkt. Zeyana Abdallah Hamid, Mb	Mjumbe
4.	Mhe. Jacqueline Kainja Andrew, Mb	Mjumbe
5.	Mhe. Adonis Alfred Bitegeko, Mb	Mjumbe
6.	Mhe. Janeth Peter Pinda, Mb	Mjumbe
7.	Mhe. Juma Mustafa Kawamba, Mb	Mjumbe
8.	Mhe. Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas, Mb	Mjumbe
9.	Mhe. Neema Gerald Mwandabila, Mb	Mjumbe
10.	Mhe. Aysharose Ndogholi Mattembe, Mb	Mjumbe
11.	Mhe. Japhael Masanja Lufungija, Mb	Mjumbe
12.	Mhe. Kassim Hassan Haji, Mb	Mjumbe
13.	Mhe. Husnain Gulamabbas Dewji, Mb	Mjumbe
14.	Mhe. Haji Ussi Muhsin, Mb	Mjumbe
15.	Mhe. Nadra Ghulam Rashid, Mb	Mjumbe
16.	Mhe. Mattar Ali Salum, Mb	Mjumbe
17.	Mhe. Eric James Shigongo, Mb	Mjumbe
18.	Mhe. Yagi Maulid Kiaratu, Mb	Mjumbe
19.	Mhe. Jamila Mahmoud Juma, Mb	Mjumbe
20.	Mhe. Neema William Mgaya, Mb	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, Napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu. Baraka I. Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema na kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - Fungu 92 kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, Naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Johannes Lembulung Lukumay, (Mb)
MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA
NA MASUALA YA UKIMWI
1 Aprili, 2026

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Johannes Lukumay kwa taarifa ya Kamati. Sasa ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Hawa Chakoma Mchafu, karibu.

MHE. HAWA M. CHAKOMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Taarifa ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Mahusiano kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi Hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Ajira na Mahusiano kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kurahisisha mtiririko wa maudhui pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge yanayohusu taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa

Bungeni, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya kwanza inatoa, Msingi wa Uchambuzi na Mawanda ya Uchambuzi;

(ii) Sehemu ya pili inachambua na kufanya tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(iii) Sehemu ya tatu inachambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;

(iv) Sehemu ya nne inafafanua Maoni ya Kamati na Ushauri unaotolewa kwa Serikali; na

(v) Sehemu ya mwisho inahitimisha taarifa ya uchambuzi na kuonesha msimamo wa Kamati

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Msingi wa Uchambuzi. Ili kukidhi masharti hayo, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira, Kazi na Mahusiano kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Katika hatua hiyo Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na kuja na matokeo kama yaliyoainishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa. Taarifa ya Kamati inahusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano inahusika na mafungu mawili ambayo ni Fungu 65 Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Mahusiano; na Fungu 15 Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Ili kukidhi masharti hayo, tarehe 23 Machi, 2026 Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Taarifa hiyo ilijumuisha Mpango na Bajeti ya Fungu 65 pamoja na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)* Fungu 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hatua hiyo, Kamati inatoa taarifa kuhusu mambo yafuatayo:-

(i) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati;
(ii) Ukaguzi wa Miradi;
(iii) Utekelezaji wa Vipaumbele;
(iv) Hali ya Ukusanyaji wa Maduhuli; na
(vi) Hali ya upatikanaji wa Fedha

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati; katika kulisaidia Bunge kutekeleza jukumu lake la kuishauri Serikali, tarehe 9 Aprili, 2025 wakati wa uwasilishaji wa hotuba ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano kwa Mwaka Fedha 2025/2026; Kamati ilitoa Maoni na Ushauri kuhusu mambo sita kwa Fungu 65 na Fungu 15. Ninaomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa baadhi ya maeneo ushauri wa Kamati umezingatiwa huku maeneo mengine utekelezaji wa ushauri wa Kamati haujafanyiwa kazi kwa kiwango cha kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaitaka Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 65) na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (Fungu 15) kuhakikisha kuwa inatekeleza ushauri wa Kamati ili kuleta matokeo chanya katika sekta ya ajira nchini. Hivyo, Kamati ilibaini kuwa ukomo wa bajeti na mtiririko wa fedha za maendeleo usioridhisha kutoka Hazina ni sababu kubwa inayochangia Mafungu haya kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha; kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika Mkoa wa Dar es Salaam. Kamati ilikagua miradi miwili ambayo ni sehemu ya miradi iliyotengewa fedha kiasi cha shilingi 13,322,106,000 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Ninaomba kubainisha na kufafanua miradi hiyo pamoja na kufanya majumuisho ya mambo yaliyojitokeza katika ukaguzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi Namba 6581; Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi Katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi

Kigamboni; kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kiasi cha shilingi 60,000,000 kilitengwa kwa ajili ya kutekeleza programu hii katika chuo cha maendeleo ya wananchi Kigamboni kwa wanagenzi wapatao 120. Hadi mwezi Machi, 2026 Serikali ilikuwa imetoa kiasi cha shilingi 30,000,000 sawa na 50% ya fedha zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi Namba 5505; Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Mashauri ya Usuluhishi na Uamuzi. Kupitia *CMA* unatekeleza Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi na Uendeshaji wa mashauri ambao unajulikana kama e-Utatuzi. Mradi huu una lengo la kuongeza ufanisi na uwazi katika kushughulikia migogoro ya ajira nchini. Aidha, utaondoa matumizi ya nakala mango *(hard copy)* na kurahisisha utunzaji na upatikanaji wa majalada na nyaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa mradi huu kutajibu tamanio la Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuacha tabasamu kwa wananchi kwani utaharakisha na kurahisisha upatikanaji wa haki katika usuluhishi na uamuzi wa migogoro ya ajira nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza mradi huu, Tume (Fungu 15) ilitengewa jumla ya shilingi 276,046,000 katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ambapo Serikali imepeleka fedha zote kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi: tathmini ya Kamati imebainisha kuwa:-

(a) Utekelezaji wa sehemu kubwa ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati imezingatia thamani ya fedha na hatua iliyofikiwa inawiana na muda wa utekelezaji wa miradi husika; na

(b) Utekelezaji wa miradi na programu zilizotembelewa na Kamati zimeshirikisha wananchi ambao ni wanufaika wa miradi na programu hizo moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 65) na Tume (Fungu 15). Kamati inalitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika kutekeleza miradi hiyo thamani ya fedha, uwekezaji, ufanisi na tija vimezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hatua iliyofikiwa katika ukusanyaji wa maduhuli. Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia masuala yafuatayo:-

(i) Kiasi kilichokusanywa ikilinganishwa na lengo la makusanyo; na

(ii) Ulinganisho wa kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano (Fungu 65) ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 55,000,000,0000. Hadi kufikia Februari, 2026 Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi 38,029,945,099, sawa na 69.15% ya lengo la makusanyo liliyoidhinishwa na Bunge. Kamati ina maoni kuwa mwenendo wa makusanyo ya maduhuli unaridhisha na Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 65) itafikia lengo la makusanyo lililoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Kamati ilipokea na kuchambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa Fungu 65 na fungu 15 kutoka Hazina kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 65 - Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano. Uchambuzi wa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa Fungu 65 hadi kufikia mwezi Februari, 2026 umeonesha mambo yafuatayo: -

(i) Upatikanaji wa jumla ya fedha zilizoidhinishwa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu Fungu 65 ni 61.40% ikiwa ni upungufu wa asilimia 5.3 ya muda wa utekelezaji wa bajeti. Ni maoni

ya Kamati kuwa ikiwa hali hii itaendelea hivi itaathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa;

(ii) Fedha za matumizi ya kawaida zilizopatikana kwa 61.6% ikiwa na upungufu wa asilimia 5.1 ya fedha zilizotakiwa katika kipindi kama hicho;

(iii) Fedha za Matumzi mengineyo *(OC)* zimepokelewa kwa 65.2% ambapo ilitakiwa kuwa zimepokelewa 66.7% kulinganisha na muda wa utekelezaji wa Bajeti;

(iv) Fedha za mishahara zilizopokelewa ilikuwa 58.03% ikiwa na upungufu wa asilimia 8.67 ya fedha zilizotakiwa katika kipindi hicho;

(v) Fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo zilipatikana kwa 60.90% ya bajeti; na

(vi) Katika fedha za kugharamia miradi ya maendeleo, Fedha za Ndani zilifikia 62.4% na fedha za nje 22.15%.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni pungufu kwa asilimia 5.8 ukilinganisha na muda wa utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaitaka Wizara ya Fedha kuhakikisha inatoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 65) kama ilivyoinidhinishwa na Bunge ili kuleta tija na ustawi wa wananchi kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Fungu 15 - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)*. Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (Fungu 15), uchambuzi wa mwenendo wa upatikanaji wa fedha hadi kufikia Februari, 2026 ulionesha mambo yafuatayo:-

(i) Tume ilipokea 55.0% ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Hii ni pungufu ya 11.7% ukilinganisha na muda wa utekelezaji wa Bajeti. Mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha

unaweza kuathiri shughuli zilizopangwa kama hautarekebishwa;

(ii) Fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa zilikuwa 53.3% ukilinganisha na 66.7% zilizotakiwa kuwa zimepokelewa hadi kipindi hiki cha utekelezaji wa ya bajeti;

(iii) Fedha za matumizi mengineyo *(OC)* zilizopokelewa ni 51.4% na huku mishahara ikiwa imepokelewa kwa 56%. Upungufu wa fedha katika mishahara imetokana na kucheleweshewa kibali cha kuajiri watumishi wapya;

(iv) Fedha za miradi ya maendeleo zilipokelewa kwa 100% kwa ajili ya utekelezaji wa Mfumo wa *e-utatuzi*. Kamati inaipongeza Serikali hata hivyo inaitaka Serikali kusimamia matumizi ya fedha hizi ili mradi huo uweze kuleta tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza Serikali katika kuhakikisha Tume imepatiwa fedha zote za Maendeleo. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa fedha za matumizi mengineyo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Tume zinapelekwa kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Kamati ilichambua na kujadili Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 65) na Tume ya Usuluhishi (Fungu 15) na makadirio kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

(i) Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; na

(ii) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Makadirio ya Mapato ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano (Fungu 65). Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano inakadiriwa kukusanya maduhuli ya shilingi 63,000,000,000. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makadirio hayo yameongezeka kwa shilingi 8,000,000,000 sawa na 14.55% ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina maoni kuwa pamoja na kuongezeka kwa lengo la ukusanyaji wa maduhuli, Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 65) iongeze ubunifu katika kuibua vyanzo vipya vya mapato. Hii inatokana na ukweli kuwa vyanzo vya mapato katika Ofisi hii vimebaki kuwa vilevile kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano (Fungu 65). Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 65) inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi 41,809,449,000 kwa ajili utekelezaji wa shughuli na vipaumbele vya Ofisi hii. Matokeo ya uchambuzi katika makadirio ya matumizi ya fedha hizo yanaonyesha kuwa:-

(i) Jumla ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 65) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepungua kwa asilimia 4.04 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(ii) Bajeti ya matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni shilingi 29,997,075,000 sawa na 71% ya Bajeti yote ya Ofisi hii. Bajeti hii imepungua kwa asilimia 0.8 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(iii) Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni shilingi 11,812,374,000 sawa na 29% ya bajeti yote. Hata hivyo, bajeti hii imepungua kwa 11% ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kushuka kwa Makadirio ya Matumizi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 65) kumechangiwa kwa uamuzi wa Serikali kuunda Wizara mahususi inayoshughulikia

Vijana na kuhamishia shughuli za Idara ya Wenye Ulemavu kwenda Ofisi Waziri Mkuu (Fungu 37).

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (Fungu 15). Kwa upande wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi 8,123,726,000 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Kamati imechambua na kubaini kuwa:-

(i) Jumla ya Bajeti kwa Tume imeongezeka kwa shilingi 882,879,000 sawa na asilimia 4.95 kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(ii) Bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa shilingi 882,879,000 sawa na asilimia 5.13 kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(iii) Kiasi cha shilingi 276,046,000 kimetengwa kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo ikiwa ni sawa na kiasi kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kuongeza bajeti ya Tume hasa katika eneo la Matumizi ya uendeshaji wa shughuli za Tume. Hata hivyo, Kamati inataka kuhakikisha kuwa fedha zote zinapelekwa kwenye Tume kama zitakavyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuchochea ufanisi katika shughuli za Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maoni na ushauri wa Kamati: Maoni ya Jumla: -

(i) Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 65) iongeze jitihada katika kutoa mafunzo ya uanagenzi kwa vijana wengi nchini ili kuwajengea uwezo wa kujiajiri katika ufundi; na

(ii) Ofisi ya Waziri ya Mkuu ihakikishe inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi kama yalivyopangwa kwenye bajeti;

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukusanyaji wa maduhuli, Kamati inaishauri Serikali kuwa: -

(i) Iongeze kasi ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kupitia ada za wakala binafsi za huduma za ajira na ada za maombi ya kufanya kazi nje ya nchi kwani imekuwa na mwenendo usioridhisha katika ukusanyaji;

(ii) Ihakikishe inaendelea kubuni na kupanua wigo wa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini, Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

(i) Iongeze fedha kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza vyuo vya mafunzo ya uanagenzi ili kuifanya sekta hiyo kuwa moja ya nyenzo kuu za utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2050;

(ii) Ihakikishe inatoa elimu kwa umma na kuwajengea uwezo wahitimu wa elimu ya kati na elimu ya juu kuhusu umuhimu wa mafunzo ya uanagenzi kama fursa ya kuwawezesha kujiajiri na kuwa na tija katika soko la ajira nchini;

(iii) Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 65) kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Utumishi kuweka utaratibu wa kutoa mafunzo ya uanagenzi kwa watumishi wa umma na sekta binafsi kwa ajili ya kuongeza ujuzi na kuboresha utendaji katika kutoa huduma kwa wananchi; na

(iv) Ihakikishe kuwa inatoa Fedha za Kukuza Ujuzi *(Skills Development Levy)* kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa kwani fedha hizi zimekuwa zikitolewa kwa kusuasua kama ambavyo inatarajiwa katika kipindi cha miaka miwili ya Fedha iliyopita. Mathalani, katika kipindi cha 2023/2024 hadi 2024/2025 ilitarajiwa iwe imepokea kiasi cha shilingi 197,497,000,000. Hata hivyo Ofisi hii katika kipindi hicho imepokea kiasi cha shilingi

19,800,000,000 tu kutokana na makusanyo ya fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Tume ya Usuluhishi na Uamuzi. Kamati inaishauri Serikali kuwa: -

(i) Tume ihakikishe inatoa elimu kwa wadau kuhusu matumizi ya Mfumo wa *e-utatuzi*;

(ii) Tume iandae utaratibu wa kushughulikia usuluhishi wa migogoro ya ajira katika hatua za awali hali itakayochangia kuboresha mahusiano na mazingira ya kazi baina ya waajiri na waajiriwa hasa kwenye sekta binafsi; na

(iii) Tume iboreshe mazingira ya kazi kwa watumishi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ikiwa ni pamoja na Ofisi za Makao Makuu na Mikoa kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha, ninapenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninapenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kwa imani yao kwangu kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii. Ninapenda kutumia fursa hii kuwaahidi ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru Wajumbe kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha ziara na uchambuzi wa Bajeti ya ofisi hii hadi kukamilika kwa taarifa hii. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda tulionao ninaomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano na Naibu Waziri Mhe. Rahma Riyadhi Kisuo, kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi ambapo hatua hii imeisaidia Kamati kufanya kazi yake kwa namna inayofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu Bi. Marry Maganga na Naibu Katibu Wakuu Bi. Zuhura Yunus.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, ninapenda kuwashukuru Watumishi wote wa Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema na kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano Fungu 65 na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)* Fungu 15 kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Ajira na Mahusiano kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, ili kurahisishisha mtiririko wa maudhui pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge yanayohusu taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano (05) kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya kwanza inatoa, Msingi wa Uchambuzi na Mawanda ya Uchambuzi;

(ii) Sehemu ya pili inachambua na kufanya tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(iii) Sehemu ya tatu inachambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2026/2027;

(iv) Sehemu ya nne inafafanua Maoni ya Kamati na Ushauri unaotolewa kwa Serikali; na

(v) Sehemu ya mwisho inahitimisha taarifa ya uchambuzi na kuonesha msimamo wa Kamati

1.2 Msingi wa Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Msingi wa Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Makadirio ya Mapato na Matumizi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano umejengwa katika Kanuni ya 6 (5) (a) ikisomwa kwa Pamoja na Kanuni ya 7(1) (a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025. Kanuni hizo zinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii. Aidha,Kanuni ya 120 (2) na 121 (4) ya Kanuni hizo imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya utekelezaji wa Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi masharti hayo, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira, Kazi na Mahusiano kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Katika hatua hiyo Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na kuja na matokeo kama yaliyoainishwa katika taarifa hii.

1.3 Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa

Mheshimiwa Spika,Taarifa ya Kamati inahusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu,Kazi,Ajira na Mahusiano inahusika na mafungu mawili ambayo ni **Fungu 65** Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Mahusiano; **na Fungu 15** Tume ya Usuluhishi na Uamuzi **(CMA).**

Mheshimiwa Spika Uchambuzi uliofanyika uligusa maeneo yafuatayo:-

(i) Utekelezaji wa Bajeti kwa Mafungu hayo kwa mwaka wa Fedha 2025/2026;

(ii) Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(iii) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; na

(iv) Mambo muhimu katika Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi Ajira,na Mahusiano.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi, Kamati iliongozwa na kigezo cha asilimia Pamoja na kufanya tathmini ya jumla na ulinganisho wa mambo mbalimbali. Mambo hayo yaliiwezesha Kamati kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji na mantiki ya mpango na makadirio kwa mwaka wa fedha unaokuja.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

2.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, sehemu hii ya taarifa inaripoti matokeo ya utekelezaji wa masharti ya Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Bunge. Kanuni hiyo ilizitaka Kamati za Bunge za Kisekta kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoisha na kufanya ulinganisho wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi masharti hayo, tarehe 23 Machi, 2026, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Taarifa hiyo ilijumuisha Mpango na Bajeti ya **Fungu 65** pamoja na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA**) Fungu 15**.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, Kamati inatoa taarifa kuhusu mambo yafuatayo:-

(i) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati;

(ii) Ukaguzi wa Miradi;

(iii) Utekelezaji wa Vipaumbele;

(iv) Hali ya Ukusanyaji wa Maduhuli; na

(v) Hali ya upatikanaji wa Fedha

Mheshimiwa Spika, mambo hayo kwa pamoja yameweka msingi wa kuliwezesha Bunge lako Tukufu kupata uwiano utakaolisaidia katika kufikia uamuzi baada ya mjadala wa hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu Ajira, Kazi na Mahusiano kama ilivyowasilishwa na Mtoa hoja.

2.1.1 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Katika kulisaidia Bunge kutekeleza jukumu lake la kuishauri Serikali,tarehe 9 Aprili, 2025 wakati wa uwasilishaji wa hotuba ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano kwa mwaka fedha 2025/2026.Kamati ilitoa Maoni na Ushauri kuhusu mambo **sita (06**) kwa **Fungu 65** Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira kazi na Mahusiano na **jambo moja (1**) kwa **Fungu 15** Tume ya Usuluhishi na Uamuzi. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa baadhi ya maeneo ushauri wa kamati umezingatiwa huku maeneo mengine utekelezaji wa ushauri wa Kamati haujafanyiwa kazi kwa kiwango cha kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, mfano wa ushauri uliozingatiwa unahusu wa kuongeza idadi ya vyuo kwa mafunzo ya kukuza ujuzi kwa njia ya uanagenzi hadi kufikia katika ngazi ya Wilaya na kwa mwaka huu wa fedha 2025/2026 vyuo vimeongezeka kwa ngazi ya wilaya na kufika 26 sawa na asilimia **56.52** ya vyuo 46 vilivyopo. Ongezeko hili limechangia kuongeza ujuzi kwa vijana **5,746** nchini kupata mafunzo yaliyowawezesha kuongeza ujuzi na stadi za maisha.

Mheshimiwa Spika, vilevile ushauri wa Kuongezea bajeti kwa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) ulizingatiwa na serikali ambapo katika mwaka wa fedha 2025/2026 waliweza kuongezewa fedha kiasi cha Shilingi 866,180,000 kwa ajili ya uendeshaji wa mashauri. Jambo lillochangia kuendesha mashauri

kwa njia ya kieletroniki kupitia mfumo wa e-Utatuzi na kuongeza ufanisi wa utatuzi wa migogoro ya ajira kwa takribani asilimia **40**.

Mheshimiwa Spika, Kamati haijaridhishwa na utekelezaji wa maeneo yafuatayo:-

a) Kuongeza kasi ya kuwaunganisha Watanzania na ajira za nje ya nchi;

b) Kuboresha Mfumo wa Kieletroniki wa Usimamizi wa Huduma za Ajira (ESMIS) ili kuwezesha kubadilishana taarifa mbalimbali za kibenki;

c) Kuendelea kutenga theluthi moja ya makusanyo ya sekta binafsi (SDL) kwa ajili ya programu ya kuwajengea ujuzi wanagenzi;

d) Kutoa elimu kwa umma kuhusu Programu ya Taifa ya kukuza Ujuzi; na

e) Kulinda Ujuzi uliopatikana kupitia uanagenzi kwa kutoa vifaa vya Kutendea kazi kwa vijana wanaonufaika na programu mara baada ya kumaliza

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Ofisi ya Waziri Mkuu **(Fungu 65)** na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi **(Fungu 15)** kuhakikisha inatekeleza ushauri wa Kamati ili kuleta matokeo chanya katika sekta ya ajira nchini. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa ukomo wa bajeti na mtiririko wa fedha za Maendeleo usioridhisha kutoka hazina ni sababu kubwa inayochangia Mafungu haya kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa Ufanisi.

2.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha

2.2.1 Ufafanuzi wa Jumla

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika Mkoa wa Dar es Salaam. Kamati ilikagua miradi miwili ambayo ni sehemu ya miradi iliyotengewa fedha kiasi cha **Shilingi 13,322,106,000** kwa

mwaka wa fedha 2025/2026. Naomba kubainisha na kufafanua miradi hiyo Pamoja na kufanya majumuisho ya mambo yaliyojitokeza katika ukaguzi wa miradi kama ifuatavyo: -

a) Mradi 6581: Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kigamboni

Mheshimiwa Spika, Programu hii inatekelezwa kwa uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu (**Fungu 65**) imelenga kuwezesha nguvukazi ya Taifa kuwa na ujuzi stahiki, maarifa na ubunifu utakaowezesha kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Taifa. Aidha, programu hiyo inalenga kutoa ushindani katika soko la ajira la Kitaifa, Kikanda na Kimataifa sambamba na kuongeza wigo wa kuajiriwa au kujiajiri kwa vijana nchini.

Mheshimiwa Spika, programu hii inatolewa katika vyuo mbalimbali kwa Mkoa wa Dar es Salaam ikiwemo Chuo cha Ufundi cha Don Bosco; Anna Collection Academy na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kigamboni. Kamati ilitembelea Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kigamboni na kukagua mafunzo yanayotolewa katika chuo hicho chini ya programu hii. Aidha, mafunzo hayo ni pamoja na kuchomelea vyuma, Ufundi wa umeme wa magari na umeme wa majumbani, ufundi wa mabomba, kushona na ufundi wa magari.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kiasi cha shilingi 60,000,000/= kilitengwa kwa ajili ya kutekeleza programu hii katika chuo cha maendeleo ya wananchi kigamboni kwa wanagenzi wapatao 120 na hadi mwezi Machi, 2026, Serikali ilikuwa imetoa kiasi cha Shilingi **30,000,000/=** sawa na **asilimia 50** ya fedha yote.

b) Mradi Na.5505: Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Mashauri ya Usuluhishi na Uamuzi

Mheshimiwa Spika, mradi huu kupitia CMA unatekeleza Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi na Uendeshaji wa mashauri ambao unajulikana kama e-Utatuzi. Mradi huu una lengo la kuongeza ufanisi na uwazi katika kushughulikia migogoro ya ajira nchini. Aidha, utaondoa matumizi ya nakala mango na

kurahisisha utunzaji na upatikanaji wa majalada na nyaraka. Kukamilika kwa mradi huu kutajibu tamanio la Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuacha Tabasamu kwa wananchi kwani utaharakisha na kurahisisha upatikanaji wa haki katika usuluhishi na uamuzi wa migogoro ya ajira nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza mradi huu Tume (Fungu 15) ilitengewa jumla ya Shilingi 276,046,000/= katika mwaka wa fedha 2025/2026 ambapo Serikali imepeleka fedha zote kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Kamati inapongeza Serikali kwa hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu.

2.2.2 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi

Mheshimiwa Spika, katika ziara ya ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu **(Fungu 65)** na Tume **(Fungu 15**), Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa miradi na kuona hali halisi kwenye maeneo ya utekelezaji wa miradi husika. Lengo ilikuwa kulinganisha na kubaini iwapo taarifa zilizowasilishwa na Wizara zinawiana na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji pamoja na madhumuni ya miradi inayohusika.

Mheshimiwa Spika, Tathmini ya Kamati imebainisha kuwa:-

a) Utekelezaji wa sehemu kubwa ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati imezingatia thamani ya fedha na hatua iliyofikiwa inawiana na muda wa utekelezaji wa miradi husika;

b) Utekelezaji wa miradi na programu zilizotembelewa na Kamati zimeshirikisha wananchi ambao ni wanufaika wa miradi na programu hizo moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu **(Fungu 65)** na Tume **(Fungu 15)**. Kamati inalitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika kutekeleza miradi hiyo thamani ya fedha, uwekezaji, ufanisi na tija vimezingatiwa.

2.3 Utekelezaji wa Vipaumbele na Majukumu ya Wizara

Mheshimiwa Spika, tarehe 23 Machi,2026 Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu **(Fungu 65)** na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi **(Fungu 15)** kwa mwaka wa Fedha 2025/2026. Wakati wa Uchambuzi wake kamati ilizingatia vipaumbele vya wizara ambavyo ni:-

(a) Kuimarisha usimamizi wa ajira za wageni Nchini;

(b) Kuratibu utekelezaji wa Mwongozo wa Majadiliano baina ya Serikali Vyama vya Wafanyakazi na Vyama vya waajiri;

(c) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008 na Mkakati wake;

(d) Kufanya tathmini ya hali ya mahusiano nchini kwa makundi ya kijamii;

(e) Kufanya mapitio ya Sheria ya Hifadhi ya jamii Sura 135;

(f) Kujenga uelewa na ufahamu wa tija na ubunifu Nchini;

(g) Kuimarisha utendaji kazi, haki wajibu na maslahi ya watumishi;

(h) Kuhamasisha masuala ya Usalama na Afya Mahali pa kazi;

(i) Kuimarisha utoaji wa huduma za utatuzi wa migogoro ya kazi kidijiti kupitia Mfumo wa Kielekroniki wa Usimamizi wa mashauri ya Usuluhishi na Uamuzi e.utatuzi

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu,Ajira kazi na mahusiano imefanikiwa kufanya baadhi ya shughuli ili kutekeleza vipaumbele ilivyojiwekea. Baadhi ya Shughuli hizo ni pamoja na:-

(i) Kufanya mapitio ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii, Sura 135;

(ii) Kufanya mapitio ya sheria ya Ukuzaji wa Huduma za Ajira Sura 243;

(iii) Kuratibu fursa za ajira kwa Watanzania nje ya Nchi;

(iv) Kuimarisha Usimamizi wa Sheria za kazi Nchini; na

(v) Kuratibu utekelezaji wa Mwongozo wa Majadiliano baina ya Serikali na Vyama vya wafanyakazi na Vyama vya waajiri.

2.3.1 Hatua iliyofikiwa katika Ukusanyaji wa Maduhuli

Mheshimiwa Spika, Lengo la uchambuzi wa taarifa za makusanyo ya maduhuli ni kuliwezesha Bunge kubaini iwapo lengo la makusanyo lililoidhinishwa na Bunge limefikiwa. Aidha, uchambuzi huu unaliweka Bunge katika nafasi ya kutumia uzoefu unaopatikana kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na kubaini uhalisia unavyostahili kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia masuala yafuatayo:-

(i) Kiasi kilichokusanywa ikilinganishwa na lengo la makusanyo; na

(ii) Ulinganisho wa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Waziri Mkuu kazi, Ajira na Mahusiano Fungu 65 ilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 55,000,000,0000/=.** Hadi kufikia Februari, 2026 Ofisi ya Waziri Mkuu kazi ajira na Mahusiano ilikuwa imekusanya **Shilingi 38,029,945,099/=** sawa na **asilimia 69.15** ya lengo la makusanyo liliyoidhinishwa na Bunge. Kamati ina maoni kuwa mwenendo wa makusanyo ya maduhuli unaridhisha na Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 65) itafikia lengo la makusanyo liliyoidhinishwa na Bunge.

2.3.2 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, Ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kazi ajira na mahusiano unategemea mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka hazina kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Kamati ilipokea na kuchambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa **fungu 65** na **fungu 15** kutoka Hazina kama ifuatavyo:-

a) Fungu 65 Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Mahusiano

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa Fungu 65 hadi kufikia mwezi Februari,2026 umeonesha mambo yafuatayo:-

(i) Upatikanaji wa jumla ya Fedha zilizoidhinishwa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu **Fungu 65** ni **asilimia 61.40** ikiwa ni pungufu ya **asilimia 5.3** ya muda wa utekelezaji wa bajeti. Ni maoni ya Kamati kuwa ikiwa hali hii itaendelea itaathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa;

(ii) Fedha za matumizi ya kawaida zilizopatikana kwa **asilimia 61.6** ikiwa na upungufu wa **asilimia 5.1** ya fedha zilizotakiwa katika kipindi kama hicho;

(iii) Fedha za Matumzi mengineyo (OC) zimepokelewa kwa **asilimia 65.2** ambapo ilitakiwa kuwa zimepokelewa **asilimia 66.7** kulinganisha na muda wa utekelezaji wa Bajeti;

(iv) Fedha za Mishahara zilizopokelewa ilikuwa a**silimia 58.03** ikiwa na upungufu wa **asilimia 8.67** ya fedha zilizotakiwa katika kipindi hicho;

(v) Fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo zilipatikana kwa **asilimia 60.90** ya bajeti; na

(vi) Katika fedha za kugharamia miradi ya maendeleo, Fedha za Ndani zilifikia **asilimia 62.4** na fedha za nje **asilimia 22.15.** Upatikanaji wa fedha kutoka hazina kwa

ajili ya miradi ya maendeleo ni pungufu ya asilimia kwa **asilimia 5.8** kulinganisha na muda wa utekelezaji wa bajeti.

KIELELEZO 1: UPATIKANAJI WA FEDHA KWA FUNGU 65

AINA YA MATUMIZI	BAJETI ILIYOIDHINISHWA	KIASI KILICHOPOKELEWA	ASILIMIA
Mshahara	15,133,941,000	8,783,587,220	58.03
Matumizi mengineyo	15,117,368,000	9,852,036,084	65.2
Jumla Ndogo	30,251,309,000	18,635,623,304	61.60
Miradi ya Maendeleo	13,322,106,000	8,112,921,077	60.90
Jumla Kuu	**43,573,415,000**	**26,748,544,381**	**61.40**

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Wizara ya Fedha kuhakikisha inatoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 65) kama iliyoinidhinishwa na Bunge ili kuleta tija na ustawi wa wananchi kama ilivyokusudiwa.

Fungu 15: Tume ya Usuluhishi na Uamuzi

Mheshimiwa Spika, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi **(Fungu 15)**, uchambuzi wa mwenendo wa upatikanaji wa fedha hadi kufikia Februari, 2026 ulionesha mambo yafuatayo:-

(i) Tume ilipokea **asilimia 55.0** ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Hii ni pungufu ya **asilimia 11.7** ukilinganisha na muda wa utekelezaji wa Bajeti. Mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha unaweza kuathiri shughuli zilizopangwa kama hautarekebishwa;

(ii) Fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa zilikuwa **asilimia 53.3** ukilinganisha na **asilimia 66.7** zilizotakiwa kuwa zimepokelewa hadi kipindi hiki cha utekelezaji wa ya bajeti;

(iii) Fedha za matumizi mengineyo (OC) zilizopokelewa ni **asilimia 51.4** na huku mishahara ikiwa imepokelewa kwa asilimia 56. Upungufu wa fedha katika mishahara imetokana na kucheleweshewa kibali cha kuajiri watumishi wapya;

(iv) Fedha za Miradi ya Maendeleo zilipokelewa kwa **asilimia 100** kwa ajili ya utekelezaji wa mfumo wa e-utatuzi. Kamati inaipongeza Serikali hata hivyo inaitaka Serikali kusimamia matumizi ya fedha hizi ili mradi huo uweze kuleta tija iliyokusudiwa.

KIELELEZO 2: UPATIKANAJI WA FEDHA (FUNGU 015)

AINA YA MATUMIZI	BAJETI ILIYOIDHINISHWA	KIASI KILICHOPOKELEWA	ASILIMIA
Mshahara	3,151,421,000	1,764,352,000	56
Matumizi Mengineo (OC)	4,313,380,000	2,216,444,583.62	51.4
Jumla ndogo	7,464,801,000	3,980,797,583.62	53.3
Miradi ya Maendeleo	276,046,000	276,046,000	100
JUMLA KUU	**7,740,847,000**	**4,256,842,583.62**	**55.0**

Chanzo: Randama ya Wizara na usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Serikali katika kuhakikisha kuwa Tume imepatiwa fedha zote za Maendeleo. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa fedha za matumizi mengineyo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Tume zinapelekwa kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

SEHEMU YA TATU

3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

Mheshimiwa Spika, ili kuzingatia masharti ya kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Bunge,Kamati ilichambua na kujadili Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu **(Fungu 65)** na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi **(Fungu 15)** na mahusiano kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027; na

(ii) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

3.1 Makadirio ya Mapato

a) Ofisi ya Waziri Mkuu,Kazi,Ajira na Mahusiano (Fungu 65)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa kuhusu lengo la ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi ulijikita zaidi kwa kuangalia uzoefu uliopatikana katika ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira, kazi na mahusiano inakadiriwa kukusanya maduhuli ya Shilingi **63,000,000,000/=**. Uchambuzi wa kamati umebaini kuwa makadirio hayo yameongezeka kwa Shilingi **8,000,000,000** sawa na **asilimia 14.55** ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

KIELELEZO 3: MCHANGANUO WA MAKADIRIO YA MADUHULI

FUNGU	Mwaka 2025/2026	Mwaka 2026/2027	Ongezeko/ punguzo	Asilimia
Wizara (65)	55,000,000,000	63,000,000,000	8,000,000,000	14.55

Mheshimiwa Spika,Kamati ina maoni kuwa pamoja kuongezeka kwa lengo la ukusanyaji wa maduhuli, Ofisi ya Waziri Mkuu **(Fungu 65)** iongeze ubunifu katika kuibua vyanzo vipya vya mapato. Hii inatokana na ukweli kuwa vyanzo vya Mapato katika Ofisi hii vimebaki kuwa vilevile kila mwaka.

3.2 Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, masharti ya Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Bunge yamelenga kuliwezesha Bunge kutumia uzoefu wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa kuzingatia lengo hilo, Kamati imechambua makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama ifuatavyo: -

a) Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira, Kazi na Mahusiano (Fungu 65)

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 65) inakadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi 41,809,449,000/=** kwa ajili utekelezaji wa shughuli na vipaumbele vya Ofisi hii. Matokea ya uchambuzi katika makadirio ya matumizi ya fedha hizo yanaonyesha kuwa:-

(i) Jumla ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu **(Fungu 65)** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imepungua kwa **asilimia 4.04** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026;

(ii) Bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ni **Shilingi 29,997,075,000** sawa na **asilimia 71** ya Bajeti yote ya Ofisi Hii. Bajeti hii imepungua kwa asilimia 0.8 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026; na

(iii) Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ni **Shilingi 11,812,374,000/=** sawa na **asilimia 29** ya bajeti yote. Hata hivyo, bajeti hii imepungua kwa **asilimia 11** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026.

KIELELEZO 4: ULINGANISHO WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 NA MWAKA 2026/2027 - FUNGU 65

AINA YA MATUMIZI	MWAKA 2025/2026	MWAKA 2026/2027	Asilimia Ongezeko /upungufu
Mishahara	15,133,941,000	15,088,975,000	-0.30
Matumizi mengineyo	15,117,368,000	14,908,100,000	-1.40
Jumla	30,251,309,000	29,997,075,000	-0.84
Miradi ya Maendeleo	13,322,106,000	11,812,374,000	-11.33
Jumla kuu	43,573,415,000	41,809,449,000	-4.05

Mheshimiwa Spika, kushuka kwa makadirio ya matumizi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 65) kumechangiwa kwa uamuzi wa Serikali kuunda Wizara mahususi inayoshughulikia Vijana na kuhamishia shughuli za Idara ya wenye Ulemavu Kwenda Ofisi Waziri Mkuu **(Fungu 37).**

b) Tume ya Usuluhisho na Uamuzi (Fungu- 15)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, inakadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi 8,123,726,000/=** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Kamati imechambua na kubaini kuwa:-

i) Jumla ya Bajeti kwa Tume imeongezeka kwa **Shilingi 382,879,000/=** sawa na **asilimia 4.95** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026; ii) Bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa **Shilingi 382,879,000/=** sawa na **asilimia 5.13** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026; na

ii) Kiasi cha **Shilingi 276,046,000/=** kimetengwa kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo ikiwa ni sawa na kiasi kilichotengwa katika mwaka wa fedha 2025/2026.

Taswira ya makadirio ya matumizi kwa **Fungu 15** Tume ya Usuluhishi na Uamuzi inaonekana katika Kielelezo Na.5

KIELELEZO 5: TASWIRA YA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA FUNGU 15 TUME YA USULUHISHI NA UAMUZI INAONEKANA KATIKA KIELELEZO NA. 5

AINA YA MATUMIZI	MWAKA 2025/2026	MWAKA 2026/2027	Asilimia
Mishahara	3,151,421,000	2,965,638,000	-5.00
Matumizi Mengineyo	4,313,380,000	4,882,042,000	+13.20
JUMLA	7,464,801,000	7,847,680,000	+5.13
Miradi ya Maendeleo	276,046,000	276,046,000	0
Jumla Kuu	7,464,801,000	8,123,726,000	+4.95

Chanzo: Randama ya Wizara ya Usanifu wa kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kuongeza bajeti ya Tume hasa katika eneo la Matumizi ya uendeshaji wa shughuli za Tume. Hata hivyo, Kamati inaitaka kuhakikisha kuwa fedha zote zinapelekwa kwenye Tume kama zitakavyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuchochea ufanisi katika shughuli za Tume.

SEHEMU YA NNE

4.0 MAONI NA USHAURI

4.1 Maoni ya Jumla

(i) Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 65) iongeze jitihada katika kutoa mafunzo ya uanagenzi kwa vijana wengi nchini ili kuwajengea uwezo wa kujiajiri katika ufundi;

(ii) Ofisi ya Waziri ya Mkuu ihakikishe inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi kama yalivyopangwa kwenye bajeti.

4.2 Ushauri wa Kamati

4.2.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

Kamati inashauri Serikali kuwa:-

(i) Iongeze kasi ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kupitia ada za wakala binafsi za haduma za ajira na ada za maombi ya kufanya kazi nje ya nchi kwani imekuwa na mwenendo usioridhisha katika ukusanyaji;

(ii) Ihakikishe inaendelea kubuni na kupanua wigo wa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

4.2.2 Programu ya kukuza ujuzi nchini

Kamati inashauri Serikali kuwa:-

(i) Iongeze fedha kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza vyuo vya mafunzo ya uanagenzi ili kuifanya sekta hiyo kuwa moja ya nyenzo kuu za utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2050;

(ii) Ihakikishe inatoa elimu kwa umma na kuwajengea uwezo wahitimu wa elimu ya kati na elimu ya juu kuhusu umuhimu wa mafunzo ya uanagenzi kama fursa

ya kuwawezesha kujiajiri na kuwa na tija katika soko la ajira nchini;

(iii) Ofisi ya Waziri Mkuu (**Fungu 65**) kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Utumishi kuweka utaratibu wa kutoa mafunzo ya uanagenzi kwa watumishi wa umma na sekta binafsi kwa ajili ya kuongeza ujuzi na kuboresha utendaji katika kutoa huduma kwa wananchi; na

(iv) Ihakikishe kuwa inatoa Fedha za Kukuza Ujuzi (Skills Development Levy) kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa kwani fedha hizi zimekuwa zikitoka kwa kusuasua kama ambavyo inatarajiwa katika kipindi cha miaka miwili ya Fedha iliyopita, Mathalani, katika kipindi cha 2023/2024 hadi 2024/2025 ilitarajiwa iwe imepokea kiasi cha **Shilingi 197,497,000,000/=.** Hata hivyo Ofisi hii katika kipindi hicho imepokea kiasi cha **Shilingi 19,800,000,000 tu** kutokana na makusanyo ya fedha hizo.

4.2.3 Tume ya Usuluhishi na Uamuzi

Kamati inashauri Serikali kuwa:-

(i) Tume ihakikishe inatoa elimu kwa wadau kuhusu matumizi ya mfumo wa e-utatuzi;

(ii) Tume landae utaratibu wa kushughulika na usuluhishi wa migogoro ya ajira katika hatua za awali hali itakayochangia kuboresha mahusiano na mazingira ya kazi baina ya waajiri na waajiriwa hasa kwenye sekta binafsi; na

(iii) Tume Iboreshe mazingira ya kazi kwa watumishi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ikiwa ni pamoja na Ofisi za Makao Makuu na Mikoa kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Tume.

SEHEMU YA TANO

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kwa Imani yao kwangu kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii, napenda kutumia fursa hii kuwaahidi ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yangu majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Wajumbe kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha ziara na uchambuzi wa Bajeti ya ofisi hii hadi kukamilika kwa taarifa hii, hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda tulionao naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge (Hansard) majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Hawa Chakoma Mchafu, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Dkt. Regina Christopher Malima, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe.Mohamed Abrahman Mwinyi, Mb - Mjumbe
4. Mhe.Mariam Nassoro Kisangi, Mb - Mjumbe
5. Mhe.Tinnar Andrew Chenge, - Mjumbe
6. Mhe. Katani Ahmadi Katani, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Said Ibrahim Mzimba, Mb - Mjumbe
8. Mhe.Lucy Similya Kombani, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Nasriya Nassir Ali, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Shadya Haji Omary, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Mohamed Kassim Salum, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Shaffin Ahmedali Sumar, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Athumin Omary Mapalilo, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Pascal Lucas Lutandula, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Kangi Alphaxard Lugola, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Kafiti William Kafiti, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Edefonce Joachim Canoni, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb - Mjumbe

20. Mhe. Happiness Daniel Ngwando, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Deus Clement Sangu, Mb, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano na Naibu Waziri Mhe. Rahma Riyadhi Kisuo, Mb kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi ambapo hatua hii imeisaidia Kamati kufanya kazi yake kwa namna inayofaa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu Bi. Marry Maganga na Naibu Katibu Wakuu Bi. Zuhura Yunus.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndg. Baraka Ildephonce Leonard, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema na kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano (Fungu 65) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja**.**

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Hawa Chakoma Mchafu, Mb

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII

01 April, 2026

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hawa Chakoma Mchafu kwa kuwasilisha maoni ya Kamati yako.

Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mheshimiwa Florent Kyombo.

MHE. FLORENT L. KYOMBO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Bajeti ya Ofisi Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea ninaomba taarifa yangu hii iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 ninatoa shukrani kwako kwa kunipa wasaa ili niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo muhimu yanayoguswa na kuelezwa kwa kina na taarifa hii ni kama ifuatavyo:-

(a) Maelezo na uchambuzi kuhusu Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(b) Uchambuzi na utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(c) Uchambuzi wa Mpango wa Bajeti wa Mwaka wa Fedha 2026/2027 (Makadirio ya Maduhuli na Matumizi); na

(d) Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maelezo na uchambuzi kuhusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi 1,791,592,207,143.72 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 Kamati ilitembelea na kukagua baadhi ya miradi hiyo ya maendeleo iliyotekelezwa na ofisi hii katika Mwaka wa Fedha 2025/2026. Miradi iliyotembelewa ni miradi ya elimu, afya, stendi za mabasi, masoko, pamoja na barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)*. Uchambuzi wa kina pamoja na maoni mahsusi kuhusu taarifa hiyo ya miradi inapatikana katika taarifa za Kamati iliyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inatoa maoni ya jumla kuhusu ukaguzi wa miradi hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa miradi katika baadhi ya mikoa katika ukaguzi wake Kamati imebaini utekelezaji unaoridhisha kwa baadhi ya mikoa. Kwa mfano, Mkoa wa Morogoro utekelezaji wa Barabara ya Muhimbili na Stendi ya Magari Madogo ya Kihonda katika mkoa huo ambayo inatekelezwa chini ya Mradi wa *TACTIC* ilikuwa ya kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia imebaini ujenzi wa miradi ya shule katika Mkoa wa Arusha imekuwa na mahitaji kadha wa kadha kama vile ukosefu wa maji katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Longido Samia, ukosefu wa uzio katika Shule ya Wasichana ya Longido Samia, Shule ya Awali na Msingi ya Lowassa pamoja na Shule ya Sekondari ya Migungani 1. Shule hizi zimepakana na mbuga za wanyama hivyo wanyama wanachunga katika maeneo ya shule na hivyo kuhatarisha maisha ya watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Kamati imetembelea pale tulikutana na nyumbu na pundamilia wakiwa katika maeneo ya shule wakichunga majani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla baada ya Kamati kufanya ukaguzi wa miradi katika maeneo yote, Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa miradi umewezeshwa kwa kutumia fedha za ndani. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii, hii ni dalili njema kwa Serikali yetu kuanza kujitegemea katika kutekeleza miradi yake ya msingi hasa miradi ambayo ni kipaumbele cha juu kwa wananchi wa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kamati imebaini kuwa miradi inayotekelezwa na halmashauri nchini ina changamoto nyingi kuliko inayotekelezwa na taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Kamati inadhani kuwa kunaweza kukawa na changamoto ya usimamizi wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo kwa ngazi ya halmashauri. Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kuimarisha usimamizi katika utekelezaji wa miradi ya halmashauri nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa, katika miradi mingi inayosimamiwa na halmashauri iliyotembelewa na kukaguliwa kumekuwa na changamoto ya usanifu. Kwa mfano, ujenzi wa Stendi ya Mabasi Mikumi umepangwa kujengwa katika eneo oevu. Pia, iko katika eneo ambalo si rafiki kwa matumizi ya stendi. Kwa hali hiyo, Kamati inashauri kuwa miradi yote inayosanifiwa kutekelezwa na halmashauri kabla ya kuomba bajeti, Wizara ya TAMISEMI itume timu kufanya ukaguzi na kujiridhisha kuhusu usanifu na upembuzi yakinifu uliofanyika kwa ajili ya miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Baada ya Wizara pamoja na Sekretarieti za Mikoa kuwasilisha Bajeti zao kwa Mafungu 28 kuanzia tarehe 19 hadi tarehe 30 Machi, 2026, Kamati ilipata wasaa wa kuichambua na kuijadili, lakini pia Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Mwaka wa Fedha 2025/2026; taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo nane. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza maoni na ushauri wa Kamati. Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanyia kazi maoni na ushauri huo. Aidha, kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu, Kamati itaendelea kuyasisitiza katika taarifa hii likiwemo, suala la shule za mchepuo wa Kiingereza, upungufu au uhaba wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini na madeni ya watumishi katika halmashauri nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara kupitia Fungu 56 ambayo ni Makao Makuu ya Wizara, Fungu 02, Tume ya Utumishi wa Walimu na Mafungu 26 kutoka Sekretarieti za Mikoa katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ilikadiria kukusanya maduhuli ya shilingi 1,925,881,323,464.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 188,960,306,000.00 sawa na asilimia 9.8 zilikadiriwa kukusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara; shilingi 1,644,835,000.00 sawa na asilimia 0.09 zilikadiriwa kukusanywa kutoka Shirika la Elimu Kibaha; shilingi 21,721,743,786 sawa na asilimia 1.2 zilikadiriwa kukusanywa kutoka Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka yaani *DART*.

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi 10,745,182,213.00 sawa na asilimia 0.6 zilikadiriwa kukusanywa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa; shilingi 3,506,815,065 sawa na asilimia 0.25 zilikadiriwa kukusanywa kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa; shilingi 7,000,000,000.00 sawa na asilimia 0.36 zilikadiriwa kukusanywa kutoka Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini yaani *TARURA*; shilingi 11,489,598,000.00 sawa na asilimia 0.59 zilikadiriwa kukusanywa kutoka Shirika la Masoko Kariakoo; shilingi 306,108,174,064.00 sawa na asilimia 0.015 zilikadiriwa kukusanywa kutoka Ofisi za Mikoa na shilingi 1,680,506,764,000 sawa na 87.2% zilikadiriwa kukusanywa kutoka katika Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitaarifiwa kwamba, hadi mwezi Februari 2026, jumla ya shilingi 1,161,087,740,803.41 zilikusanywa, sawa na 90.43% ya lengo la makusanyo yote kwa

mwaka. Kuhusu ulinganisho wa makusanyo ya maduhuli kuanzia mwaka 2023/2024 hadi mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa kumekuwa na mwendelezo mzuri wa upangaji wa makisio katika Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, taasisi zake pamoja na Makao Makuu ya Mikoa na Halmashauri zake kwa muda wa miaka mitatu mfululizo. Hali hii inaonesha kuwa vyanzo vya mapato kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI vinaendelea kukua na kuimarika kila mwaka. Kamati inaamini kuwa hali hii inatokana na kukua kwa uchumi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuimarisha usimamizi wa mapato pamoja na kubuni njia nzuri za ukusanyaji wa mapato na kuendelea kuzuia mianya ya upotevu wa mapato na hivyo kuchagiza ustawi wa jamii. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweka mikakati inayosababisha ukuaji huu wa uchumi na maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wake pia Kamati ilibaini kuwa kuna ongezeko la utengaji wa makisio ya makusanyo ya maduhuli kutoka shilingi 1,199,287,592,146 zilizotengwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 hadi shilingi 1,925,881,323,464 zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, sawa na ongezeko la shilingi 726,593,731,318 sawa na 60.5%. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa ya Wizara ya ulinganisho wa randama za vipindi vitatu tofauti, Kamati imebaini kuwa halmashauri zimeendelea kufanya vyema kwenye utengaji na ukusanyaji wa maduhuli ambapo unaongezeka kila mwaka wa fedha. Hata hivyo, Kamati pia imebaini pamoja na ukuaji huo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa kipindi hicho kukua bado kuna taasisi ambazo mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli umekuwa ukishuka. Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar-es-Salaam *(DART)* makusanyo yake yamekuwa yakishuka kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa shilingi bilioni 4.9 na shilingi bilioni 3.7 mtawalia. Aidha, Chuo cha Serikali za Mitaa (Hombolo) mapato yake yamekuwa yakishuka kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa shilingi 5,063,370,896.00 na shilingi 3,316,295,239.00 mtawalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utolewaji fedha za matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu Juni, 2024, Wizara kupitia Fungu 56, Fungu 02 pamoja na Mafungu 26 ya mikoa iliidhinishiwa jumla ya shilingi 11,612,594,336,000. Kati ya fedha hizo shilingi 7,836,140,708,000.00 sawa na 67.5% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 3,776,453,628,000.00 sawa na 32.5% ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida ambazo ni shilingi 7,836,140,708,000.00, shilingi 6,292,557,648,000.00 sawa na 80.3% ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 1,543,583,060,000.00 sawa na 19.7% ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi mwezi Februari, 2026, Wizara, taasisi zake pamoja na Sekretarieti za Mikoa zilipokea jumla ya shilingi 7,293,003,173,591.86 sawa na 62.8% ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 5,501,410,966,448.14 sawa na 75.4% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 1,791,592,207,143.72 sawa na 24.6% ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, kati ya shilingi 1,791,592,207,143.72 za matumizi ya maendeleo zilizopokewa shilingi 1,597,047,240,601.97 sawa na 89.1% ni fedha za ndani na shilingi 194,544,966,541.75 sawa na 10.9% ni fedha za nje. Taarifa zaidi inapatikana katika Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefanya uchambuzi kuhusu mwenendo huu wa upokeaji wa fedha na kubaini mambo kadhaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenendo wa Upokeaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na za Maendeleo; Kamati imebaini kuwa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo zilizopokelewa ni 24.6% tu. Aidha, fedha za maendeleo kutoka vyanzo vya ndani zilizopokelewa ni 89.1% ya fedha zote za maendeleo zilizopokelewa, wakati huohuo fedha za maendeleo zilizopokelewa kutoka vyanzo vya nje ni 10.9% tu. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuhakikisha fedha za miradi kutoka vyanzo vya ndani zinapelekwa kwa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo huu wa upokeaji wa fedha za maendeleo unaonyesha kuwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika halmashauri na mikoa yetu nchini ni duni. Hii ni dalili kuwa ukuaji wa maendeleo jumuishi kwa wananchi unaanza kurudi nyuma. Hali hii inarudisha nyuma juhudi za Serikali za kukuza uchumi na ustawi wa wananchi. Kamati inashauri kuwa Serikali iweke mikakati mahsusi na kabambe ya kuhakikisha kwamba inaanza kutenga bajeti yake kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa kutegemea zaidi vyanzo vyake vya ndani kuliko kutegemea vyanzo vya nje. Kamati inaendelea kushauri halmashauri ziendelee kuongeza mikakati ya kuibua vyanzo vipya vya mapato na kuendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Kamati imefanya uchambuzi wa mchanganuo wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Wizara kwa kuzingatia vipaumbele vilivyowekwa na Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara pamoja na taasisi zake, (Fungu 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu 02) pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa (Mafungu 26) imekadiria kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 2,336,528,152,302.47. Hili ni ongezeko la shilingi 412,291,663,838.47 kutoka shilingi 1,924,236,488,464.00 iliyokadiriwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, hii ni sawa na 21.4% (Kielelezo Na.9 katika taarifa iliyowasilishwa Mezani).

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 188.9 zimekadiriwa kukusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara, shilingi bilioni 22.9 kutoka Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka yaani *DART*, shilingi bilioni 125.1 kutoka Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam na shilingi bilioni 11.9 kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa, shilingi bilioni 4.2 kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, shilingi bilioni 5.4 kutoka kwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* na shilingi bilioni 11.4 kutoka Shirika la Masoko ya Kariakoo. Aidha, shilingi bilioni 305.05 zinakadiriwa kukusanywa kutoka Makao Makuu ya Mikoa na

shilingi 1,966,193,000,000.00 zimekadiriwa kukusanywa kutoka Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla makisio ya ukusanyaji wa maduhuli yameongezeka kwa halmashauri, Bodi ya Mikopo ya Serikail za Mitaa, Chuo cha Serikali za Mitaa (Hombolo), pamoja na Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam *(DART),* kielelezo Na. 10 katika taarifa kinaonyesha. Kamati inazipongeza halmashauri pamoja na taasisi za TAMISEMI zilizoongeza makisio ya ukusanyaji wa maduhuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 – Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI (Fungu 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu 02) na Sekretarieti za Mikoa (Mafungu 26) linaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi 12,268,472,643,000. Kati ya hizo shilingi 8,542,154,664,000, sawa na 69% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 3,726,317,979,000 sawa na 31% ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoombwa shilingi 6,844,897,496,000 sawa na 80.1% zimetengwa kwa ajili ya mishahara na shilingi 1,697,257,168,000, sawa na 19.86% ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, kati ya shilingi 3,726,317,979,000 za miradi ya maendeleo shilingi 2,938,501,239,000, sawa na 78.8% ni fedha za ndani na shilingi 787,816,740,000 sawa na 21.2% ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Uwiano wa Mpango wa Bajeti kwa Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 na Bajeti ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na kulinganisha Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 na bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Nia ni kupima mabadiliko ya

matumizi na mapato katika Wizara na kufuatilia utekelezaji wa mipango kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wa bajeti, Kamati imebaini kuwa kuna ongezeko la upangaji wa bajeti ya Wizara kutoka shilingi 11,612,594,336,000 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 hadi shilingi 12,268,472,643,000 kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, sawa na ongezeko la shilingi 655,878,307,000 ambalo ni sawa na asilimia 5.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kuwa matumizi ya kawaida kwa upande wa mishahara yameongezeka kutoka shilingi 6,292,557,648,000 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 hadi shilingi 6,844,897,496,000 katika Mwaka wa Fedha 2026/2027; sawa na ongezeko la shilingi 552,339,848,000, sawa na asilimia 8.78. Kwa upande wa matumizi mengineyo yameongezeka kutoka shilingi 1,543,583,060,000 hadi shilingi 1,697,257,168,000 sawa na ongezeko la shilingi 153,674,108,000 sawa na asilimia 9.96.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, matumizi ya maendeleo kwa upande wa fedha za ndani yameongezeka kutoka shilingi 2,496,431,476,000 Mwaka wa Fedha 2025/2026 hadi shilingi 2,938,501,239,000 kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 sawa na ongezeko la shilingi 442,069,763,000 sawa na 17.7%; huku matumizi ya maendeleo kwa upande wa fedha za nje yamepungua kutoka shilingi 1,280,022,152,000 kwa Mwaka 2025/2026 hadi shilingi 787,816,740,000 kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 sawa na punguzo la shilingi 492,205,412,000 ambayo ni sawa na 38.45%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maoni na ushauri wa Kamati, baada ya uchambuzi wa bajeti, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara hii katika kuwahudumia wananchi:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Upungufu wa matundu ya vyoo katika Shule za Msingi na Sekondari katika taarifa ya Kamati iliyotolewa Katika Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya iliyokuwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Kamati iliwasilisha maoni yake. Moja ya maoni ilikuwa ni kuhusu kufanya tathmini ya upungufu wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na

sekondari nchini, pamoja na kuelezea mikakati ya utatuzi wa changamoto hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya jitihada za kutatua changamoto hiyo. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa changamoto hiyo bado ni kubwa ukilinganisha na juhudi zilizochukuliwa na Serikali katika kutenga bajeti na kujenga matundu ya vyoo. Wakati wa uchambuzi wa taarifa za bajeti za halmashauri mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati, Kamati ilibaini kuwa pamoja na jitihada zilizowekwa na Serikali katika kufanya tathmini ya uhitaji wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini na katika ujenzi wa matundu ya vyoo, bado kuna upungufu wa matundu vya vyoo katika shule nyingi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya jitihada za kutatua changamoto hiyo. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa changamoto hiyo bado ni kubwa ukilinganisha na juhudi zilizochukuliwa na Serikali katika kutenga bajeti na kujenga matundu ya vyoo. Wakati wa uchambuzi wa taarifa za bajeti za halmashauri mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati, Kamati ilibaini kuwa pamoja na jitihada zilizowekwa na Serikali katika kufanya tathmini ya uhitaji wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini na katika ujenzi wa matundu ya vyoo, bado kuna upungufu wa matundu vya vyoo katika shule nyingi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Wizara ifanye tathmini upya kuhusu mahitaji halisi ya upungufu wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini;

(ii) Pamoja na halmashauri nchini kuchukua hatua mbalimbali katika kutatua changamoto hii, Kamati inaishauri Wizara pia kuweka mkakati wa kuzisaidia Halmashauri kutatua tatizo la upungufu wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini; na

(iii) Halmashauri pamoja na Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kuwashirikisha wadau mbalimbali kushiriki katika kutatua tatizo la upungufu wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa shule za michepuo ya Kiingereza. Vilevile, taarifa ya Kamati iliyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu wakati wa Mkutano wa Bajeti Aprili 16, 2025, Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu utekelezaji wa ujenzi wa shule za mchepuo wa Lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilieleza kwa kina athari zinazoweza kujitokeza ikiwa Serikali itaendelea kujenga shule zenye mlengo wa ufundishaji kwa Lugha ya Kiingereza. Kamati ilishauri kwa ufasaha kwamba halmashauri nchini ziache kabisa kutekeleza miradi hiyo isipokuwa kwa kibali maalum cha Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na kwa sababu za msingi za uanzishwaji wa shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza halmashauri zilizotekeleza ushauri huo kwa umakini na kwa ufanisi. Hata hivyo, kuna baadhi ya halmashauri zimeendelea kutekeleza miradi hiyo. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaendelea kusisitiza halmashauri nchini kufuata ushauri kama ulivyoletewa na Bunge katika Mkutano wako wa Kumi na Tisa wa Bunge la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwongozo wa utoaji wa mikopo ya 10% kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Serikali imeanza kutoa mikopo ya 10% kwa ajili ya wanawake, vijana na wenye ulemavu baada ya miongozo mbalimbali kuwekwa sawa. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa katika utoaji wa mikopo ya 10% kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu, baadhi ya halmashauri hazikufuata kanuni ya utoaji wa mikopo ya 4:4:2, huku halmashauri nyingine zikishindwa kusimamia utaratibu uliowekwa kuhusu urejeshaji wa mikopo hiyo. Kutokana na hali hiyo, Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Halmashauri zizingatie utoaji wa mikopo kwa uwiano wa 4:4:2 kama ilivyotakiwa bila ubaguzi wowote wa jinsi, au hali ya ulemavu;

(ii) Halmashauri zizingatie utaratibu wa kisheria uliowekwa kuhusu fedha za marejesho zinazorejeshwa na wanufaika wa mikopo hiyo;

(iii) Katika halmashauri nyingi nchini watu wenye ulemavu hawakufikiwa na mikopo hii kwa madai ya kukosekana kwa vikundi vya watu wenye ulemavu au vikundi hivyo kukosa vigezo na hivyo kukosa kunufaika kama ilivyokusudiwa;

(iv) Halmashauri ziweke mikakati ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu namna na vigezo vya utoaji wa mikopo hiyo; na

(v) Ikiwa halmashauri zina ukwasi wa fedha zinazotokana na marejesho au utengaji wa fedha hizo, halmashauri hiyo iombe kibali kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kufanya ugawaji upya *(reallocation)* wa fedha hizo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa utaratibu utakaokubaliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzalishaji wa madeni ya watumishi Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa iliyokuwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambayo kwa sasa ni Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kuhusu kuweka mkakati wa kumaliza madeni ya watumishi katika halmashauri nchini. Kamati imetaarifiwa kuwa utekelezaji huo unaendelea. Hata hivyo, wakati wa uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 Kamati ilibaini kuwa zipo halmashauri ambazo zimeendelea kuzalisha madeni mapya ya watumishi, kinyume na maoni na ushauri wa Kamati. Kutoka na hali hiyo, Kamati inaendelea kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo: -

(i) Halmashauri ziache kuzalisha madeni mapya yasiyo ya lazima ya watumishi;

(ii) Halmashauri zitenge bajeti ya kuhakikisha kuwa madeni yaliyopo kwa watumishi yanalipwa; na

(iii) Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI iweke mkakati wa kusaidia jitihada zinazofanywa na halmashauri nchini za kulipa madeni ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu wa watumishi; Kamati imebaini kwamba katika halmashauri nyingi nchini kuna upungufu wa watumishi hususan katika sekta za afya, elimu na uhandisi. Hii imepelekea baadhi ya shughuli kama vile utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji wa huduma katika halmashauri zenye upungufu wa watumishi kutofanyika kwa ufanisi hivyo kushuka kwa ubora wa huduma hizo. Kutokana na hali hiyo, Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI pamoja na halmashauri nchini zifanye msawazo wa watumishi ili kupunguza ukali wa tatizo la upungufu wa watumishi katika maeneo yenye upungufu mkubwa; na

(ii) Serikali kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuajiri watumishi katika kada zenye upungufu mkubwa wa watumishi katika halmashauri nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi kutokukamilika kwa wakati. Kuna baadhi ya miradi ya maendeleo katika halmashauri mbalimbali nchini haijakamilika ndani ya muda uliopangwa na hivyo kushindwa kuleta tija iliyokusudiwa katika jamii. Aidha, kuchelewa au kutokupelekewa kwa fedha za miradi ya maendeleo hususan katika miradi ambayo ilikuwa ikitegemea fedha za nje katika utekelezaji wake ni miongoni mwa sababu zilizopelekea miradi hiyo kutokukamilika kwa wakati. Kutokana na hali hiyo, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI iimarishe vitengo vya ufuatiliaji na tathmini *(monitoring and evaluation)* ili vitengo hivyo vitekeleze jukumu la kuimarisha ufuatiliaji na tathmini kwenye miradi yote katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ufanisi; na

(ii) Serikali iendelee kubaini vyanzo vipya pamoja na kuimarisha vyanzo vyote vya mapato ili kuzifanya

halmashauri nchini, pamoja na Taifa kwa ujumla kutegemea kwa asilimia kubwa fedha za ndani katika utekelezaji wa miradi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; kwa mara nyingine ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Spika Mussa Azan Zungu na kwako pia Mheshimiwa Naibu Spika kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha maoni ya Kamati, lakini pia kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu vyema kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusimamia Wizara hii kwa ufanisi mkubwa na tunasema nyota njema huonekana asubuhi kwa sababu Wizara hii inaendelea kupiga hatua kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi ya pekee, ninawashukuru Mheshimiwa Profesa Riziki Silas Shemdoe, Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Mheshimiwa Reuben Kwagwilwa, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anayeshughulikia masuala ya elimu; na Mheshimiwa Jafar Rajab Seif, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anayeshughulikia masuala ya afya, kwa ushirikiano walioupatia Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninamshukuru Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu Adolf Ndunguru; Naibu Makatibu Wakuu, Profesa Tumaini Nagu, Ndugu Sospeter Mtwale, *Engineer* Rogatus Mativila; na Ndugu Atupele Mwambene, pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati tangu tulipoanza kufanya nao kazi na kushiriki vizuri kwenye uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninaomba Kamati ichukue nafasi hii kuwashukuru wakuu wa mikoa yote 26 ya Tanzania Bara na Makatibu Tawala wote wa mikoa 26 na Wakurugenzi wate katika halmashauri 184 pamoja na wakuu wao wa divisheni na vitengo kwa ushirikiano wao mbele ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa ushirikiano mzuri ambao wananipatia. Wajumbe hawa ni wachapa kazi na wameshiriki kikamilifu katika uchambuzi wa bajeti kwa kuhakikisha wanahoji ili kupata ufafanuzi wa kina. Ninawapongeza sana na ninaomba majina yao kama yalivyoorodheshwa yaingie katika kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuwashukuru Sekretarieti ya Kamati inayoongozwa na Emmanuel Mdidi, Thuwaiba Jumbe na Sikudhani Mbinga ambao wapo chini ya uongozi thabiti wa Katibu wetu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema. Pamoja naye ninamshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athumani Brambati *ndc*, Wakurugenzi Wasaidizi Ndugu Michael Chikokoto, *ndc*, na Ndugu Gerald Magili kwa ushirikiano wanaoipa Kamati yetu wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inatoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Spika wetu, Mheshimiwa Azan Mussa Zungu kwa kuondokewa na Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu. Tunamwombea apumzike kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu lipokee, likubali, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja kwa Fungu 56, 02, 36 ,47, 54, 63, 70, 71, 72, 79, 74, 75, 76, 77, 78, 79, 80, 81, 82, 83, 84, 85, 86, 87, 88, 89, 90 na 95. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 ninatoa shukrani kwako kwa kunipa wasaa ili niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, Maeneo muhimu yanayoguswa na kuelezwa kwa kina na taarifa hii ni kama ifuatavyo: -

(a) Maelezo na uchambuzi kuhusu ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(b) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(c) Uchambuzi wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 (Makadirio ya Maduhuli na Matumizi); na

(d) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati.

SEHEMU YA PILI

2.0 MAELEZO NA UCHAMBUZI KUHUSU UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliidhinishiwa na Bunge jumla ya **shilingi 1,791,592,207,143.72** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 Kamati ilitembelea na kukagua baadhi ya miradi hiyo ya maendeleo iliyotekelezwa na ofisi hii katika Mwaka wa Fedha 2025/2026. Miradi iliyotembelewa ni miradi ya elimu, afya, stendi za mabasi, masoko, pamoja na barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)*.

2.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha na kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilifanya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2025/2026. Ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ilifanywa kwa kuzingatia Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata wasaa wa kutembelea na kukagua miradi katika Mikoa minne ya Morogoro, Pwani, Kilimanjaro, na Arusha, ambako jumla ya miradi kumi na mbili (12) iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ilikaguliwa. Matokeo ya uchambuzi wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo: -

2.1.1 Ujenzi wa Stendi ya Mabasi – Mikumi

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa Mradi wa Stendi ya Mabasi Mikumi unatekelezwa na Halmashauri ya Mji Mdogo wa Mikumi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa.

Faida ya Mradi

Mheshimiwa Spika, mradi huu utakapokamilika utakuwa na manufaa yafuatayo:-

(i) Kuboresha huduma za usafiri kwa abiria kwa kuwapatia eneo salama na lenye miundumbinu bora ya kusafiria;

(ii) Kuongeza mapato ya Halmashauri kupitia ushuru, ada na kodi mbalimbali zitakazotokana na shughuli za usafiri na biashara ndani ya stendi;

(iii) Kutoa ajira zipatazo 195 za muda mfupi na ajira za muda mrefu zaidi ya 50 baada ya kukamilika kwa mradi.

(iv) Utaongeza usalama wa abiria na mali zao pamoja na kuchochea maendeleo ya kiuchumi katika kata ya Mikumi na maeneo ya Jirani.

Hali ya Utekelezaji wa Mradi

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia wakati wa ukaguzi wa Kamati, mradi huu ulikuwa bado haujaanza kutekelezwa kutokana na fedha kutokupokelewa kutoka Hazina.

Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada ya taratibu za ukaguzi wa miradi, baada ya kupokea taarifa hii ya mradi Kamati ilifanya uchambuzi kuhusu na utekelezaji wa mradi huu. Katika uchambuzi wake Kamati imebaini masuala mbalimbali ya msingi kama ifuatavyo: -

a) Umbali wa eneo inakotarajiwa kujengwa Stendi kutoka Barabara Kuu ya Morogoro – Iringa

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa Mradi wa Ujenzi wa Stendi ya Mabasi Mikumi umepangwa kujengwa katika eneo lililo mbali kwa mita 350 kutoka Barabara Kuu ya Morogoro – Iringa. Kwa hulka ya ujenzi wa stendi, eneo hilo ni mbali kutoka ilipo Barabara hiyo kuu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaka kujua sababu ya stendi hiyo kupelekwa umbali huo na kujibiwa kuwa ni kutokana na kukosekana kwa eneo lililo karibu na Barabara. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa Halmashauri ina eneo lililo karibu na Barabara ambalo linatumika kama soko. Aidha, Kamati ilibaini kuwa eneo hilo linalotumika kama soko awali lilitengwa kwa ajili matumizi ya stendi. Kamati ilihoji sababu ya eneo hilo lililotengwa kwa ajili ya stendi kutumika kama soko na kujibiwa kuwa ni kutokana na wananchi wenyewe kuanza kutumia eneo hilo kwa shughuli za biashara.

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika uchunguzi wake Kamati ilibaini kuwa wananchi walipewa eneo hilo ili litumiwe na wafanyabiashara ndogondogo kwa kujenga miundombinu isiyo ya kudumu. Kamati pia ilibaini kuwa, eneo linalotakiwa kujengwa Stendi ya Mabasi lilitengwa kwa ajili ya kuwa Bustani kwa wananchi kupumzika.

b) Eneo la stendi kuwa Katikati ya makazi ya watu

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa eneo inapotakiwa kujengwa stendi ni katikati ya makazi ya watu. Hii inaweza kusababisha hatari pale mabasi yatakapoanza kuingia stendi huku maeneo hayo yakiwa na watu hasa watoto.

Mheshimiwa Spika, ni Dhahiri kuwa mabasi yatakayokuwa yanaingia katika stendi hiyo yatazalisha kelele. Hali hii si inaweza kusababisha matatizo ya afya ya mwili kwa wakazi wanaoishi maeneo ilipo stendi. Aidha, inaweza kuwasababishia ama kuwaongeza tatizo la afya ya akili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maeneo haya yana makazi ya watu, kupitisha mabasi na vyombo vingine vya usafiri katika maeneo hayo kunaweza kusababisha foleni na hivyo kuleta usumbufu kwa wananchi wakazi wa maeneo hayo. Aidha, ni dhahiri kuwa mabasi yatakayokuwa yanapita katika barabara za mitaa hiyo yanaweza kusababisha mtikisiko wa ardhi na hivyo kuweza kusababisha nyufa na hata hatari ya kubomoka kwa nyumba za wananchi.

c) Udogo wa eneo inapotaka kujengwa stendi

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa Mji Mdogo wa Mikumi unakua kwa kasi, hasa kutokana na kukua na kuongezeka kwa mizigo inayohudumiwa na Bandari ya Dar es Salaam, kuongezeka kwa shughuli za utalii na kukua kwa uchumi wa wananchi wa mji huo. Katika uchunguzi wake Kamati imebaini kuwa eneo inapotaka kujengwa stendi ni dogo. Kutokana na kwamba matarajio ya kukua kwa Mji Mdogo wa Mikumi ni makubwa. Kamati inaona kwamba eneo hilo la eka 3.5 halitoshi kujengwa stendi hiyo.

d) Eneo inapotaka kujengwa stendi kuwa oevu

Mheshimiwa Spika, Kamati imejulishwa kuwa eneo linalokusudiwa kujengwa stendi ni oevu. Maeneo oevu ni maeneo yanayoweza kunyonya maji ya mafuriko ya mvua na hivyo kuweza hupunguza mafuriko ya maji yanayotokana na mvua. Kujenga stendi eneo hilo kutasababisha mafuriko ya maji ya mvua kuweza kuathiri makazi ya watu.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeona kuwa eneo hilo la stendi linazungukwa na barabara za mitaa. Kamati imebaini kuwa ikiwa stendi hiyo itajengwa na kuzuia mtiririko wa maji yanayotokana na mvua kunaweza kutokea mafuriko yatakayoathri barabara za mitaa katika eneo hilo.

e) Barabara zinazoingia eneo la Stendi kuwa nyembamba

Mheshimiwa Spika, Upimaji wa ramani wa Mji wa Mikumi umetenga barabara zinazoingia eneo linakotakiwa kujengwa

Stendi ya Mabasi Mikumi kuwa nyembamba. Sababu ya kusanifu barabara hizo kuwa nyembamba ni kutokana na barabara hizo nyingi kuwa ni barabara za mitaa. Hivyo, haikutarajiwa maeneo hayo kupitisha magari yenye uzito mkubwa. Stendi ya Mabasi Mikumi imepangwa kujengwa kwa madhumuni ya kupokea mabasi madogo na makubwa. Kutokana na hilo, Kamati inaona kuwa stendi hiyo haitakuwa na ufanisi kutokana na miundombinu ya barabara zinazoelekea itakapokuwa stendi kuwa finyu.

Maoni na Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa masuala mbalimbali yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa mradi huu Kamati inatoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo: -

(a) Kutokana na sintofahamu iliyobainika kwa Kamati kuhusu eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa stendi ya mabasi ya Mikumi; Kamati inashauri Serikali itume timu ya uchunguzi eneo hilo ili kusimamia utengaji wa eneo la stendi ya mabasi kwa kuzingatia maslahi ya wananchi;

(b) Kamati inashauri eneo lililopo kati ya eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa stendi na eneo la wazi ambalo lina makazi ya wananchi litwaliwe kutoka kwa wananchi kwa kuwalipa fidia ili eneo hilo liwe sehemu ya eneo la Mamlaka ya Mji; na

(c) Kamati inashauri Halmashauri kutenga bajeti walau asilimia mbili (2%) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati ili kutokutegemea fedha kutoka Serikali Kuu pekee katika utekelezaji wa miradi.

2.1.2 Utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji wa Barabara za Mikumi Mjini *(Upgrading of Mikumi Town Roads 1.45 km to Rigid Pavement in Kilosa District)* (Mradi Na. S01/014/2024/2025/W/73)

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa inatekeleza Mradi wa Uboreshaji wa Barabara za Mikumi Mjini kwa

kujenga barabara yenye urefu wa Km. 1.45 kwa kiwango cha zege. Mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi mzawa anayejulikana kama *Trinity Manufacturing Services Limited* ya Dar es Salaam; chini ya Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA).

Faida ya Mradi

Mheshimiwa Spika; mradi huu utakapokamilika utarahisisha usafiri na usafirishaji wa bidhaa na watu kutoka sokoni na maeneo ya machinjio, kuunganisha maeneo ya kulala watalii na hoteli, kuongeza thamani ya ardhi na makazi ikiwemo kuunganisha viwanja vipya zaidi ya 1,153 vya matumizi ya makazi, biashara, elimu na hoteli.

Hatua za Utekelezaji wa Mradi

Mheshimiwa Spika, Mradi huu ulianza kutekelezwa mnamo tarehe 13/12/2024 kwa gharama ya shilingi 1,322,436,066.00 ambazo ni fedha za tozo ya mafuta. Mradi huu unatarajiwa kukamilika tarehe 12/05/2026. Hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu kwa ajili ya ukaguzi ulikuwa umefikia asilimia 55 ya utekelezaji wake. Mradi unatarajia kukamilika tarehe 20 Aprili, 2026.

Changamoto

Mheshimiwa Spika, wakati wa utekelezaji wake mradi huu umekumbana na changamoto kadhaa ikiwemo ucheleweshaji wa malipo ya awali *(Advance Payment),* mvua kubwa zilizonyesha Mkoani Morogoro pamoja na kuchelewa kwa msamaha wa kodi, hali iliyoathiri kasi ya utekelezaji wa mradi.

Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Barabara ya Mikumi Kamati ilifanya uchambuzi kuhusu na mradi huo. Katika uchambuzi wake Kamati imebaini masuala mbalimbali ya msingi kama ifuatavyo: -

a) Kukosekana kwa mitaro

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa usanifu wa ujenzi wa barabara hiyo haukuhusisha ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya mitaro pamoja na njia ya watembea kwa miguu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa kukosekana kwa mitaro kunaweza kusababisha uhai wa barabara hiyo kuwa mdogo kutokana na uwezekano wa maji ya mvua kusababisha mmomonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Spika, barabara hiyo inapita katika makazi ya watu. Ni wazi kuwa wananchi watembea kwa miguu watakuwa wakiitumia barabara hiyo. Kukosekana kwa njia ya watembea kwa miguu pembezoni mwa Barabara hiyo kunaweza kukasababisha usumbufu, ama hata ajali kwa watembea kwa miguu.

Maoni na Ushauri wa Kamati

Kwa kuwa barabara hii inaelekea katika stendi ya mabasi na eneo la soko, Serikali iangalie namna ya kuiboresha ili iweze kumudu uzito wa magari unaoruhusu shughuli za kiuchumi.

2.1.3 Kuendeleza Ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Morogoro (Mradi Na. 3249)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro unatekelezwa katika Kata ya Kihonda Mtaa wa Nguvu Kazi.

Mheshimiwa Spika; Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Morogoro ulianza kutekelezwa kwa kutumia mfumo wa *force account* katika mwaka wa Fedha 2021/2022 ambapo hadi kukamilika kwake ulikadiriwa kutumia jumla ya **shilingi 7,000,000,000.00** kwa kujenga jumla ya majengo/miundombinu 28 ya Afya. Hadi kufikia muda wa ukaguzi wa Kamati, tayari fedha kiasi cha **shilingi 3,024,800,000.00**, kilikuwa kimeshatumika, ikiwa **shilingi 2,878,800,000.00** kutoka Serikali Kuu na **shilingi 146,000,000.00** kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri.

Hatua za Utekelezaji wa Mradi

Mheshimiwa Spika; hadi kufikia wakati wa ukaguzi wa Kamati tayari majengo 13, ambayo ni Jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD), Maabara, Jengo la mionzi (Radiology), Jengo la Upasuaji (Theatre), Wodi ya Wanawake, Wodi ya Wanaume, Wodi ya upasuaji Wanaume, Wodi ya kina Mama Wajawazito na Upasuaji *(Maternal Complex),* Wodi ya Watoto *(Pediatric),* Jengo la kuhifadhia miili *(Mortuary),* Jengo la kufulia, Jengo la kuhifadhia dawa *(Pharmacy)* na Nyumba ya Watumishi *(Three in one*) yalikuwa tayari yamekwishakamilika kwa asilimia 100.

Faida ya Mradi

Mheshimiwa Spika; kukamilika kwa mradi huu kumepelekea faida mbalimbali zikiwemo: -

i) Kutoa huduma za afya kwa wananchi wa Manispaa na maeneo ya Jirani; na

ii) Kuwa Kituo cha rufaa cha kutolea huduma za Afya kwa Vituo vya Afya na Zahanati zilizopo katika Manispaa ya Morogoro.

Changamoto

Mheshimiwa Spika; Kamati ilitaarifiwa kuwa wakati wa utekelezaji wa mradi huu hakukuwa na changamoto yoyote. **Kamati inatilia shaka taarifa hii.**

Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Morogoro Kamati ilifanya uchambuzi wake kuhusu na mradi huo. Katika uchambuzi huo Kamati imebaini masuala mbalimbali ya msingi kama ifuatavyo: -

a) Ujenzi kufanyika katika eneo oevu

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa eneo ilipojengwa Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ni oevu na linalokusanyika maji kutoka uwanda wa juu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu unaweza kusababisha maeneo ya jirani, ambako kuna makazi ya watu kukumbwa na mafuriko ya mvua ya mara kwa mara. Vilevile, Kamati imebaini kuwa, matenki ya maji taka yaliyojengwa maeneo hayo oevu yanaweza kujaa mara kwa mara na maji ya mafuriko. Hii inaweza kusababisha magonjwa ya mlipuko kwa wananchi.

b) Ujenzi usiofuata utaratibu

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa majengo mengi yamekuwa yakitinduliwa kwa ajili ya kuweka miundombinu ya umeme na maji baada ya kupigwa plasta. Kamati inatambua kuwa ujenzi wa majengo ya Serikali hufuata utaalam; na katika hili Kamati ilifahamishwa kuwa kwa utaalam wa ujenzi, kabla ya kupiga plasta inawekwa miundombinu ya maji safi na maji taka pamoja na miundombinu ya umeme. Suala la kuweka miundombinu hiyo baada ya kupiga plasta ni kukosa weledi na utaalam. Ujenzi huu usioufuata utaalam na taratibu za ujenzi unaweza kusababisha athari kubwa na kuleta hasara kwa Serikali.

c) Usimamizi hafifu wa mradi

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa mradi huu unatumia *force account,* hivyo mafundi wanaotekeleza mradi huu ni mafundi wasio na elimu ya uhandisi wa darasani *(local fundi)*. Mafundi hawa huhitaji usimamizi wa karibu ili kuhakikisha kuwa wanaelekezwa kuhusu viwango vya ujenzi vinavyohitajika katika utekelezaji wa mradi. Kamati imebaini kasoro kadha wa kadha zilizosababisha kuleta hisia kuwa wataalam wa Halmashauri hawakuwa makini katika usimamizi wa mradi huu.

d) Ujenzi kutokufuata BOQ

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa mbao zilizotumika kwa ajili ya kupaua katika baadhi ya majengo iliyoyakagua, hasa kwenye njia za kupitia kuunganisha majengo *(walkways)* ni za kawaida ilihali *BOQ* inataka mbao za kupaua majengo ziwe *treated*. Hii inaonesha kuwa kulikuwa na udhaifu kwa upande wa manunuzi.

Maoni na Ushauri wa Kamati

(a) Kamati inashauri Serikali kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi. Wakuu wa Idara na Vitengo watekeleze majukumu yao ipasavyo pamoja na kushughulikia dosari zote zilizobainika kwenye mradi;

(b) Serikali kupitia OWM- TAMISEMI iendelee kusisitiza Halmashauri kufuata ramani, michoro na miongozo inayotolewa na OWM-TAMISEMI katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi ili miradi hiyo itekelezwe kwa ufanisi na kuleta tija iliyokusudiwa kwa wananchi;

(c) Serikali ifanye msawazo wa watumishi wa afya na kuendelea kutenga ikama itakayowezesha kuajiri wataalamu wa afya 113 wanaohitajika katika hospitali ya Manispaa Morogoro ili kuwezesha kupatikana kwa huduma zote muhimu kwa wananchi; na

(d) Kwa kuwa Serikali iliomba kuongezewa muda wa kukamilisha mradi huu hadi tarehe 15 Mei, 2026, Kamati inasisitiza Serikali kuhakikisha kuwa mradi unakamilika ndani ya muda huo na katika ubora unaotakiwa ili kutoa huduma zilizokusudiwa kwa wananchi.

2.1.4 Uboreshaji wa Miundombinu ya Miji kwa ushindani Manispaa ya Morogoro (Mradi LGA/079/2022/2023/HQ/W/16/PCKG/01)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Miji *(Tanzania Cities Transforming Infrastructures and*

Competitiveness Project) kwa ushindani unatekelezwa na Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia, ukiwa na lengo la kuboresha miundombinu ya miji, manispaa na majiji.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikagua miradi iliyo sehemu ya utekelezaji wa mradi huo inayotekelezwa katika Mkoa wa Morogoro. Katika mkoa huo Kamati ilikagua ujenzi wa Barabara ya Muhimbili (1.2km) ambayo utekelezaji wake ulifanyika katika Awamu ya Kwanza *(TACTIC Package 1)* na ulishakamilika kwa asilimia 90.9 pamoja na mradi wa Ujenzi wa Stendi ya Mabasi Madogo Kihonda, ambao unatekelezwa katika Awamu ya Pili *(Package 2)*.

Mheshimiwa Spika; mradi huu unatekelezwa kwenye eneo lenye mita za mraba 55,723.32, na unatekelezwa na Mkandarasi M/S TIL Construction Limited kwa gharama ya shilingi 13,460,689,504.61 na kusimamiwa na Mhandisi Mshauri M/S Mhandisi Consultancy Limited akishirikiana na M/S CORE Consulting Engineers PLC kwa gharama ya Shilingi 1,743,927,140.00.

Hatua za Utekelezaji:

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu ni wa muda wa miezi 12, kuanzia tarehe 21/07/2025 hadi tarehe 21/07/2026. Hadi kufikia wakati wa ukaguzi wa Kamati mradi huu ulikuwa umefikia asilimia 52 ya utekelezaji.

Faida za Mradi

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa mradi huu wa ujenzi wa stendi kutaleta manufaa yafuatayo:-

i) Kuboresha mazingira ya usafiri na usafirishaji hususani kwa wananchi wanaotumia usafiri wa reri ya kisasa, ambao watapata eneo rasmi la kupata usafiri wa kuelekea maeneo mbalimbali ndani ya Manispaa ya Morogoro;

ii) Kurahisisha huduma ya usafiri na usafirishaji kwa wananchi wa maeneo ya Kata ya Kihonda na Kata za jirani;

iii) Kuwepo kwa ajira za moja kwa moja kwa wananchi ambao wataendesha biashara zao ndani ya stendi hii; na

iv) Kuongeza makusanyo ya Halmashauri.

Uchambuzi wa Kamati
Ubora wa Barabara

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa Barabara ya Muhimbili imejengwa kwa ubora. Kamati inaipongeza Serikali kwa utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imebaini kuwa barabara hii ndiyo Barabara ya kwanza ya mzunguko katika Manispaa ya Morogoro iliyo mchepuko *(bypass)* ya Barabara ya Dar es Salaam Kwenda Dodoma bila kupitia maeneo ya mjini. Kamati inaona kuwa barabara hii ni ya muhimu sana kwa kuwa itapunguza foleni iliyoko katika Barabara ya Dar es Salaam kuanzia maeneo ya Njiapanda ya Kihonda – VETA, Mzunguko *(roundabout)* wa Msamvu hadi Nanenane. Kamati inaipongeza TARURA na Serikali kwa ujumla kwa usanifu wa barabara hii.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i) Kwa kuwa mradi ulisanifiwa bila kuweka eneo kwa ajili ya maegesho ya magari madogo, Kamati inashauri kuwa Serikali iangalie uwezekano wa kutenga eneo kwa ajili ya kuegesha magari madogo;

ii) Serikali ihakikishe kuwa inatenga bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ili ikamilike kwa wakati ili kusaidia kupunguza foleni Katikati ya Mji wa Morogoro.

2.1.5 Ujenzi wa Barabara ya Picha ya Ndege – Bokotimiza (0.52km) kwa kiwango cha lami

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Picha ya Ndege - Bokotimiza yenye urefu wa kilomita (0.52km) utekelezaji wake umeanzia kwenye makutano ya Barabara ya Morogoro na kupitia maeneo muhimu ikiwemo magereza, hospitali na shule kabla ya kufika eneo la Bokotimiza kwa urefu wa kilometa 7.88.

Faida za Mradi

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuborehsa usafiri wa watu na usafirishaji wa miradi katika eneo hilo na hivyo kukuza uchumi na kuleta ustawi kwa wananchi wanaoishi karibu na wanaotumia barabara hiyo.

Uchambuzi wa Kamati

a) Barabara kutokuwa na stendi za mabasi *(bus bay)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Barabara ya Picha ya Ndege – Bokotimiza haina maeneo ya kusimama magari *(bus bay)*. Pamoja na magari mengine kupita katika barabara hiyo, barabara hiyo pia itatumiwa na vyombo vya usafiri wa umma kama mabasi ya abiria, daladala na bajaji.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa maeneo ya kusimama mabasi *(bus bay)* kutasababisha magari ya abiria yatakayokuwa yanapita katika barabara hii kukosa mahala pa kusimama kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria. Hali hii inaweza kusababisha magari ya aina hiyo kusimama Katikati ya barabara, hali inayoweza kusababisha ajali na foleni.

b) Barabara kutokuwa na taa za barabarani

Mheshimiwa Spika, ni utaratibu uliowekwa na Serikali kuhakikisha kuwa barabara zote zinazojengwa, zikipita katika makazi ya watu kusimikwe taa za barabarani.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ukaguzi wa barabara hii Kamati imebaini kuwa hakuna taa za barabarani zilizosimikwa katika vipande vya barabara vilivyojengwa huku vikiwa vimekamilika kwa asilimia 100.

c) Barabara kujengwa vipande vifupivifupi kwa mita zisizozidi 600 kila mwaka,

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa barabara hii inajengwa kwa vipande vya wastani wa mita 500 kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati imetaarifiwa kuwa barabara hii inajengwa kutoka Picha ya Ndege hadi Bokotimiza, ambapo inagusa hadi katika stesheni ya SGR ya Soga, (7.8km). Hivyo Kamati inaona kuwa barabara hii ni muhimu kwa kuwa inawezesha wasafiri wanaotumia usafiri wa treni ya SGR kwenda na kurudi Morogoro, Dodoma, na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa, ikiwa Barabara hii itaendelea kujengwa kwa vipande vya mita 500 kila mwaka itachukua miaka takriban 12 ili kuikamilisha. Hali hii inaweza kupoteza umaana na umuhimu wa barabara hii. Aidha, inawezekana kabisa kabla barabara kuanza kuharibika kabla haijakamilika.

Maoni na Ushauri wa Kamati

(a) Kamati inashauri Serikali kutenga bajeti ya kujenga kipande chote cha barabara kilichobaki kwa changarawe ili ianze kutumika wakati bajeti ya kujenga kwa lami inaendelea kutengwa;

(b) Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya makaravati na mitaro inaelekeza maji karibu na makazi ya watu kabla ya kufika kwenye mkondo uliokusudiwa na hivyo kuweza kusababisha mafuriko kwenye makazi ya watu. Kamati inashauri mitaro hii kurefushwa ili kuondoa uwezekano wa mafuriko kwenye makazi ya watu;

(c) Kamati inashauri Serikali kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kujumuisha uwekaji wa taa za barabarani katika miradi yote ya ujenzi wa barabara.

2.1.6 Ujenzi wa Barabara ya Kongowe – Forest – Yombo (0.7km) kwa kiwango cha Lami.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu ulianza rasmi tarehe 21 Novemba, 2024 na unatarajiwa kukamilika tarehe 04 Mei, 2026. Hadi kufikia kipindi cha ukaguzi wa mradi tayari mkandarasi alikuwa ameshalipwa jumla ya shilingi 661,849,315.00 na kazi ilikuwa imefikia asilimia 95 ya utekelezaji wake.

Faida ya Mradi

Mheshimiwa Mwenyekiti; Kukamilika kwa ujenzi wa Barabara hii ambayo inaanzia kwenye makutano ya Barabara ya Morogoro na inapitia kwenye maeneo muhimu ikiwemo Ofisi za Misitu (TFS), Hosptali na Shule kabla ya kufika eneo la Yombo kwa urefu wa kilomita 19.69**,** pamoja na kuwa ni kiungo muhimu kati ya Wilaya ya Kibaha na Bagamoyo, ina umuhimu mkubwa katika kuimarisha maendeleo ya jamii na ukuaji wa uchumi, itarahisisha usafiri wa watu na bidhaa, itaboresha upatikanaji wa huduma za afya na elimu, na inachochea shughuli za kibiashara na uzalishaji.

Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kongowe – Forest – Yombo, pamoja na kufanya ukaguzi, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina kuhusu taarifa hiyo. Katika uchambuzi huo Kamati imebaini masuala mbalimbali ya msingi kama ifuatavyo: -

a) Kutokuwepo kwa mabamba *(slabs)* ya kutosha kuelekea katika makazi ya wananchi

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kongowe – Forest – Yombo hauna mabamba *(Slabs)* ya kutosha kutoka barabarani kwenda katika makazi ya wananchi. Aidha, Kamati imeona mitaro iliyowekwa kwa ajili ya

kupitisha maji ya mvua kwa ajili ya kulinda barabara kuwa inawazuia wananchi kutekeleza majukumu yao kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, pembeni mwa barabara hii kuna makazi ya wananchi. Aidha, katika makazi hayo imebainika kuwa kuna shughuli mbalimbali kama vile biashara zinazoendelea.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i) Serikali iendelee kutenga fedha ili barabara hii iweze kukamilika kwa wakati na kuleta tija iliyokusudiwa;

ii) Kamati inashauri Serikali kuongeza vivuko vya kuingia maeneo ya wananchi na maeneo yao ya kiuchumi (*slabs*) katika ujenzi wa barabara hii. Aidha, ujenzi wa barabara uende sambamba na kuweka njia au matoleo ya miundombinu mengine kama vile maji na umeme; na

2.1.7 Ujenzi wa Barabara ya Bomang'ombe – Kikavuchini kwa kiwango cha Lami (3.5km) (Mradi Na. S10/009/2023/2024/W/229)

Mheshimiwa Spika; mradi wa ujenzi wa Barabara ya Bomangómbe – Kikavuchini kwa kiwango cha lami *(Double Surface Dressing)* yenye urefu wa Km 25.7 ambayo inaanzia Bomangómbe hadi TPC una gharama ya shilingi 2,999,000,000.00. utaratibu wa ujenzi wa mradi huu ni kujengwa kwa awamu kadri ya upatikanaji wa fedha.

Faida za Mradi

Mheshimiwa Spika; baada ya kukamilika kwa mradi huo kutakuwa na faiida kama ifuatavyo:-

i) Kutafungua fursa mpya na kukuza shughuli za utalii katika eneo la kivutio cha Chemka Hotspring;

ii) Itakuwa njia mbadala wa Barabara kuu ya Arusha – Njiapanda ya Himo;

iii) Itarahisisha usafiri wa watu na mizigo kuelekea katika mashamba ya TPC, Chuo cha Ufundi Arusha (ATC – Kikuletwa Campus), Chuo cha Ufundi VETA, Chuo cha Afya na Ualimu Mongáre; na

iv) Kuunganisha kata za Bomangómbe, Bongeni na Weruweru.

Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya hii (3.5km), pamoja na kufanya ukaguzi, Kamati ilibaini kuwa Barabara ya Bomang'ombe Kikavuchini ni barabara inayozifikia taasisi mbalimbali za umma na binafsi, ambazo ni; Chuo cha Ufundi Arusha *(Arusha Technical College),* Chuo cha Ualimu Mangare (Mangare Teachers College, Kituo cha Mafunzo ya Ufundi, pamoja na Kiwanda cha Sukari cha TPC.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaarifiwa kuwa barabara hii imetolewa agizo na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhama kutoka TARURA na kwenda TANROADS. Kamati inapongeza uamuzi huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa barabara hii imewekwa vivuko (mabamba) vya kutosha kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kuyafikia makazi yao. Kamati inapongeza jambo hili kwa kuwa litarahisisha wananchi kuendelea na shughuli zao bila usumbufu wowote.

Maoni na Ushauri wa Kamati

(a) Kamati inashauri ujenzi wa barabara hii uendelee wakati taratibu za kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kuhamisha mradi wa barabara hii kutoka TARURA kwenda TANROADS zinafuatwa ili kuwezesha wananchi kupata huduma iliyokusudiwa; na

(b) Kamati inashauri Serikali ihakikishe kwamba barabara zinazojengwa maeneo mbalimbali nchini zinawekwa

vivuko vya vya kutosha kwa ajili ya wananchi kuvitumia ili kuingia katika maeneo yao, na kuweka matoleo ya kuwezesha kujengwa miundombinu mingine itakayohitajika.

2.1.8 Ujenzi wa Sekondari ya Wasichana ya Longido Samia (Mradi Na. 4390)

Mheshimiwa Spika; mradi wa ujenzi wa Sekondari ya Wasichana ya Longido Samia ambao umeanzishwa kwa lengo la kuboresha mazingira bora ya ufundishaji na ujifunzaji katika shule za sekondari na pia kuongeza idadi ya Shule za Sekondari katika wilaya ya Longido, umetekelezwa kwenye Kata ya Orbomba Kijiji cha Oltepes. Shule hii ni mojawapo ya Shule 26 zilizojengwa Tanzania nzima chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika jitihada zake za kuelimisha na kuendeleza jamii ya Tanzania hasa Watoto wa kike. Shule hii ambayo ina usajili wa wa S.6575 ilianza kutekeleza majukumu yake mnamo tarehe 01/07/2024 ikiwa na Wanafunzi wa kidato cha tano ikiwa na michepuo ya sayansi (PCB, PCM na CBN).

Mheshimiwa Spika; Mradi wa Ujenzi wa shule ya Sekondari ya Wasichana ya Longido Samia umetekelezwa kwa fedha kiasi cha Shilingi 4,450,000,000.00 ambapo utekelezaji wake umefanywa katika Awamu 3.

Changamoto

Mheshimiwa Spika; wakati wa ukaguzi wa Kamati ilielezwa kuwa mradi huu wakati wa utekelezaji wake ulikumbana na changamoto za upandaji wa gharama za vifaa vya ujenzi tofauti na fedha zilizopokelewa awali, kuwepo kwa tofauti kati ya fedha zilizopokelewa na gharama halisi za mradi ukilinganisha na mwongozo wa TAMISEMI na kuwepo kwa ongezeko (*variation*) ya idadi ya malighafi/vifaa vilivyohitajika kweney ujenzi.

Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Sekondari ya Wasichana ya Longido Samia pamoja na kufanya ukaguzi, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina kuhusu mradi huu. Katika uchambuzi wake Kamati imebaini mambo mbalimbali ya msingi kama ifuatavyo: -

a) Uwepo wa nyufa nyingi katika baadhi ya majengo

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa katika majengo kadhaa yaliyokaguliwa na Kamati kuna nyufa katika baadhi ya kuta. Uwepo wa nyufa hizi unaweza kusababisha madhara makubwa kwa kuta hapo baadaye.

b) Kubanduka kwa rangi za kuta za nje katika baadhi ya majengo

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imebaini kuna baadhi ya majengo rangi yake imeanza kubanduka katika maeneo mengi. Hali hii inaweza kusababishwa na ubora mdogo wa rangi iliyotumika, umakini mdogo wakati wa ujenzi, na, ama usimamizi mdogo. Aidha, ikiwa kuta hizo zitaendelea kuachwa bila kushughulikiwa kuna uwezekano wa tatizo hili kukua.

c) Matumizi ya milango ya mabati

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya majengo, kama vile maabara na bwalo milango iliyowekwa ni ya bati gumu. Kamati ilitaka kujua ikiwa matumizi ya milango hiyo ni maelekezo ya Wizara. Katika majibu yake Wizara imesema kuwa maelekezo ya Wizara ni kutumia mbao ngumu au malighafi inayofanana na hiyo. Kamati inafahamu kuwa malighafi ya bati si malighafi inayofanana na malighafi ya aina ya mbao.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Kamati imetaka kujua ubora, madhara, na umaridadi wa matumizi ya milango ya bati. Kamati ilijibiwa kuwa milango hiyo haina shida kubwa. Kamati imebaini kuwa kati ya shule zote na mejengo yote ya Serikali

yaliyokaguliwa na Kamati mradi huu ni wa kwanza kuwa na milango ya aina hiyo. Kamati ilitaka kujua sababu za matumizi ya milango hiyo, na kwa nini isiwe milango ya mbao na kujibiwa kuwa ni kutokana na changamoto ya upatikanaji wa malighafi za mbao.

Mheshimiwa Spika, katika uchunguzi wake Kamati imeng'amua kuwa matumizi ya milango ya mabati katika majengo ya Serikali haina kiwango kizuri kwa mwonekano na hakuyafanyi majengo kuwa maridadi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa kina na kubaini kuwa milango ya mabati ina gharama nafuu zaidi ya milango ya mbao. Aidha, upatikanaji wa milango ya bati ni rahisi zaidi kuliko milango ya mbao. Vilevile, Kamati imebaini kuwa milango ya mbao huongeza thamani ya jengo na kulifanya jengo kuwa maridadi na bora zaidi.

d) Utofauti wa viwango vya magodoro ya wanafunzi katika mabweni

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa magodoro wanayoyatumia wanafunzi wa shule hii yana viwango tofautitofauti. Kamati ilitaka kufahamu sababu ya viwango hivi kutofautiana na kujibiwa kuwa ni kutokana na wanafunzi kuagizwa kuja na magodoro yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inafahamu kuwa utofauti wowote wa kimsingi *(basic difference)* kati ya wanafunzi huweza kusababisha hisia za unyonge kwa baadhi ya wanafunzi. Hali hii huweza kuathiri uwezo wa mwanafunzi aliyeathirika kutokufanya vizuri katika masomo yake.

e) Fedha za ujenzi kutokutosha

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa mradi huu, Kamati imebaini kuwa majengo ya mabweni manne yanayojengwa hayajakamilika ilihali fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni hayo imekwisha. Kamati iliuliza kutaka kujua sababu ya fedha kutokutosha na kujibiwa kuwa fedha zilizopangwa kwa ajili ya

majengo hayo hazikutumika zote kwa kuwa sehemu ya fedha hizo zilitumika kwa ajili ya kumalizia majengo ya nyuma ambayo pia fedha zake hazikutosha. Kamati ilitaka kujua ikiwa wametumia utaratibu kuhamisha fedha hizo na kujibiwa kuwa wametumia utaratibu wa kawaida wa kuhamisha fedha *(funds reallocations)*. Hali hii imekuwa ikisababisha usumbufu wa kuomba fedha kidogo kidogo.

f) Ofisi ya RAS kutenga bajeti kwa ajili ya kuajiri maafisa milki kwenye shule za kimkakati

Wakati wa uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa uwepo wa uchakavu wa majengo pamoja na nyufa mbalimbali kunahitajika kuwe na afisa atakayesimamia utunzaji wa majengo. Kutokuwepo kwa mtu wa kusimamia majengo kunafanya kusiwepo na mtu wa kuyatazama majengo na kumshauri mwenye mamlaka kuhusiana na namna bora ya kutunza majengo, lakini pia namna bora ya kufanya matengenezo mbalimbali ya kawaida.

g) Kutokuwepo kwa uzio

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa katika shule hii ambayo ni moja ya shule za kimkakati haina uzio kwa ajili ya ulinzi wa wanafunzi. Kamati inatambua kuwa eneo hili la Longido ni eneo ambalo linazungukwa na mbuga zenye wanyamapori wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, shule hii ya Sekondari ya Wasichana ya Longido Samia iko kwenye hatari kubwa kwa watoto wanaosoma shule hii kushambuliwa na wanyamapori. Kukosekana kwa uzio katika shule hii kunasababisha wanafunzi kuishi kwa hofu ya wanyamapori wakali. Hali hii inaweza ikaleta shida ya kisaikolojia na hivyo kuweza kusababisha kushuka kwa kiufanisi katika masomo yao.

Maoni na Ushauri wa Kamati

(a) Kamati inashauri Serikali kuimarisha usimamizi wa ndani ya shule pamoja na shule kufanyiwa matengenezo ya

mara kwa mara (*routine maintenance*) ili kuongeza muda wa matumizi wa mali za shule na kuepusha kutumia gharama kubwa baadaye katika matengenezo ya miundombinu ya shule;

(b) Kamati inashauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa shule ili kulinda usalama wa wanafunzi dhidi ya Wanyama wa porini, kulinda miundombinu ya shule lakini pia ili kudhibiti mienendo ya wanafunzi.

2.1.9 Ujenzi wa Shule Mpya ya Msingi ya Mkondo Mmoja - Shule ya Msingi Lowasa (Mradi Na. 4312**)**

Mheshimiwa Spika, katika ukaguzi wake Kamati ilitembelea na kukagua mradi wa Ujenzi wa Shule Mpya ya Msingi ya Mkondo mmoja, ambao unatekelezwa na Serikali kupitia mradi wa *BOOST*. Mradi huu ulianza kutekelezwa rasmi tarehe 04/09/2024 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 30/03/2026.

Faida ya Mradi

Mheshimiwa Spika; kukamilika kwa mradi huu pamoja na kuwezesha wanafunzi kupata mazingira mazuri na rafiki ya kujifunzia pia utasaidia kuongeza idadi ya shule za msingi katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido kutoka shule 99 zilizopo na kufikia shule 100, kuondoa msongamano madarasani na kupandisha kiwango cha udahili wa wanafunzi wa awali na wa msingi kila mwaka.

Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati baada ya kuutembelea, kupokea taarifa na kuukagua Mradi wa Ujenzi wa Shule hii, ilifanya uchambuzi wake ili kufahamu ikiwa mradi huu umetekelezwa kama ilivyokusudiwa. Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini masuala mbalimbali kama ifuatavyo: -

a) Kutofautiana kwa ramani za majengo

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati ikichambua kuhusu utekelezaji wa mradi huu ilibaini kuwa kuna utofauti wa ramani za majengo kati ya jengo moja na lingine. Kamati imebaini kuwa utofauti wa ramani hizo umesababisha pia kuonesha utofauti katika ubora wa majengo. Kamati inaamini kuwa ujenzi wa majengo ya shule za Serikali hufuata mitindo inayofanana ili kuyafanya kuwa bora na maridadi, imara na ya kuvutia. Kamati haikupendezwa na utaratibu wa ujenzi wa majengo haya kutofautiana.

b) Ujenzi usiofuata utaratibu

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa ujenzi wa shule hii haukufuata utaratibu. Hii ni kutokana na Kamati kugundua kuwa kuna miundombinu ya maji safi na maji taka iliyojengwa baada ya majengo kupigwa plasta. Hali inaonesha kuwa aidha kuna uzembe kwa mafundi waliojenga jengo hilo, au mafundi waliojenga hawana ujuzi katika mambo ya ujenzi, au hapakuwa na usimamizi wa kutosha kutoka kwenye mamlaka za usimamizi.

Maoni na Ushauri wa Kamati

(a) Kamati inashauri Serikali kuhakikisha shule hii inatengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa shule ili kulinda usalama wa wanafunzi dhidi ya wanyama wa porini, kulinda miundombinu ya shule lakini pia kudhibiti mienendo ya wanafunzi;

(b) Serikali ihakikishe shule ijengwa mabweni kwa ajili ya wanafunzi ili kulinda usalama wa wanafunzi watakaotakiwa kutembea umbali mrefu kufika shuleni lakini pia kuwezesha wanafunzi hao kupata elimu pale ambapo familia zao za kifugaji zitakapokua zinahama; na

2.1.10 Ujenzi wa Sekondari ya Migungani (Mradi Na. 4390)

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari Migungani One umetekelezwa kwenye Halmashauri ya Monduli kupitia Shule mama ya Sekondari Manyara. Mradi huu ulianza kutekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 na ulikamilika katika mwaka wa fedha 2024/2025, ukiwa na gharama ya Shilingi 882,158,029.

Hatua za Utekelezaji wa Mradi

Mheshimiwa Spika; mpaka kufikia wakati wa ukaguzi wa Kamati, mradi huu ulikuwa umekamilika na majengo mengi yameshaanza kutumika, isipokuwa madarasa mawili yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi, ambayo Kamati ilielezwa kuwa yataendelea kukamilishwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

Faida za Mradi

Mheshimiwa Spika; uwepo wa mradi huu kumesaidia kupunguza mlundikano wa wanafunzi katika shule za sekondari zilizo ndani ya Halmashauri. Vilevile umeogeza idadi ya shule zilizo ndani ya Halmashauri ya Monduli kutoka shule 27 hadi kufikia shule 28.

Maoni na Ushauri wa Kamati

(a) Kamati inashauri Halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya kumalizia maboma mawili ya madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi ili madarasa hayo yaweze kukamilika na kutumika na tija iliyokusudiwa iweze kupatikana;

(b) Kamati inashauri Halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika Shule ya Sekondari Migungani One ili kulinda usalama wa wanafunzi dhidi ya wanayama wa porini; na

(c) Kamati inashauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa bwalo la wanafunzi kula chakula ili kuwezesha wanafunzi hao kula katika mazingira bora na kuzuia mlipuko wa magonjwa yanayoweza kutokea.

2.1.11 Ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi yaendayo Mikoani (*Bondeni City Bus Terminal*) (Mradi Na. 7003/TACTIC/P171189/2024-2025/W/01)

Mheshimiwa Spika; mradi wa ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi (*Bondeni City Bus Terminal*) unatekelezwa na Kampuni ya M/S MOHAMMED BUILDERS LIMITED kwa gharama ya Shilingi 14,317,331,493.00 na unasimamiwa na Mhandisi Mshauri kutoka kampuni ya Mhandisi Consultancy Ltd kwa ushirikiano na kampuni ya GBS Consultant Ltd za Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, muda utekelezaji wake ulikadiriwa kuwa ni wa mwaka mmoja, kuanzia tarehe **30/05/2025 hadi tarehe 30/05/2026**. Mradi umesanifiwa kuwa na miundombinu mbalimbali ikiwemo sakafu ya chini yenye ukubwa wa mita za mraba 8,400, sakafu ya pili yenye ukubwa wa mita za mraba 2,575, maeneo ya maegesho ya magari, vyumba vya biashara 46, maliwato za jinsia zote 2, maliwato za watu wenye mahitaji maalum, vyumba viwili vya ibada kwa Dini za Kiislamu a Kikristo, vyumba 80 vya kulala (Hostel) kwa wasafiri wanaohitaji kupumzika, Kituo cha Polisi, miundombinu rafiki kwa wazee na watu wenye ulemavu kuweza kufikia maeneo yote ya jengo ikiwa ni pamoja na sakafu za juu, vyumba maalumu kwa ajili ya ofisa wa uhamiaji, Idara ya Uokoaji na Zima Moto na miundombinu okozi wakati wa dharura ikiwemo moto, Matetemeko na vingineyo. Hadi kufikia kipindi cha ukaguzi wa Kamati mradi huu ulikuwa umefikia asilimia 70.96% ya utekelezaji wake na mkandarasi alikuwa ameshalipwa fedha kiasi cha Shilingi 2,564,307,482.00 sawa na asilimia 17.91 ya gharama za mradi.

Changamoto

Mheshimiwa Spika; wakati wa ukaguzi wa mradi Kamati ilielezwa kuwa utekelezaji wa mradi huu ulikuwa umekumbana na changamoto mbali mbali ambazo zilimchelewesha Mkandarasi

kuweza kufikia malengo yake kwa kiasi cha asilimia kumi na nne (**14%**) na kufanya Mkandarasi kuomba na kukubaliwa kuongezewa muda wa miezi sita ili kukamilisha kazi hiyo. Miongoni mwa changamogo hizo ni pamoa na:-

a) Eneo lililosanifiwa awali liligundulika kuingiliana na miundombinu ya umeme mkubwa, hivyo ikalazimika kusogeza majengo upande mwingine wa eneo lilipo mradi sasa; na

b) Uwepo wa tabaka la udongo usiofaa kwa ujenzi *(black cotton soil)* ambapo kwa maelekezo ya mhandisi mshauri, ililazimu kuondoa tabaka lote kabla ya kuanza Msingi wa ujenzi wa kituo.

Uchambuzi wa Kamati

a) Uwepo wa vyumba vya kulala katika eneo la stendi

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa Stendi hii, pamoja na huduma nyingine itakazotoa lakini pia itatoa huduma ya uwepo wa vyumba vya kulala kwa ajili ya wageni. Kamati inapongeza ubunifu huo. Hata hivyo, Kamati imetilia shaka ikiwa vyumba hivyo vitaweza kuleta faida kwa halmashauri kutokana na uzoefu uliopo wa kutokufanya vizuri kwa vyumba vya hote katika maeneo yenye vyumba vya aina hiyo, kama vile Stendi Kuu ya Mabasi ya Mkoa wa Iringa.

b) Kutokumaliza shughuli za ujenzi kwa muda uliopangwa

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa mradi huu ulipaswa kumalizika tarehe 30 Mei, 2026. Hata hivyo mradi umeongezewa miezi mingine sita ili kukamilisha ujenzi wake. Ucheleweshwaji wa kukamilika kwa mradi huo umetokana na eneo lililopaswa kujengwa stendi hiyo kupitiwa na njia kubwa ya umeme. Kamati ilitaka kujua ni kwa nini mkoa usingehamisha umeme huo badala ya kusanifu upya majengo katika eneo jipya. Kamati ilijibiwa kuwa baada ya kufanya upembuzi wa kina ilionekana kuwa ni rahisi kufanya usanifu upya kuliko kuhamisha nguzo na njia hizo za umeme.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeendelea kubaini kuwa changamoto hiyo imetokana na ukosefu wa umakini wakati wa usanifu wa awali.

Maoni na Ushauri wa Kamati

(a) Serikali ihakikishe inaimarisha usimamizi wa mradi na unakamilika kwa wakati ili kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi;

(b) Kwa kuwa ujenzi wa Kituo Kikuu cha mabasi yaendayo mkoani ni mradi wa kimkakati, Serikali iangalie uwezekano wa kupata wawekezaji katika stendi hiyo ili kuongeza mapato ya halmashauri; na

2.1.12 Ujenzi wa Soko la kwa Mrombo

Mheshimiwa Spika; Mradi wa Ujenzi wa Soko la kwa Mrombo, unatekelezwa katika eneo lenye mita za mraba 3,682, ambapo jumla ya eneo litakalojengwa ni mita za mraba 7,260 ukihusisha uboreshaji wa mazingira ya nje *(landscaping),* mifumo ya maji ya mvua, maji taka, pamoja na miundombinu ya kisasa ya maegesho ya magari na vyombo vingine vya moto.

Mheshimiwa Spika; Mradi huu unaotekelezwa kwa gharama ya Shilingi 2,286,643,323.00, unatekelezwa na Kampuni ya **M/S MOHAMMED BUILDERS LIMITED** na unasimamiwa na Mhandisi Mshauri kutoka kampuni ya **Mhandisi Consultancy Ltd** kwa ushirikiano na kampuni ya **GBS Consultant** Ltd za Dar es Salaam.

Faida za Mradi

Mheshimiwa Spika; mradi huu utakapokamilika utawapatia wananchi wa eneo la mradi na maeneo Jirani faida mbalimbali zikiwemo: -

a) Ongezeko la wateja wa hali ya chini, kati na juu;

b) Kuongeza kipato cha maafisa usafirishaji (madereva wa bodaboda na bajaji); na

Changamoto

Mheshimiwa Spika, mradi huu ambao awali ulipangwa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka mmoja (**30/05/2025 – 30/05/2026**) utekelezaji wake ulichelewa kwa takribani miezi mitatu ili kutoa muda wa kufanya mapitio ya usanifu *(design review)* pamoja na maboresho ya michoro ya mradi, kulikotokana na ufinyu wa eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa soko. Hadi kufikia kipindi cha ukaguzi wa Kamati mradi huu ulikuwa umefikia asilimia 53.79% ya utekelezaji wake na tayari Mkandarasi alikuwa ameshalipwa asilimia 30% ya gharama za mradi sawa na Shilingi 692,607,264/=.

Uchambuzi wa Kamati kuhusu Mradi

a) Ujenzi wa soko kutokuzingatia uwepo wa stoo katika jengo

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa ujenzi wa Soko la Kwa Mrombo haukuzingatia uwepo wa stoo kwa ajili ya kuhifadhia nafaka. Kamati inafahamu kuwa soko hili, pamoja na bidhaa nyingine itakuwa na wafanyabiashara watakaokuwa wanauza nafaka, kama vile mahindi, mchele, maharage na vinavyofanana na hivyo. Kamati inaona kuwa kutokuwepo kwa miundombinu ya stoo kunaweza kusababisha usumbufu kwa wafanyabiashara.

b) Baadhi ya maeneo yanayopakana na soko kuwa katika hali duni

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa kuna majengo upande mmoja (Magharibi) mwa soko hilo majengo yake yanayotumika kama maduka madogo ni ya kiwango kidogo huku yakiwa yamechakaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa soko jipya la Kwa Mrombo linalojengwa ni la kisasa. Kamati inaona kuwa upande wenye majengo ya hali ya chini na yaliyochakaa hayataleta sura nzuri kwa soko la kisasa linalojengwa. Kamati inatambua kuwa maeneo hayo pamoja na majengo yake ni mali ya Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Maoni na Ushauri wa Kamati

Serikali ihakikishe wananchi waliokuwa wanafanya biashara zao katika soko hili wanapewa kipaumbele cha kupewa nafasi kuendelea na biashara zao;

2.1.13 Ujenzi wa Soko la Kilombero

Mheshimiwa Spika; Mradi wa Ujenzi wa Soko la Kilombero unatekelezwa katika eneo lenye mita za mraba 18,215, ambapo jumla ya eneo litakalojengwa ni mita za mraba 10,885, ikihusisha uboreshaji wa mazingira ya nje *(landscaping)*, mifumo ya maji ya mvua, maji taka pamoja na miundombinu ya kisasa ya Maegesho ya magari na vyombo vingine vya moto.

Mheshimiwa Spika; utekelezwaji wa mradi huu unaogharimu Shilingi 9,502,042,553, unatekelezwa na Kampuni ya **M/S MOHAMMED BUILDERS LIMITED** na unasimamiwa na Mhandisi Mshauri kutoka kampuni ya **Mhandisi Consultancy Ltd** kwa ushirikiano na kampuni ya **GBS Consultant** Ltd za Dar es Salaam.

Hatua za Utekeleza wa Mradi

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia wakati wa ukaguzi wa mradi huu mkandarasi tayari alikuwa ameshalipwa asilimia 41.66%, ambayo ni shilingi 3,958,851,898,00.

Mheshimiwa Spika; Soko hili limesanifiwa kuwa na miumbombinu mbalimbali ikiwemo, Vizimba 518, vitakavyopokea wafanyabiashara 2,072 kwa wakati mmoja; maliwato ya kike na ya kiume, vyumba viwili vya mapumziko kwa kina mama wajawazito na wanaonyonyesha watoto vyenye uwezo wa kuweka vitanda 32 kwa wakati mmoja, vyumba viliwi vya Ibada kwa dini za Kikristu na dini ya Kiisalamu, maeneo manne (4) kwa maduka makubwa, benki, ofisi na huduma nyinginezo, vyumba viwili vya kuhifadhia mazao yanayoweza kuharibika kama vile nyama na vinginevyo *(cold rooms)*, kituo cha polisi, chumba cha huduma ya kwanza, miundombinu rafiki inayokidhi mahitaji ya watu wote kufikia sehemu zote za soko ikiwemo ngazi ya watu wenye ulemavu *(ramp)* na ngazi pande zote mbili; eneo la bustan

kwa ajili ya mapuziko ya Wafanyabiashara na Wateja na maegesho ya vyombo vya moto.

Changamoto

Mheshimiwa Spika; utekelezaji wa Mradi huu umekumbwa na changamoto ya upatikanaji wa vifaa vya ujenzi, hali iliyochelewesha mkandarasi kuweza kufikia lengo kwa asilimia 5%, ambapo sasa mradi huu umeongezewa muda wa miezi sita ili kukamilika, badala ya tarehe 30/05/2026.

Uchambuzi wa Kamati

a) Uchakavu wa Soko la Awali la Kilombero

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Soko Kuu la Kilombero Mkoani Arusha linajengwa pembeni kidogo ya Soko Kuu la Zamani la Kilombero. Kamati imebaini kuwa soko hilo la zamani ni soko duni, na kwamba ni soko lililochakaa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa katika usanifu wa soko jipya limewekwa daraja litakalounganisha soko jipya na soko la zamani. Kamati inapongeza sana ubunifu huo. Hata hivyo, Kamati inaona kuwa Soko Kuu la Kilombero la zamani lina hali mbayá sana kwa miundombinu yake. Kamati inaona kuwa kuunganisha daraja kati ya Soko Kuu Jipya la Kilombero lenye miundombinu ya kisasa na lenye ubora wa hali ya juu ni kutolitendea haki Soko hili.

b) Usanifu wa Soko unaokidhi matumizi ya kisasa ya Masoko ya Kimataifa

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Soko Kuu la Kilombero la Mkoa wa Arusha limesanifiwa kwa usanifu wa kisasa unaokidhi mahitaji yote muhimu ya binadamu yanayohusiana na masoko. Kamati imeona kuwa soko hili lina maeneo maalum kwa ajili ya akina mama walio na watoto ambalo litatumika kwa ajili ya kuwanyonyesha watoto. Aidha, soko lina sehemu maalum iliyowekwa kwa ajili ya watu wa dini ya Kiislam na Kikristu kufanya

ibada kwa nyakati tofautitofauti. Usanifu wa soko umetenga hata maeneo kwa ajili ya taasisi za fedha kama vile benki na kadhalika. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa usanifu huu maridadi.

Maoni na Ushauri wa Kamati

(a) Serikali ihakikishe utekelezaji wa ujenzi wa mradi unakamilika ndani ya muda uliokusudiwa;

(b) Serikali ihakikishe wananchi waliokuwa wanafanya biashara zao katika soko hili wanapewa kipaumbele cha kupewa nafasi kuendelea na biashara zao;

2.1.14 Mradi wa Uboreshaji wa Bustani ya Mapumziko Themi (*Themi living Garden*)

Mheshimiwa Spika; Mradi wa Uboreshaji wa Bustani ya Mapumziko Themi unatekelezwa na Kampuni ya M/S MOHAMMED BUILDERS LIMITED kwa gharama ya shilingi 1,315,655,048.00, na unasimamiwa na mhandisi mshauri kutoka kampuni ya Mhandisi Consultancy Ltd kwa ushirikiano na kampuni ya GBS Consultant Ltd za Dar es Salaam.

Faida za Mradi

Mheshimiwa Spika; faida zitakazopatikana kutokana na mradi huu ni pamoja na kuongeza ajira, kipato cha wananchi, pamoja na mapato ya Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Chagamoto za Utekelezaji Mradi

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu ambao mpaka kufikia tarehe ya ukaguzi wa mradi ulikuwa umefikia asilimia 20.17% ya utekelezaji wake, ulipangwa kuanza tarehe 30/05/2025 na kukamilika tarehe 30/05/2026, ulikumbwa na changamoto mbalimbali zikiwemo michoro ya usanifu iliyokuwa imeandaliwa awali haikuwa ya kina kwa baadhi ya maeneo kutokana na asili ya eneo la bustani pamoja na uwepo wa mimea adimu, na ukamilishaji wa mapitio ya usanifu (design review) kwa kina hali

iliyopelekea utekelezaji wa mradi kuchelewa kuanza na badala yake kuanza tarehe 09/10/2025.

Uchambuzi wa Kamati

Usanifu wa Mradi

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa usanifu wa mradi huu ni wa kisasa na unaoweza kuhudumia (to accommodate) watu wa aina zote. Bustani ina maeneo kwa ajili ya watu kuembea kwa miguu, kuna maeneo kwa ajili ya kutembea bila kuvaa viatu, maeneo kwa ajili ya viburudisho na vinywaji, madaraja na mambo mengi yanayofanana na hayo. Kamati inapongeza usanifu wa bustani hii.

Maoni na Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali ihakikishe kuwa mradi wa uboreshaji wa Bustani ya Mapumziko Themi unakamilika kwa wakati ili wananchi waweze kufaidika na huduma iliyokusudiwa;

2.2 Tathmini ya Jumla ya Utekelezaji wa miradi, kwa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026, kutembelewa na kukaguliwa na Kamati

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kufanya ukaguzi wake wa miradi katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Kilimanjaro na Arusha imefanya uchambuzi wa jumla wa ukaguzi wake kama ifuatavyo: -

2.2.1 Udhaifu wa Utekelezaji wa Miradi katika Mkoa wa Morogoro

Mheshimiwa Spika, Katika ukaguzi wake Kamati imebaini kuwa kumekuwa na udhaifu wa utekelezaji wa miradi katika Mkoa wa Morogoro. Miradi kama ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro pamoja na ujenzi wa Stendi ya mabasi madogo ya Mji wa Mikumi. Aidha, utekelezaji

wa miradi ya Barabara ya Muhimbili na Stendi ya Magari Madogo ya Kihonda katika mkoa huo ni ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imebaini kuwa ujenzi wa miradi ya shule katika Mkoa wa Arusha imekuwa na kasoro kadha wa kadha kama vile ukosefu wa maji katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Longido Samia, ukosefu wa uzio katika shule ya Wasichana ya Longido Samia, Shule ya Awali na Msingi ya Lowasa pamoja na Shule ya Sekondari ya Migungani One.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, baada ya Kamati kufanya ukaguzi wa miradi katika miradi yote, Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa miradi umewezeshwa kwa kutumia fedha za ndani. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii. Hii ni dalili njema ya Serikali yetu kuanza kujitegemea katika kutekeleza mambo yake ya msingi, hasa miradi ambayo ina kipaumbele cha juu kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati imebaini kuwa miradi inayotekelezwa na Halmashauri nchini ina changamoto nyingi kuliko inayotekelezwa na taasisi zilizo chini ya OWM-TAMISEMI. Kamati inadhani kuwa kunaweza kukawa na changamoto ya usimamizi wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo kwa ngazi ya Halmashauri. **Kamati inashauri OWM-TAMISEMI kuimarisha usimamizi katika utekelezaji wa miradi ya Halmashauri nchini**.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa katika miradi mingi inayosimamiwa na Halmashauri iliyotembelewa na kukaguliwa kumekuwa na changamoto ya usanifu. Kwa mfano, mradi wa Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro umesanifiwa kujengwa katika eneo ambalo ni oevu. Aidha, ujenzi wa stendi ya Mabasi ya Mikumi umepangwa kujengwa katika eneo oevu lakini pia lililo eneo ambalo si rafiki kwa matumizi ya stendi. Vilevile, Soko Kuu la Mkoa wa Arusha limesanifiwa bila kuzingatia soko la zamani huku soko hilo la zamani likitegemewa kuendelea kutumika. Stendi Kuu ya Mabasi ya Mkoa wa Arusha ilisanifiwa kujengwa katika eneo ambalo lina njia kubwa ya umeme. **Kwa hali hiyo, Kamati inashauri kuwa miradi yote inayosanifiwa kutekelezwa na halmashauri, kabla ya kuomba bajeti Wizara ya TAMISEMI itume timu ya kufanya ukaguzi na**

kujiridhisha kuhusu usanifu na upembuzi yakinifu uliofanyika kwa ajili ya miradi hiyo. Kamati inaendelea kushauri kuwa, Serikali izingatie kanuni za uendeshaji miradi (*Principles of Projects Management*) kwa kufanya upembuzi yakinifu *(Feasibility study)* na Tathmini ya Athari kwa Mazingira (*Enviromental Impact Assessment*) kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi ili kuhakikisha miradi inayotekelezwa inaleta athari chanya na tija iliyokusudiwa kwa jamii;

SEHEMU YA TATU

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

Mheshimiwa Spika, Baada ya Wizara pamoja na Sekretarieti za Mikoa kuwasilisha Bajeti zao kwa mafungu 28 Kuanzia tarehe 19 hadi tarehe 30 Machi, 2026, Kamati ilipata wasaa wa kuichambua na kuijadili, lakini pia Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara kama ifuatavyo:-

3.1 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Mwaka 2025/2026

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo nane (8). Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza Maoni na Ushauri wa Kamati. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanyia kazi Maoni na Ushauri huo.** Aidha, kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu Kamati itaendelea kuyasisitiza katika taarifa hii likiwemo, suala la shule za mchepuo wa Kiingereza, upungufu/uhaba wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini, na madeni ya watumishi katika Halmashauri nchini.

3.2 Uchambuzi wa ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia **Fungu 56** (Makao Makuu ya Wizara), Fungu 02 (Tume ya Utumishi wa Walimu) na Mafungu 26 kutoka Sekretarieti za Mikoa katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ilikadiria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 1,925,881,323,464.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 188,960,306,000.00** sawa na **asilimia 9.8** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara, **Shilingi 1,644,835,000.00** sawa na **asilimia 0.09** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Shirika la Elimu Kibaha; **Shilingi 21,721,743,786** sawa na **asilimia 1.2** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka – Dar es Salaam (DART); **Shilingi 10,745,182,213.00** sawa na **asilimia 0.6** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa; **Shilingi 3,506,815,065** sawa na **asilimia 0.25** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa; **Shilingi 7,000,000,000.00** sawa na **asilimia 0.36** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA); **Shilingi 11,489,598,000.00** sawa na **asilimia 0.59** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Shirika la Masoko ya Kariakoo; **Shilingi 306,108,174,064.00** sawa na **asilimia 0.015** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Ofisi za Mikoa na **Shilingi 1,680,506,764,000** sawa na **asilimia 87.2** zilikadiriwa kukusanywa kutoka katika Halmashauri. *(Kwa maelezo zaidi tazama Jedwali Namba 1*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaarifiwa kwamba, hadi Mwezi Februari 2026, jumla ya **Shilingi 1,161,087,740,803.41** zilikusanywa, sawa na **asilimia 90.43** ya lengo la makusanyo yote kwa mwaka. Kati ya fedha hizo **Shilingi 61,133,297,699.50** sawa na **asilimia 5.26** zilikusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara, **Shilingi 954,965,067.69** sawa na **asilimia 0.08** kutoka Shirika la Elimu Kibaha; **Shilingi 3,736,392,132** sawa na **asilmia 0.32** kutoka Wakala wa Mabasi yaendayo Kasi Dar es Salaam (DART), **Shilingi 5,316,295,239.00** sawa na **asilimia 0.45** kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa, **Shilingi 757,866,828.21** sawa na **asilimia 0.0065** kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, **Shilingi 2,324,910,186.15** sawa na **asilimia 0.2** kutoka Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA); **Shilingi 839,795,987.56** sawa na **asilimia 0.07** kutoka Shirika la Masoko ya Kariakoo, **Shilingi 172,874,155.3** sawa na

asilimia 0.014 kutoka Makao Makuu ya Mikoa na **Shilingi 1,085,852,343,508.00** sawa na **asilimia 93.5** kutoka halmashauri. *(Tazama Kielelezo Na. 1)*

JEDWALI NA 1: *Hali ya ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026, hadi mwezi Februari, 2026*

Taasisi	Makisio	Kiasi Kilichokusanywa	Asilimia ya makusanyo
Makao Makuu ya Wizara	188.960,306,000	61,133,297,699.50	48.53
Shirika la Elimu Kibaha	1,644,835,000.00	954,965,067.69	87
Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar-es-Salaam (DART)	21,721,743,786.00	3,736,392,132.00	25.80
Chuo cha Serikali za Mitaa	10,745,182,213.00	5,316,295,239.00	7.21
Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa	3,506,815,065.00	756,866,828.21	32.37
Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)	7,000,000,000	2,324,910,186.15	49.82
Shirika la Masoko ya Kariakoo	11,489,598,000.00	839,795,987.56	10.96
Maduhuli - Mikoa	306,079,400.00	172,874,155.30	84.72
Halmashauri za Wilaya	1,680,506,764,000	1,085,852,343,508	96.92

***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2026)*

KIELELEZO NA 1: *Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli ya OR-TAMISEMI (Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu 26 ya mikoa kwa mwaka 2025/2026*



***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2026)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa kati ya taasisi zote zilizo chini ya OWM-TAMISEMI Halmashauri za Wilaya ndizo zilizofanya vyema kwenye makusanyo ya maduhuli ambapo zimekusanya maduhuli kwa **asilimia 90** ya makadirio yake. Kiasi hiki ni kikubwa ukilinganisha na asilimia 66 iliyotarajiwa kufikiwa hadi mwezi Februari, 2026. Kamati ilihoji sababu ya makusanyo hayo kuwa makubwa kwa kiwango hicho na kujibiwa kuwa ni kutokana na matumizi ya mifumo mbalimbali ya ukusanyaji wa mapato iliyoanzishwa na Wizara kwa Halmashauri. Kamati inapongeza hatua hii. Kamati inashauri Wizara iendelee kuimarisha ukusanyaji wa mapato katika halmashauri na taasisi zake zote.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati imebaini kuwa Shirika la Masoko ya Kariakoo ndilo lililo chini zaidi katika makusanyo ya maduhuli. Hadi mwezi Februari, 2026 Shirika hilo lilikuwa limekusanya maduhuli kwa asilimia 10.9 badala ya asilimia 66 iliyotarajiwa hadi mwezi Februari, 2026. Kamati ilihoji ili kufahamu sababu ya Shirika la Masoko ya Kariakoo kukusanya kiwango cha chini zaidi na kujulishwa kwamba ni kutokana na soko hilo kuzinduliwa Mwezi Februari, 2026.

Mheshimiwa Spika, matarajio ya Kamati ilikuwa OWM-TAMISEMI, taasisi zake pamoja Sekretarieti za Mikoa, kufikia asilimia 66 ya makusanyo ya maduhuli hadi Februari, 2026. Hata hivyo,

taasisi zilizokusanya maduhuli yake kuzidi asilimia 66 iliyowekwa ni nne tu kati ya tisa. Kamati imebaini kuwa makusanyo ya OWM-TAMISEMI yameonekana kuwa juu kwa sababu ya taasisi mbili zilizo chini ya Wizara za Shirika la Elimu Kibaha (asilimia 87.09) na Chuo cha Serikali za Mitaa (Hombolo) (asilimia 74.21). Aidha, Makao Makuu ya Mikoa pamoja na Halmashauri zimekusanya maduhuli, hadi mwezi Februari, 2026 kwa asilimia 74.21 na 96.92 mtawalia.

KIELELEZO NA 2: *Makadirio ya makusanyo ya maduhuli na asilimia ya makusanyo halisi kwa mwaka 2024/2025*





***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2026)*

Ulinganisho wa Makusanyo ya Maduhuli kuanzia mwaka 2023/2024 – 2025/2026

***Mheshimiwa Spika**,* Kamati imebaini kuwa kumekuwa na mwendelezo mzuri wa upangaji wa makisio katika OWM-

TAMISEMI, taasisi zake pamoja na Makao Makuu ya Mikoa na Halmashauri zake kwa muda wa miaka mitatu mfululizo. Hali hii inaonesha kuwa vyanzo vya mapato kwenye OWM-TAMISEMI vinaendelea kukua na kuimarika kila mwaka. Kamati inaamini kuwa hali hii inatokana na kukua kwa uchumi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuimarisha usimamizi wa mapato pamoja na kubuni njia nzuri za ukusanyaji wa mapato na kuendelea kuzuia mianya ya upotevu wa mapato; na hivyo kuchagiza ustawi wa jamii. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweka mikakati inayosababisha ukuaji huu wa uchumi na maendeleo kwa jamii.**

JEDWALI NA 2: *Makusanyo ya Maduhuli kwa ulinganisho kuanzia Mwaka wa Fedha 2023/2024 – 2025/2026 kwa miaka mitatu mfululizo*

A.	Taasisi	2023/2024	2024/2025	2025/2026
	Makao Makuu ya Wizara	0	188,960,306,000	188,960,306,000
	Shirika la Elimu Kibaha	1,634,835,000.00	1,634,835,000	1,644,835,000
	Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar-es-Salaam (DART)	17,172,749,540.00	21,577,652,305	21,721,745,786
	Chuo cha Serikali za Mitaa	10,437,966,865.00	10,535,182,220	10,745,182,213
	Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa	4,131,215,065.00	4,131,215,065	3,506,815,065
	Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)	15,200,000,000.00	5,600,000,000	7,000,000,000
	Shirika la Masoko ya Kariakoo	6,565,654,276.00	11,948,802,000	11,489,598,000
	Maduhuli - Mikoa	261,890,400.00	315,939,400	306,079,400
	Halmashauri	1,143,883,281,000	1,356,340,664,000	1,680,506,764,000
JUMLA		**1,199,287,592,146**	**1,601,044,595,990**	**1,925,881,323,464**

***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2026)*

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake pia Kamati ilibaini kuwa kuna ongezeko la utengaji wa makisio ya makusanyo ya maduhuli kutoka **Shilingi 1,199,287,592,146** zilizotengwa mwaka 2023/2024 hadi **Shilingi 1,925,881,323,464** zilizotengwa kwa mwaka **2025/2026**, sawa na ongezeko la **Shilingi 726,593,731,318** sawa na **asilimia 60.5**. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii. Kamati inaamini kuwa mapato hayo yataendelea kuongezeka kutokana na kukua kwa uchumi, kuongezeka kwa idadi ya watu na kuongezeka kwa shughuli za wananchi nchini. Kamati inashauri Serikali iendelee kubuni vyanzo vya kuimarisha mapato ili kuendelea kukuza uchumi na hivyo kuleta ustawi kwa wananchi.

Kielelezo Na. 3: *Mwenendo wa Utengaji wa Makisio ya Maduhuli kuanzia 2023/2024 hadi 2025/2026 kwa bilioni*



Kielelezo Na. 4: *Mwenendo wa Utengaji wa Mapato na Matumizi ya OWM-TAMISEMI kwa muda wa miaka mitatu mfululizo 2023/2024 hadi 2025/2026*



***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2026)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na ya taarifa ya Wizara kwa ulinganisho wa randama za vipindi vitatu tofauti Kamati imebaini kuwa Halmashauri zimeendelea kufanya vyema kwenye utengaji na ukusanyaji wa maduhuli ambapo unaongezeka kila mwaka wa Fedha. Wakati huo huo, Kamati imebaini kuwa Makao Makuu ya Wizara pamebaki na makadirio yaleyale ya makusanyo ya maduhuli kwa miaka miwili mfululizo. Aidha, makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli katika Makao Makuu ya Mikoa yamekuwa yakishuka kwa miaka miwili mfululizo. **Kamati inashauri Makao Makuu ya Wizara pamoja na Makao Makuu ya Mikoa kubadilisha mtazamo huo na kuanza kubuni vyanzo vipya vya mapato.**

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ukusanyaji wa maduhuli hadi mwezi Februari ya kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo, kuanzia mwaka 2023/2024 hadi mwaka 2025/2026 kumekuwa na ongezeko katika Halmashauri. Kamati inazipongeza sana Halmashauri kwa juhudi zake. Hii inaonesha kuwa halmashauri zimeendelea kuwa bunifu katika kuongeza vyanzo vya mapato, na hivyo kuendelea kujenga uwezo wa halmashauri katika kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi wake pia Kamati imebaini kuwa kwa ujumla mwenendo wa ukusanyaji wa

maduhuli kwa taarifa zinazoishia mwezi Februari kwa kila mwaka Wizara, taasisi zake na Mikoa 26 imekuwa ikiongezeka. Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato kwa ujumla umekuwa ukikua kutoka **shilingi 756,389,752,472.27 mwaka 2023/2024 hadi shilingi 1,161,087,740,803.41 mwaka 2025/2026. Hili ni ongezeko la shilingi 404,697,988,331.14,** sawa na asilimia 53.5. Kamati inasifu mwenendo huu wa ukusanyaji wa maduhuli.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati pia imebaini pamoja na ukuaji huo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa kipindi hicho kukua bado kuna taasisi ambazo mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli umekuwa ukishuka. Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar-es-Salaam (DART) makusanyo yake yamekuwa yakishuka kwa kipindi cha miaka ya fedha 2024/2025 na 2025/2026 kwa shilingi 4,969,343,555.00 na shilingi 3,736,392,132.00 mtawalia. Aidha, Chuo cha Serikali za Mitaa (Hombolo) mapato yake yamekuwa yakishuka katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2025/2026 kwa shilingi 5,063,370,896.00 na shilingi 3,316,295,239.00 mtawalia.

Jedwali Na. 3: *Ulinganisho wa mwenendo wa makusanyo ya maduhuli kuanzia mwaka 2023/2024 hadi 2025/2026*

A.	Taasisi	2023/2024	2024/2025	2025/2026
	Makao Makuu ya Wizara	0	48,957,910,165.36	61,133,297,699.50
	Shirika la Elimu Kibaha	784,156,491.50	810,710,840.00	954,965,069.69
	Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar-es-Salaam (DART)	5,859,457,872.73	4,969,343,555.00	3,736,392,132.00
	Chuo cha Serikali za Mitaa	4,881,583,363.61	5,063,370,896.00	3,316,295,239.00
	Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa	437,544,255.44	598,232,080.07	756,866,828.21

	Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)	1,555,811,906.48	1,002,864,956.17	2,324,910,186.15
	Shirika la Masoko ya Kariakoo	190,185,134.51	129,837,745.77	839,795,987.56
	Maduhuli - Mikoa	193,798,600.00	130,925,932.00	172,874,155.30
	Halmashauri	742,487,214,848	818,236,439,347.78	1,085,852,343,508.00
JUMLA		**756,389,752,472.27**	**879,899,635,518.15**	**1,161,087,740,803.41**

***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2026)*

Kielelezo Na. 5: *Mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli hadi mwezi Februari, kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizi (2023/2024 – 2025/2026 (OWM – TAMISEMI)*



***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2025)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na kielelezo cha hapo juu sura ya ukusanyaji wa maduhuli kwa upande wa Halmashauri hadi mwezi Februari ya kila Mwaka wa Fedha husika (2023/2024 – 2025/2026) umekuwa ukiongezeka.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Halmashauri zimefanikiwa kuongeza makusanyo ya maduhuli kutoka shilingi

756,389,752,472.27 hadi **shilingi 818,236,439,347.78,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na 2024/2025, ambapo ni ongezeko la **shilingi 61,846,686,875.51**, sawa na **asilimia 8.2 kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2025/2026** makusanyo ya maduhuli yamepanda kutoka **shilingi 818,236,439,347.78** hadi shilingi **1,085,852,343,508.00,** sawa na ongezeko la **shilingi 267,615,904,161,** sawa **na asilimia 32.7**. **Kamati inapongeza sana juhudi za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa makusanyo hayo.**

Utolewaji fedha za matumizi kwa Mwaka 2025/2026

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2025/2026 iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu Juni, 2024 Wizara kupitia Fungu 56, Fungu 02 pamoja na mafungu 26 ya mikoa iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 11,612,594,336,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 7,836,140,708,000.00** sawa na **asilimia 67.5** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 3,776,453,628,000.00** sawa na **asilimia 32.5** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida ambazo ni **Shilingi 7,836,140,708,000.00, Shilingi 6,292,557,648,000.00** sawa na **asilimia 80.3** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 1,543,583,060,000.00** sawa na **asilimia 19.7** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, hadi Mwezi Februari, 2026 Wizara, taasisi zake pamoja na Sekretarieti za Mikoa zilipokea jumla ya Shilingi **7,293,003,173,591.86** sawa na **asilimia 62.8** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **5,501,410,966,448.14** sawa na **asilimia 75.4** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 1,791,592,207,143.72** sawa na **asilimia 24.6** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya **Shilingi 5,501,410,966,448.14** za matumizi ya kawaida zilizopokelewa **Shilingi 4,299,038,507,722.81** sawa na **asilimia 78.1** ni kwa ajili ya matumizi ya mishahara na **shilingi 1,202,372,458,725.33** sawa na **asilimia 17.9** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)*. Aidha, kati ya Shilingi **1,791,592,207,143.72** za matumizi ya maendeleo zilizopokewa **Shilingi 1,597,047,240,601.97** sawa na **asilimia 89.1** ni fedha za ndani na shilingi **194,544,966,541.75** Sawa na **asilimia 10.9** ni fedha za nje. *(Tazama Jedwali Na. 4 pamoja na Kielelezo 6)*

Kielelezo Na 6. *Ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na zilizopokelewa hadi Februari, 2026 (OWM-TAMISEMI)*



Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi kuhusu mwenendo huu wa upokeaji wa fedha na kubaini mambo kadhaa kama ifuatavyo: -

a) Mwenendo wa upokeaji wa fedha za matumizi ya kawaida na za maendeleo

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa fedha kwa ajili ya miradi miradi ya maendeleo zilizopokelewa ni asilimia 24.6 tu. Aidha, fedha za maendeleo kutoka vyanzo vya ndani zilizopokelewa ni asilimia 89.1 ya fedha zote za maendeleo zilizopokelewa, wakati huohuo fedha za maendeleo zilizopokelewa kutoka vyanzo vya nje ni asilimia 10.9 tu. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kuhakikisha fedha za miradi kutoka vyanzo vya ndani inapelekwa kwa kiwango cha juu.**

Mheshimiwa Spika, mwenendo huu wa upokeaji wa fedha za maendeleo kutoka nje unakwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri na mikoa yetu nchini utaathirika. Hii ni dalili kuwa ukuaji wa maendeleo jumuishi kwa wananchi unaanza kurudi nyuma. Hali hii inarudisha nyuma juhudi za Serikali za kukuza uchumi na ustawi wa wananchi. **Kamati inashauri kuwa Serikali iweke mikakati mahsusi na kabambe ya kuhakikisha kwamba inaanza kutenga bajeti yake kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa kutegemea zaidi vyanzo vyake vya ndani kuliko kutegemea vyanzo vya nje**. **Kamati inaendelea kushauri Halmashauri ziendelee kuongeza mikakati ya kuibua**

vyanzo vipya vya mapato na kuendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato.

Kielelezo Na 7. *Ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na zilizopokelewa hadi Februari, 2026*



***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2026)*

Jedwali Na 4. *Mchanganuo wa mapokezi ya fedha hadi Februari, 2026*

MATUMIZI YA KAWAIDA		MATUMIZI YA MAENDELEO	
Mishahara	**Mengineyo**	**Ndani**	**Nje**
4,299,038,507,722.81	1,202,372,458,725.33	1,597,047,240,601.97	194,544,966,541.75
5,501,410,966,448.14		**1,791,592,207,143.72**	

***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2026)*

***Kielelezo Na 8.** Upokeaji wa fedha za matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo OWM-TAMISEMI hadi Februari, 2026*



***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2026)*

SEHEMU NNE

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

Mheshimiwa Spika, Kamati imetaarifiwa kuwa Bajeti ya mwaka 2026/27 ya OWM Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itatekeleza vipaumbele katika usimamizi wa utawala bora; ukusanyaji wa mapato ikijumuisha mapato yanayotokana na hewa ukaa, ujenzi wa miundombinu kwenye sekta za barabara, elimu na afya, kusimamia mifumo ya TEHAMA, uendelezaji wa vijiji na miji, na kujenga uwezo wa watumishi katika ngazi zote za usimamizi wa Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI. Kamati imeridhishwa na vipaumbele hivyo vilivyowekwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa mchanganuo wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Wizara kwa kuzingatia vipaumbele vilivyowekwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama ifuatavyo:-

4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara pamoja na taasisi zake, (Fungu 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu 02) pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa (Mafungu 26) imekadiria kukusanya maduhuli ya jumla ya **shilingi 2,336,528,152,302.47.** Hili ni ongezeko la **shilingi 412,291,663,838.47** kutoka **shilingi 1,924,236,488,464.00** iliyokadiriwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, sawa na asilimia 21.4**.** *(Tazama kielelezo Na 9)* Kati ya fedha hizo **Shilingi 188,960,306,000.00,** shilingi zimekadiriwa kukusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara, shilingi 22,922,343,786.00 kutoka Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART), shilingi 125,115,565,696.00 kutoka Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (UDART), shilingi 11,922,250,620.20 kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa, shilingi 4,220,034,839.27 kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, shilingi 5,400,000,000.00 kutoka kwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), na **shilingi 11,489,598,000.00** kutoka Shirika la Masoko ya Kariakoo. Aidha, shilingi 305,050,361.00 zinakadiriwa

kukusanywa kutoka Makao Makuu ya Mikoa, na s**hilingi 1,966,193,000,000.00** zimekadiriwa kukusanywa kutoka Halmashauri.

Kielelezo Na. 9: Ulinganifu wa Utengaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027



Mheshimiwa Spika, kwa ujumla makisio ya ukusanyaji wa maduhuli yameongezekaka kwa Halmashauri za Wilaya, Bodi ya Mikopo ya Serikail za Mitaa, Chuo cha Serikali za Mitaa (Hombolo), pamoja na Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART) (Tazama kielelezo Na 10). **Kamati inapongeza Halmashauri pamoja na taasisi za TAMISEMI zilizoongeza makisio ya ukusanyaji wa maduhuli**.

Kielelezo Na 10. Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

Mheshimiwa Spika, Kutokana na kielelezo hapo juu Kamati imebaini kuwa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imeongoza kwa kupanga kukusanya maduhuli kwa asilimia 30 ikifuatiwa na Halmashauri. Kamati imetaarifiwa kuwa ongezeko la makisio ya

makusanyo ya maduhuli kwa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa limetokana na Halmashauri nne, (4) za Songea MC, Makambako TC, Kasulu TC na Nyangh'wale DC ambazo zimekopeshwa na Bodi, na kwamba, zitaanza kurejesha mikopo yao mwaka 2026/27; Kuwekwa Kifungu Maalum cha kutenga marejesho ya mikopo na MCR kwenye mfumo wa PlanRep kudhibiti utengaji na uidhinishwaji wa fedha hizo kuhakikisha kuwa zinawasilishwa bodi kama zilivyokasimiwa. Aidha, kwa upande wa Halmashauri Kamati imeelezwa kuwa kufanyika kwa tathmini ya makusanyo ya mapato ya ndani kwa ajili ya uandaaji wa Mipango na Bajeti katika mwaka wa fedha 2025/26 na hivyo kuongeza makisio ya mapato ya ndani kumefanya makisio ya makusanyo ya maduhuli kuongezeka. Aidha, matumizi sahihi ya Mfumo wa kukusanyia Mapato wa TAUSI umedhibiti makusanyo yote ambayo yalikuwa yanakusanywa nje ya bajeti na hivyo kulazimisha Halmashauri kuiingiza katika bajeti za makusanyo.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) imepunguza makisio ya makusanyo ya maduhuli kwa asilimia 22 huku Sekretarieti za Mikoa zikipunguza makisio ya makusanyo yake ya maduhuli kwa asilimia 0.34. Kamati imetaarifiwa kuwa TARURA imepunguza ukomo wa mapato ya ndani kutokana na mabadiliko na kushuka kwa ada ya utozaji ya matumizi ya hifadhi ya barabara kulikosababishwa na mabadiliko ya sheria kwenye viwango vya utozaji wa ada hizo. Aidha, Makadirio ya makusanyo ya maduhuli katika ofisi za wakuu wa mikoa yamepungua kutokana na baadhi ya kumbi za mikutano kutumika kwa ajili ya vikao vya ndani vya serikali na kufanyika kwa ukarabati wa kumbi za mikutano na migahawa.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake, Kamati pia imebaini kuwa Makao Makuu ya Wizara pamoja na Shirika la Masoko ya Kariakoo makadirio yao ya maduhuli hayakuongezeka wala kupungua. Kamati ilihoji sababu ya makisio hayo kutokuongezeka wala kupungua na kutaarifiwa kuwa; kwa upande wa Makao Makuu ya Wizara sababu iliyoelezwa ni kutokana na jukumu la ukusanyaji wa kodi ya majengo kupewa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, kwa upande wa Shirika la Masoko ya Kariakoo, Kamati ilitaarifiwa kwamba ni kutokana na Shirika kutenga bajeti kama hiyo mwaka wa 2025/2026 kwa

matarajio ya soko kufunguliwa rasmi lakini halikufunguliwa kutokana na sababu mbalimbali, hivyo kulilazimu shirika kurejea makadirio yale yale.

Jedwali Namba. 5: *Mwenendo wa utengaji wa makisio ya makusanyo ya maduhuli kwa kipindi cha 2024/2025 hadi 2026/2027*

TAASISI	KIWANGO CHA MADUHULI KILICHOPANGWA		
	2024/2025	2025/2026	2026/2027
OWM-TAMISEMI	188,960,306,000	188,960,306,000	188,960,306,000
Shirika la Elimu Kibaha	1,634,835,000.00	1,644,835,000	
DART	21,577,652,305	21,721,743,786	22,922,343,786
UDART			125,115,565,696
Chuo cha Serikali za Mitaa	10,535,182,220	10,745,182,213	11,922,250,620
Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa	4,131,215,065	3,506,815,065	4,220,037,839
TARURA	5,600,000,000	7,000,000,000	5,400,000,000
KMC	11,948,802,000	11,489,598,000	11,489,598,000
Makao Makuu ya Mikoa	315,939,400	306,079,400	305,050,361,
Halmashauri	1,356,340,664,000	1,680,506,764,000	1,966,193,000,000
JUMLA	**1,601,044,595,990**	**1,924,236,488,464**	**2,336,528,152,302**

Chanzo: *Randama ya Wizara pamoja na Usanifu wa Kamati (Aprili, 1, 2026)*

Mwenendo wa Upangaji wa maduhuli kwa Kielelezo Na 11. *Ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa miaka mitatu mfululizo (2024/2025 hadi 2026/2027 – OWM TAMISEMI*









Chanzo: Randama ya Wizara pamoja na Usanifuw a Kamati (Aprili, 1, 2026)

4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 – OWM-TAMISEMI

a) Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya OWM-TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 OWM-TAMISEMI (Fungu 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu 02), na Sekretarieti za Mikoa (Mafungu 26) inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi **12,268,472,643,000.** Kati ya hizo shilingi **8,542,154,664,000, sawa na asilimia 69** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **3,726,317,979,000** sawa na asilimia 31 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo (Tazama kielelezo Namba 12) . Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoombwa shilingi

6,844,897,496,000 sawa na asilimia 80.1 zimetengwa kwa ajili ya mishahara na **shilingi 1,697,257,168,000**, sawa na asilimia 19.86 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, kati ya shilingi **3,726,317,979,000** za miradi ya maendeleo shilingi **2,938,501,239,000,** sawa na asilimia 78.8 ni fedha za ndani na shilingi 787,816,740,000 sawa na asilimia 21.2 ni fedha za nje.

b) Uwiano wa Mpango wa Bajeti ya Matumizi ya Wizara (Fungu 56, Fungu 02 pamoja na Mafungu 26 ya Sekretarieti za Mikoa) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 na bajeti ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na kulinganisha mpango wa bajeti wa mwaka 2026/2027 na bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka 2025/2026. Nia ni kupima mabadiliko ya matumizi na mapato katika Wizara na kufuatilia utekelezaji wa mipango kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa bajeti, Kamati imebaini kuwa kuna ongezeko la upangaji wa bajeti ya Wizara kutoka **Shilingi 11,612,594,336,000** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 hadi **Shilingi 12,268,472,643,000** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, sawa na ongezeko la **Shilingi 655,878,307,000** ambalo ni sawa na **asilimia 5.6.** Aidha, matumizi ya kawaida yameongezeka kutoka **Shilingi 7,836,140,708,000** hadi **Shilingi 8,542,154,664,000** sawa na ongezeko la **Shilingi 706,013,956,000,** sawa na **asilimia 9** huku matumizi ya maendeleo yakipungua kutoka **Shilingi 3,776,453,628,000** hadi **Shilingi 3,726,317,979,000** ikiwa ni punguzo la **Shilingi 50,135,649,000** sawa na **asilimia 1.33**.

Kielelezo Na. 12: Sura ya utengaji wa Makisio ya matumizi ya kawaida na maendeleo (OWM – TAMISEMI kwa mwaka 2026/2027





Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa matumizi ya kawaida kwa upande wa mishahara yameongezeka kutoka **Shilingi 6,292,557,648,000** kwa Mwaka 2025/2026 hadi **Shilingi 6,844,897,496,000** katika Mwaka 2026/2027; sawa na ongezeko la **Shilingi 552,339,848,000**, sawa na **asilimia 8.78** na kwa upande wa matumizi mengineyo yameongezeka kutoka **Shilingi 1,543,583,060,000** hadi **Shilingi 1,697,257,168,000** sawa na ongezeko la **Shilingi 153,674,108,000** sawa na **asilimia 9.96.** Aidha, matumizi ya maendeleo kwa upande wa fedha za ndani yameongezeka kutoka **Shilingi 2,496,431,476,000** mwaka 2025/2026 hadi **Shilingi 2,938,501,239,000** kwa Mwaka 2026/2027 sawa na ongezeko la **Shilingi 442,069,763,000** sawa na **asilimia 17.7;** huku matumizi ya maendeleo kwa upande wa fedha za nje yamepungua kutoka **Shilingi 1,280,022,152,000** kwa Mwaka 2025/2026 hadi **Shilingi 787,816,740,000** kwa Mwaka 2026/2027 sawa na punguzo la **Shilingi 492,205,412,000** sawa na **asilmia 38.45**; kama inavyoonekana katika kielelezo Namba 13 na Jedwali Namba 6.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilihoji sababu ya kupungua fedha za nje kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Wizara imeeleza kuwa, miongoni mwa sababu zilizopelekea kupungua kwa bajeti hiyo ni kubadilika kwa sera za washirika wa maendeleo ambazo zimeathiri mapokezi ya fedha za maendeleo za nje.

Kielelezo Na. 13: Mwenendo wa upangaji wa Bajeti OWM-TAMISEMI kuanzia mwaka 2024/2025 hadi 2026/2027



JEDWALI NA 6: ***Ulinganisho wa Bejeti (Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu 26 ya Mikoa) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Hadi 2026/2027***

MATUMIZI	2024/2025	2025/2026	2026/2027
Mishahara	5,524,636,066,000	6,292,557,648,000	6,844,897,496,000
OC	1,185,339,122,500	1,543,583,060,000	1,697,257,168,000
Maendeleo Ndani	2,269,830,464,000	2,496,431,476,000	2,938,501,239,000
Maendeleo Nje	1,145,414,750,667	1,280,022,152,000	787,816,740,000
Jumla	**10,125,220,403,167**	**11,612,594,336,000**	**12,268,472,643,000**

Chanzo*: Randama ya Wizara na usanifu wa Kamati*

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza jitihada inayoendelea kufanywa na Wizara katika upangaji wa bajeti ya maendeleo kwa kutumia mapato ya ndani. Hii itapelekea kuondokana na utegemezi wa fedha za wafadhili, kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuongeza juhudi katika ukusanyaji wa mapato na kuendelea kuibua vyanzo vipya vya mapato pamoja na kuboresha uwajibikaji na usimamizi wa fedha.

SEHEMU YA TANO

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Baada ya Uchambuzi wa bajeti, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo kwa lengo la Kuboresha Utendaji kazi wa Wizara hii katika kuwahudumia wananchi: -

(a) Upungufu wa matundu ya vyoo katika Shule za Msingi na Sekondari

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Kamati iliyotolewa Katika Bunge lako Tukufu kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya iliyokuwa OR-TAMISEMI, kamatili iliwasilisha maoni yake. Moja ya maoni ilikuwa ni kuhusu kufanya tathmini ya upungufu wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini, pamoja na kuelezea mikakati ya utatuzi wa changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya jitihada za kutatua changamoto hiyo. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa changamoto hiyo bado ni kubwa ukilinganisha na juhudi zilizochukuliwa na Serikali katika kutenga bajeti na kujenga matundu ya vyoo. Wakati wa uchambuzi wa taarifa za bajeti za halmashauri mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati, Kamati ilibaini kuwa pamoja na jitihada zilizowekwa na Serikali katika kufanya tathmini ya uhitaji wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini na katika ujenzi wa matundu ya vyoo, bado kuna upungufu wa matundu vya vyoo katika shule nyingi nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Wizara ifanye tathmini upya kuhusu mahitaji halisi ya upungufu wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini ;

(ii) Pamoja na Halmashauri nchini kuchukua hatua mbalimbali katika kutatua changamoto hii, Kamati

inashauri Wizara pia kuweka mkakati wa kuzisaidia Halmashauri kutatua tatizo la upungufu wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini;

(iii) Halmashauri pamoja na Wizara ya OWM-TAMISEMI kuwashirikisha wadau mbalimbali kushiriki katika kutatua tatizo la upungufu wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini.

(b) **Ujenzi wa Shule za Michepuo ya Kiingereza Nchini**

Mheshimiwa Spika, vilevile katika taarifa ya Kamati iliyowailishwa katika Bunge lako Tukufu wakati wa Mkutano wa Bajeti Aprili 16, 2025 Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu utekelezaji wa ujenzi wa shule za mchepuo wa lugha ya kiingereza.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilieleza kwa kina athari zinazoweza kujitokeza ikiwa Serikali itaendelea kujenga shule zenye mlengo wa ufundishaji kwa lugha ya kiingereza. Kamati ilishauri kwa ufasaha kwamba Halmashauri nchini ziache kabisa kuteleza miradi hiyo isipokuwa kwa kibali maalum cha OWM-TAMISEMI na kwa sababu za msingi za uanzishwaji wa shule hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Halmashauri zilizotekeleza ushauri huo kwa umakini na kwa ufanisi. Hata hivyo kuna baadhi ya halmashauri zimeendelea kutekelza miradi hiyo. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaendelea kusisitiza halmahsuri nchini kufuata ushauri kama ulivyotolewa na Bunge katika Mkutano wa 19 wa Bunge la 12.

(c) Mwongozo wa utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa ajili ya wanawake, vijana na wenye ulemavu baada ya miongozo mbalimbali kuwekwa sawa. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa katika utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, baadhi ya halmashauri hazikufuata kanuni ya utoaji wa mikopo ya 4:4:2;

huku Halmashauri nyingine zikishindwa kusimamia utaratibu uliowekwa kuhusu urejeshaji wa mikopo hiyo. Kutokana na hali hiyo, Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

(i) Halmashauri zizingatie utoaji wa mikopo kwa uwiano wa 4:4:2 kama inavyotakiwa bila ubaguzi wowote wa jinsi, au hali ya ulemavu;

(ii) Halmashauri zizingatie utaratibu wa kisheria uliowekwa kuhusu fedha za marejesho zinazorejeshwa na wanufaika wa mikopo hiyo;

(iii) Katika halmashauri nyingi nchini watu wenye ulemavu hawakufikiwa na mikopo hii kwa madai ya kukosekana kwa vikundi vya watu wenye ulemavu au vikundi hivyo kukosa vigezo na hivyo kukosa kunufaika kama ilivyokusudiwa;

(iv) Halmashauri ziweke mikakati ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu namna na vigezo vya utaji wa mikopo hiyo;

(v) Ikiwa Halmashauri zina ukwasi wa fedha zinazotokana na marejesho au utengaji wa fedha hizo, Halmashauri hiyo iombe kibali kutoka OWM-TAMISEMI kufanya ugawaji upya (reallocation) wa fedha hizo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa utaratibu utakaokubaliwa na OWM-TAMISEMI.

(d) Uzalishaji wa Madeni ya Watumishi

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa OWM-TAMISEMI kuhusu kuweka mkakati wa kumaliza madeni ya watumishi katika Halmashauri nchini. Kamati imetaarifiwa kuwa utekelezaji huo unaendelea. Hata hivyo, wakati wa uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya Mwaka 2025/2026 Kamati ilibaini kuwa zipo halmashauri ambazo zimeendelea kuzalisha madeni mapya ya watumishi, kinyume na maoni na ushauri wa Kamati. Kutoka na hali hiyo, kamati inaendelea kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Halmashauri ziache kuzalisha madeni mapya yasiyo ya lazima ya watumishi;

(ii) Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI pamoja na Halmashauri zitenge bajeti ya kuhakikisha kuwa madeni yaliyopo ya watumishi yanalipwa;

(iii) OWM-TAMISEMI iweke mkakati wa kusaidia jitihada zinazofanywa na Halmashauri nchini za kulipa madeni ya watumishi.

(e) Upungufu wa Watumishi

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba katika halmashauri nyingi nchini kuna upungufu wa watumishi hususan katika sekta za afya, elimu na uhandisi**.** Hii imepelekea baadhi ya shughuli kama vile utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji wa huduma katika halmashauri zenye upungufu wa watumishi kutofanyika kwa ufanisi na hivyo kushuka kwa ubora wa huduma hizo. Kutokana na hali hiyo, Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo:-

(i) OWM-TAMISEMI pamoja na Halmashauri nchini zifanye msawazo wa watumishi ili kupunguza ukali wa tatizo la upungufu wa watumishi katika maeneo yenye upungufu mkubwa;

(ii) Serikali kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuajiri watumishi katika kada zenye upungufu mkubwa wa watumishi katika Halmashauri nchini;

(f) Miradi Kutokukamilika kwa Wakati

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya miradi ya maendeleo katika halmashauri mbalimbali nchini haijakamilika ndani ya muda uliopangwa na hivyo kushindwa kuleta tija iliyokusudiwa katika jamii. Aidha, kuchelewa au kutokupelekwa kwa fedha za miradi ya maendeleo hususan katika miradi ambayo ilikuwa ikitegemea fedha za nje katika utekelezaji wake ni miongoni mwa

sababu zilizopelekea miradi hiyo kutokukamilika kwa wakati. Kutokana na hali hiyo Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) OWM-TAMISEMI iimarishe vitengo vya ufuatiliaji na tathmini (monitoring and evaluation) ili vitengo hivyo vitekeleze jukumu la kuimarisha ufuatiliaji na tathmini kwenye miradi yote katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ufanisi;

(ii) Serikali iendelee kubuni vyanzo vipya pamoja na kuimarisha vyanzo vyote vya mapato ili kuzifanya Halmashauri nchini, pamoja na Taifa kwa ujumla kutegemea kwa asilimia kubwa fedha za ndani katika utekelezaji wa miradi yake.

SEHEMU YA SITA

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine ninapenda kutoa shukrani zangu kwako kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati lakini pia kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu. Ninawashukuru sana Mheshimiwa Prof. **Riziki Silas Shemdoe** (Mb) – Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Reuben **Nhamanilo Kwagwilwa (Mb)** Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mheshimiwa **Jafar Rajab Seif (Mb)** Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ushirikiano wanaoipa Kamati. Aidha, ninamshukuru Katibu Mkuu Wizara ya TAMISEMI, Ndg. Adolf Ndunguru, Naibu Makatibu Wakuu, Prof. Mary Nagu, Ndg. Sospeter Mtwale, Ndg. Eng. Rogatus Mativila na Ndg. Atupele Mwambene, pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati tangu tulipoanza kufanya nao kazi na kushiriki vizuri kwenye uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kipekee ninawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa ushirikiano mzuri ambao

wananipa. Wajumbe hawa ni wachapa kazi na wameshiriki kikamilifu katika uchambuzi wa Bajeti na kuhakikisha wanahoji ili kupata ufafanuzi wa kina. Ninawapongeza sana na ninaomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Florent Laurent Kyombo	–	**Mwenyekiti**
2.	Mhe. Jafari Wambura Chege	–	**M/Mwenyekiti**
3.	Mhe. Zacharia Paulo Isaay	–	Mjumbe
4.	Mhe. Margaret Semwanza Sitta	–	Mjumbe
5.	Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis		"
6.	Mhe. Hawa Subira Mwaifunga		"
7.	Mhe. John Fransisco Nzilanyingi		"
8.	Mhe. John John Nchimbi		"
9.	Mhe. Asha Omr Rashid		"
10.	Mhe. Lucy Edward Mwakyembe		"
11.	Mhe. Jesca John Magufuli		"
12.	Mhe. Tamima Haji Abass		"
13.	Mhe. Alaudin Hasham Salim		"
14.	Mhe. Benjamin Lukubha Ngayiwa		"
15.	Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo		"
16.	Mhe. Moses Ludovico Kaegele		"
17.	Mhe. Lucy Thomas Mayenga		"
18.	Mhe. Wilson Charles Mahera		"
19.	Mhe. Mariam Abdallah Ibrahim		"
20.	Mhe. Kassim Ali Khamis		"
21.	Mhe. Henry Charles Kabeho		"
22.	Mhe. Agnesta Lambert Kaiza		"
23.	Mhe. Silvestry Francis Koka, Mb		"
24.	Mhe. Mary Daniel Surati		"

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wetu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leonard, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema. Pamoja naye ninamshukuru Mkurugenzi wa Idara ya kamati za Bunge Ndg. Athumani Brambat, *ndc*, Wakurugenzi Wasaidizi Ndg. Michael Chikokoto, *ndc,* na Ndg. Gerald Magili kwa ushirikiano wanaoipa Kamati yetu wakati wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya

Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja, **Fungu 56, 02, 36 ,47, 54, 63, 70, 71, 72, 79, 74, 75, 76, 77, 78, 79, 80, 81, 82, 83, 84, 85, 86, 87, 88, 89, 90, na 95.**

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha, naunga mkono Hoja.

Florent L. Kyombo, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

01 APRILI, 2026

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kuwasilisha vizuri maoni ya Kamati yetu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea maoni ya Kamati zetu zote ambazo zinasimamia Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Wizara zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake sasa tunaanza mjadala na hapa ninayo orodha ya wachangiaji. Tutaanza na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, atafuatiwa na Mheshimiwa Benjamin Lukubha Ngayiwa, Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera ajiandae.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaanza kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi jioni ya leo kuwa mchangiaji wa kwanza katika Hotuba ya Waziri Mkuu pamoja na Taarifa za Kamati zilizo chini ya Wizara hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaanza kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia kwa kazi kubwa nzuri ambayo ameendelea kufanya. Kwa muda wote ambao sisi kama Wabunge tumetoka kwenye maeneo yetu, tumeona mchango mkubwa kwenye maeneo yote na nyanja zote namna alivyowagusa wananchi wanyonge hasa kwenye maeneo

mbalimbali ambayo ndiyo kimbilio lao kwenye maeneo mbalimbali kulingana na taarifa zilizosomwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili niendelee kumshukuru sana, ninachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa nzuri, namna alivyoanza katika utendaji wake. Ziara alizofanya kwenye maeneo mengi ya nchi yetu zimeacha alama kwa namna ambavyo amekuwa akitatua changamoto za wananchi hawa wanyonge ambao sasa wanaamini kimbilio peke limekuwa yeye pamoja na Wizara yote kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninachukua nafasi kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri hasa Mawaziri wote walio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu hususan Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Profesa Shemdoe, Naibu Mawaziri wawili pamoja na Makatibu Wakuu kwa kazi kubwa nzuri ambayo wameendelea kuifanya. Sisi kama Kamati tunajua mchango wao na namna walivyojitoa kuhudumia Wizara yetu hii ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna msemo unasema: "Mwenye macho haambiwa tazama," tulio wengi tuna macho na tunaona kazi kubwa nzuri inayofanywa na Serikali yetu chini ya jemedari Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye leo ameweka hotuba na bajeti yake kwenye Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mambo kadhaa kama Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI na leo nitajikita kwenye eneo moja tu la Wizara ya TAMISEMI kama sehemu ya kutoa ushauri na kuboresha taarifa yetu ambayo Mheshimiwa Mwenyekiti wetu ametoka kuiwasilisha vizuri, ameisoma hapo mbele. Nitachangia mambo kadhaa katika mazingira ya kushauri na muktadha wa kushauri Serikali ili kuweza kuyaboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni *TARURA*. Kwanza ninachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kama upande wa Serikali kuridhia fedha zote za Mfuko zilizokuwa zinakatwa kutoka kwenye tozo ya mafuta sasa kwenda moja kwa moja kwenye mifuko husika ili ziende zikatoe huduma *TARURA*. Hili ni jambo kubwa, ni jambo la kihistoria. Changamoto ya *TARURA*

haikuwa fedha peke yake kuongezwa, pamoja na fedha kuongezwa, changamoto kubwa ya *TARURA* kutokufika kwenye maeneo mengi kutekeleza wajibu wao, ilikuwa ni pamoja na fedha kutokufika kwenye yale maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa na fedha ilikuwa haifiki kwa sababu fedha nyingi tulikuwa tukikata kwenye tozo zilikuwa haziendi moja kwa moja katika kuhudumia barabara zetu kwenye maeneo yetu. Kwa maamuzi haya ya Serikali kama itaamua sasa fedha hizi zinazokatwa kutoka kwenye mafuta, moja kwa moja ziende kuhudumia *TARURA*, tunaamini kabisa *TARURA* sasa watakuwa na uwezo wa kujipambanua na kusimamia kufanya kazi kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiukweli kwenye hili tunaipongeza sana Serikali kwa kuliona hili na ndilo lilikuwa ni wazo na maoni ya Kamati kuona kwamba fedha hizi kwa muda mrefu *TARURA* wamekuwa wakilia, fedha ilikuwa inakwenda kidogo ukilinganisha na mahitaji waliyokuwa nayo. Tuipongeze sana Serikali kwa kuliona hili, lakini pia tunapongeza Serikali kwa kuridhia sasa kuongeza bajeti ya *TARURA*, walikuwa wanapokea shilingi 944,000,000, sasa wanakwenda kupata fedha zaidi ya shilingi bilioni 1.2 katika utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko hili likienda sambamba na fedha hizi zinazokatwa kutoka kwenye tozo, kwenye miradi ya mafuta, ikienda huko tunaamini changamoto za barabara kwenye maeneo mengi itakuwa ni historia. Hili sisi kama Kamati tunalipongeza sana na tunajua ni kazi kubwa nzuri ambayo inafanywa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutambua mchango mkubwa wa *TARURA* kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko jambo ambalo na sisi kama Kamati tumeliona. Pamoja na chanzo cha *TARURA* kuwa ni tozo, zipo halmashauri ambazo mwongozo wa TAMISEMI unasema, kama zinakusanya zaidi ya shilingi bilioni 10 na kuendelea, wanapaswa kupeleka 10% kuihudumia barabara zetu kwenye maeneo yetu. Sisi kama TAMISEMI, kama upande wa Kamati tumeona kwamba hili na lenyewe Wizara iisimamie Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha halmashauri na majiji yote yanayokusanya zaidi

ya shilingi bilioni 10 na kuendelea wapeleke fedha hii 10% iende ikahudumie barabara za wananchi wetu kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni upande wa matundu ya vyoo. Kwanza ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuliona hili na kutoa miezi sita kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kulitekeleza, lakini jambo hili ni kubwa kuliko vile tunavyolitazama. Wakati wa mapitio ya bajeti, sisi kama TAMISEMI kwenye mikoa husika, tumegundua changamoto na upungufu wa matundu ya vyoo ni zaidi ya 100,000 mpaka 150,000 kwenye maeneo yote waliyokuwa wanaleta ile tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini ushauri wetu sisi kama Kamati, tukiziachia Mamlaka ya Serikali za Mitaa peke yake waende wakatatue changamoto ile, itachukua zaidi ya miaka mitano mpaka miaka sita kutatua changamoto ya kero kwenye maeneo yetu. Nami nichukue nafasi kuwapongeza viongozi kwa kuliona hili kwa sababu si jambo jema kuendelea kuzungumza matundu ya vyoo hasa kwenye Bunge hili. Ninakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kuliona hili na kutoa maelekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nini maoni yetu sisi juu ya hili; la kwanza, Wizara ya TAMISEMI ifanye tathmini ya kupitia sera ili waje na *ratio* ambayo inahitajika kwa wanafunzi 20 wanatumia matundu mangapi ya choo. Sasa hivi sera inasema wanafunzi 20 wanatumia tundu moja. Wanafunzi 20 kutumia tundu moja ukiweka kwenye shule ya wanafunzi zaidi ya 1,000, au 1,200 utahitaji matundu 50 mpaka 60 kuzunguka lile eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukaona sisi kama TAMISEMI kwamba vinginevyo kuna mahali itafika shule ukuta wake utazungukwa na matundu ya vyoo peke yake. Kwa hiyo tukasema, kwanza wapitie sera ile, waje na *ratio* ambayo inakwenda na dhana na uhalisia uliopo hivi sasa kwa sababu matundu haya wingi wa zaidi ya 100,000, 150,000 ni kwa sababu tunatumia *ratio* ambayo kimsingi inawezekana haiendi na uhalisia ulioko maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakifanya ile tathmini, wakapata uhalisia wa matundu mangapi yanatakiwa kwa mwanafunzi mmoja, *then* waje sasa Serikali itenge fedha na ninaamini watatekeleza kwa muda kwa namna ambayo litatakiwa lifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, tulijadili juu ya *NeST* kwa maana ya bakaa. Hili jambo ni jambo mtambuka. Kwanza mimi binafsi ni miongoni mwa Wabaunge wachache ambao hawaamini kwamba *NeST* inatakiwa ifutwe turudi kule tulikotoka. Kama Waheshimiwa Wabunge wanakumbuka, wakati ule Afisa Manunuzi mmoja alikuwa anaamua nani ampe mradi na anatanguliza za kwake juu, anatoa, bila usimamizi wowote wa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NeST* inazo changamoto zake ambazo zingine ziko ndani ya uwezo wa Serikali wanapaswa kuzitatua. La kwanza, lazima *PPRA* waendelee kutoa elimu namna ya kutumia Mfumo wa *NeST* kwenye maeneo yote, kwenye halmashauri zote. La pili, Serikali lazima ipeleke fedha za miradi ya maendeleo zinazopotakiwa kupelekwa kabla ya muda haujafika mwisho wa mwaka wa bajeti. Kwa mfano, leo tutanazungumza mwezi Aprili, fedha za miradi ya maendeleo kwenye halmashauri nyingine bado hazijaenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawapelekea halmashauri fedha, mwezi wa sita tunafunga mwaka (tunakwenda kumaliza ule mwaka) na tunataka wazitumie kabla ya tarehe 31 Juni, wataitumiaje hii fedha? Kwa hiyo, utakuta kwamba tunamaliza mwaka wakati wanakwenda kutangaza kunakuwa na mrundikano wa maombi kwenye Mfumo wa *NeST* na kunapokuwa na mrundikano wa maombi kwenye Mfumo wa *NeST*, tunajikuta tunavuka na ile fedha kwenda kwenye mwaka mwingine wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kurundikana kwa fedha hizi mwishoni kwenye hatima yake tunagundua kwamba *NeST*, watu wengine wanaweza wakasema *NeST* haifanyi kazi. Ni kweli ninakiri kwamba wapo watu ambao wamejificha kwenye kivuli cha *NeST,* wanashindwa kusimamia majukumu yao, wanashindwa kutenda

kazi. Sasa malengo yao ni kuhakikisha ule Mfumo unafutwa turudi tulikotoka kule nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wabunge lazima tuiombe Serikali iboreshe namna ya matumizi bora ya Mfumo wa *NeST*, lazima wasimamie fedha za miradi ya maendeleo ziende kwa muda ndani ya *quarter* ya tatu fedha ziwe zimekwenda. Kuanzia mwezi Desemba, hadi mwezi Januari, fedha za miradi ya maendeleo zianze kwenda, halmashauri zitangaze kazi ili tuwe na muda wa kufanya *assessment* ya kujiridhisha akina nani wanaomba na tuweze kuisimamia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala lingine la migogoro ya ardhi ambalo kwenye hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu ameligusa. Lazima tukubaliane hapa, pamoja na kwamba hati ni zao la mwisho la umiliki wa ardhi kwa mwananchi yeyote, lazima kuna hatua kadhaa zinazopitiwa. La kwanza, lazima uwe na *PP* lazima eneo lile lipangwe matumizi bora ya ardhi. La pili, lazima eneo lile lipimwe. Ukipima ukipata *survey plan* ndiyo unakwenda hatua ya tatu ya umilikaji wa kupewa hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi, lazima tu-*plan* na Waziri wa Ardhi alichukue hili. Mfumo wetu wa utoaji wa hati, mfumo wetu wa TEHAMA ambao unasimamia mlolongo mzima wa utoaji wa hati mpaka sasa una changamoto nyingi sana. Leo Mbunge ukienda pale unaenda kuomba hati Dodoma, utakaa zaidi ya siku moja, siku mbili, shida ni mfumo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kabla ya kwenda kwenye hatima yetu ya mwisho, ninashauri sana Mheshimiwa Waziri afanye mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, apitie mfumo wenyewe, mfumo wa TEHAMA wa utoaji na usimamizi wa utoaji wa hati, wenyewe kwanza. Uwe na uwezo wa ku-*generate Town Planning* yenyewe, iwe na uwezo wa ku-*generate TP* yenyewe na uwe na uwezo wa kutoa hati bila kuingiliwa na mtu yeyote na utoe kwa uharaka ili angalau hizi changamoto zisiwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni kuhakikisha kwamba ardhi maeneo yote inapangwa na kupimwa. Changamoto katika kijiji na kijiji kwa sababu maeneo mengi hakuna mipaka kati ya kijiji na kijiji, hazijapangwa na kupimwa. Ile *collision* ya wananchi kwamba kijiji kingine na kijiji kingine wakiingiliana wanazalisha mgomo kwenye maeneo yetu. Tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri alione hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa Serikali ni kuwekeza fedha kuhakikisha maeneo yote yanapangwa kwa matumizi sahihi ili kupunguza changamoto zilizoko kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kwa harakaharaka nitakwenda kumalizia, ni 10% ya mikopo ya vijana. Hapa tumegundua changamoto kubwa sana sisi kama Kamati. Leo hii ukichukua halmashauri kwa maana ya manispaa zilizo Mkoa wa Dar es Salaam peke yake fedha ambazo wameweka benki 10%, waliyokata hapa ni mapato wanayokusanya, 10% wakaweka benki, siyo chini ya zaidi ya shilingi bilioni 60 kwenye Halmashauri za Dar es Salaam peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya tathmini halmashauri zote nchini 186, zaidi ya shilingi bilioni 100 na kitu zipo benki zinasubiri vijana waende wakakope. Changamoto tuliyoiona ni kwamba, kwanza ni upungufu wa vijana; elimu haijatoka vizuri ya kuwahamasisha kwenda kukopa, hilo la kwanza, lakini Maafisa Maendeleo ya Jamii hawajajitoa kuona hii fursa pekee ya kutoa elimu, ili vijana waende wakakope.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachofanyika ni fedha ile sasa imekaa benki, fedha nyingi ambayo imerundikana kule ndani, ninashauri, lazima Serikali itazame. Tunachoogopa ni fedha ile ikikaa zaidi ya miaka mitatu/minne anayefaidika ni benki hizi za kibiashara, sisi kama Serikali hakuna mtu atafaidika kwa sababu, wao wana-*earn interest* kutokana na ile fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati fedha ile inakwenda kukaa benki unakuta halmashauri hizo hawana chai, hawana madawati, hawana zahanati, lakini wamechukua mabilioni ya fedha yamewekwa, wanasubiri vijana wakope. Ninaishauri

Wizara, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, wafanye-*assessment* ya kujiridhisha kama kuna uwezokano wa kufanya mabadiliko ya mwongozo na kanuni, ili fedha hizo wakati mwingine zikizidi ziende zikatumike kwenye mahitaji muhimu yanayowagusa wananchi wa maeneo yale badala ya kubaki kurundikana benki. Kimsingi, mwisho wake hatujui ni upi kwa sababu, fedha zimekaa kule na hatujajua mwongozo wake mwishoni unasema nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi niwe mchangiaji wa kwanza jioni ya leo. Ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, ahsante sana.

Nilimtaja Mheshimiwa Benjamin Lukubha Ngayiwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera. Mheshimiwa Anna Richard Lupembe ajiandae.

MHE. BENJAMIN L. NGAYIWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi kuwa mchangiaji wa pili kwenye Hotuba hii nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri, tumemwona anazunguka katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu na kwa kweli, amesaidia sana kurudisha tabasamu kwa wananchi wetu. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza pia, Mawaziri wote waliowasilisha leo na Wenyeviti wote wa Kamati ambazo ziko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kipekee zaidi ninamshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuwa mtulivu na *focused* kwenye ile mipango yake ya miaka mitano kuhakikisha kwamba, wananchi wetu wanaenda kupata maendeleo kama ambavyo tumeweza kujipangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kupita katika eneo la *TARURA* kwa udharura na umuhimu wake. Mheshimiwa Rais wakati anafungua Bunge letu alieleza kwamba, anaenda kuongeza bajeti. Tumesikia pia, katika Hotuba ya Mheshimiwa

Waziri Mkuu kwamba, Serikali inaenda kuongeza bajeti, sasa ninaendelea kusisitiza na kuiomba Serikali kwamba, bajeti hizi zielekezwe upande wa *TARURA,* ili waweze kukidhi na kutekeleza ile miradi yote ya maendeleo ambayo ipo huko imekwama kwa muda mrefu kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia, kutoa maoni hapo kama ambavyo tumeweza kujadili katika Kamati yetu ya TAMISEMI kwamba, tumeshuhudia kila mwaka wa fedha, Serikali imekuwa inatenga fedha, kwa ajili ya kukarabati na kutengeneza barabara hizo kila mwaka. Unakuta ndani ya miaka mitatu, miaka minne, barabara moja imetumia shilingi milioni mia wakati mwingine zaidi ya shilingi milioni mia moja, lakini mwaka unaofuata unakuta barabara hiyo bado ni mbovu na haipitiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukashauri kwamba, kama ambavyo tumekuwa tunatenga fedha za 10% za mikopo, halmashauri hizi zetu pia, zielekezwe kutenga kiasi cha fedha, kwa ajili ya kuhudumia hizi barabara, kuzijenga na kuzikarabati, ili ziwe imara na ziweze kupitika msimu mzima wa kiangazi na msimu wa mvua. Pia, hapa kama inawezekana itungwe sera, ili kuziwezesha hizi halmashauri zikope fedha, kwa ajili ya kuzipeleka katika hii sekta ya miundombinu; tutajikuta kwamba, tunapunguza gharama ya kutengeneza barabara hizi kila mwaka kwa kukopa hizo fedha, tunapata wakandarasi wanatengeneza hizi barabara kwa uimara kwa kuweka mifereji na barabara zetu zikawa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifika pale Jimboni kwangu Kahama, Jimbo ni zuri sana, Mji wa Kahama ni mzuri sana, lakini changamoto ya barabara inaweza ikakufanya utamani kuondoka kesho yake kwa hiyo, hali iko hivi katika maeneo mengi. Pale Kahama tuna mtandao wa barabara karibu kilometa 923, hizi ziko chini ya *TARURA,* lakini lami tunayo kilometa 14 tu. Kuna halmashauri zingine zina kilomita saba, mbili kwa hiyo, kwa kweli, *TARURA* tuiongezee uwezo wa kuangalia uwezekano wa kuweza kuzifanya halmashauri zetu zikope, ziweze kuzielekeza katika maeneo haya au ziweze kutenga 10% nyingine, kwa ajili ya kuhudumia barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najielekeza pia, katika 10% ya mikopo kule kwenye *Local Government*. Kama alivyotangulia kusema mchangiaji aliyepita, Mheshimiwa Wambura Chege hapa, zile idara zetu za maendeleo ya jamii kwa kweli, inabidi waongeze uwezo na wapite kuelimisha vikundi hivi vya vijana, vikundi vya akinamama na watu wenye ulemavu, ili waweze kukopa na kuweza kurejesha ile mikopo kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunapitia taarifa kutoka mikoa mbalimbali tumeona tangu Juni, 2024 mpaka Februari, 2026 halmashauri imekopesha fedha nyingi sana, lakini vilevile fedha hizo nyingi hazijarejeshwa. Hii ni kwa sababu gani? Inaonyesha kwamba, ama vikundi hivi na watu hawa waliokopa hawajapata elimu nzuri ya kwenda kutumia hizi fedha ili warejeshe au ufuatiliaji wa madeni haya, ili waweze kukopesha tena hauendi vizuri. Sasa tulikuwa tunajiuliza, tutaendelea kutenga hizi fedha mpaka lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina nia njema ya kukopesha watu wetu, wananchi wetu wafanye biashara, waweze kuinua vipato vyao, lakini fedha zinazodaiwa ni nyingi sana. Pia, fedha nyingi zinazotengwa wakati mwingine unakuta hazikopeshwi, zinakaa benki wakati watu wetu kule wanalalamika; vikundi viko safi vinatimiza masharti, lakini havikopesheki, havikopeshwi fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana hilo eneo twende tukaliboreshe, elimu itolewe na watu waweze kukopesheka. Wakati mwingine tukawa tunatamani hata wasikopeshwe fedha labda, wakopeshwe vitu vya kwenda kufanyia ile biashara; kama mtu anataka kwenda kufanya biashara ya kutotolesha mayai anunuliwe mashine ya kutotolesha mayai na aweze kuendelea kuliko kupewa fedha ambazo wakati mwingine anaishia kuzitumia katika matumizi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamalizia eneo la bakaa. Tumeona halmashauri nyingi zimekuwa zinavuka na bakaa nyingi sana na kisingizio chake wakati mwingine watu wanasema mtandao au huu mfumo wetu wa *NeSTS*. Kwa kweli, *NeSTS* pamoja na mazuri yake mengi na ninaunga mkono kwamba, hali

ilivyokuwa hapo nyuma na kwa sasa tulivyo na huu Mfumo wa *NeSTS* unahitaji kuboreshwa tu, ni mfumo mzuri unaotakiwa kuboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaweza nikakwambia baada ya ziara yetu ya Kamati ya TAMISEMI tumeweza kushuhudia kwamba, mkandarasi mmoja anapewa miradi zaidi ya saba kwenye mkoa mmoja. Wakati mwingine kwenye nchi nzima ukifuatilia ana barabara kilometa tatu Geita, ana barabara kilometa saba Kahama, ana barabara kilometa nne Songea. Sasa ukiangalia katika kutengeneza barabara inahitaji *mobilization* ya mitambo, upeleke kule wataalam, upeleke *capital,* sasa unakuta wakati mwingine mashine hizi na mitambo inakuwa ni michache. Kwa hiyo, unakuta huyu mkandarasi anagusa kidogo Mradi wa Songea, anagusa kidogo Mradi wa Geita, anagusa kidogo Mradi wa Kahama na yote haikamiliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapendekeza pale kwenye *NeSTS,* ule mfumo uweze kuwekwa vizuri. Kwamba, uweze kuwezesha hii miradi midogomidogo ya kilometa mbili, kilometa tatu, wachukuliwe wakandarasi wa eneo husika waweze kufanya hiyo kazi kwa umahiri na kwa muda, ndani ya muda ambao unatarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi bakaa pia, tunaomba Serikali iweze kupeleka hizi fedha *timely*. Halmashauri nyingi zinapokea fedha baada ya nusu ya mwaka kupita, sasa wakianza kutangaza *tender;* kwa mfano, tuliona Mkoa wa Lindi kule unakuta mkandarasi ameomba *tender,* anaenda mpaka *site,* halafu akifika anaona ile kazi haimlipi ana-*withdraw*, halmashauri inaamua kutangaza upya, inatangaza mpaka mara tatu. Kwa hiyo, tuangalie pia, hii michakato ya ku-*award tender* tusiende tu kwa ku-*award* hawa wanao-*tender,* kwa wale *low bidder* wanaotenda kwa chini halafu na hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, huwezi kumpa mtu a-*supply apple* kwa shilingi mia mbili wakati linauzwa shilingi mia tano na wewe unampa huyo kazi, unajua kabisa atafeli. Kwa hiyo, tuangalie kabisa tathimini ifanyike vizuri hata mtu anayepewa hiyo *tender* tunajua kabisa anaenda kufanikisha hiyo

kazi na kuifanya kwa umahiri mkubwa. Ninakushukuru sana na ninaomba niunge hoja mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Benjamin, ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe.

MHE. DKT. WILSON C. MAHERA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaanza kushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bunge la Bajeti, kama mtu wa tatu. Nikiwa natokea Jimbo la Butiama naomba kwanza nianze kwa kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kutupatia dira ambayo inatuwezesha kulipeleka Taifa hili katika Dira ile ya Mwaka 2050. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Waziri Mkuu kwa utendaji kazi wake mzuri, viongozi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na wasaidizi wao pamoja na Katibu Mkuu. Ukiangalia Hotuba ya Waziri Mkuu, ya leo kwa kweli, ina mikakati mizuri ya kutuonesha kwamba tunakwenda kuitekeleza Dira hii ya Mwaka 2050 na hasa mpango wa maendeleo wa miaka minne ambao tayari dhima yake ni kukuza uchumi na kuzalisha ajira. Lengo kwa kweli, ni itakapofika Mwaka 2050 tuwe na Taifa la watu ambao wanajitegemea kwa hiyo, mambo mengi ya msingi yameelekezwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza pia, Rais kwa mambo yafuatayo; ukiangalia katika bajeti ya leo, hasa kipaumbele kinatolewa katika kuimarisha barabara za mijini na vijijini. Kwa hili pia, ninachukua nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu kwa kuielekeza Wizara ya Fedha kuimarisha upatikanaji wa fedha za Mfuko wa Barabara na kuelekeza zipelekwe moja kwa moja. Kwa hili ninaungana na Wabunge wenzangu waliotangulia kwamba, sasa angalau ile 30% ambayo ilikuwa inakwenda tena *TANROADS* halafu ndiyo ipelekwe *TARURA* sasa itaenda moja kwa moja *TARURA* na itawezesha utekelezaji wa barabara za *TARURA* kufanyika kwa umakini wa hali ya juu sana, kwa sababu, tatizo la *TARURA,* kama walivyosema watangulizi siyo kwamba, wana upungufu wa fedha bali fedha zilikuwa haziendi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini sasa kwa agizo hili kwa kweli, mambo yatakwenda kuwa mazuri zaidi na hii tumeona kabisa hata katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Leo kuna baadhi ya barabara za kimkakati zinakwenda kujengwa, hasa barabara za kwenye majimbo, pamoja na madaraja yale 13 ikiwemo ile Barabara ya Suguti, Mkoa wa Mara kwa hiyo, ninapenda kuipongeza sana Serikali kwa hatua hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia,kuipongeza Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuunganisha Mkongo wa Taifa katika wilaya 120 kati ya wilaya 139, hii ni 86%. Sasa ninashauri hizi wilaya 19 ambazo zimesalia nazo zikamilishwe. Hii itasaidia katika kuongeza utekelezaji wa shughuli za Serikali za kidigitali na kuongeza mawasiliano inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua pia, nafasi hii kuipongeza Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan na Hotuba ya Waziri Mkuu leo, hasa kwa kuendelea kujenga utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Mwaka 2004, Toleo la 2023, ambapo mambo ya msingi yaliyoko mle ni pamoja na kuwapatia watoto wa kike elimu ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Pia, lengo ni kuhakikisha kwamba, elimu ya amali inatolewa, lakini unaona shule 26 za wasichana zimejengwa kwenye kila mkoa na tayari shule saba zinajengwa, kwa ajili ya wavulana, lakini shule 103 za amali zimejengwa na kati ya hizo 29 ni zile za amali za ufundi na nyingine 74 siyo za ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia pia, shule 158 zinatekeleza mkondo wa amali. Sasa ushauri wangu hapa ni kwamba, tujitahidi kuhakikisha kwamba, tunakamilisha majengo yale yanayohitajika pamoja na kuajiri walimu wa masuala haya ya amali, pamoja na kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ili angalau mambo yaweze kwenda vizuri kwa sababu, hiyo ndiyo itakayokuwa njia pekee ya kusaidia kuhakikisha kwamba, ajira zinapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza pia, Serikali kwa kujenga *VETA* 64 ambazo zitasababisha kila wilaya iwe na *VETA* na ile moja ya Mkoa wa Songwe. Cha muhimu hapa ninachoshauri ni kwamba, tuongeze upatikanaji wa vifaa vya

kufundishia na kujifunzia. Pia, tuongeze kasi katika kuajiri Watumishi, ili angalau masuala ya amali *vocational* yaweze kufundishwa kwenye halmashauri zetu. Sasa tunazo *VETA* katika kila Wilaya, lakini ifikie mahali kwa sababu, tunayo *VETA* kila mkoa sasa twende kwenye *VETA* kila halmashauri, ili kila halmashauri iwe na mambo ya ufundi wanayofundisha kutokana na mazingira halisi ya huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia, kushauri kwamba, tuwekeze sana katika ajira za walimu wa sayansi na mambo ya hisabati. Tujenge *lab* kwenye hizi shule zetu za sekondari ambazo zimejengwa maana kuna juhudi kubwa sana ya ujenzi wa madarasa na maabara, hivyo vitu vikikamilika vitasaidia sana kuhakikisha kwamba, elimu inayotolewa ni ile ambayo itasababisha tuweze kufikia malengo ambayo tunayataka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kwamba, kuna *campus* 14 zimejengwa katika mikoa yote kwa hiyo, Tanzania kwa sasa, mikoa yote, inakwenda kuwa na *campus* za vyuo vikuu. Nadhani ni wakati muafaka wa kutumia hizi *campuses* kuhakikisha kwamba, zinatoa fursa za kufundisha masomo haya ya *innovations* kwenye maeneo yetu ya Mikoa, ili kuweza kuhakikisha kwamba, watu wanapata ujuzi wa kuweza kujiajiri wao wenyewe, ili tuweze kuhakikisha tunapunguza tatizo la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii pia, kuipongeza Serikali kwa kuhakikisha kwamba, katika kipindi cha mpaka Februari, 2026 zaidi ya shilingi bilioni 43.5 zimetolewa, kwa ajili ya kaya maskini. Pia, mikopo imetolewa kwa wanafunzi 3,179 wanaotoka katika kaya maskini na wanasoma katika vyuo vyetu; hilo ni jambo la kuipongeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninashauri, kupitia *TASAF,* kama mnavyojua, malengo ya Mheshimiwa Rais sasa hivi ni kuhakikisha kwamba, Bima ya Afya kwa Wote inatumika. Sasa hili suala limeanza kutekelezwa, lakini linasimamiwa sana na Wizara ya Afya. Hivi karibuni walikuwa wanafanya ubainishaji wa kaya maskini ambazo zitanufaika na hili suala la Bima ya Afya kwa Wote, wanaokwenda ni watu wa *NHIF,* wakifika kule wanashirikiana na wale waratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kwamba, kwa sababu, zaidi ya 80% ya Watanzania wanatibiwa katika huduma ya afya ngazi za msingi, hapohapo ni TAMISEMI, nadhani ni vizuri tukaboresha ubainishaji wa wahusika watakaopata hii Bima ya Afya kwa Wote kwa kushirikiana na Watendaji na Wenyeviti wa Vijiji. Kwa maana nyingine ni kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ishirikiane kwa karibu sana na Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye suala la mikopo nadhani 10% hii, tunaishukuru tena Serikali kwa kuleta zile kanuni, imeboresha kanuni. Tunadhani ifike mahali fulani majiji nayo ya-*graduate* kusudi zile fedha ambazo wanapeleka kwenye vikundi wapeleke chache, nyingine wapeleke kwenye miradi ya maendeleo, ili Serikali iweze kuwa na uwezo wa kupeleka fedha kwenye halmashauri ambazo ni za hali ya chini. Huo nao ni ushauri ambao ninajaribu kuutoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya fedha za mikopo ya madeni ya watumishi. Hapa napo tumeona kwamba, bado watumishi wengi sana wa halmashauri, Mamlaka za Serikali za Mitaa wanadai fedha. Kwa hiyo, tunashauri hapa Serikali, kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, wajitahidi sana kadri inavyowezekana kutathmini haya madeni na kuyalipa kwa kadri inavyowezekana kwa haraka iwezekanavyo kwa sababu, tumeona hiyo ni changamoto ambayo ni kubwa kwa kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matundu ya vyoo; ninadhani vilevile hii moja kwa ishirini na tano kwa wavulana na moja kwa ishirini kwa wasichana iangaliwe kati ya Wizara ya Elimu na Wizara ya TAMISEMI kusudi tuwe na uhalisia. Hii itasaidia kupunguza gharama hizi au kuonekana kwamba, tunadaiwa matundu mengi sana kumbe hali halisi ya Watanzania ni, labda tundu moja wanaweza wakatumia wanafunzi 30 au 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile madarasa; ifikie mahali hii *one to forty* nadhani bado ni *requirement* ya hali ya juu sana. Tuangalie, hiyo nayo itasaidia kupunguza upungufu mkubwa ambao unaonekana upo wa madarasa. Kwa hiyo, ninapenda kuchangia hayo na pia, kwa sababu tuna changamoto ya walimu kwenye masuala haya ya amali, ninaishauri Serikali iweze

kuajiri watumishi zaidi na ikiwezekana waende kwenye Nchi za Ulaya Mashariki kupata walimu ambao watakuja kusaidia kufundisha kwenye masomo haya ya sayansi, teknolojia pamoja na amali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala ya afya, hotuba inaonesha kwamba tutawekeza zaidi katika maboma ya zahanati, lakini zaidi ya akinamama waliofanyiwa upasuaji wanapojifungua, 75% wamejifungua kwa wamefanyiwa upasuaji katika vituo vya afya. Kwa hiyo, ninashauri kwamba bajeti hii tuwekeze sana katika ujenzi wa vituo vya afya badala ya kukamilisha maboma ya zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera kwa mchango wako. Mchangiaji wetu wa mwisho jioni hii ni Mheshimiwa Anna Richard Lupembe. *(Makofi)*

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninaomba nimshukuru Mungu ambaye ameendelea kututetea na kutulinda leo ni tarehe Mosi Aprili tuko mahali hapa. Ninaomba nimpongeze sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipekee sana ninaomba nimpongeze Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwa Watanzania, ameleta imani kubwa kwa Watanzania kwa ajili ya Serikali yao, hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niwapongeze Waziri wa TAMISEMI pamoja na Naibu Mawaziri wake wote wawili, Naibu Waziri wa Afya pamoja na Naibu Waziri wa Elimu. Pia ninaomba nimpongeze Mkuu wangu wa Mkoa, Mwanamvua Mrindoko kwa kazi kubwa ya usimamizi wa shughuli zote za Mkoa wetu wa

Katavi. Ninaomba nimpongeze Mkuu wetu wa Wilaya, Mheshimiwa Jamila Yusuf ambaye anasimamia maendeleo yetu na mipango yote ya Wilaya yetu ya Mpanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze *Chief* wa *TARURA* Ndugu yetu *Engineer* Victor H. Seff kwa kazi kubwa na usimamizi wa barabara zetu katika maeneo yetu ya vijijini, lakini ninawapongeza mainjinia wetu wa Mkoa wetu wa Katavi pamoja na mainjinia wa Wilaya yetu ya Mpanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mtu atasimama hapa kwa ajili ya *TARURA*. Kwa Wabunge wa vijijini *TARURA* ni chombo muhimu sana. Nimesimama hapa tukiomba pesa za dharura kwa sababu hali imekuwa ngumu, madaraja, barabara zimekatika, vijito vyote vinatoa maji, chemchemi zimeibuka barabara hazipitiki. Maeneo ya vijijini tunaomba Serikali kwa unyenyekevu mkubwa, tunajua wametoa na wameongeza bajeti, lakini kwa kipindi hiki cha Mwenyezi Mungu ameleta neema kubwa ya mvua katika nchi yetu ya Tanzania, tunapokea neema hiyo kubwa, lakini kwenye neema hiyo kuna changamoto ambazo zimetokea, lazima tuzipokee tuzikubali. Tunaomba kwa sababu uharibifu umekuwa mkubwa, tunaiomba Serikali yetu kwa unyenyekevu itoe pesa za dharura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoongea kuna maeneo yangu, watoto sasa hivi hawaendi kabisa shule. Kumegawanyika kabisa hawaendi shuleni. Ninaomba Serikali yangu sikivu, tupewe pesa za dharura. *TARURA* wapewe pesa za dharura ili waweze kwenda kurekebisha barabara za muhimu ili watoto warejee katika maeneo yao ya shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* kwa vijijini ndiyo kiungo chetu kikubwa kwa uchumi. *TARURA* imefanya kazi kubwa sana, imetujengea madaraja, imetengeneza barabara vizuri sana, imewafikia wananchi kijiji kwa kijiji, kitongoji kwa kitongoji. Ninaomba niipongeze Serikali kwa kuiongezea bajeti *TARURA*, kwa sababu Wabunge wengi kilio chetu *TARURA* wakipata pesa wakiwa na bajeti nzuri watatengeneza barabara za vijijini kwa uhakika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niipongeze Serikali yangu kwa kuongeza bajeti ya *TARURA* kwa sababu tunajua sasa barabara zitakuwa nzuri, barabara zitatengenezwa, madaraja yatajengwa na wananchi wa vijijini wataongeza uchumi wao kwa sababu mazao yote tunayatoa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nishukuru upande wa afya. Nimeletewa katika siku 100 za Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, nimeletewa pesa za kituo cha afya, nimeletewa pesa kwenye shule za msingi na sekondari. Ninaomba niipongeze sana Serikali kwa kazi kubwa nzuri inayoendelea kuifanya katika nchi yetu. Watoto wanakwenda shule, watoto sasa hivi wanajivunia Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu ninaomba vituo vya afya, lakini katika hospitali yangu ya Halmashauri ya Nsimbo, nimejengewa hospitali nzuri ina kila kitu, nimejengewa *theater* kwa ajili ya akinamama wajawazito, lakini bado ninaomba kwa unyenyekevu nijengewe *theater* kubwa ya ujumla kwa ajili ya wagonjwa wote ili niweze kukidhi mahitaji ya hospitali yangu ya Wilaya yangu ya Nsimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa inafanyika kwenye vituo vya afya, zahanati, pamoja na shule ya msingi, pamoja na sekondari, lakini kuna miradi mbalimbali ambayo Waziri Mkuu tunaomba tumpongeze, amesisitiza sana kuwa shule zote zihakikishe zimejengwa vyoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wenzangu waliopita na tunaomba tupongeze taasisi ambayo inasimamia *PPRA*, mpango mzuri unaoendelea katika nchi yetu kwa kuendelea kusimamia ununuzi lakini bado kuna tatizo. Hili tatizo changamoto tunaomba basi kwenye upande wa *NeST*, kuna vijiji ambavyo sasa hivi vina pesa lakini hawajui wafanye nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawaomba *PPRA* watoke kwa sababu huu mpango ni mzuri, tumeweza kuboresha mambo mengi na mafanikio makubwa, watoke sasa waende kwenye halmashauri zetu, kwa sababu Wenyeviti wa Vijiji, Watendaji wa Vijiji, wanagoma kutoa zile pesa na wakienda kwenye

halmashauri zetu wanasumbuliwa njoo kesho, kesho mfumo haufanyi kazi, hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunaomba basi *PPRA* sasa wachukue jukumu la kuwapatia semina Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Kata, ili waweze kuelewa jinsi ya mfumo unavyoenda kwa sababu pesa nyingi zinakwenda katika maeneo yetu ya vijiji. Sasa unakuta vijijini kule hela zote zimekaa zimeganda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tumshukuru Waziri Mkuu alivyosema kuwa apate tathmini ya miradi yote iliyokwama ili waweze kujua watafanya nini, lakini ninaomba niishauri Serikali, *PPRA* sasa watoke waende wakatufanyie semina kwenye halmashauri zetu, kwa Watendaji wa Vijiji na wa Kata ili waweze kuelewa jinsi gani ya kuweza kuingia kwenye mfumo wa *NeST*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye 10% ninaipongeza Serikali yangu kwa kazi kubwa nzuri, 10% Halmashauri zetu wanatoa, lakini kuna changamoto kwa upande wa walemavu. Ninaomba niishauri Serikali, hatuwezi kumpata mlemavu mmoja au kundi la walemavu katika eneo moja, ninaomba nishauri kwamba akipatikana mlemavu mmoja katika maeneo apewe huyo huyo mmoja katika eneo hilo ili ufanisi na yale malengo ya 10% yaweze kutimilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua Rais ametoa ajira, tunaomba tushukuru tumepata ajira katika maeneo yetu, lakini bado kuna changamoto ya ajira, tunao upungufu, tunaiomba Serikali yetu iendelee kuajiri ili katika meneo yetu, vituo vya afya, zahanati, shule za msingi na sekondari tuweze kupata watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nikushukuru sana, ninaendelea kumpongeza Rais kwa kazi kubwa ambayo anaendelea nayo. Vilevile Waziri Mkuu wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Mwigulu Nchemba tutaendelea kumwombea ili Mungu asimame naye kwa kazi hii kubwa ngumu

aliyoibeba, kuhakikisha Watanzania wanapata amani na utulivu kwa Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Anna Lupembe ambaye ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa jioni ya leo. Nami nichukue fursa hii kumpongeza mtoa hoja Waziri Mkuu wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuonesha mwelekeo wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi ambazo ziko chini ya Wizara hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, ninawapongeza pia Wenyeviti wetu wa Kamati zote waliotoa maoni na mapendekezo, pia Wajumbe wa Kamati hizo zote kwa kazi kubwa waliyoifanya.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho tarehe 2 Aprili, 2026 saa 3.00 asubuhi.

(Saa 1:28 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamis, Tarehe 2, Aprili 2026 Saa Tatu Asubuhi)